

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 2 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU WA MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU WA MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Swali letu la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara Mbunge wa ukonga, linalekezwa kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 162

**Hospitali ya Kivule Kutumika Kama Hospitali ya Wilaya**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza:-

Hospitali ya Amana imepelekwa Wizarani, hivyo Wilaya ya llala kwa sasa haina Hospitali ya Wilaya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia Hospitali ya Kivule itumike kama Hospitali ya Wilaya ya llala?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya llala imeandaa mikakati mbalimbali kuhakikisha kuwa inapata Hospitali ya Wilaya ikiwa ni pamoja na kutenga fedha jumla ya shilingi bilioni tatu katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Kivule. Kati ya hizo shilingi 2,000,000,000 ni mapato ya ndani ya Halmashauri na shilingi 1,000,000,000 ni ruzuku ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ujenzi wa Hospitali ya Kivule, Serikali inaendelea na ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mzinga, Kinyerezi na upanuzi wa Kituo cha Afya Buguruni. Lengo la kuimarisha vituo hivyo ni kupunguza

msongamano katika Hospitali ya Wilaya na kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika ngazi za msingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini naomba niwashukuru sana Serikali ya Korea, Serikali ya Tanzania na Manispaa ya llala ambayo inaongozwa na UKAWA na wananchi wa Kata ya Chanika kwa kutoa ushirikiano wa kupata hospitali kubwa ya mama na mtoto katika eneo hilo. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anaonesha kwamba fedha kutoka Serikali Kuu ni shilingi bilioni moja, lakini kwenye bajeti ya TAMISEMI ambayo tumeshapitisha katika Bunge letu Tukufu ilionesa shilingi bilioni 1.5. Napenda nijue hii ni nyiningine imeongezeka au ni ile ya shilingi bilioni 1.5 ambayo sasa imeshuka tena imekuwa *one billion?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa kuna changamoto kubwa katika eneo hili na Mheshimiwa Waziri anakubali kwamba kuna mpango wa kujenga hospitali hii; je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutembelea eneo hili aone kwanza eneo lipo vizuri, wananchi wametoa ushirikiano wa ekari 45 twende tufanye ziara ili waweke msukumo kwa kujengwa kwa haraka na kwa uhakika ili huduma ya afya iweze kupatikana katika eneo hili ambayo itahudumia Jimbo la Ukonga, Mkuranga na eneo la Kisarawe? Ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara anauliza kwamba katika orodha ya Hospitali za Wilaya 67 ambazo zinajengwa, kwa hesabu yake anaona ilikuwa inaonesha

kwamba Hospitali ya Kivule imetengewa shilingi bilioni 1.5, lakini taarifa nilizonazo ni kwamba imetengewa shilingi bilioni moja kutoka Serikali Kuu, lakini ukiunganisha na shilingi bilioni mbili ambayo ni mapato ya ndani ya Manispaa, maana yake wao wanakuwa na shilingi bilioni tatu. Kwa ramani ambazo zinatolewa kwa ajili ya awamu ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya ni shilingi bilioni 1.5. Kwa hiyo, wao wako mara mbili yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba hospitali zinajengwa za kisasa, lakini kwa kutumia utaratibu wa *Force Account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kiasi hicho ni cha kutosha tukisimamia tukahakikisha kwamba kila shilingi ambayo inatoka inaenda kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili juu ya kwenda kutembelea maeneo hayo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nina mpango wa kwenda kutembelea eneo ambalo kinapanuliwa Kituo cha Afya cha Buguruni, Kinyerezi na maeneo mengine yote ili na mimi njiridhishe tuwe katika *page* moja tunapoongea na Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Edward Mwalongo.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Njombe, Hospitali ya Kibena ndiyo hospitali inayotumika kama Hospitali ya Mkoa, lakini imechakaa sana na haina wodi ya wanaume wala *x-ray*.

Je, ni lini Serikali itatusaidia watu wa Njombe kupata wodi ya wanaume na *x-ray*?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu. Ni lini mtawasaidia wananchi wa Njombe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyezekiti, kuhusiana na suala zima la kuchakaa Hospitali ya Wilaya ya Njombe ambayo kimsingi ilijengwa miaka ya zamani sana, tunakiri na tunatambua juu ya uchakavu huu. Kwa kadri bajeti itakavyoruhusu, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunazikarabati Hospitali za Wilaya ili zifanane na hadhi ya sasa hivi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika zile Hospitali ambazo zitakarabatiwa wakati bajeti ikiruhusu na Njombe nao hatutawasahau.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa Mbunge wa Longido nabado linalekezwa kwa ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kiruswa.

Na. 163

**Hitaji la Mabweni kwa Shule za Jamii ya Wafugaji**

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA** aliuliza:-

Ubora wa elimu wanayopata watoto wa jamii ya kifugaji wanaosoma shule za kutwa vijijini unaathiriwa sana na umbali mrefu wanaotembea wanafunzi kutoka makazi yao (maboma) hadi shuleni.

(a) Je, ni kwa nini Serikali isijenge mabweni katika baadhi ya shule zilizo kwenye vijiji vyenye mtawanyiko mkubwa wa maboma?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Longido kujenga vyumba 177 vya madarasa, nyumba 291 za walimu na matundu 561 ya vyoo?

(c) Je, Serikali imepanga lini kuziba upungufu wa walimu 234; Waratibu Elimu Kata 18 na maafisa ngazi ya Wilaya 12 katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali refu la Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mbunge wa Longido, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto inayowakabili watoto wa jamii ya kifugaji ndivyo maana katika kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 imekamilisha ujenzi wa bweni la wasichana na matundu 14 ya vyoo na inaendelea na ujenzi wa bweni la wavulana na nyumba tatu za Walimu katika Shule ya Msingi Sinya.

Vilevile nyumba ya Walimu *two in one* na madarasa matatu yanaendelea kujengwa katika Shule ya Msingi Kitumbeine ambao yatakamiliwa Juni, 2018.

Aidha, katika Shule ya Msingi Longido, ujenzi wa vyumba nne vya madarasa uko katika hatua ya msingi. Shule hizo tatu zina uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,323. Utekelezaji huo unafanyika ili kuwapunguzia adha watoto wa jamii ya kifugaji ambao kwa wastani hutembea zaidi ya kilometra 15 kutoka nyumbani hadi shulenii.

Aidha, ujenzi wa madarasa 24 kwenye Shule za Ranch, Imatiani Sokoni, Olmoti, Olmolog na Engurusai vimekamilika wakati ujenzi wa madarasa 18 katika shule mbalimbali unaendelea. Ujenzi wa bweni katika Shule ya Msingi Ngerenyai umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 515. Kwa

ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo, vyumba vya madarasa na nyumba za walimu. Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi na wadau itaendelea kujenga mabweni kwenye maeneo ya wafugaji na maeneo mengine yenye uhitaji kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Longido ina Kata 18 ambazo kwa sasa Kata zote zina Maafisa Elimu Kata. Katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya kuna upungufu wa Afisa Elimu vielelezo baada ya aliyekuwepo kuhamishwa kwenda Tume ya Utumishi wa Walimu (*TSC*). Serikali itaziba pengo hilo hivi karibuni, sambasamba na kupunguza upungufu wa walimu katika Shule za Msingi na Sekondari.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kiruswa.

**MHE. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri aliyonipa Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza, nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa sababu ya kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kuinua hali ya elimu katika Wilaya ya Longido. Historia ya Wilaya ya Longido...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa. Swali ni kwamba kwa upande wa ubora wa elimu ukizingatia kwamba ubora wa elimu unategemea uboreshaji wa shule kuanzia ngazi ya chekechea; na kwa kwa sababu vitongoji vya Wilaya ya Longido viko mbali na shule za msingi zenye elimu za chekechea (shule za awali).

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani katika kuhimiza wananchi wajenge shule na Serikali ipeleke walimu waliosomea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa tatizo la shule za msingi la miundombinu halina tofauti na Shule zetu za Sekondari katika Wilaya ya Longido; je, Serikali imejipangaje kutusaidia kuziba mapengo yaliyopo katika madarasa yapatayo 58, maabara 27, mabweni 73, nyumba za walimu 252, maktaba nane...

**MWENYEKITI:** Ahsante. umeeleweka.

**MHE. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna uhaba wa walimu wa sayansi wapatao 27? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu. Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS - TAWALAZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, katika muda mfupi tangu alipochaguliwa kuwa Mbunge amefanya mengi, ofisini kwangu ameshakuja zaidi ya mara tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zake nazipokea kwa niaba ya Serikali, naomba sana nimhakikishie kwamba wananchi waendelee na juhudi wanazozifanya. Tunatambua juhudi zao. Pale ambapo atakamilisha darasa lolote la awali, tuwasiliane ili tuweze kupeleka walimu wa madarasa ya awali ambao wamesomeshwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili kuhusu kumalizia maboma ambayo wananchi wameanzisha na yamefika kwenye lenta, naomba nimhakikishie kwamba katika fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo tutazipeleka kuanzia mwezi wa Saba tumewapa kipaumbele Wakurugenzi wazingatie sana kumalizia maboma ambayo yameanzishwa na wananchi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa ukosefu wa mabweni ni tatizo la nchi nzima na hasa katika shule za sekondari za kata, hivyo kufanya baadhi ya wanafunzi kupanga katika nyumba za watu binafsi; je, Serikali haioni umefikia wakati kuhamasisha wadau mbalimbali wa elimu kujenga *hostel* karibu na shule ili kuepuka kadhia hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalitambua sana tatizo la mabweni katika shule za sekondari za kata. Lengo la kujenga shule za sekondari za kata ilikuwa ni kuwawezesha watoto ambao wako ndani ya kata waweze kusoma, lakini tatizo ni kwamba kuna baadhi ya vijiji kweli viko mbali sana na Makao Makuu ya Kata au mbali sana na eneo ambalo ipo shule. Kwa hiyo, kuna tatizo kwamba wanafunzi wengi wamekuwa wakipanga nyumba kwa sababu hawawezi kutembea kilometra labda 15,20 kutoka nyumbani kwao kwenda katika shule kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo tatizo tunalielewa na ninaungana naye na tutaendelea kuhimiza wadau wajenge mabweni na *hostel* karibu na shule hizi ili kusudi ziweze kutoa huduma nzuri kwa watoto na hasa watoto wa kike waweze kuepuka matatizo mengine ambayo yanawapata kupanga katika nyumba za watu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa kuuliza swali la nyongeza. Matatizo yaliyopo katika Jimbo la Longido ni sawa kabisa na matatizo ambayo yapo katika Jimbo la Ludewa. Jimbo la Ludewa kwa sasa lina upungufu wa walimu 500

wa shule za msingi. Je, Serikali ina mpango gani kutuletea walimu wa shule ya msingi katika Jimbo la Ludewa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Deo Ngalawa kwa kunirejesha vizuri katika kumbukumbu zangu kwamba tunaendelea na mchakato chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Baraza la Mitihani linaendelea kuchakata na kuvikagua vyeti vyaa walimu 1,0140 ambao tunategemea waajiriwe kwa ajili ya shule za msingi ifikapo tarehe 30 Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ngalawa tuendelee kuwasiliana ili tutakapofika wakati wa kuwapangia maeneo ya kwenda, basi tuwe na mawasiliano ya karibu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizawa na Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Martha Mlata.

Na. 164

### **Utunzaji wa Mazingira**

**MHE. MARTHA M. MLATA (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati ipi kisheria kushughulikia suala la ulinzi wa maeneo ya vyanzo vyaa maji ili kunusuru maeneo hayo dhidi ya uvamizi na matumizi mengine yasiyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 katika Ibara ya 7 imeweka misingi ya kisheria ya ulinzi na usimamizi wa mazingira ikiwemo mazingira ya vyanzo vya maji.

Aidha, kifungu cha 57(1) kinaweka katazo la kufanya shughuli za binadamu ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji na kifungu cha 60(3) kinaelekeza Bodi za Maji ya Bonde kuhakikisha kunakuwa na maji ya kutosha kwa mazingira.

Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009 inaelekeza umuhimu wa kutunza na kulinda vyanzo vya maji na rasilimali za maji. Vilevile llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020 Ibara ya 152(d) nayo inasisitiza kuhusu umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji kwa kuendelea kufanya tathmini ya vyanzo vya maji vilivyohifadhiwa, kubaini vyanzo vipyta na kufufua vilivyopotea ama kuharibika ili kuwa na uhakika wa kuwa na maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa kuzingatia sheria hizi na maelekezo haya, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji kwa mwaka 2006 na mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mikakati hii, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuhamasisha jamii zinazozunguka vyanzo vya maji; Serikali za Mitaa na Vijiji kushiriki kikamilifu katika jitihada za kuhifadhi

vyanzo vya maji; kutoa elimu juu ya umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji; kuvitambua vyanzo vya maji na kuviveka mipaka; kuondoa watu waliovamia vyanzo vya maji; kupiga marufuku au kusitisha shughuli zisizo endelevu katika maeneo ya vyanzo vya maji; kuondoa miti isiyo rafiki kwa mazingira; kuondoa mifugo katika maeneo ya vyanzo na kuandaa mipango ya matumizi endelevu ya ardhi katika maeneo ya mabonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tanzania ni mwanachama wa Makataba wa Kimataifa wa Ardhi Oevu (*Ramsar Convention*) kwa mwaka 1971 na Mkataba wa Kimataifa wa Baioanuai wa mwaka 1992 ambayo moja ya lengo lake ni kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa ili kuwa na maji ya kutosha kwa kizazi cha sasa na cha baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kuhamasisha shughuli za hifadhi ya mazingira hususan kutunza vyanzo vya maji kwa kuendelea kutoa miongozo ya utekelezaji wa sheria na mikakati inayohusiana na kutunza vyanzo vya maji. Aidha, Sekta Binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali wataendelea kuhamasishwa kutekeleza mikakati inayolenga kuhifadhi mazingira ya vyanzo vya maji kwa vizazi vya sasa na vya baadaye. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa amezungumzia mikakati ya Serikali katika kuhakikisha inatunza na kuhifadhi vyanzo vya maji, ninaomba kujua, kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais ilishawahidi kutoa maelekezo kwa Wakurugenzi wote nchi nzima iweze kubaini vyanzo vyote vya maji na kupeleka orodha ili Serikali sasa ije na mkakati wa kutekeleza, siyo kwa ajili ya kuweka mikakati ya kufikiria kuanza; je, mkakati huo na agizo hilo limetekelizwa kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali ina mpango wa kufufua vyanzo; kuliko kusubiri kuja kufufua vyanzo ambavyo vilishakufa, Singida tuna maziwa mawili, Singidani pamoja na Kindai na ukienda Singidani lile ziwa limeshaanza kujaa tope. Je, kuna mkakati gani sasa wa kuja pale Singida ili mje muondoe lile tope, kina cha maji kibaki kama kilivyokuwa mwanzo? Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Kangi Lugola.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze swalii la msingi Mheshimiwa Catherine Magige kwa namna ambavyo anawakilisha Mkao wake wa Arusha na wananchi wa Arusha wanadhani yeye ndiye Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Ofisi ya Makamu wa Rais ilishatoa agizo kwa Wakurugenzi wote nchi nzima kubaini na kuorodhesha vyanzo vya maji na tuliwapa muda wa kutosha, lakini mpaka sasa ni mikoa mitatu tu katika ya mikoa yote ambao wamewasilisha orodha ya vyanzo vya maji pamoja na changamoto zake. Sasa mikoa mingine wameshindwa kutekeleza agizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya sasa ni kuhakikisha kwamba orodha ya Halmashauri zote nchini ambazo hazijawasilisha orodha ya vyanzo vya maji, tunaiwasilisha kwa Waziri Mkuu wa nchi yetu ili aweze kuamua hatma ya Wakurugenzi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, Mheshimiwa Martha Mlata naye amekuwa akifuatilia sana kero za Mkao wa Singida hasa upande wa mazingira. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Martha Mlata kwamba maziwa mengi katika nchi yetu likiwemo hilo la Singidani yamekuwa yakijaa tope kutokana na shughuli za kibinadamu. Sasa

nitamwagiza Mkurugenzi wa Mazingira wa nchi yetu aambatane na timu yake washirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Singida na ya Mji wa Singida ili waweze kuona ni mikakati gani tunayoweza kuifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunadhibiti hali hiyo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Aah, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu vyanzo vya maji katika Halmashauri zote, napenda kulipa taarifa Bunge hili kama nyongeza ya majibu kwamba mwaka 2006 wakati wa kuandaa Programu ya Maji nchi nzima ilifanyika stadi ya vyanzo vya maji nchi nzima. Kwa hiyo, kwa Wakurugenzi siyo kazi mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa agizo kwa Wakurugenzi wote, ndani ya mwezi mmoja waweze kuwasilisha Ofisi ya Makamu ya Rais hivyo vyanzo vya maji vyote kwa sababu wanavyo katika vitabu vyao. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri ametusaidia. Hili tatizo liko kutoka mwaka 2006. Sheria zipo, kanuni zipo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema hivyo, lakini iaonekana ni hadithi na ni mazungumzo tu humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuambia ni vyanzo vingapi ambavyo tayari

wamevifanyia *demarcation* na *rehabilitation* kama *sampling areas* ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kama kweli wana nia ya kuhifadhi vyanzo vya maji?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais TAMISEMI. Ooh, leo naona kila Waziri na Naibu Waziri wanataka kujibu. Sawa kabisa, ndiyo maana ya Serikali. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vyanzo vingapi. Hadi mwaka 2017 tayari tulishabaini vyanzo 18, tumeshaviwekea mipaka tayari. Mwaka huu wa Fedha tulionao tulibaini vyanzo sita, tunaendelea kuvivekeea mipaka na tutaendelea kufanya hivyo. Mheshimiwa Mbunge usubiri hotuba yangu inaanza Jumatatu tarehe 7 Mei, kwa hiyo, taarifa kamili utaipata vizuri zaidi kupitia kwenye hotuba yangu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hivi vyanzo vya maji kuvihakiki ni kwingine, Ziwa Tanganyika hakuna kazi inayofanyika, watu wanajenga majumba mpaka yanagusa Ziwa Tanganyika, lakini hakuna *operation iliyofanyika*, hakuna chochote. Hivi vyanzo vya maji ni kwingine tu, Ziwa Tanganyika mbona hakuna chochote kinachofanyika katika nchi hii? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Kangi Lugola.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama

nilivyojibu kwenye swalı letu la msingi, ni kwamba katika maziwa yote, mito yote pamoja na bahari ni kweli kabisa kwamba Sheria yetu Na. 20 ya 2004 ya Usimamizi wa Mazingira inakataza shughuli za binadamu kufanyika ndani ya mita 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyoko Ziwa Tanganyika ni sawa na changamoto ambazo ziko kwenye maeneo mengine. Ndiyo maana tunesema tunataka tubaini ili tujue ukubwa wa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wale wanaofanya shughuli za binadamu kwenye mita 60 katika Ziwa Tanganyika. Inawezekana wanafanya kwa mujibu wa kifungu cha 57(2) lakini tutatuma timu ya wataalam chini ya Mkurugenzi wa Mazingira kwenda kuona kama hao alioswasema Mheshimiwa Keissy wanaruhusiwa kwa mujibu wa kifungu cha 57(2) au la ili tuweze kuchukua hatua stahiki. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Swalı letu namba 165 linaulizwa na Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini. Linaelekezwa kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Na. 165

### **Tanzania Kuwa Nchi ya Viwanda na Uchumi wa Kati**

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha inashirikisha sekta binafsi ili kufikia dhamira ya kuwa nchi ya viwanda na yenye uchumi wa kati?

(b) Je, Serikali haioni kwamba dhamira hiyo ya kuelekea nchi ya viwanda na uchumi wa kati ni ndoto tu na haiwezi kufikiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTONY P. MAVUNDE K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya mpango wa pili wa miaka mitano ni kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Katika mpango huo, imebainishwa wazi kuwa ni jukumu la sekta binafsi kujenga viwanda. Serikali inabaki na jukumu la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Serikali iweze kutekeleza majukumu ya ujenzi wa viwanda kwa ufanisi, Serikali imeteketeza yafuatayo; kwanza, kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara kuhakikisha vikwazo vyote vinaondolewa.

Pili, kupitia Wizara na mamlaka husika kutenga maeneo ya kujenga viwanda kuanzia ngazi ya vijiji mpaka ngazi ya Taifa; tatu, kuweka miundombinu ya umeme, barabara, maji, mawasiliano na usafiri wa anga; nne, kupitia taasisi kama *SIDO*, *TIRDO*, *TANTRADE* na kutoa elimu na mwongozo wa kujenga viwanda na tano, kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika maeneo ya kipaumbele.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Dira ya Taifa 2025 ni kuona nchi yetu inakuwa Taifa lenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Ili kutimiza dhamira hiyo, tunatekeleza Mipango ya Maendeleo mitatu ya miaka mitano mitano. Pia upo mkakati wa fungamanisho la maendeleo ya viwanda ukiongoza utekelezaji wa mipangi tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa mipango mitatu ya maendeleo ambapo sasa tumefikia nusu,

inaonesha dhahiri kuwa Taifa letu litafikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 likiongozwa na Sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kuna hitaji kubwa la uwekezaji katika viwanda vinavyotegemea malighafi kutoka kwa wananchi, mpaka sasa maendeleo ni mazuri kwa viwanda vinavyozalisha biashara zinazotumika kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa uchumi wa viwanda ni jambo ambalo limeshaanza na kufikia uchumi wa kati mwaka 2025 ni jambo linalowezekana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Muhammed.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu ambayo ni ya kawaida, hayana *details* za kutosha kutoka kwa Serikali na kwamba yako zaidi kimaelezo, kwenye *implementation stage* hayaonekanani kwamba yako hivyo; je, Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba wanashirikisha ipasavyo; yaani wanaitumiaje *PPP* ili kuona kwamba tunafika kwenye huo uchumi wa viwanda ifikapo 2025?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ni kwamba kumekuwa na kero na manyanyaso makubwa sana yanayofanywa na *TRA* kwa wafanyakishwa hususan hawa wenye maduka kwa kuwapa kodi ambazo hazistahiki. Je, Serikali haioni kwa manyanyaso haya itasababisha hayo malengo ya kufika uchumi wa kati na kwenda kwenye viwanda ifikapo 2025 ni ndoto tu kwa Watanzania? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kwamba

hakuna mipango inayoshikika ya kuipeleka Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Ni dhahiri kuwa Serikali inachokifanya ni kuandaa mazingira wezeshi ya kuwafanya wawekezaji ambao kwa kiwango kikubwa sana tunategemea sekta binafsi kuja kuwekeza na kuifanya nchi yetu ifikie katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ambayo yanaweza yakaifanya nchi ikafikia katika uchumi wa viwanda, mojawapo ikiwa ni masuala ya miundombinu ambayo ni dhahiri kwamba Mheshimiwa Mbunge naye ni shahidi, anaona kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali katika eneo hili, lakini pia katika usafirishaji na maeneo mengine ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba tulichokisema hapa kama Serikali, siyo maneno tu, lakini mipango na mikakati ya kuifanya Tanzania kufikia katika nchi ya viwanda, imeelezwa katika majibu yangu ya msingi na ninaomba nisirudie, lakini tu niseme tu kwamba ni dhamira ya Serikali kuifanya nchi yetu iwe nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swalii lake la pili, ameuliza kuhusu manyanyaso wanayopata wafanyabiashara kutokana na kodi inayotozwa na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya mambo ambayo Wizara tumekuwa tukifanya muda wote ni kuhakikisha tunaweza mazingira rahisi ya kufanya biashara katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka utaratibu wa kukutana na wafanyabiashara kila baada ya muda mchache kusikiliza kero zao na yale ambayo wamekuwa wakituwasilishia tumekuwa tuliya fanya kazi. Hivi sasa tuna *blue print document* ambayo imeelezea namna gani Serikali itasaidia kutatua vikwazo ambavyo vinawakabili wafanyabiashara ili kuifanya nchi hii iende katika nchi ya uchumi wa viwanda. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, linalekezwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 166

### **Kujinasua Kutoka Kwenye Hali ya Umaskini – Kigoma**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Katika nchi yetu suala la usawa na haki kwa wananchi wetu ni jambo linalozingatiwa sana na utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano; taarifa ya hali ya umaskini nchini imebainisha kwamba ipo mikoa minne ambayo kiwango cha umaskini kipo juu sana na mojawapo ya mikoa hiyo ni Kigoma.

Je, ni hatua zipi za makusudi (kibajeti) zinazochukuliwa ili Mkao wa Kigoma ujinasue na hali ya umaskini ambayo kwa kiasi cha asilimia 80 umesababishwa na madhila ya kihistoria (*historical injustices*) na Serikali kuacha au kushindwa kujenga miundombinu ya maendeleo kama barabara, vituo vya afya na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 Wizara ya Fedha na Mipango, Idara ya Kuondoa Umaskini kwa kushirikiana na *REPOA* ilifanya uchambuzi wa kina wa hali ya umaskini kwa lengo la kupata takwimu za hali ya umaskini katika ngazi ya Mikoa na Wilaya (*poverty mapping*). Kwa mujibu wa takwimu zilizopatikana, Mkao wa Kigoma ulikuwa na

kiwango kikubwa cha watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini cha asilimia 48.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba siyo kweli kwamba Serikali iliacha au kushindwa kujenga miundombinu ya maendeleo kama barabara, vituo vya afya na kadhalika katika Mkoa wa Kigoma na hivyo kusababisha watu wa Kigoma kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo iliyotekelizwa na Serikali katika Mkoa wa Kigoma ni pamoja na Daraja la Jakaya Kikwete katika Mto Malagarasi, Kivuko cha MV Malagarasi, barabara ya Kidahwe hadi Uvinza, Kigoma – Kidahwe na Mwandiga – Manyovu. Aidha, miradi ya barabara inayoendelea ni pamoja na Kidahwe – Kasulu, Kibondo – Nyakanazi na Kibondo – Mabamba mpaka mpakani mwa Burundi. Miradi mingine ni kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya kitega uchumi ya *NSSFna NHC*, miradi ya umeme vijijiini na uwanja wa ndege Kigoma awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii yote imelenga kufungua fursa za kiuchumi kwa Mkoa wa Kigoma na hivyo kuongeza kasi ya kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/2017 hadi 2020/2021), Serikali imepanga kuendeleza eneo maalum la uwekezaji Kigoma, upanuzi na uboreshaji wa bandari ya Kigoma, ujenzi na upanuzi wa uwanja wa ndege wa Kigoma, ujenzi wa mradi wa kuzalisha megawati 44.7 za umeme wa maji kutoka mto Malagarasi na kuunganishwa na Gridi ya Taifa ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imepanga kujenga reli ya Kisasa na kuimarisha reli ya zamani na kununua vichwa 63 vya treni na mabehewa ya mizigo 1,960 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za usafiri na usafirishaji kwa watu,

bidhaa na huduma ifikapo mwaka 2020. Ni matarajio yetu kuwa kukamilika kwa miradi niliyoitaja kutafungua fursa za kiuchumi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini kwa kiwango kikubwa katika Mkoa wa Kigoma.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ingawa maelezo yenyecheo yanajikanganya sana. Msingi wa swali ni hatua za makusudi za kibajeti, kwa sababu Mkoa wa Kigoma kama ilivyo mikoa mingine unapata bajeti kwa mujibu wa *ceiling*. Sasa nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo barabara anazozizungumza, zimesimama kujengwa. Zimeanza kujengwa tangu mwaka 2006. Barabara hizo hazijengwi tena na Wizara ya Fedha nyie ndiyo mnatoa fedha. Ni lini sasa kwa makusudi mtatoa fedha ili barabara hizi ziweze kukamilika baada ya kukaa kwa miaka 12 hazijakamilika? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni dhahiri kabisa kukamilika kwa majengo ya *NSSF* na *National Housing* hakuwezi kuondoa umaskini wa watu wa Kigoma. Hoja ya msingi ni kwamba tunataka kuwe na *special strategy* ya mikoa hii minne ambayo iko nyuma, ndiyo hoja ya msingi iko hapo. Majengo haya yapo tu! Kwa hiyo, msingi wa hoja yangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri atueleze ni mkakati upi wa kuiondoa mikoa hii minne katika lindi la umasikini kuweka katika mikoa ambayo ni bora zaidi kama ilivyo mikoa mingine? Hiyo ndiyo hoja ya msingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, majibu, karibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeonesha dhahiri

miradi inayotekelizwa ili kuweza kuwaondoa wananchi wa Kigoma kutoka kwenye lindi la umaskini. Huwezi kuwaondoa wananchi katika lindi la umaskini bila kuwa na miundombinu ambayo nimeionesha. Ndiyo msingi wa jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara zilizosimama, Wizara tupo katika majadiliano, tulimaliza uhakiki na sasa tunaelekea kulipa na barabara hizi zitaendelea kujengwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anauliza kuhusu *special strategy*, napenda kuliambia Bunge lako tukufu kwamba *special strategy* ipo na tumeanza kuitekeleza kwa mikoa yote. Kwa Mkao wa Kigoma aliouliza, mfano wa *special strategy* ni upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma ambapo ndege kubwa zilikuwa hazitui na sasa ndege kubwa zinatua, watalii wanafika kwa wakati, wawekezaji wanafika kwa wakati, wafanyabiashara wanafika kwa wakati na tunafungua uchumi wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekamilisha kwa asilimia 100 ujenzi wa magati mawili; Gati la Kagunga limekamilika kwa asilimia 100, Gati la Kibwesa limekamilika kwa asilimia 80. Hii ni kuufanya Mkao wa Kigoma uwe ni *hub* ya biashara kwa *landlocked countries* zinazotutegemea sisi Tanzania ili tuweze kufungua uchumi wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge pamoja na ndugu zangu wote wa Kigoma, Serikali yao ipo makini. Tunaelewa kulikuwa na shida ya *bottleneck inflation* na sasa tunafungua kwa kukamilisha miradi hii, ndio maana reli yetu ya kuwa kiwango cha kisasa tunakwenda kuikamilisha kufungua mikoa yetu hii. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Nassir.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi na mikoa mingine ambayo imekuwa inapokea wakimbizi ni mikoa ambayo iliathirika sana kiuchumi kwa sababu nguvu yao kubwa sana ilipelekeea kubeba mzigo wa wakimbizi kutoka nchi jirani na kupelekeea kuwa na umasikini kwenye maeneo hayo.

Je, Serikali imejipanga vipi kusaidia maeneo ambayo yalitoa nguvu zao kubwa sana kusaidia ndugu zetu wa nchi za jirani na hali ya maisha sasa ya wananchi ambaao walifanya kazi ya kuwapokea ndugu zetu wamekuwa na mazingira ya maisha duni?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Umeeleweka.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Tunaomba Serikali itupe majibu, inatusaidia vipi katika mikoa hiyo?

**MWENYEKITI:** Umeeleweka ahsante sana. Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi nao ni hivyo hivyo. Tumeweke vipaumbele hasa kuhakikisha tunafungua mikoa hii kwa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Mheshimiwa Mbunge ni shahidi kwamba miundombinu inafunguka ili wakulima wetu waweze kusafirisha mazao yao kwa haraka na nguvu zote kama Serikali tunaelekeza kwenye mikoa hii iliyoonyeshwa kwenye utafiti ule kwamba ni ya mwisho katika hali ya umasikini ndani ya Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassir.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Ripoti mbalimbali ikiwemo Ripoti ya MVSna REPOA inaoneesha kwamba hali ya njaa na umasikini nchini imeongezeka kwa mwaka 2018 ukililinganisha na miaka iliyopita. Je, Serikali ina kauli gani juu ya hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu sana kusema kwamba hali ya njaa imeongezeka ndani ya mwaka 2018. Katika bidhaa zinazochangia mfumuko wa bei au *inflation rate* kuongezeka ni upatikanaji wa chakula. *Inflation* kwa mwezi wa Tatu ilikuwa asilimia 3.9. Hii ni *indicator* kwamba hali ya njaa kwa Tanzania haipo na mvua zimenyesha za kutosha, wananchi wetu wako katika amani kabisa ya upatikanaji wa chakula ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge, yawezekana taarifa anazozisoma ni za mwaka 2016/2017 kulikokuwa na shida hiyo, siyo kwa mwaka 2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea kwa sababu ya muda. Swalii la 167 linaulizwa na Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum linaelekezwa kwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Na. 167

### **Hitaji la Mahakama ya Mkoa Simiyu**

**MHE. GIMBI D. MASABA** aliuliza:-

Mkoa wa Simiyu hauna Mahakama ya Mkoa licha ya Mkoa huo kuanzishwa zaidi ya miaka mitano iliyopita.

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya ngazi ya Mkoa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi katika mikoa yote Tanzania Bara. Mkoa wa Simiyu kama ilivyo mikoa mingine unayo Mahakama ya Hakimu Mkazi ambayo kwa sasa inatumia jengo la kupangisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kuwa na jengo la Mahakama kwa kila ngazi kwa kadiri itakavyowezekana. Tayari tunao mpango wa kujenga majengo katika kila ngazi ya Mahakama kwa awamu katika mwaka wa fedha 2017/2018. Simiyu ni moja ya mikoa mitano ambayo ujenzi wake wa Mahakama umeanza ambapo kwa sasa msingi umekamilika na hatua nyingine za ujenzi zinaendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gimbi Masaba, swali.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali kuwa mepesi kabisa, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Machi, 2012 Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Pinda aliutangaza Mkoa wa Simiyu kuwa mkoa mpya, lakini mpaka ninavyoongea hivi ni takriban miaka sita mkoa huu hauna Mahakama ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo linalotumika kuendeshea Mahakama ya Mkoa na Wilaya ya Bariadi ni jengo ambalo ni la Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi ambaye ndio ameipangisha Mahakama.

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, kwa kitendo cha kumpangisha Mwenyekiti wa Halmashauri njambo ambalo linaleta mkanganyiko na hofu kwa wananchi kwamba kwa kuchelewesha kujenga jengo la Mahakama ya Mkoa ni moja ya maslahi kati ya Mwenyekiti wa Halmashauri na Serikali. (*Makof!*)

Je, ni lini Serikali italeta mkakati wa haraka ili kuweza kujenga Mahakama hiyo ya Mkoa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; Mkoa wa Simiyu tuna changamoto ya Mahakimu. Mkoa wa Simiyu una Hakimu mmoja ambaye anahudumia Wilaya sita, lakini pia Hakimu wa Mahakama ya Wilaya anahudumia Wilaya nne; Wilaya ya Busega, Wilaya ya Itilima, Wilaya ya...

**MWENYEKITI:** Uliza swalii tu sasa.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mkakati wa Serikali wa kuharakisha kujenga Mahakama hizi katika Mkoa wa Simiyu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa kifupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swalii la msingi, tayari ujenzi wa Mahakama ya Mkoa katika Mkoa wa Simiyu imeshaanza kujengwa, msingi umeshakamilika na hatua nyingine za ujenzi zinafuata. Kwa sababu tunatumia ujenzi wa aina ya moladi tuna hakika kabisa jengo hilo litakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Mahakama ya Mkoa, pia Mkoa wa Simiyu utajengewa Mahakama Kuu katika mpango huu unaoendelea. Kuhusu idadi ya Mahakimu, ni kweli kumekuwa na upungufu wa Mahakimu siyo tu kwa Mkoa wa Simiyu, bali nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mahakama iko katika utaratibu wa kuajiri Mahakimu zaidi baada ya kuwa imepata ikama kupitia Tume ya Ajira ya Mahakama na hao wakipatikana, miongoni mwa mikoa ambayo itakumbukwa na kupangiwa Mahakimu ni Simiyu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda mnauangalia Waheshimiwa? Nachukua mawili tu; Mheshimiwa Oliver na Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona niulize swali dogo la nyongeza. Swali liliolulizwa namba 167 linafanana kabisa na Wilaya ya Ngara. Wilaya ya Ngara haina jengo la Mahakama, inatumia jengo la DC.

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya Ngara? (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ni lini? Kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara imepangiwa kujengewa Mahakama ya Wilaya katika mwaka wa 2019/2020 na pia Mahakama ya Mwanzo Lulenge mwaka 2019/2020. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Mkundi.

**MHE. JOSEPH MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mahakama ya Mwanzo ya Bukindo, Bukonyo na Ukara zina hali mbaya sana kimiundombinu, achilia mbali upungufu wa watumishi. Nataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuboresha mazingira haya ili haki ya wananchi wa Visiwa vya Ukerewe iweze kupatikana kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wilaya ya Ukerewe, imepangiwa kujengewa Mahakama ya Mwanzo katika eneo la Ilangala katika mwaka wa fedha unaoanza sasa wa 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea swali namba 168, linaulizwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo. Bado linaelekezwa kwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Na. 168

## **Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) Kuongezewa Uwezo**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Chuo cha Mahakama Lushoto (*IJA*) kinatoa taaluma ya Stashahada za Sheria.

(a) Je, ni lini sasa Serikali itaongeza uwezo wa Chuo hicho ili kitoe elimu ya sheria kwa ngazi ya Shahada?

(b) Je, ni kwa nini Serikali sasa isione umuhimu wa kukifanya Chuo hicho kiwe Wakala wa *Law School*/ili mafunzo ya uwakili pia yaweze kutolewa chuoni hapo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya kuwepo kwa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ni kutoa elimu endelevu kwa watumishi wa Mahakama na watumishi wa sekta nyingine za umma wakitokea kazini na siyo kutoa elimu ya sheria kwa ngazi ya shahada. Nia na makusudi hayo inalenga katika kuwaimarisha watumishi hao wanapokuwa kazini kwa kuwapatia mbinu na nyenzo muhimu ambazo ni nadra kupatikana wakati wanapokuwa shulen/vyuoni na hivyo kuwasaidia katika kutekeleza majukumu yao ya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara bado tunaona kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kusimamia lengo la kuanzishwa kwa chuo hicho kwani bado ni la msingi katika kuimarisha kitaaluma watumishi wa Mahakama na sekta nyingine nchini. Hata hivyo, kimeunda kikosi kazi cha kutafiti maeneo mapya ya uanzishwaji wa kozi mpya ikiwemo

mafunzo ya ngazi ya Shahada ya Sheria katika Uongozi wa Mahakama (*Bachelor of Law in Judicial Administration*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, msingi wa kuanzishwa kwa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ni kutoa elimu kwa wanaotokea kazini ili kuwapatia nyenzo muhimu kuweza kutekeleza majukumu yao vema. Mafunzo yatolewayo na Chuo cha Uanasheria kwa vitendo yanalenga kumuandaa mhitimu wa shahada ya kwanza kutekeleza kazi ya Uwakili ya Uanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Chuo cha Lushoto lengo ni kumwongezea mbinu za kutekeleza kazi za kutoa haki yaani Mahakimu na Majaji, mafunzo ambayo yanatolewa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nachukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ili kuangalia namna njema ya kuoanisha mafunzo yanayotolewa na vyuo hivi viwili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa amesema lengo la chuo hiki cha mahakama ni kutoa elimu ambayo inasaidia watumishi walioko makazini waweze kuboresha ufanisi na utendaji wao; je, haoni sasa ni muhimu kwa chuo hiki pia kuanzisha kozi maalum kwa watumishi wengine wa Idara ya Mahakama wakiwemo makarani na wakalimani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali imeanzisha msaada wa huduma ya msaada wa kisheria na kwa kuwa kule Lushoto nako tuna watoa msaada wa kisheria; je, haoni kwamba ni muhimu chuo hiki kikasaidia watoa msaada wa kisheria katika Halmashauri ya Lushoto kuwajengea uwezo ili waende kuwasaidia wananchi huko vijijini? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kuhusu kutoa elimu kwa ngazi ya makarani na watu wa masijala ya mahakama, nakubaliana naye kabisa kwamba wakati umefika na maadam chuo kimeweka kikosi kazi cha kupitia upya mitaala na mafunzo mbalimbali ya kozi mbalimbali katika chuo hicho, nachukua maoni yake na nitawasilisha katika kikosi kazi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kutoa elimu kwa *paralegal* kwa ajili ya msaada wa kisheria pia wazo hilo ni zuri na siyo tu kwa Lushoto, nadhani kwa maeneo yote ya Mikoa ya Kaskazini ambayo yako karibu na Chuo cha Lushoto.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swalii la 169, linaulizwa na Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, linaulizwa kwa Waziri wa Nishati.

Na. 169

**Kupatia Umeme Vijiji na Vitongoji Vilivyorukwa  
na REA I na II**

**MHE. OMARY T. MGUMBA** aliuliza:-

*REA I na II* ilikuwa ni kupeleka miundombinu ya umeme vijiji na baadhi ya Makao Makuu ya vijiji tu na kuacha vitongoji vya vijiji husika.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwapatia umeme vitongoji vyote na vijiji vilivyorukwa katika *REA I na II*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Omary Tebweta

Mgumba, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) inatekeleza mradi wa kupeleka umeme katika vijiji vyote ifikapo mwezi Juni, 2021. Katika kufikia azma hii, Serikali inatekeleza mradi wa REA awamu ya tatu kupitia maeneo ya fua: kwanza, *grid extension* unaohusu kupeleka umeme katika vijiji vyote ambavyo havikufikiwa na miundombinu ya umeme. Mradi huu wa REA III mzunguko wa kwanza umekwishaanza. Mzunguko wa kwanza unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2019 na mzunguko wa pili unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya pili ya mradi wa REA ni mradi wa *densification*. Mradi huu umepangwa kutekelezwa katika vijiji ambavyo tayari vimefikiwa na miundombinu ya umeme lakini baadhi ya taasisi za huduma za kijamii na Vitongoji havikupata umeme wakati wa utekelezaji wa REA I na II.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina ya tatu ni mradi wa kupeleka umeme katika vijiji nje na miundombinu ya umeme wa gridi kwa kutumia nishati jadidifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji na vitongoji vilivyorukwa wakati wa utekelezaji wa miradi ya REA I na II vitapatiwa umeme kupitia miradi ya *densification* na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya miradi ya *densification* ulikwishaanza katika mikoa nane ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Pwani, Tanga, Arusha na Mara. Serikali inafanya maandalizi ya *densification* awamu ya pili unaotarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki jumla ya vitongoji 55 vimeainishwa kwa ajili ya kupatiwa umeme kupitia *densification* awamu inayofuata. Mkakati wa Serikali ni kuvipatia umeme vitongoji vyote ifikapo mwezi Juni, 2021.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake anasema kwamba *REA* Awamu ya Tatu lengo lake kubwa ni kupeleka umeme katika vijiji ambavyo havina miundombinu ya umeme, lakini kosa lile lile liliolofanyika katika *REA* I na II, kuruka Vitongoji na Vijiji tumeliona tena katika *REA* hii ambavyo inatekelezwa. Kwa mfano, sasa hivi kimepewa Kijiji cha Bagilo ambapo vimerukwa Vijiji vya Hewe, Mgozo na Tegetero, lakini pia...

**MWENYEKITI:** Swalii.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kidunda kimepewa, vimerukwa vijiji vya Mkulazi na Chanyumbu; je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vijiji hivyo ambavyo vimerukwa katika *REA* III ili tusirudie kosa lile la *REA* I na II?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mradi huu umeanza. Ni kweli umeanza, lakini mkandarasi huyu ana miezi sita sasa tangu alipokuja kufanya tathmini tu, hajarudi *sitempaka* leo. Baada ya kumfutilia inaonekana kwamba hajapewa *advance* wala *letter of credit* ya kuanza kazi. Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri anasema mradi huu unatakiwa ukamilike Julai, 2019, mpaka leo kazi haijaanza. Je, ni lini Serikali itaweza kutoa *letter of credit* kwa mkandarasi huyu ili aweze kuanza kupata vifaa na vitendea kazi ili aweze kuanza mradi na kutekeleza ndani ya wakati? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lazima nimpongeze Mheshimiwa Mgumba kwa kazi

anayoifanya. Ndani ya kipindi kifupi amkeshauliza zaidi ya maswali manne ya Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza alijielekeza kwenye changamoto zilizojitokeza katika *REA* ya I na *REA* II ya urukwaji wa vijiji. Naomba nikiri kweli changamoto hiyo ilikuwepo, lakini pia naomba niseme kupitia mradi huu wa *REA* Awamu ya Tatu, baada ya kupokea maombi mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, awali mpango ulikuwa ni vijiji 3,559 lakini baada ya kupokea malalamiko ya kurukwa kwa vijiji, vitongoji na taasisi za umma tumefanya tathmini nyingine na upembuzi yakinifu, tumeضا vijiji kama 1,541 ambavyo vinatakiwa viongezeke awamu hii tunapoendelea kutekeleza mzunguko huu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge vijiji alivyovitaja ni mionganoni mwa vijiji 1,541 ambavyo vitaongezeka kwenye vijiji 3,559 na vitakuwa vijiji 5,100 kwa awamu ya kwanza ambavyo vitapelekewa miundombinu ya umeme. Pamoja na kwamba nakiri, lakini gharama zitaongezeka. Pia kwa kuwa kazi ya Bunge hili ni kuidhinisha bajeti kwa miradi hiyo na uhitaji unaonekana ni mkubwa, sina mashaka kwamba Bunge litatimiza wajibu wake na kwamba vijiji ambayo tumeviona lazima viongezeke ili kutimiza lengo ambalo limekusudiwa kwamba tusirudie makosa ya awamu nyingine, litatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, amejiielekeza kwamba ni kweli Mkandarasi wa Mkoa huu wa Morogoro, *State Grid* alifanya tathmini na kwamba hajalipwa *advance*. Nataka niseme wakati wa malipo ya *advance* kulikuwa na masharti na sharti mojawapo lilikuwa malipo lazima wa-*submit performance bond*. Bahati mbaya mkandarasi huyu haku-*submit* kwa wakati, lakini nakiri mpaka sasa hivi Wakandarasi wote wamesha-*submit*, utaratibu wa malipo unaendelea kwenye Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, utaratibu wa ufunguaji wa *letter of credit*, tunashukuru tumepokea barua wiki

iliyopita kwamba sasa tunaweza tukaendelea na utaratibu huo. Kwa hiyo, tunajipanga pamoja na Wakala wa Nishati Vijiji ili kuifanya kazi hiyo kwa haraka na miradi hii itekelezeke kwa haraka. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mtanisamehe sana. Mnafahamu juzi Mheshimiwa Spika, alielekeza, angalieni Wabunge waliosimama humu, kuna tatizo. Mimi nadhani Serikali ifuatilie maelekezo ya Spika. Lipo tatizo, haiwezekani. Angalieni! Eeh, lakini suala la *letter of credit* ndiyo linasemwa na Makandarasi wote, hazijafunguliwa *letters of credit*. Eeeh, ni tatizo! (*Makof*)

Haya, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata 170, linaulizwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, linaelekezwa kwa Waziri ya Maliasili na Utalii.

Na. 170

**Serikali Kuyaondolea Hadhi ya Uhifadhi Baadhi ya Maeneo ya Hifadhi**

**MHE. OSCAR R. MUKASA** aliuliza:-

Serikali inakusudia kuyaondolea hadhi ya uhifadhi baadhi ya maeneo ya hifadhi kwa kuwa yamepoteza sifa hiyo. Kwa mujibu wa kauli ya Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii alipokuwa akihitubia huko Benaco Wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera mnamo tarehe 22 Desemba, 2015.

(a) Je, Serikali imeshaanza kuandaa mpango kupitia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvubi ili kuhakikisha kuwa kuna matumizi yenye tija na usawa baina ya wakulima na wafugaji pindi maeneo hayo yatakapokuwa huru ili kukuza uchumi na kuondoa hatari ya uvunjifu wa amani unaotokana na mgawanyo usio sawia kama ilivyo sasa?

(b) Je, kama Serikali imeshaanza kuandaa mpango huo, ipo tayari kuzishirikisha mapema Halmashauri za Wilaya

zitakazoguswa na jambo hili ili nazo zianze kufanya maandalizi ya suala hili kwa ngazi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharumulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya hifadhi yameanzishwa na kutangazwa kisheria kwa kuzingatia umuhimu wake kiikolojia, kiuchumi, kiusalamu na kijamii kwa maslahi ya Taifa. Aidha, baadhi ya maeneo yanakabiliwa na uvamizi unaotokana na shughuli za kibinadamu kama kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababisha baadhi ya maeneo yaliyohifadhiwa kupoteza sifa ya kuendelea kuhifadhiwa. Kutokana na hali hiyo, Wizara yangu ilifanya tathmini ya maeneo hayo na kubaini jumla ya mapori tengefu 12 yaliipoteza sifa na hivyo kuanzisha mchakato wa kuyarudisha kwa wananchi ili yatumike kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara yangu imepanga kufanya tathmini ya maeneo yaliyopoteza sifa kuititia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (*TAWIRI*). Maeneo yaliyohifadhiwa pamoja na vitalu vya uwindaji wa kitalii yatafanyiwa tathmini ili kubainisha yale yote yaliyopoteza sifa za kuendelea kuwa hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini kukamilika, Serikali itaandaa mpango ambao utahusisha Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Halmashauri za Wilaya ili kuhakikisha kuwa maeneo yatakayoondolewa hadhi ya uhifadhi yanatumika ipasavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru kwa majibu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa ni miaka miwili na miezi minne sasa toka Serikali imetamka hilo ililolitamka kuhusu maeneo yaliyopoteza sifa mpaka leo na bado habari ya tathmini inazungumzwa mpaka leo, naomba Kauli ya Serikali kuhusu dhamira ya kukamilisha kazi hii ili tupeleke maendeleo kwa pamoja utalii, kilimo na mifugo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, asilimia 54 ya eneo la Wilaya ya Biharamulo ni maeneo yaliyohifadhiwa. Naomba kujua kutoka kwa Serikali, miongoni mwa maeneo yanayoonesha dalili za kupoteza sifa, yako yale yaliyozunguka Wilaya ya Biharamulo? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu Mheshimiwa NaibU Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Oscar kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika kuwatetea wananchi wa Jimbo lake, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kweli tathmini ilishakamilika katika hayo mapori tengefu 12 na tulishamaliza kazi. Kazi iliyobaki sasa ni kuhaulisha. Tararatibu za kisheria za kufuta yale maeneo lazima zizingatiwe. Kwa hiyo, huo ndio mchakato ambao bado unaendelea kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kuhusu maeneo ambayo yanahusika katika Jimbo la Biharamulo; kwanza, kuna *Masasi River*, Biharamulo ambalo lina ukubwa wa kilometra 180 lipo kwenye orodha ya hayo mapori tengefu ambayo tunayaangalia. Lakini pia, kuna eneo lingine, Inchwakima nalo ni eneo ambalo bado tunaliangalia katika lile Jimbo la Biharamulo. Kwa hiyo, maeneo haya mawaili ndio yale ambayo yako katika mapori ya akiba ambayo

tunayafanya kazi, ili yaweze kurudishwa kwa wananchi pale ambapo utaratibu utakamilika.

Kwa hiyo, baada ya hapo naamini Mheshimiwa Mbunge utafurahi na wananchi wako watayatumia maeneo hayo vizuri na ipasavyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya Maliasili na utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Prof. Norman Sigalla King, Mbunge wa Makete.

Na. 171

### **Ujenzi wa Barabara ya Lami Toka Chimala – Makete**

**MHE. PROF. NORMAN S. KING** aliuliza:-

Hifadhi ya Kitulo iliyoko Mkoa wa Njombe, Wilaya ya Makete ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na ni hifadhi ya kipekee katika Afrika kwa sababu ina aina tofauti ya maua zaidi ya 120.

Je, ni lini *TANAPA* kwa kushirikiana na *TANROADS* itaona umuhimu wa kujenga kwa lami barabara ya kutoka Chimala – Matamba – Kitulo – Makete ili kurahisisha uingiaji wa watalii kwenye mbuga hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla King, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, kujenga barabara ya Chimala – Matamba – Kitulo kwa kiwango cha lami ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na hasa jamii zitakazotumia barabara hiyo ikiwa ni pamoja na hifadhi ya Kitulo. Napenda kuchukua fursa hii kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa hivi sasa Wizara yangu ina mchakato wa kuboresha

miundombinu ya barabara, utalii na utawala kwenye hifadhi zetu, mojawapo ikiwa ni Hifadhi ya Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la ujenzi wa barabara zilizo nje ya hifadhi ni jukumu la Halmashauri za maeneo husika ikishirikiana na *TANROADS*. Kutokana na hali halisi ya mapato ya Shirika la Hifadhi ya Taifa, Hifadhi ya Taifa haina uwezo wa kuchangia ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ili barabara hiyo iwekwe kwenye mpango wa ujenzi wa lami. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla.

**MHE. PROF. NORMAN S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kidogo kwa sababu, kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 51 iko bayana, barabara hii imetajwa kwamba ni muhimnu iwekwe kiwango cha lami. Ni lini Serikali itapeleka nguvu kuhakikisha kwamba hili linatekelezwa ili kuboresha miundombinu hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mwaka 2017 Serikali ilikuwa imeahidi kupeleka wanyama kwenye hifadhi hii ili kuongeza vivutio kwenye Hifadhi ya Kitulo. Ni lini mpango wa kupeleka wanyama wasio wakali, ukiacha simba, kwenye hifadhi hii utakamilika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Hasunga, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu maswali hayo naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya, lakini pia nimpongeze kwa jitihada kwamba sasa hivi anaenda kuoa na amesambaza kadi. Kwa

hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wamchangie ili akamilike, aendelee kufanya kazi vizuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa hii barabara iko katika llani ya Chama cha Mapinduzi kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge tu kwamba hivi sasa barabara ambayo inawekwa lami ni ile ambayo inatoka Njombe hadi Makete, inawekwa lami sasa hivi na bado kuna barabara nyingine ya kutoka Isonje – Makete mpaka Mbeya, nayo iko kwenye *feasibility study*. Hii barabara ya tatu itakuja kuunganishwa na hizi barabara nyingine mibili ambazo nimezisema na ninaamini kabisa hali itakuwa ni nzuri na Mheshimiwa Mbunge utafurahia baada ya hilo suala kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kuhusu ni lini wanyama wale ambaao tuliahidi kwamba tutawapeleka katika Hifadhi yetu ya Kitulo, Serikali ina mpango wa kupeleka wanyama 25. Ili kuhamisha wanyama kutoka hifadhi moja kwenda hifadhi nyingine kuna taratibu za kisheria ambazo ni lazima zikamilike. Hivi sasa zimeshakamilika na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii amesharidhia wanyama 25 wahamishiwe katika Hifadhi yetu ya Kitulo kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge naamini baada ya muda mafupi utawaona hao wanyama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu wa maswali tumepitiliza kidogo, lakini tumemaliza maswali.

Naendelea kuomba majibu yanaanza tena kurudi kuwa marefu. Baadhi ya majibu mliyoyasikia, yapo matatu yalikuwa marefu sana. Naomba upande wa Serikali tuzingatieve kuwa na majibu mafupi kwa sababu ya muda wetu.

Matangazo ya wageni wetu; wageni waliopo Bungeni asubuhi hii; tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni nane wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Mbunge na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaao ni viongozi wa Chama cha Walimu Nchini (CWT), wakiongozwa na Mwalimu Luya Ngonyani. Wako wapi?

Karibuni sana. Halafu na Umoja wa Serikali ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TAHLISO*), wakiongozwa na Ndugu George Munari, Rais wa *TAHLISO*. Wako wapi? Karibuni. (*Makofi*)

Wageni 28 wa Mheshimiwa *Engineer Atashasta* Nditiye, Mbunge na Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mipango kilichopo Mkoani Dodoma. Wanafunzi, mko wapi? Karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Hamida Abdallah, Mbunge, ambaye ni mume wake Ndugu Kitesh Chagani. Karibu sana ndugu yetu. Wananchi wa Lindi na wewe nadhani ulimsikia mwenza wako akichangia vizuri sana Bungeni siku ya Jumanne. (*Makofi*)

Tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Mbunge, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira wanaotoka Chama cha Wanafunzi wa Kiswahili wa Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (*CHAWAKAMA*) Kanda ya Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Masau Bwire. Karibuni sana wanafunzi. (*Makofi*)

Tunao wageni 88 wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Waislamu kilichopo Morogoro wakiongozwa na Ndugu Omary Bakari. Wako wapi wanafunzi? Karibuni. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge, ambaye ni Mheshimiwa Anthony Genda, Diwani wa Mbulu Mjini. Karibu sana Mheshimiwa Diwani. (*Makofi*)

Wageni nane wa Mheshimiwa Hamad Maalim, Mbunge, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Jimbo la Kojani, Kaskazini Pemba. Karibuni sana, Kojani Pemba huko, eeh. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo nilionayo kwa sasa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mwongozo wa Spika. Mussa Sima.

**MWENYEKITI:** Katibu. Kuna mtu, Mheshimiwa mmoja amewasha huko.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Elimu,  
Sayansi na Teknolojia**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tujifunze tu Kanuni. Nikimaliza matangazo, kinachofuata lazima nimwite Katibu ili sasa *process* ya kazi ya leo iwe imekaa kwenye mstari, hatuwezi kuanza na miongozo. (*Makofi*)

Naanza na Mheshimiwa Lubeleje halafu Mheshimiwa Mapunda.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja. Nawachukua tu, nachukua tu majina. Nani kule?

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mussa Sima.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Anatropia Theonest.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Cecil Mwambe.

**MWENYEKITI:** Nimekuchukua Mheshimiwa Mwambe. Anayefuata?

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Sabreena Sungura.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Anatropia Theonest.

**MWENYEKITI:** Nani?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Anatropia Theonest.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Sabreena Sungura.

**MWENYEKITI:** Haya, tunaanza. Mheshimiwa Mapunda.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kutoa Mwongozo. Leo katika kipindi cha Maswali na Majibu, swali namba 166 liliolulizwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko na majibu ya Serikali katika ujumla wake yalijikita kwenye kuondoa umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuondoa umaskini wa kipato kuna uhusiano wa moja kwa moja na ongezeko la mishahara ya watumishi wa Serikali wa kada zote; na kwa kuwa jana siku ya Mei Mosi Mheshimiwa Rais aliji-*commit* kuwa ongezeko la mshahara pamoja na mambo mengine litazingatia hali halisi ya uchumi, uwezo wa Serikali kulipa na mahitaji halisi ya Serikali; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameshaji-*commit* kuwa kutakuwa na ongezeko la mishahara litakalozingatia mahitaji hayo ya msingi; Serikali inatoa kauli gani kuhusu lini hiyo mishahara itapanda kwa sababu hili suala jana ni kama liko hewani limeacha sitofahamu nyingi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nilikuwa nina hoja kidogo hapa kwa swali namba 162.

Kwa kuwa Sera ya Wizara ya Afya ni kuchukua hospitali zote za Mikoa kurudi Wizarani, sasa hoja yangu ni hivi; kwa kuwa Hospitali ya Mkao wa Dodoma iko Makao Makuu ya Dodoma na inahitaji maboresho makubwa sana; kuna upungufu wa watumishi na madawa, sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya atatoa kauli gani ya kuhusu Hospitali ya Dodoma kwa sababu hapa ni Makao Makuu ya nchi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mwongozo wangu pia unajikita katika kanuni namba 68(7), na mimi niliangalia swali namba 166 la Mzee wangu Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko wakati Naibu Waziri wa Fedha na Mipango akitoa majibu. Miongoni mwa hatua za kuondoa umaskini Tanzania, hakuweza kuonesha hatua mojawapo ya nyongeza ya mishahara kwa watumishi.

Sasa na mimi nichukue fursa hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa kwenye Mei Mosi, lakini ni vizuri kama Bunge tukahitaji *commitment* ya Serikali kwa ajili ya watumishi, ni lini sasa Serikali itahakikisha watumishi hawa wanapandishwa mishahara kama hatua mojawapo ya kuondoa umaskini? Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nasimama kwa kanuni ya 68(7) sitaisoma. Mwongozo wangu ni kutoka kwenye Kipindi cha Maswali na Majibu hasa swali alilouliza Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, swali namba 167 kuhusu Mahakama na majibu ya Serikali. Serikali imeonesha dhamira ya kuendelea kusaidia mikoa ambayo bado iko nyuma ikiwa ni pamoja na majengo ya Mahakama na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua maendeleo yanayoletwa kwenye hiyo mikoa mipya yanategemea kwa kiwango kikubwa kodi za wananchi katika mikoa yote. Ni hivi

karibuni wakati Mheshimiwa Rais akizindua barabara, ametoa kauli kwamba maendeleo yatasitishwa katika Kanda ya Kaskazini. Kauli hii imezua tataruki, imeleta wasiwasi kwa sababu watu wameichukulia kama sura ya kibaguzi, kama sura ya kutenga na huku wakijua na wananchi wa Kaskazini wanaendelea kulipa kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba uiombe Serikali ije na ufanuzi juu ya kauli hiyo inayoonesha kwamba inaweza ikawabagua watu na *actually* imeleta tataruki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo juu ya hilo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nachuma.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mapema leo kumeletwa Orodha ya Shughuli ambazo zitaendelea ndani ya Bunge hili na nikipitia hii karatasi kuna hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia; ni hoja ambayo inatarajiwa kuendelea leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Kumi kila mchangiaji wa ndani ya Bunge, hoja ambazo ziko ndani ya Bunge alikuwa anapewa dakika 15 za kuchangia, lakini tulipoingia kwenye Bunge hili la Kumi na Moja, dakika za kuchangia zimekuwa ni 10. Nitoe masikitiko yangu makubwa kabisa, hoja inayoendelea ndani ya Bunge siku mbili zilizopita Wabunge tuliweza kupewa dakika chache sana za kuchangia hali ya kuwa lengo la Bunge hili ni kwamba kila Mbunge aweze kushiriki sawa sawa na kuwasilisha hoja za wananchi wake katika Jimbo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachoendelea ndani ya Bunge, kumekuwa na *scramble* kubwa sana ya dakika za kuchangia hali ambayo inarudisha nyuma lengo la Wabunge sisi kuwepo ndani ya Bunge kwamba tuko hapa kwa ajili ya kuzungumza, kufanya *debating* kufanya *scrutinizing* ndani ya Bunge kwa lengo la kuwasilisha matatizo ya wananchi lakini

kumekuwa na changamoto kubwa sana juu ya dakika za kuchangia zinakuwa ni chache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwongozo wako kwamba dakika hizi tunazopewa chache ambazo tunashindwa kuzungumza hoja za wananchi ambazo wametutuma tuje kuwasilisha ndani ya Bunge, mwongozo wako ni upi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sabreena.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami nilikuwa naomba mwongozo wako, wananchi wanaotokea Mkoa wa Kigoma hususan Kigoma Mjini, Kasulu, Uvinza, Nguruka na maeneo ya Usinge wamekuwa wanapata shida kubwa sana ya adha ya usafiri kutokana na mvua zinazoendelea. Maeneo ya Usinge kuna kipande takribani kilometra moja hakipitiki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea pale ni magari yanayotoka Kigoma yanakuja yanafika njiani yanasimama, yanaanza mpango wa kufaulisha wananchi, wananchi wanatembea kwenye maji na watoto na mizigo, wengine wakibebwa na baiskeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maji kuna vyupa, mawe na hatari ya kuwa na nyoka, wanatembea umbali wa takribani kilometra moja kwenda kufuata magari ambayo yamekuja na abiria kutoka Dar es Salaam, Dodoma na mikoa mingine ya Morogoro na kadhalika ili waweze kufaulishwa na wale pia wanafanya kitu hicho hicho kutembea kwenye maji hayo mpaka kufika upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kauli ya Mheshimiwa Waziri kuhusu mpango wa dharura juu ya jambo hili linaloendelea na limekuwa ni adha kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) lakini nisome pamoja na Kanuni 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa karibuni baada ya Serikali kuamua kubadilisha *SH-Code* na namna ya kutoza kodi kwenye mafuta ya kawaida na mafuta ghafi, kumetokea mkanganyiko mkubwa sana kati ya *TBS*, *TRA* pamoja *TFDA*. Hawa ndio watu ambao mwanzoni kabisa wanataka wafanye ukaguzi wa mafuta kabla ya kumshauri *TRA* kiasi gani kinatakiwa kilipie na hayo mafuta yaliyoko kwenye hizo meli zinazobeba shehena zinaangukia kwenye *SH-Code* ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna uhaba mkubwa sana Tanzania, mafuta ambayo yalikuwa yanauzwa shilingi 48,000 yamepandishwa bei mpaka shilingi 67,000 kwa sababu kuna meli zimekwama bandarini Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba Mwongozo wako, kwa nini usiitake Kamati ya Viwanda na Biashara kukutana na wadau hawa au pamoja na Bunge lako lijadili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Hamuwezi kuhamasishana. Nimeshawajua waliosimama, nimeshawahesabu hawakufikia idadi inayotakiwa.

**MBUNGE FULANI:** Tupo!

**MWENYEKITI:** Hamna.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana. Nimeombwa Mwongozo na Waheshimiwa hawa saba. Nianze na hili la mwisho la Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Hukuwa na haja ya kutumia 68(7). Kama unataka Kanuni ya 47 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 48 unaenda *straight* tu, haikuzuili. Hata kama shughuli za Bunge zingekuwa zimeanza, kama unadhani ni suala la dharura unaweza ukasimama, lakini kwa Mwongozo wangu kwa suala hilo, wewe mwenyewe umeanza vizuri sana, umesema hapa karibuni. Ni maneno yako. Hapa karibuni kumekuwa na" hiyo ulioendelea kuisema.

Sasa kwa kuwa ultaka hiyo kuja kwenye dharura na hukujenga hoja yako kwa sura hiyo na ndiyo maana nilisema hata niliowaona waliosimama walikuwa watatu tu wakaongezeka wakahamasishana wakawa sita, akasimama mwingine wakawa saba, hawajatimia 10; kwa hiyo, inaishia hapo. Nadhani ujumbe huo Serikali imo ndani na ndiyo maana haya mambo mengine mnayasema Waheshimiwa Wabunge lakini mna lengo fulani. Nadhani watayachukua tu vizuri.

Mheshimiwa Sabreena, niseme tu kwamba siwezi kutoa mwongozo kwa suala ambalo halijatokea mapema humu Bungeni, lakini ni tatizo. Mimi naiachia Serikali wataona kama wana haja ya kuja kueleza upande wa Magharibi hali hiyo, lakini kuelekea Mpanda nafahamu shida na ndugu zangu kule wamekwama huko, lakini naamini na maeneo mengine. Sasa haya Serikali inaweza ikafanya majumuisho ya pamoja kuona namna gani katika maeneo ambayo barabara zimekatika, kuweza kurejesha *pass ability* yaani maeneo hayo yaweze kupitika. Hata hivyo ni suala ambalo halikutokea mapema leo.

Mheshimiwa Nachuma, umetumia tu kisingizio cha *Order Paper* lakini *Order Paper* hiyo ukiisoma haituambii mambo ya kuchangia dakika tano au kumi. Nadhani hoja yako ni kwamba muda wa kuchangia Wabunge humu dakika 10 bado mnafikiri ni kidogo. Dakika tano ni kidogo; dakika 15 kama Kanuni zinavyosema.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wangu kwa hili, ratiba yetu hii huwa inapangwa na Kamati ya Uongozi.

Wizara hizi zichukue siku ngapi, unaangalia hiyo. Kwa hiyo, ikishawekwa hiyo, kama leo ni Wizara ya Elimu, lazima tumalize leo. Tunajipanga vipi kuchangia, inategemea wengi wa Wabunge walioomba kuchangia.

Sasa kwa uwiano wetu lazima tuseme uwazi hapa. Walioletwa na wananchi wa Tanzania walio wengi ni Chama cha Mapinduzi, ndio walio wengi. Wanafuatiwa na Chama cha CHADEMA, wanafuatiwa na Chama cha CUF. Kwa uwiano wetu unacheza kwa kutegemea na waombaji. Zaidi utapata Wabunge 17 upande wa CCM; Wabunge watano au wanne; kama leo ni Waheshimiwa Wabunge wanne tu upande wa CHADEMA; Wabunge 15 upande wa CCM; na wawili upande wa CUF. (*Makofii*)

Kuna Wawakilishi wengine wawili humu kutoka vyama viwilli kwa *formula* hii ukiifuata *strictly* hawawezi kuchangia humu. Chama cha *ACT* na ndugu yangu Mheshimiwa Mbatia, lakini kwa busara ya Kiti, maana ni Wabunge hawa, huwa tunawapa nafasi waweweze kuchangia.

Sasa naamini Mheshimiwa Nachuma Mwongozo wangu tubakie tu kwenye reli yetu hii ya kanuni, tuzitumie vizuri, ninyi wenyewe mnajua namna ya kujipanga kwenye kambi zenu. Kama mnataka dakika 10 hizo, tumia dakika 10 hizo. Kama mko wengi, gawaneni kama mnavyokubaliwa na kanuni, mnagawana na juzi mmefanya vizuri sana. Niliwamaliza wote siku ya Jumatatu; kuwamaliza kwa maana ya kuchangia wote. Mwongozo wangu ni huo, tubaki kwenye utaratibu ambaeo tuiwekeea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Anatriopia, majibu ya Serikali, nilivyomzikiliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria anasema, mpango mkakati ambaeo wanao ni kwa mikoa mipyä *sensibly*, eeh! Haya ni maeneo mapya ya utawala, lazima yaendane na miundombinu yote inayotakikana kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Hiyo haimaanishi kwamba eti inabagua. Sasa hayo mengine uliyoyasema maana sikuyasikia leo asubuhi hapa. Wewe kama unataka ujibiwe vizuri na Serikali nakuomba kabisa, maana suala hilo

halikuwa la kwako, lilikuwa la Mheshimiwa Dotto Gimbi Masaba. Ila kama unataka uje ujibiwe vizuri zaidi, rejea/omba wewe mwenyewe swali lako ili tuone mantiki itakuwa ni nini? Huo ndiyo Mwongozo wangu kwa hicho ulichokisema.

Kwa Mheshimiwa Sima, hapana nianze na Mheshimiwa Mapunda niunganishe na Mheshimiwa Sima. *Technically* ni hivyo hivyo, swali hilo la Mheshimiwa Nsanzugwanko limeulizwa vizuri likajibowi na Serikali vizuri tu. Nimempatia Mheshimiwa Kakoso wa Rukwa nikaangalia Muungano, tumesikia, lakini najua na wengine wangelienda kuuliza maswali kwenye eneo hilo. *Technically* kikanuni kwa Mwongozo; kikanuni nasema, mwenye swali hakusimama na kusema hajaridhishwa na majibu ya Serikali. Kauliza maswali yake, wale wengine, hao ambao tunataka ufanuzi zaidi, lazima twende kwenye msingi wa kanuni zetu, wewe hukatazwi kuja kuuliza swali la kwako *specific* kwa kuulizia hilo.

Hata hivyo kwa vile ni swali ambalo linahusu maslahi ya wafanyakazi wa Tanzania nadhani ndillo lilikuwa limelengwa na Mheshimiwa Sima, Mheshimiwa Sixtus Mapunda, wawili hawa, mimi nadhani Serikali mnaweza mkapata nafasi nzuri mkalielezea na kuwapa matumaini wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, lakini jana nimemsikiliza sana Mheshimiwa Rais; na alisema na mnapokuwa na kiongozi msema kweli, eeh ndiyo hiyo, amelisema vizuri sana. Kwa sasa Serikali yake haiwezi ikaongeza mshahara, lakini hali itakaporuhusu na amesema atakapoongeza mshahara haitakuwa hii ya shilingi 10,000, ataiongeza kikweli kweli. Eeh, amesema hivyo.

Sasa ni lini, hayo ni maswali sasa unaiachia Serikali. Hali ya uchumi itakaporuhusu. Tufanye haya makubwa yatakayowezesha kukuza uchumi wetu kwa haraka. Siri ya maendeleo ni hiyo tu. Tufanye kazi kwa bidii tukuze uchumi. Nadhani Serikali kwa wakati muafaka wanaweza kulitolea maelezo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Lubeleje nimekuelewa lakini na wewe nakushauri kwa Kanuni hizi hizi uweze kuiliza swali *specific* kwa nini Serikali inachukua hospitali hizi za Manispaa kwa upande wa kwako badala ya kuchukua hizi za Mkoa. Mimi nadhani hili ukiliuliza vizuri mwongozo wangu ni kwamba nakuomba tu ujiandae kuliulizia swali zuri lakini Serikali imekusikia. Huo ndiyo mwongozo wangu kwa maeneo yote saba ambayo nimeombwa.

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWNEYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji. Wachangiaji wetu nimesema uwiano wetu ni huo tunao kwa leo siku nzima tunao hao tukibahatika Wabunge 21 hivi au 22 tutabana tuone, lakini nitaanza na Mheshimiwa Catherine Ruge, atafuatiwa na Mheshimiwa Othman Omar kwa dakika tano.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza ninapenda kutoa pole kwa Mwenyekiti wangu wa Kanda na Mbunge wa Tarime Vijijini Mheshimiwa John Heche kwa msiba wa mdogo wake ambaye alifariki kwa kuchomwa kisu mikononi mwa polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba niende moja kwa moja kwenye hoja zangu. Mheshimiwa Waziri Profesa Ndlichako nimesoma hotuba yako na nimegundua mapungufu makubwa matatu. Pungufu la kwanza bajeti hii haina jicho la kijinsia (*it is not a gender responsible budget*). Nasikitika kwamba wewe ni mwanamke ni Mama lakini umeshindwa kuliona hili. Umeonesha takwimu mbalimbali mfano udahili wa wanachuo, wanafunzi

waliopata mikopo elimu ya juu, kwamba unaenda kujenga mabweni, kuboresha miundombinu lakini huonyeshi *beneficiaries* (wanufaika) kwa kuangalia jinsia. Tunataka kuona rasilimali za nchi hii zikitumiwa sawa na zikiwafaidisha sawa watu wote bila kujali jinsia kwa maana ya jinsia ya wanawake na wanaume lakini huoneshi, kwa hiyo tunashindwa kujua *beneficiaries* wanawake ni wangapi na wanaume ni wangapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pungufu la pili bajeti yako haina *consistency* kwa maana kwenye takwimu ambazo unacionesha ukurasa huu unaweka asilimia, kurasa nyininge hauweki asilimia, pale ambapo Serikali imefanya vibaya kwa maana ya Wizara hujaonesha kabisa takwimu. Uki-*compare* na hotuba ya Kamati wamefanya vizuri kuliko bajeti ya Wizara, wakati Wizara ina Wataalam. Wameweza kuonesha asillmia kwenye takwimu zao zote mpaka wametuwekea *bar chart* na tunaweza kuona ulinganifu wa *performance indicators* tofauti tofauti. Mpaka natia shaka inawezekana Waziri hii hotuba umekuja kukutana nayo hapa Bungeni kama Wabunge na hukuipitia. Siamini kama kwa umakini wako *Madam Professor* uliweza kuipitia na ukaliacha hili likaja hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pungufu la tatu bajeti hii haina *continuity* kwa maana ya muendelezo. Bajeti ya mwaka 2017/2018 na 2019 vitu ulivyoviandika 2017/2018 ambavyo unaona kabisa vinatakiwa kwenye bajeti hii vionekane vinaendelea havina mwendelezo.

Naomba nikupe mfano, ukienda ukurasa wa 10 wa kitabu chako unaelezea kuainisha mahitaji ya nchi katika ujuzi na kuendeleza na ukataja huo mradi ambaao unaitwa *Education Skills for Productive Job* na ukataja maeneo ambayo unaenda kuendeleza stadi za kazi na ujuzi ukasema kilimo, TEHAMA, nishati, ujenzi, uchukuzi na utalii, lakini *Madam Professor* hakuna *statistic*, where the *statistic Madam?* Ukienda ukurasa wa 76 umeenda kuelezea jambo hilo kwamba kuainisha mahitaji ya nchi katika ujuzi na kuendeleza, lakini vile vipaumbele...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ruge samahani kidogo, wasiliana na Kiti. Unachangia vizuri tu lakini usimu-*address* Waziri ni-*address* mimi. Ahsante.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija ukurasa wa 76, 77 kuainisha mahitaji ya nchi katika ujuzi na kuendeleza huku ametaja maeneo ambayo anaenda kuendeleza kwa maana ya elimu, TEHAMA, nishati na kadhalika, lakini huku hicho kitu hakijatajwa kabisa na hamna takwimu. Kwa hiyo, ina maana hii programu imeisha au? Sielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ningependa kuzungumzia ni usajili wa watoto wa kike vyuo vikuu. Uksoma ukurasa wa 35 wa hotuba ya Kamati imeonesha idadi ya watoto wa kike wanaosajiliwa vyuo vikuu ni ndogo sana na wametoa takwimu hapa kwa mfano, Chuo Kikuu cha Mbeya mwaka wa masomo 2017/2018 jumla ya wanafunzi ambao wanafanya Shahada ya Kwanza ni 1,759 lakini kati ya hao ni wanafunzi 344 tu ambao ni wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunasema tunajenga uchumi wa viwanda na kama tunajenga uchumi wa viwanda haiwezekani, huwezi kumuacha mwanamke lazima mwanamke *ata-contribute* kwenye uchumi wa viwanda kwa maana ya nguvu kazi kwa kuajiriwa au kwa kujiajiri. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri wakati unakuja ku-*wind up* utuambie mkakati mahsus wa Serikali wa kuhakikisha tunaongeza namba ya watoto wa kike wanaosoma masomo ya sayansi kuanzia shule za Awali mpaka vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ningependa kuchangia kuhusu ubora wa elimu nchini, bado unazidi kuporomoka kwa miaka Sita mfululizo bado Serikali inazidi kufanya vibaya kwa maana ya shule za Serikali uki-*compare* na shule binafsi. Ukiangalia ukurasa kuanzia wa 21, 22, 23 wa kitabu cha Kamati wameonesha *indicators* tofauti za

ubora wa elimu. Kwa mfano, asilimia 37.8 ya Walimu ndiyo wana hamasa. Mwalimu mmoja anafundisha wanafunzi 159 upungufu wa walimu bado uko juu, lakini ukiangalia matokeo ya mwaka 2016 katika ukurasa wa 23 wa kitabu cha kamati inaonekana asilimia 73.3 walipata *division four* na *division zero*. Napata shaka kwamba miaka 10/20 ijayo tutakosa nguvu kazi, tutakosa watu ambao wanaenda kuajiriwa kwenye hiyo Tanzania ya viwanda kwa maana ya viwanda. Nasikitika pia kwamba tunaweza tukakosa maprofesa, madaktari kama tutaenda kwa mtindo huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwanafalsafa mmoja anasema *if any organization want to be successful it must invest in people*. Kwa hiyo, kama tunataka kuboresha elimu yetu ni lazima tu-invest kwa walimu, *whether* tunataka hatutaki ni lazima tu-invest kwa walimu kwa maana ya kuboresha maslahi yao, kwa maana ya kuongeza namba ya walimu wanaofundisha watoto tufuate ile *ratio* ya moja kwa 25, kwa maana ya kulipa malimbikizo ya madeni yao, kuwapandisha madaraja kwa wakati na maslahi mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Mwanafalsafa anasema kama unataka kupata matokeo tofauti lazima ufanye kitu tofauti. Tumeona miaka sita iliyopita bado ni *business as usual* lazima kama Serikali tu-take *initiative* ya kufanya vitu tofauti kabisa ili tuweze kupata matokeo bora na kukuza elimu ya watoto wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuiomba Serikali kujenga shule ya watoto wa mahitaji maalum Mkoa wa Mara kwa sababu mkoa ule hauna shule ya watoto wa mahitaji maalum na wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kwenda kutafuta elimu. Kwa hiyo, hii inawanyima haki yao ya msingi ya kupata elimu, naomba uliangalie hilo na Mkoa wa Mara tunaomba shule ya watoto wenye mahitaji maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nipende

kuzungumzia jinsi mvua ambavyo imeharibu miundombinu mbalimbali ya shule katika nchi hii. Mvua zilizokuja ziliikuwa kubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Othman Omar.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuchangia katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpe angalizo kwanza Mheshimiwa Waziri kwamba nchi yetu kitakwimu inakuwa na idadi kubwa ya watu. Idadi hii inakwenda kuathiri kwa njia moja au nyingine katika sekta yetu ya Wizara ya Elimu, sasa sijui Mheshimiwa Waziri ameliona hili na ikiwa ameliona amejipanga namna gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nchi yetu imetangaza kwamba inakwenda kuwa Taifa la viwanda. Taifa la viwanda linahitaji rasilimali watu wenye ujuzi ambao wataweza kuzalisha kwa ufanisi na wenye tija. Kama ulivyozungumza katika hotuba yako *page namba 42* kwamba vyuo vikuu ni nguzo moja muhimu sana katika kuhakikisha kwamba Serikali inakwenda kutekeleza malengo yake muhimu yaliyojipangia kwa kuzalisha rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vikuu kuna changamoto zake, nafikiri unafahamu Mheshimiwa Waziri kwamba vyuo vikuu kuna changamoto za wanafunzi wanaosoma elimu ya juu. Moja ya changamoto hizo Mheshimiwa Waziri ni kwamba wanafunzi wanaosoma masomo ya Uzamili, baadhi ya masomo wanachukua si chini ya miaka minne. Mafunzo hayo Mheshimiwa Waziri ikiwa utakwenda kusoma nchi za nje yanachukua si chini ya miaka miwili. Tatizo hili Mheshimiwa Waziri inakuwaje hapa nchini wanafunzi wetu wasome zaidi ya miaka minne ambapo nchi

za wenzetu wanakuwa ni chini ya miaka miwili, nini kimeongezeka hapa kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika mafunzo ya Uzamivu utakwenda kusoma ikiwa hujaoa utaoa, ikiwa hujazaatutazaa, utapata wajukuu na ustaota mvi bado *degree* hujahitim, nini tatizo? Matatizo haya Mheshimiwa Waziri yanakwenda kusababisha uhaba wa Wahadhiri katika vyuo vyetu. Napenda Mheshimiwa Waziri hili ulione kwamba tatizo la kuaweka wanafunzi muda mrefu katika masomo yao linakwenda kusababisha kuwa na uhaba wa Wahadhiri ndani ya vyuo. Tatizo ambalo halitakwenda sambamba na ongezeko la watu na ndiyo ukaona kuna idara nyine pale vyuo vikuu wanachukua chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano mmoja, Idara ya Fizikla pale Chuo Kikuu ambayo katika vyuo vyote vinavyotoa *Masters* hapa nchini ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam peke yake, lakini wanafunzi wanaoingia kwa mwaka hawavuki wanafunzi 11. Wanafunzi 11 kweli Mheshimiwa Waziri wanatosheleza nchi nzima kwa mwaka? Hao miaka minne hujahitim pale. Hii ni kwa sababu Wahadhiri wetu hawataki kurithiwa, hawataki wasaidiwe pale Chuo Kikuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mhadhiri anabakia pale hawesi kutoka mpaka apelekwe kaburini pale. Namuomba Mheshimiwa Waziri suala hili la kuwatesa wanafunzi wa vyuo vikuu linawarudisha nyuma, ukitilia maanani kwamba wanafunzi wengi wanaosoma vyuo vyetu nya ndani ni watoto wa kimaskini. Hili linapelekea wengi wao warudi nyuma wasipende kusoma katika vyuo vyetu nya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Wahadhiri wetu wa vyuo vikuu walione hili na waone kwamba wao wapo pale ili kulisukuma Taifa hili na Taifa linawategemea wao ili lisonge mbele. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Wabunge kabla hatujaendelea nitoe

tangazo lingine. Tuna wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni wanafunzi 10 wa Chuo cha Theolojia Mpwapwa wakiongozwa na Ndugu Godfrey Nyamwaji, karibuni sana endeleeni na mafunzo muhimu hayo ya theolojia, tunawatachia kila la heri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed atafuatiwa na Mheshimiwa Mbatia ajiandae.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia mada iliypopo hewani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhaba wa muda nitaenda moja kwa moja na ajenda yangu. Awali ya yote nitapenda kuzungumzia ufaulu mbaya kabisa wa wanafunzi wa *form four*. Mwenzangu ameenda Chuo Kikuu moja kwa moja huko kwenye *masters*, mimi nitakuja hapa kwenye vijana wetu hawa wa *form four*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukijigamba sana Watanzania kwamba tunafanya vizuri sijui tuko vizuri, tumepata sijui wanafunzi hamna, sana sana tuko *below 30 percent*ya wanafunzi wote wanaofanya mitihani. Kwa wakati huu na kwa ukubwa wa nchi hii na kwa wataalam tulionao ndani ya nchi hii, hii ni aibu, kwamba tunafanya mitihani ya Taifa wanaofaulu *below 30 percent* nchi nzima ni aibu, sana ni *private schools* ndiyo zinajikakamua kidogo, lakini hizi za kwetu hizi / *mean government school*hamna kitu. Ukiangalia matokeo acha shule hizi za vijijini ukiachia labda hizi za mijini kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza pengine na Zanzibar pale mjini, huko vijijini "F" zinatafunana pale. Unaweza ukafikiria labda...

## T A R I F A

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba shule za *private* ni za kwetu pia kwa sababu zinasomesha watoto wetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muhammed endelea.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba uniachie tu niendelee nimuachie na hayo yake kwa sababu tunajua kwamba wajenga shule ni sisi Watanzania, lakini hiyo ni lugha ya kiswahili na yeye ni mswahili anafahamu hiyo lugha maana yake nini. Kwa hiyo, naomba unilindie muda wangu niendelee na kuchangia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tungeangalia hapa *form four* kuna tatizo gani hapa, shule zinazofanya vizuri zaidi ni za *private*, narejea tena hizi za kwetu bado. Kwa hiyo, kwanza tungeangalia yawezekana kuna matatizo kidogo kwa walimu wetu hawa, yawezekana *there are some of the topics* zinawasumbua, ni vema tungefanya *research* tukatumia ile Idara ya Ukaguzi shulenii, tukafanya *research through nationwide*, tukazungumza na walimu wetu wanaofundisha madarasa haya ya *form three* na *form four*, watasema hawa zile *topics* ambazo zinawasumbua zile tukatengenezea *module*, tukaandaa *in service training* kwa walimu wetu ili kuwa *upgrade* waweze kufundisha *grade* ile ya *form three* na *form four*. Kwa kufanya hivyo ninaamini kwamba hizi "F" nyangi kabisa zingepungua. Huo ulikuwa mchango wangu wa mwanzo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa pili, sayansi inakufa mashulenii, kwenye shule za sekondari hizi ukiangalia matokeo ya wanafunzi wa *form four* hata *form six* hawa wanaenda *form six* zaidi ya asilimia 70 wanasoma *arts*, hata wale wengine ambaao *form four* walisoma sayansi. Kwa hiyo, kwa kipindi sasa hizi *subject* za sayansi zinaendelea kufa na zinakufa kifo kibaya. Sasa tutafute namna hapa ya kuweza kuwasaidia hawa vijana na hizi *science subject*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye shule zetu hizi na *ni-declare interest* mimi mwenyewe ni mwalimu wa sayansi na nimefundisha zaidi ya miaka 25 katika shule hizi za Serikali, kwa hiyo, kuna matatizo tunayaolewa. Kuna uhaba mkubwa sana wa *laboratory*, achilia mbali hata vile vifaa

vya kuviweka. Lile jengo angalau tukipata *at least tube* moja tuweke tunakosa hizi *laboratory*, sasa huwezi kufundisha sayansi *without laboratory*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, saa nyingine mwalimu mwenyewe, kuna wakati mmoja alikuja mwalimu pale katika shule ananiuliza hii *variable mass* ndiyo ikoje, yeye ni mwalimu lakini kwa ni mwalimu mgeni na hakupata vizuri *practical* wakati akiwa anasoma kwa hivyo anashindwa hata baadhi ya *terminology* zinazotumika kule maabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali itafute namna ya kuweza kuziboresha hizi *laboratory* zetu ili tuihuishe sayansi. Huko tunapokwenda kwenye nchi ya viwanda, viwanda vinahitaji wasomi waliosoma sayansi baadae wapelekwe kwenye kusoma ufundi, baada ya kufaulu vizuri katika kiwango cha *form fourna form four six*, kama hii sayansi itaendelea kulemazwa hivi sijui itakuwaje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbaya tunayopenda sana kuitumia Watanzania kwamba kilimo kwanza, mimi siyo muumini wa kauli hii, mimi nasema elimu ni mwanzo. Juzi moja nilikuwa nasoma gazeti wenzetu Afrika ya Kusini hivi karibuni tu kama hawajarusha watarusha *satellite* moja kubwa sana... (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tutaiona baadae *satellite*, tunaendelea Mheshimiwa Mbaitia, wafuatao watamuata baadae, Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Oscar Mukasa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubongo wa mtoto ni *very delicate*, ili nieleweke vizuri nitatumia mfano wa yai la kuku.

Yai la kuku ukiliwekea joto stahiki utapata kifaranga, kitakuwa kuku na baadae litataga, lakini ukiwekea joto ambalo ni la juu sana yai hilo litaiva na likiiva linaliwa na itakuwa mwisho wake, lakini ukiwekea joto lingine yai hilo hilo unaweza ukariharibu au kulidumaza. Huu ni mfumo unaokufa au unaodumaa utakuwa na *deterioration or stagnation* katika system. Naomba tusiue au kudumaza akili za watoto wetu, lulu zetu, zawadi ya mama Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza na hilo kwa sababu kinga ni bora kuliko tiba, tumeamua kupitia Wizara yetu ya Elimu kukumbatia ujinga ambaao ndiyo umesababisha umaskini, maradhi, rushwa na mambo mengine katika jamii ya Tanzania. Imeandikwa kwamba watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa yaani mfumo endelevu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema watu wanaagamia, ukichukua vitabu kwa mfano, nilikuwa nasoma hivi vitabu vilivyofanyiwa maboresho sasa. Ukitumba cha darasa la pili unaambiwa unganisha sauti za herufi, tangu lini ukaunganisha sauti za herufi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *consonant* a, e, i, o, u hata kuiandika ni tatizo. Hivi vilivyofanyiwa maboresho vinavyosambazwa sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwhali kuimba kwenye Bunge hili, ukiangalia kitabu cha darasa la tatu cha Kiingereza vinavyosambazwa sasa kina makosa lukuki. Unawezaje ukaanza na *alphabet unit* ya tatu wakati *unit* ya kwanza unaanza na sentensi, nimetaja machache tu. Vitabu vyetu hivi havina majina ya Wahariri, vina maudhui mabovu na vinakiuka hata sheria na maadili vinaonesha ukatili, tangu lini polisi akawa ni mzungu na wanatesa watu, kwa nini vitabu hivi vilivyofanyiwa maboresho? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule binafsi. Shule binafsi ni wadau muhimu sana katika elimu ya Taifa letu la

Tanzania. Wengi wetu ni zao la shule binafsi hata Marais wastaafu Mzee Nyerere, Kikwete, Mkapa na Rais wa sasa Magufuli ni zao la shule binafsi na hasa mashirika ya dini. Mimi mwenyewe ni-*declare* ni zao la hizi shule binafsi. Leo hii kama siyo shule binafsi tuorodheshwe Wabunge humu ndani ya Bunge wangkuwa kwenye hali ya namna gani? Shule binafsi nyingi hata zilizotaifishwa kwa mfano shule ya Pugu, Ihungo, Umbwe, Peramiho, Masasi, Minaki, Weruweru, Kilakala nitaje chache tu na vyuvo vya ualimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kilimanjaro una shule 314, mwaka jana kidato cha nne wamekuwa wa kwanza Kitaifa niwapongeze sana, nipongeze shule ya Anuarite ambayo ipo Jimboni Vunjo ambayo imekuwa ni shule ya tano kati ya shule kumi bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya vyuvo vikuu inakuwa na ubaguzi wa hali ya juu sana. Ninapende kuuliza na Serikali injibui vizuri *student unit cost* mfano mwanafunzi anayesoma Shahada ya Kwanza ya Udaktari pale KCMC Serikali inachangia kiasi gani na mzazi/mwanafunzi anachangia kiasi gani. *TCU* inalazimisha chuo kile waweze kuchangia shilingi 3,100,000; je, vyuvo vingine vya tiba wanachangia kiasi gani ili kuwe na *standard* ambayo inaeleweka badala ya kupiga huku na kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo mengi, Mzee Nyerere amesema nina kitabu chake hapa na nimesoma, ukisoma hotuba ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 1967 anasema elimu yoyote iwe ya darasani au isiyo ya darasani ina shabaha yake, shabaha yenyewe ni kurithisha kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine maarifa na mila za Taifa kwa kuandaa vijana wake tayari kuchukua nafasi zao katika kulitumikia na kuliendeleza Taifa. Mzee Mkapa amesema elimu yetu tunahitaji mjadala wa Kitaifa na Mzee Kikwete naye ametamka, nani atamke zaidi mpaka tuhakikishe kwamba tunaangamiza elimu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme *the way forward*, tukubali elimu yetu tupo kwenye janga ni maafa na ukiwa

na maafa naomba tusiwe na tofauti za kiti kadi humu ndani, tusimame sote kwa pamoja na Mheshimiwa Waziri yote tunayoyasema uyachukulie *very positive* kwa ajili ya kujenga Taifa, Wizara, watoto wetu na kizazi chetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu tuwe na mjadala mpana wa Kitaifa, hata urejee hoja yangu niliyoitoa humu Bungeni ya tarehe 31 mwaka 2013. Mjadala huu tukiwa nao tuwe na matokeo ya muda mfupi, kwa mfano matokeo ya muda mfupi.

Kuhusu shule binafsi kwa nini Wizara ya Fedha ianze kwenda kwenye majengo, mabwalo, mabweni, kumbi, waanze kutoza kodi ya majengo, kodi za ardhi na viwanja vya michezo. Hilo wala halihitaji mjadala ni suala la muda mfupi jadilini Serikalini ondoa zote wala usijadili, ada za mitihani ondoa wala msijadili masuala kama haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde suala la kusimamia ubora wa elimu Tanzania, tuwe na chombo kimoja cha kusimamia *standard* ya elimu Tanzania na hili lisichukue muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunaihitaji dunia kuliko dunia inavyoihataji Tanzania, tupende tusipende. Tuone kwa wenzetu karne hii ya sayansi na teknolojia, sayansi ni maarifa na teknolojia ni namna gani ya kutumia ya kutumia yale maarifa, duniani wenzetu wanafanya nini ili tuweze tukaondoka hapa Tanzania badala ya kila siku kulia. Lengo la nne la maendeleo endelevu ya dunia linasema elimu shirikishi, sawa, bora kwa wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni miundombinu ya binadamu, ukombozi wa mtoto wa kike ni elimu, lakini nimefanya utafiti miaka ya 1978 ndiyo tatizo la lishe lilianza Tanzania kwa kasi kubwa na zaidi ya asilimia 42 ya Watanzania walikuwa na tatizo la lishe kwenye shule zetu. Kwa hiyo, kunakuwa na *intellectual disability* ya hali ya juu sana. Unaweza kuona labda hata wengi walio madaktari, wahandisi na hata mionganoni mwetu miaka ya 1978 hiyo

hatujapata lishe vizuri labda ndiyo maana tunashindwa kufanya maamuzi yaliyo sahihi katika mazingira ya ajabu tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba chonde chonde walemaru wetu, kuna shule ya walemaru pale Moshi ya Kanisa Katoliki ipo Kimashuku ambapo Kanisa Katoliki wanajenga shule nzuri tu pale lakini wamewekewa vikwazo kwa kuwekewa vigezo vingi na ni shule kwa ajili ya walemaru, sasa tunafanya mambo gani ya namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisema kwa uangalifu kabisa, unajua Mzee Mwinyi alinifundisha namna ya kuhifadhi. Kwa mfano, nilivyosoma darasa la kwanza, *Sister Benedicta* na *Sister Protasia* walikuwa wananifundisha wananiambia ukitaka kumjua Yesu ni kujua elimu na tulikuwa tunaimba hivi tunasema: "Wa rohoni ndiye mwalimu kwake ni hunifumbulia, kukujua nipe elimu, Yesu mwema nijalie, eeh Yesu wataka nikupende." Yaani mwanafunzi unahifadhi kwa sababu ya ubongo wa mtoto na unajua umuhimu wa elimu katika Taifa. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtume Muhamad anasema nini ukitaka akhera usome, ukitaka dunia usome, elimu ni kitu chake kilichompotea muislam popote akipatapo na akichukue. Baba Askofu Mstaafu Dkt. Shoo anatuambia hivi: "Matendo yetu mema tunayoyafanya hapa duniani ni sauti huru na hai miili yetu ikiwa kaburini." Leo hii tunamsikiliza sana Baba wa Taifa yupo kaburini lakini kazi nzuri aliyoifanya ya elimu kwa Taifa letu. Sasa nani tena aseme ili tuweze tukaelewa (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara chonde chonde, hapa tulipofika sasa kwa nini tusifundishe watoto wetu; "a, e, i, o, u hizi ni herufi kuu, tamka kwa sauti kuu, ndiyo a, e, i, o, u; na jicho eee, kama mpira ooo, ni kikombe uuu" tunakuwa *very focused* ili watoto wetu na bongo zao zilivyo *delicate* waweze kuelewa badala ya kuwarundikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, michezo na sanaa kwa sababu ya muda nitashindwa kurudia. Michezo na sanaa mtoto wa darasa la kwanza michezo na sanaa unamsaidia nini kwenye KKK! Anatakiwa kusoma, kuhesabu na kuandika. Sasa unamrundikia masomo yote na vitabu vyote hivi, huyu mtoto atafanyaje? Tumesema mara nyingi, angalia sera hii ya elimu ya mwaka 2014 iliyozinduliwa na Rais Kikwete ile siku ya Ijumaa tarehe 16 Februari, 2015 yapo mambo mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kuomba baada ya kuizindua hii Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 haviendani vitu hivi. Sasa haya mambo ya kushindana huku shule binafsi huku hivi hapana. Hebu tuje pamoja kama Taifa na rai yangu kwa Bunge hili kwenye suala la elimu tuondoe itikadi... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea Mheshimiwa Juma Nkamia atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Oscar Mukasa ajiandae.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu *Subuhhana – Wataala* ametuamsha salama. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoifanya, Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nitazungumza kuhusu huu mradi wa *Education Programme For Results (EP4R)*. Niwapongeze sana Wizara kwa kweli kwa sababu kwa kupitia programu hii tumeona mabadiliko

makubwa sana kwenye shule za zamani au shule kongwe vilevile katika baadhi ya shule ambazo zilikuwa na hali mbaya, kwa hili kwa kweli nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yako yote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukipita ukienda katika shule zilizokuwa zamani mfano Mpwapwa, Sengerema kule ambapo na mimi nilisoma ukienda Pugu, shule zimebadilika kutokana na kazi nzuri mnayoifanya. Hizi hela ni za wafadhili na mfadhlili anatoa fedha anapoona unafanya vizuri lakini nasikia TAMISEMI wanataka sasa ziende kwao, Serikali ni moja tu mnagombea nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara ya Elimu wanashughulika na elimu, wanatengeneza miundombinu bado TAMISEMI wanataka nao hizo fedha ziende kwao, mnataka nini? Wakati mwingine hata mfadhlili anaweza tu aka-doubt kwamba kwa nini hizi fedha mnataka ziende kule TAMISEMI wakati huku pia zinasimamiwa vizuri, Serikali ni hiyo moja tu.

Nashauri Serikali kwa kuwa ni moja, acheni Wizara ya Elimu wasimamie na wanafanya vizuri tu na isitoshe hata fedha zinapokwenda kwenye Halmashauri kwenye shule zetu bado maelekezo yanatoka TAMISEMI kwamba watumie *force account*, hizi fedha zisimamiwe vizuri na matunda yake tunayaona, ulikuwa ni ushauri wangu wa kwanza, msigombee fito mnajenga nyumba moja, nadhani Mheshimiwa Kakunda umenielewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie hizi shule za *private*, amesema pale kaka yangu James Mbatia kwamba shule hizi zimetoa mchango mkubwa sana. Bahati mbaya tu mimi sikusoma *private*, lakini watoto wangu wanasoma *private*. Hawa watu wa *private* ni Watanzania na wanaosomeshwa ni Watanzania wenzetu, tusiwaone kama *competitors*, hawa ni *partner* wa elimu ya Tanzania. Hii ni kwa sababu hata ukiangalia kodi zao ni nyingi sana lakini kodi zinazotozwa kwenye *private sector* kwenye elimu wanaoumia ni wazazi ambao ni Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Mheshimiwa Waziri tafuteni muda muwe mnakaa na hawa *private sector* ya elimu mara kwa mara, ni vizuri kushauriana kwa sababu wanatoa mchango mkubwa sana kwa kweli. Wakati mwingine pia ni vizuri kumsikiliza tatizo lake na ukilisikia vizuri inawasaidia, kwa sababu utaona hata Mheshimiwa Rais anakutana na wafanyabiashara wanajadiliana, wanafikia muafaka na wakati mwingine maamuzi yanatoka palepale. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni jambo jema mkaliangalia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hata ufunguaji wa shule, mimi nina mtoto wangu mdogo ana miaka 10 mtoto wa mwisho, anasoma *private school* lakini anaamka saa kumi basi linalomchukua yule mtoto linapita saa 11 alfajiri kwa sababu madarasa yanaanza saa mbili, lakini huwa najiuliza hivi hawa watoto wanaenda kusoma au wanaenda kulala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu angalieni hata uwezekano, kwa sababu Kamishna wa Elimu anapotoa kwamba shule zifunguliwe tarehe fulani na zifungwe tarehe fulani, hii ni changamoto kubwa sana. Hivi kuna haja ya kuanza madarasa saa mbili? Hebu angalia kwa mfano Dar es Salaam ile, mtoto anachukuliwa Mbagala anaenda kusoma Masaki au Tegeta kwa mfano, anachukuliwa saa kumi alfajiri, akifika darasani analala tu huyu. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani hata hii mihula muiangalie pia halafu kwani ni lazima shule zifunguliwe siku moja na zifungwe siku moja, kila mtu na utaratibu wake! Nilikuwa nadhani ni jambo ambalo Mheshimiwa Waziri mliangalie, kwa sababu hata hiyo *private school* ukiangalia asilimia 80 ya wanafunzi wanaokwenda katika *university* wanatoka kwenye *private school, almost 80 percent. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye *form four* asilimia 80 ya wanafunzi wanaokwenda *A - Level/wanatoka private school*. Tuwajengee mazingira hawa kwa sababu wanafanya vizuri na wakati huo huo Serikali tunafanya vizuri pia katika shule zetu. Nilikuwa nadhani nitoe ushauri kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho, shule hizi wakati mwingine michezo ni kivutio kikubwa sana kwa watoto wetu kusoma, lakini michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA tumeishusha sana hadhi na heshima yake. Leo akina Zamoyoni Mogella, Mkweche, Makumbi Juma na Abeid Mziba tuliwatoa huko kwenye UMISETA, lazima tuwekeze huko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu ishirikiane na TAMISEMI na Wizara ya Michezo ili tuwatengeneze vijana wawe wazuri. Leo tusishangilie tu kwamba timu yetu imefanya vizuri vijana hawa, lakini baada ya pale hatuna tunachokifanya, watoto wanasaambaratika, hatujengi Taifa bora. Mimi nadhani na bahati nzuri Mheshimiwa Kakunda wewe ni mtu wa michezo hebu tengenezeni mazingira ili vijana hawa wa shule zetu, UMISETA na UMITASHUMTA wafanye vizuri kwenye michezo na Taifa liweze kuwekeza zaidi, kwa sababu michezo ya UMISETA ndipo unapopata vijana watakaokwenda kucheza kwenye *national teams* zetu, iwe riadha, iwe *football*, huko ndiko tunakowapata, lakini tukisubiri kuokoteza mitaani bila kuweka msingi tutakuwa tunafanya makosa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mheshimiwa Rais alipokuteua Mheshimiwa Kakunda kwenda Wizara hii nadhani pia aliona kwamba una uwezo mkubwa sana wa kushawishi namna gani michezo ya UMISETA iwe na tija na iwe na nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya ninashukuru sana na nirudie kusema Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana, endelea kusimamia huu Mradi wa EP4R na niliombe Bunge...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nkamia kwa mchango wako.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janet Mbene atafuatiwa na Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Ester Mmasi ajandae.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Naibu Waziri na Maafisa wote kwenye Wizara yake kwa hotuba nzuri. Naomba nianze kwanza kwa maombi maalum kwa Wilaya yangu ya lleje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya lleje kwa ufadhili wa Balozi wa Japan tulijengewa Chuo cha Ufundı VETA tukaweza kupata majengo mawili na karakana na *condition* moja wapo ilikuwa Halmashauri imalizie jengo la utawala, vyoo na sehemu ya kulia chakula. Niliiwaomba Wizara watusaidie wakatupa *conditions* kuwa tupanue eneo la hiki chuo, tusajili ile ardhi, kwa mfano tuwe na *title deed*, halafu ndiyo tutaikabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuliwaandikia baruwa mwezi tarehe 8 Novemba, 2017 kuwa tumekamilisha na tunaomba sasa waichukue ili waiendeshe na kumalizia miundombinu iliyobakia kama ambavyo wenywewe walikuwa wameahidi wangefanya. Sasa naangalia katika kitabu hiki cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 26 - 27 ambako ndiyo amezungumzia masuala ya VETA, sioni sehemu yoyote ambapo imetajwa lleje na sielewi sasa hiki chuo kimeshasimama zaidi ya miaka mitatu hakifanyi kazi na ndicho chuo pekee cha ufundı Mkoa mzima wa Songwe. Pengine sasa wangetufikiria jinsi gani watatusaidia, japo kianze kufanyakazi. Kwa sababu hata mfadhili wa kwanza ameahidi kurudi tena kutusaidia lakini mradi kianze kwanza, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, lleje ni Wilaya ya pembezoni na ni Wilaya kongwe na kwa miaka mingi hatuna shule ya wasichana ya *boardingwala ya day*. Watoto wetu wa kike inabidi wakae ama kwenye mabweni

machache ambayo hayatoshi au wapange kwenye nyumba za watu au wanakwenda Wilaya nyingine kabisa kwenda kusoma shule za sekondari. Tuna tatizo kubwa la mimba za utotoni kwa sababu ya matatizo yanayowapata wasichana katika hekaheka hizi za kutafuta elimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wazazi wanakuwa na gharama kubwa sana inapobidi wasafirishé watoto wao kwenda kuwapeleka kusoma Wilaya nyingine. Je, kwa nini Serikali haina utaratibu wa kuwa na shule ya wasichana ya sekondari kila Wilaya kama ambavyo ni utaratibu wa mambo mengine katika Wizara zingine? Tunaomba sana tusaidiwe tayari wenyewe tuna mikakati ya kuanza ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana, lakini tutahitaji Serikali na yenye we kutia mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maoni mengi yametolewa na Waheshimiwa Wabunge pande zote, ningependa hayo pia yazingatiwe. Kamati imetoa maoni mazuri sana, naomba yote kama ikiwekeza yazingatiwe kwa sababu ninaamini kabisa yakifanyiwa kazi hayo hii Wizara itafanya kazi nzuri zaidi na watoto wetu watafaidika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije sasa kwenye suala zima la VETA na Vyuo vya Ufundı Stadi au Vyuo vya Kati. Imetokea tabia au mtindo kuwa vyuo vya kati vikifanya vizuri vinapandishwa na kufanya kuwa vyuo vikuu, nafikiri tunafanya makosa makubwa sana kwa kufanya hivyo. Vyuo vya Kati ni vyuo vinavyofundisha masuala ambayo ni ya moja kwa moja yanaweza kuingia katika ajira, kwenye viwanda na hali kadhalika, kwa sasa hivi tunazungumzia uchumi wa viwanda, huu ndiyo ulikuwa wakati sasa wa kuboresha vyuo vya kati, kuviongezea mitaala ambayo inalingana na mahitaji ya viwanda tunavyotaka kwenda kuvijenga na kuvifanya viwe vinatoa ufundı mzuri zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuhamasisha kama itawezekana, vyuo vya ufundı vyote vifundishe kwa mitaala yao kwa kiswahili, itawasaidia hawa mafundi wadogowadogo ambao wanatusaidia mitaani magari,

redio, *television*, karakana mbalimbali hizi wale vijana wangefundishwa kwa Kiswahili kwa sababu wengi ni darasa la saba na *form four* tungejikuta tuna mafundi ambao wana weledi mzuri badala ya ule wa kubahatisha, vilevile tukajikuta kuwa tumeanzisha ajira nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko katika masuala ya vyuo vya ufundi, hasa *VETA*. *VETA* tumekuwa tukiichangia fungu la *skills development levy* ya asilimia 4.5; theluthi moja ndiyo imekuwa ikienda *VETA* moja kwa moja, theluthi mbili ya tatu imekuwa ikienda Serikali Kuu. Sasa hii inachangiwa na waajiri. Waajiri hawa hawajui ile theluthi mbili inakwenda kufanya kazi gani, kwa sababu lengo ilikuwa ni kupeleka *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tayari waajiri wanakuwa na wasiwasi kwa nini hela halendi yote *VETA*? Nashauri kwamba sasa hivi tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda, *VETA* zetu lazima ziimarishwe, basi lile fungu lote la asilimia 4.5 liende *VETA* moja kwa moja kama ambavyo hiyo theluthi moja inakwenda. Hii kwanza itawafanya waajiri wenyewe wanaochangia kuwa na imani, lakini vilevile wanaweza hata kuweza kuchangia zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhusu *VETA* na vyuo vya ufundi stadi viko chini ya Wizara ya Elimu lakini vinalenga waajiri ambao wako chini ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Ninapenda kuihamasisha Serikali kama itawezekana na kama ambavyo inafanyika kwenye nchi nyingine nyingi, *VETA* na vyuo vya ufundi stadi viende chini ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa sababu kwanza itakuwa ina uhusiano wa moja kwa moja na itajibu moja kwa moja hoja za waajiri juu ya mahitaji yao ya ajira. Jinsi ilivyo sasa hivi waajiri hawana namna ya kuongea na Wizara ya Elimu kuhusiana na masuala haya kwa sababu hakuna ule uhusiano wa moja kwa moja, lakini wakiwa kwenye kazi na ajira moja kwa moja kutakuwa kuna mahusiano ya waajiri ambao ndiyo wanawahitaji hao wafanyakazi wenyewe weledi na Wizara, lakini vilevile

itapunguzia Wizara hii kazi nyingi. Hii Wizara inashughulikia mambo mengi mno, matokeo yake hata ufuatiliaji wa ufanisi unapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara moja inashughulikia elimu ya msingi, sekondari, vyuo vikuu, ufundu stadi, maktaba, taasisi mbalimbali, sasa vitu vyote hivi viko chini ya Wizara moja halafu haohao wasimamie ubora, wasimamie utoaji huduma, wasimamie miradi, kwa kweli naona kama tumerudhika vitu vingi sana kwa Wizara moja. Serikali... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbene kwa mchango wako. Mheshimiwa Mukasa.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kutupa afya, nawashukuru wananchi wa Biharamulo kwa kuendelea kutoa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Ndalichako, Naibu Waziri na timu nzima, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo nafahamu kwa kina nini kinaendelea. Anafanya kazi nzuri ingawa ni wazi lazima tupate maeneo ya kusema ili kufanya kazi iwe nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na pongezi. Pongezi ya kwanza ni kuhusiana na ujenzi wa nyumba za walimu. Biharamulo kwenye shule zenye mazingira magumu nimepata shule mbili, Shule ya Sekondari Katahoka ujenzi unaendelea, Shule ya Sekondari Nemba tumepata mgao lakini naona kuna kuchelewa kidogo, naomba tufuatilie ili tuende kwa kasi. Lakini naomba tuzitazame shule nyingine

mbili moja ni Nyakahura Sekondari mpakani kabisa kule na Ngara na Karenge Sekondari hali yake ni mbaya sana. Tunashukuru kwa tulichopata, lakini tunaomba tuzitazame hizo mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, napenda kupongeza suala moja ambalo ni la Kitaifa, hili la Bodi ya Mikopo. Ukiangalia takwimu zinaonesha kabisa mwaka 2015/2016 mwaka ambao Serikali ya sasa iliukuta tayari umeanza, urejeshaji wa mikopo ulikuwa shilingi bilioni 32, lakini 2016/2017 tukaenda shilingi bilioni 116; 2017/2018 tumekwenda shilingi bilioni 130. Ni kazi nzuri kwa kweli, inaonesha kabisa namna gani tunafanya kazi nzuri kwa upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba naomba tutafute namna ya kimkakati zaidi ya kuweza kuboresha zaidi kwenye eneo hili kwa sababu tumeshaonesha tunaweza. Nadhani inawezekana kabisa tukaondoka kwenye Bodi ya Mikopo tukaibadilisha ikawa *Higher Education Loan Fund* ili ubunifu ukae vizuri zaidi na mianya ya kutapakaa na kuwa na mambo mengine ya kufanya zaidi kuweza kusimama yenye we iweze kuwa mingi zaidi na wawe na ile *autonomy* ya kutosha zaidi watafanya kazi vizuri. Hili ni eneo ambalo kwa kweli napongeza lakini tutafute namna ya kufanya vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie habari ya ubora wa elimu nikihusianisha na hii habari ya shule za Serikali na shule za binafsi. Namshukuru sana Mheshimiwa Mbaitia, ameisema vizuri sana leo muda mfupi uliopita, kwamba jamani hizi shule zote ni za kwetu na zote zina mchango wa kutosha kwenye kutoa elimu ya nchi hii kwa watoto wetu. Kwa hiyo, tuna wajibu wa kuwasikiliza na kuwasaidia lakini pia tuna wajibu wa kuwasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na upande wa kuwasikiliza. Ilitokea mjadala mwaka jana nakumbuka na wote mnaukumbuka wa habari ya shule za *private* hizi, wanatoa mitihani mtoto anapotaka kutoka kidato kimoja

kwenda kingine, mitihani ndani ya shule na wanaitumia kama kigezo cha kumwambia asiendelee ama arudie. Ni wazi nakubaliana na msimamo wa Serikali, kwamba tukilifanya jambo hili kiholela itakuwa ni hatari, kwamba haujui, huwezi kupima kwamba shule "X" imetumia kipimo gani na shule "Y" imetumia kipimo gani, ni vizuri tukawa na kipimo kimoja ili tuweze kujua nani anafanya nini na kwa manufaa yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili, naiomba Wizara pia kuacha bila kupima nayo ni hatari, tutafute namna ambayo kila mtu asipime kiholela, lakini tuwe na namna ambayo tunawapima hawa watoto wajue kwamba nisipofanya bidii nitashindwa kutoka kidato cha kwanza kwenda cha pili na ule umri mnafahamu ni umri amba bado wako kwenye hali ambayo wengine hawajielewi, kama hatuna namna ya kupima tunawaacha kiholela, matokeo yake ndiyo tunapata matokeo mabovu sana huko mbele, kwa hiyo naomba hilo Serikali tuliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili ni upande wa kuwasimamia. Mimi nina mawili, mtanisamehe wenzangu amba kwa bahati nzuri ama mbaya ni wamiliki wa shule, nalisema hili kwa nia njema tu. Kuna hili suala la shule inachagua watoto kwenda kidato cha kwanza kutoka darasa la saba "A" zote ili matokeo ya kidato cha nne yakitoka ionekane yeye alifafulu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijawahi kuona hospitali ambayo Mheshimiwa Waziri naona hanisikilizi, sijawahi kuona hospitali ambayo mtu akienda daktari anaangalia anasema wewe ninavyokuona unachechemea naomba hapa usije kabisa unaweza ukafia hapa! Ni kazi ya hospitali kwenda kuchukua mtu hata aliye hoi kwa sababu ni kazi yako kutibu.

Sasa kazi ya shule ni kufundisha watu, naomba tuwe na utaratibu ambapo katika watoto mia unaotaka kuchukua wewe shule ya *private*, chukua 30 *cream*, chukua 30 wa kat, chukua 40 siyo waliofeli kabisa lakini ile ngazi

inayofuata, waliofeli kabisa tuwaache, lakini tuwe na namna tuchanganye ili hata ukija kusema umefaulu tunajua ulifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tunakupa wenye "A" zote halafu unakuja unasema mimi nimekuwa wa kwanza, tutafute utaratibu, tuchanganye ili tupime kwa usawa na kila mmoja apate fursa ya kufundishwa. Vinginevyo na hospitali nazo ukienda unachechemea zaidi unaambiba wewe usiingie bwana utatufia hapa ni kazi yao kukutibu, wakashindwa watakupeleka mahali ambapo kuna ujuzi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kusimamia kwenye hizi shule za *private* ni habari ya likizo. Mtoto humuoni mwaka mzima wanasema mwezi wa sita hawaji, mwezi wa 12 hawaji, halwezekani, hata kuja kusalimla wazazi ni sehemu ya shule. Hebu angalia shule za Seminari za Katoliki, wale ukikutwa unasoma saa ya michezo unafukuzwa kwa sababu unafundishwa kutumia muda wako wa kusoma vizuri ili muda wa kula uutumie vizuri, muda wa kucheza uutumie vizuri, lakini ndiyo wanaongoza kufaulu kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna shule yaani mtoto haonekani mwaka mzima wanasema wana masomo maalum! kuja nyumbani kuzungumza na wazazi ni sehemu ya shule, tunaomba usimamie Mheshimiwa Waziri, hizi shule zote ni za kwetu, tusimamie wasome, saa ya kucheza wacheze, saa ya kula wale, saa ya kusoma wasome, likizo waje nyumbani, ni sehemu ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuongelea pia ukurasa wa 112, ameongelea Chuo cha Mkwawa, kuna shilingi bilioni mbili pale inapelekwa kwa ajili ya maabara ya kompyuta na vitu kama hivyo. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kama nilivyosema, nimeshuhudia mwaka huu tumekwenda Mkwawa pale. Serikali imepeleka pesa pale ya kujenga ukumbi wa mikutano lakini mambo yanayoendelea ni maajabu ni ubadhirifu mtupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tubadilishe namna ya kusimamia pesa hizi. Tutakuwa tunafurahi hapa kwamba imekwenda bilioni mbili lakini kama usimamizi haukai vizuri mwisho wa stori ni kutumbua watu kutafuta nani ameiba ambayo haitusaidii, tutafute namna ya kusimamia kabla hazijaabiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Mmasi atafuatiwa na Mheshimiwa Jasmine Bunga na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na mimi niweze kuchangia kwenye Bunge lako hili tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa William Tate Olenasha, kimsingi mnafanya kazi nzuri. Niwape moyo, hakuna kazi ambayo mtaifanya mithili ya malaika, sisi ni binadamu kazi yetu ni kukosoa, lakini msife moyo kazi mnaifanya na sisi tunaiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichangia ndugu yangu Mheshimiwa Catherine Ruge, nadhani hayupo, nilipenda angekuwepo naye anisikilize. Alikuita *Madam Professor sioni statistics usiogope!* Mheshimiwa Waziri unakumbuka niliposimama hapa nililia na wewe nikakuomba *hostels* za wanafunzi umetupa. Tulikulilia kuhusu Mloganzila umetupa, Mheshimiwa Oscar amekiri pale aliquumba nyumba za Walimu wake umempa. Mheshimiwa Waziri tunataka vitu *tangible* chini ya Wizara yako, vitu ambavyo tutaviona, hatutadai *statistics*, tutakudai llani ya Chama cha Mapinduzi ilielekeza nini na wewe unafanya nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakupa hongera, isitoshe ninakushukuru sana kwa kuwa tayari katika *kui-support Uni Life Campus Program* na kwa hakika tumeona

utayari wako katika kutengeneza Taifa linalojiheshimu na taifa ambalo lina uwezo wa kushindana kwenye soko la ajira. Mheshimiwa Waziri pokea pongezi zangu za dhati kutoka kwa wanafunzi wote Vyuo Vikuu nchi nzima. *UniLife Campus Program* inazunguka nchi nzima na hii ni *feedback* ya wanafunzi wao, ni *feedback* ya walimu, ninakupa pongezi, endeleeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama kuchangia kuhusu Mfuko wa Bodi ya Mikopo. Nina machache sana ya kuongea katika hili na nitaongea hapo tu sitataka kwenda mahali pengine. Mheshimiwa Waziri, pamoja na pongezi ambazo hata ndugu yangu Mheshimiwa Oscar amezitoa, ni kweli, tumeona mafanikio mazuri sana. Tunapoongelea Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, tumeona kumekuwa na ongezeko kubwa la wafaidikaji wa Bodi ya Mkopo. Utakumbuka miaka kumi, ninapoongelea hivi ninamaanisha mwaka 2005 mpaka mwaka 2015, tumekuwa na wafaidika 390,922 lakini kwa miaka miwili tu 2015 mpaka 2017, tumekuwa na wafaidika wapya 113,922.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hii ni pongezi ambayo haipaswi kubewa, sisi tuliokuwa na llani ya Chama cha Mapinduzi, tuliokuwa na *party manifesto* mikononi mwetu tunasema hii ndiyo kazi ambayo tulipewa dhamana na wananchi wetu na sisi tukaiteweza bila hofu. Makelele haya yasiwatishe, tuna mengi ya kujibu tunapofika mwaka 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tumeona masuala mazima ya urejeshwaji wa mikopo Bodi ya Mikopo, tumeona kuna hatua kubwa imepigwa. Tunapoongelea katika miaka kumi iliyopita, urejeshwaji wa Bodi ya Mikopo tofauti na alivyokuja Badru, tuliweza kukusanya shilingi bilioni 101 katika miaka kumi, lakini katika miaka miwili tu 2015 hadi 2017, chini ya uongozi wa Ndugu Badru, tumeweza kukusanya shilingi bilioni 285. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri hizi ni pongezi zetu kwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa sababu sisi ndiyo wenye llani na tunajua kwenye ilani kuna nini.

Endelea na kazi hii kwa sababu huu ni utume wa kanisa na sisi tuna imani na wewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya, tunasema kabisa ukiangalia kwenye ripoti ya *CAG* na ripoti ya Bodi ya Mikopo tunapoongelea katika mwaka 2005 toka uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo mpaka muda huu tuliosimama hapa pesa ambayo ilipaswa kuiva na kurejeshwa ilikuwa shilingi bilioni 585 lakini katika pesa hizi, shilingi bilioni 235 bado hazijaweza kurejeshwa. Pamoja na ukusanyaji mzuri lakini zipo pesa ambazo imeshindikana kurejeshwa lakini *explanation* tofauti na *explanation* ya *CAG* Bodi ya ya Mikopo inasema hawa ni pamoja na wanafunzi ambao wako kwenye *grace period* ya miezi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka hata Wabunge tulipitisha *Miscellaneous Amendment* ya kutaka asilimia 15 kutoka kwenye asilimia nane, hapa kuna kitu ambacho inabidi tukiangalie, *something is alarming*. Kwa sababu mwisho wa siku lazima tuone mfuko huu unaweza kuijendesha na ukisoma ripoti ya *CAG* ziko pesa nydingi hazijaweza kurejeshwa. Sasa tunatoa wapi, vyanzo ni vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nasema *something is alarming* kwa sababu sioni nguvu ya Serikali ilipojikita katika kuona kwamba vijana hawa wanaajirika kwa wakati. Mheshimiwa Waziri mwaka jana 2017 ukiangalia ikama ya Serikali tulisema tutaajiri vijana 52,000 lakini *sad enough* tumeweza kuajiri vijana 16,800 sawa na asilimia 32, Mheshimiwa Waziri tunakwenda wapi? Je, tulitengeza ile *Paralegals Act* katika kuja kutoa hukumu isiyio kuwa na hatia kwa vijana wetu. Mwisho wa siku hawa watapaswa kurejesha pesa hizi, watazitoa wapi endapo Serikali yetu inashindwa kujipanga katika kuandaa ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninapoongea suala hili hapa katika Wizara hii ya Elimu utakubaliana na mimi tuna *graduates* zaidi ya laki sita kwa mwaka, lakini *it is less than ten percent* wanaingia kwenye ajira rasmi za Serikali. Mheshimiwa Waziri inabidi tukaze buti

kuona kwamba vijana wetu tunawaandalia mazingira makini ya wao kuweza kuajirika na kuweza kuona kwamba bodi hii inajientesha kwa fedha hii kuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukiangalia *page* ya 15 ripoti ya Waziri Mkuu alisema kwamba ametoa shilingi milioni 783 kwa vijana 840 sawa na asilimia 0.105. Mheshimiwa Waziri sioni mwelekeo kidogo ninapata giza hapa ukiangalia vijana wanaomaliza, wanao *graduate* na vijana wanaoingia kwenye soko la ajira hata kwa kujajiri bado *hai-reflect* nguvu yetu, *hai-reflect* majibu ambayo tunapaswa kutoa kama wabeba ajenda na kama wabeba llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongea suala la *VETA* ambalo hata dada yangu Mheshimiwa Janet Mbene ameliongelea, *VETA is almost dying*, Mheshimiwa Waziri ni vema ukaangalia. Ripoti ya *CAG* *page* 138 inaonesha kabisa kuna matatizo pale, *VETA* hajulikani ni *regulator*, hajulikani ni *key player!* Anatuambia kabisa ukisoma *page* ya 138 kwenye chuo kimoja ambacho kilikuwa *sampled* hapa Dodoma unaambiwa uwiano wa wanafunzi ni moja kwa kwa 113, mwalimu mmoja wanafunzi 113! Mheshimiwa Waziri ubora wa elimu unatoka wapi hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajiandaa kuingia kwenye Tanzania ya viwanda tunaongea nini katika takwimu hizi. Licha ya hivyo utaangalia kwenye moja ya mipango ya Ofisi ya Waziri Mkuu tumesema tuna programu ya uanagenzi kwa nini programu hii ya uanagenzi katika mwaka huu wa fedha 2018 tumesema wafaidika watakwenda kuwa 10,500. Kwa nini programu hii nguvu kazi ya Taifa inayoelekezwa katika programu hizi tena kwa kupeleka vijana wetu kwenye vyuo holela vya mtaani, mathalani Don Bosco siwezi kuita holela sijui! Hatujui mitaala yake mnapeleka vijana kule kwenda kujifunza kuandaa na Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri atakapokuja kuhitimisha mada yake atuambie amejiandaaje kutumia fursa hizi katika kuona kwamba Bodi ya Mikopo

inajidesha, vijana wanaingia kazini akija hapa atuambie nini mipango yake kama Wizara, nini mipango yake kama Waziri mwenye dhamana katika kuona kwamba bodi hii inaweza kujikimu kutokana na fedha ambazo zinatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mipango mingi ukiangalia Ofisi ya Waziri Mkuu pia kuna hela nyingi zimebekwa bilioni 15 katika kusaidia vijana waingine kwenye kilimo, umejiandaaje Mama Ndalichako, umejiandaaje Bodi ya Mikopo ili vijana hawa waweze kurudisha pesa? Hizi ni fursa umejipangaje. Ukienda kwenye *private sector* ambazo tunategemea vijana wengi wanaweza kuajiriwa tazama *TBL* ni *almost* imefungwa, wamebaki *gate keepers* wamebaki, wamebaki watu wachache sana pale, vijana wetu wamekosa ajira *TBL*, angalia *payroll* ya *TBL* inafanyikia Mauritius, kule wana *enjoy tax...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Elimu. Niungane na Wabunge waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote katika Wizara hii ya Elimu kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, bila kigugumizi tunaona mabadiliko makubwa ambayo yanatokea katika sekta yetu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi tulikuwa tunalia na hizi shule kongwe Kilakala, Ilboru na zingine, mmeweza kuzikarabati ili sasa ziweze kuendelea kutoa elimu nzuri na mazingira mazuri kwa wanafunzi wetu tunashukuru sana. Pia katika usimamizi wa elimu bure kwa wanafunzi wetu shule ya msingi kuanzia Darasa la Kwanza mpaka *form four* tunapongeza sana Serikali. Pongezi kubwa ziende kwa

Mheshimiwa Rais kwa kuweza kupitisha sera hii ya elimu bure moja kwa moja pale alipopata uongozi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie zaidi na nijikite kwenye suala la ubora kwa sababu ukiangalia taarifa zote mbili, Wizara pamoja na taarifa ya Kamati zote kwa kweli kwa masikitiko inaonesha ubora wa elimu hasa shule za Serikali jinsi ubora wa elimu unavyozidi kushuka ndiyo maana watu hapa wanafanya *comparison* kati *perfomarnce* ya shule za *private* na shule za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana wadau wa shule za *private* wanafanya kazi kubwa sana, wanalenga hata fursa na soko la dunia hii linaendaje, hasa niwapongeze kwa kuweza kuipa kipaumbele lugha ya kiingereza katika taaluma. Kwa sababu hapa tunazungumzia lugha sawa kiswahili ni yetu lakini tunapozungumzia taaluma kwa sababu hii lugha ina mambo mengi ambayo ninaweza nikaeleza baadae. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ubora ubora huu wengi tumezungumzia hii *performance*, kuna *factors* ambazo zinafanya mwanafunzi afaulu, mioundombinu, walimu wa kotosha, motisha kwa walimu *participation* ya wadau mbalimbali wakiwemo wazazi, wanafunzi na lugha ya kufundishia, hivi ni vitu muhimu sana katika sekta hii ya elimu, lakini upande wa shule zetu za Serikali hizi *factors* zote zinasuasua zinayumba na ndiyo maana shule za *private* zina *performance* nzuri kwa sababu miuondombinu ni mizuri ya kufundishia, walimu wapo wa kutosha, motisha kwa walimu ni *imporntant factor* katika kufanya elimu bora wanapata, pia wazazi wako karibu sana na wanafunzi wao.

Ukiangalia kama walivyosema wachangiaji wengine hawa wanachukua wanafunzi wale *cream* ndiyo wako pale. Halafu na lugha ya kufundishia hao wanaanza toka chekechea mpaka *form four* wanatumia lugha ya kiingereza na ili mtu aweze kueleza *ideas* zake lugha ni muhimu sana, shule zetu za Serikali hivi vitu tuna-*miss*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ushauri wangu ili shule za Serikali uonekane unafanya kazi boresheni miundombinu ya kufundishia. Sasa hivi tumeingia kwenye suala la elimu bure miundombinu haiko tayari, tatizo letu tunaanza ku-*implement* sera na kuifanyia kazi kabla ya maandilizi, hii ni changamoto kubwa sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi unasema watoto waishie darasa la sita mmeefanya utafiti gani, mmewaandaa hawa watu kwa kiasi gani, mnachukua walimu wa sekondari mnawapeleka kufundisha Shule ya Msingi kweli wanafaa? Hivyo, hizi changamoto mzifanyie kazi ili siku moja na shule za Serikali tusimame kidedea. Ingawa kwangu nasema nakumbuka maneo ya Mwalimu Nyerere wakati anazungumza nchi matajiri na sisi ambao siyo, anakuambia unamchukua mtu wa *heavy weight* unaenda kumshindanisha na huyu wa *featherweight* thaiwezekani huyu mwenye *heavyweight* atamshindwa. Kwa hiyo, hizi shule za *private* unazishindanisha na shule za Serikali moja kwa moja kati ya watu 100 Serikali itakuwa nne kutokana na ubora wa miundombinu na changamoto nytingine. Kwa hiyo Serikali muweze kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine nizungumze suala la lugha, kwamba lugha ni tatizo katika shule zetu. Mwanafunzi anaanza shule za Serikali zilizo nydingi kiswahili hadi darasa la saba, *form one* anaenda kiingereza hawezি kufanikiwa. Kwa hiyo, lazima tuchague lugha ya kiingereza ni rahisi kutengeneza vitabu vya kiada kuliko kule Chuo Kikuu. Chuo Kikuu ili mtu awe daktari alisomee sikio kwa wale ambao wamesoma *degree* mpaka *Ph.D* huko huwezi ukafanya utafiti kwa kutumia *text book*, unahitaji *reference* na *bibliography*, sikio lina vitabu zaidi ya 1,000 sasa wewe ukisema leo kwenye taaluma ukaweke lugha ya kiswahili hapana, hatutafika na fursa za dunia tutazikosa. (*Makofii*)

Mshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwa upande wa Vyuo Vikuu, nakupongeza sana suala la mikopo lilikuwa tatizo sasa hivi umejitahidi wanafunzi wetu wanaendea vizuri.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Kwa hiyo, ninaomba sana kwa upande wa vyuo vikuu uweze kuboresha mambo yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bima ya Afya kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, wanafunzi wanapofika *term* ya kwanza *semester* ya kwanza wanalipa zile fedha za bima, lakini baadae wanakuja kuipata *semesterya* pili, kwa hiyo, naomba uboreshe hiyo. Pia suala la kuhama chuo kutoka chuo kimoja kwenda chuo kingine bado mfumo hauko vizuri muufanyie kazi, kwenye mikopo ninataarifa kwamba wanafunzi 35 wa *DIT* wamepunguziwa ile ada ya mikopo kumetokea nini, badala ya shilingi 900,000 wanalipiwa shilingi 600,000 kumetokea nini? Mnawa-*frustrate* hawa wanafunzi. Vilevile muendeleze miundombinu kama *hostel* za wanafunzi ili kuwaokoa hawa... (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Aisharose Matembe ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kipekee kabisa namshukuru Mungu kwa kuwepo sisi hapa salama na tuko katika mambo haya ya maendeleo. Nawashukuru wale wanawake wa Kilimanjaro walioniwezesha kufika hapa na leo nazungumzia jambo la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu haina mwisho naamini hata Wabunge walioko hapa bado wanajisomesha, bado wanajiendeleza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Profesa Ndalichako na wote ambao wameshiriki katika kuandaa hotuba hii ya bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika ule ukurasa wetu wa 62 mpaka ukurasa wa 64 wanapozungumzia *EP4R*. Nimeona wanafanya maandiko tofauti wanapata hela za kutosha wanakarabati majengo, wafadhili wanaenzi shughuli zao. Ombi langu na naomba hata ninyi Wabunge ikiwapendeza iletwe hapa tuazimie hela hizo zisimamiwe na Wizara hii ya Elimu zisiende tena kule TAMISEMI, kwa sababu kama zinapatika na zimekuja na sasa zinafanya jambo la elimu na wengi mmekwenda kutembea mmeona ukarabati hata wa zile shule za zamani kwa nini sasa zinakwenda TAMISEMI, hapo bado inanikanganya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ombi hilo na pongezi hizo kwa Mheshimiwa ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa elimu bila malipo kuanzia darasa la awali mpaka kufikia *form four* hili ni jambo jema na wazazi wengi wamependa, sasa hakuna sababu ya mtoto yoyote asiende shule. Baada ya elimu hiyo nini kinachoendelea, mwanafunzi akishafunguliwa mlango wa kusoma nawaomba na nawapongeza wanafunzi wote walio mashulenii leo na hata siku za baadae nawapongeza sana kwa kupiga vita ujinga, nawapongeza sana na nawaambia elimu yenye ni vita.

Niwaombe tu sasa ukishamaliza *form four* usibweteke kwamba wewe ni *graduate* ukae tu, endelea kuijendeleza. Nasema hivyo kwa sababu hata yule *graduate* aliyemaliza Chuo Kikuu ajira zimekuwa ni shida, kila siku Wabunge wanapigiiwa simu wanaombwa wawatafutie kazi, kazi hazipo! Tatizo tu siyo kazi kutokuwepo nadhani hata Walimu na wazazi tunakosea mahali pa kumjenga mwanafunzi au mtoto achukue taaluma gani ambayo mbeleni itamfungua zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndani tunasema sayansi, je wewe mzazi unamsisitizia mtoto wako hata kujifunza kuhesabu, kwa sababu msingi wa sayansi ni hesabu. Nawaomba wazazi wote sasa wawe wanapitia vitabu vyatya wanafunzi wao au watoto wao wajue kwamba wanafunzi hawa wanasoma wanavyotakiwa. Huko mbele tunaona wazi kuna ajira ambazo hazitahitaji tena wafanyakazi, kuna ajira ambazo zinajifuta kwa sababu sayansi sasa imeshafunguka. Kuna fani ambazo sasa hivi zinafanywa na roboti, zinafanywa na mashine, mtu mmoja anakaa anaendesha kiwanda kikubwa, hatuhitaji tena wale mashine *operator* wengi ni kwa nini sasa wazazi, walimu, wasimwambie mtoto achana kiasi na haya masomo ya sanaa nenda kwenye masomo ya sayansi ambako baadae unaweza kuwa na ajira unayotaka wewe kuingia kwenye *payroll*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kabisa kwamba tulianza kujenga maabara lakini imefika mahali inasuasua, naomba ule mpango wa kujenga maabara uendelezwe. Pia kuwa na maabara bila walimu wa kufundisha sayansi haisaidii, kuna wakati ambapo wazazi tulikuwa tunachangia wale walimu wa sayansi kwa kipindi, ikafika mahali likatoka Toleo la 16 la mwaka 2015 michango isifanyike tena, sasa wale walimu *temporary* wa kufundisha sayansi mashulenii hawapo tena, nataka ufanuzi kutoka Serikalini endapo wale walimu hawatakuwepo wale wanafunzi wallopo shuleni sasa hivi watafundishwa na nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona kabisa kwenye maabara tunazungumza kupata walimu wa sayansi, naomba pamoja na walimu wa sayansi tuna wale *lab. technician* ambao wanafanya maandalizi ya vifaa vyatya *experiment*. Naomba wafikiriwe ajira zao ziongezwe tunahitaji *lab. technicians* ambao wana usoefu au hata kama ni wageni, lakini wawepo kila *lab* inalojengwa lipate *lab. technicians* wawili, kama ni la sayansi labda la *physics, chemistry* au *biology* tupate angalau wawili kwa shule moja. Haielezeki tuwe na *labs* lakini hazina *technicians* unamtarajia mwalimu huyo aandae vifaa vyatya *experiment* mwalimu huyo

aje sasa awafanyie vijana hao *experiment*. Kwa hiyo, hii ajira ya *lab. technicians* naomba sana ifunguke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwenye suala tunalosema kwamba Walimu wetu hawapati stahiki wanazostahili. Tumeona Serikali imejitahidi, lakini kuna wale walimu ambao kwa kweli wanafanya masomo ambayo yanababisha wao wakae vipindi zaidi pale shulen. Naomba hawa walipwe *hardship allowance*. Mwalimu siku zote alikuwa mtu wa maana sana, mwalimu alikuwa akipita anaheshimika, anasalimiwa kwa heshima, nyumba yenye heshima ni nyumba ya mwalimu, lakini sasa hivi walimu wengi wamedhalilika ile heshima imekwenda wapi? (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeona labda irudishe walimu wengine wa sekondari kwenda *primary* wenzangu wamezungumza, tunaomba wale walimu wa sekondari wanaokwenda *primary* waandalie pia, kwa sababu mwanafunzi akishapata msingi mzuri kama tunavyosema tu nyumba nzuri ni msingi, mwanafunzi akianza hapa chini basi akienda huko juu ameshajii marisha na ameshajitambua. Naomba sana tuwaanzishie wanafunzi hawa msingi mzuri ili huko wanakoenda sasa waweze kwenda kufanyakazi wakiwa wanajua wanafanya nini. Siku zote elimu haina mwisho, hata wale ambao wameshamaliza *Masters* wanakwenda kwenye ajira lakini pia wananyanyasika labda kwa vile hawana uzoefu. Naomba ule muda wa kwenda kufanya *field* weze kuandikwa kwenye vyeti vyao kwamba amefanya *field* mahali fulani na amekuwa na ufaulu wa kiasi fulani. Kwa sababu mwanafunzi anapokuja kua-*apply*kazi kwa mara ya kwanza, swali linakuja ana uzoefu ama *experience* gani? (*Makoff*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. (*Makoff*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Aisharose na Mheshimiwa Mary Chatanda ajiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Lakini pia niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yao nzima kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya, ningependa kushauri katika baadhi ya maeneo ambapo ushauri huu ukizingatiwa naamini kwamba tunaweza kuleta mabadiliko makubwa katika sekta hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunahitaji kuwekeza zaidi katika *vocation training* yaani katika masuala ya ufundi wa hasa katika shule zetu za *VETA*. Mwaka 2014 Serikali ilileta hoja Bungeni kwa dharura kwamba ilikuwa inahitaji kutumia zile fedha za *Skills Development Levy (SDL)* ile *four percent*; asilimia mbili iende kwa ajili ya kusaidia kutoa mikopo kwa wanafunzi kipindi hicho hali ilikuwa ni mbaya na kweli ilisaidia Watanzania wengi. Sasa kwa ajili ya urejeshwaji wa ile mikopo ni mzuri sana na unakusanya fedha nyingi, naomba ile *two percent* ambayo inaenda kwenye Bodi ya Mikopo ya *Skills Development Levy* irudi sasa na ile asilimia zote nne ziweze kutumika kwenye *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* yetu bado tunaenda na mfumo ule wa zamani teknolojia ya zamani, leo hii kwa sera yetu ya viwanda tunahitaji kuwa na mafundi mchundo (*technicians*) ambapo leo hii wengi wenye *degree* tunao, lakini hao ngazi ya *technicians* hatuna kabisa yaani ni wachache mno. Sasa ni vizuri *VETA* zote zikaboreshwaa kwanza kwa vifaa na vifaa vingi vinatakiwa tubadilishe pia mfumo uendane na masuala ya *IT*, leo hii hata fundi wa umeme wa nyumbani, fundi wa magari suala la kupima na ile teknolojia ya zamani imepitwa, leo hii ni lazima wajue namna ya kufanya *programming*, kwenye magari yote ya kisasa lazima unaenda pale unatumia *diagnostic equipment* ambapo *VETA* zetu hazifundishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa majumbani kote siku hizi unaona kuna *sensors*, watu kama hawajui ku-*program* hata akipata ufundi pale *VETA* akitoka mtaani hatapata kazi kwa sababu ni masuala ya kutumia *IT*. Kwa hiyo, ni vizuri tuwe na *transformation* kubwa, mabadaliko makubwa kwenye *VETA* kwenda na wakati na njia pekee ya kwenda na wakati na kuwekeza zaidi na kuwekeza zaidi kunahitaji fedha kwa hiyo, ile asilimia mbili ambayo inakwenda Bodi ya Mikopo tuirudishe ije huku na *VETA* ikifanya vizuri Watanzania wengi watakuwa wanaweza kujajiri kwa sababu Serikali haina uwezo wa kuajiri watu wote ambao wanahitimu vyuo. Sasa ni vizuri tukahakikisha kwamba *VETA* zetu zote zinapata, ile fedha na irudishwe na ziboreshwwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ile programu ya *entrepreneurship* iweze kurudishwa, mafundi wetu ambao wamejifunza wenyewe kwa kufanya *practicals*, yaani kujunga na maeneo mbalimbali na mafundi wenye uzoefu sasa waweze kufanya programu ndogo ndogo za muda mfupi ili na wao sasa wahitimu na wawe na vyeti na wanaweza kujiedeleza kusoma. Kwa hiyo, suala la *VETA* ni muhimu sana.

Mheshimiwa, lakini lingine ilikuwa ni suala la kuhakikisha kwamba tunakuwa na mfumo wa kuhakikisha masuala ya utafiti yanapata fedha, kwa sababu masuala ya sayansi na teknolojia yako katika Wizara hii, mimi nilikuwa napendekeza ule mfumo, kwa mfano, ile pesa ya *TTMS* ambayo ilikuwa *COSTECH*, leo hii ile fedha imeondolewa kwa sababu *COSTECH* imehama Wizara sasa haipo kule kwenye wizara nyininge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tuangalie na vyanzo vingine kwasababu ahadi huko ilikuwa tupate *one percent* ya bajeti nzima kwenda kwenye utafiti lakini ikashindikana, tukaahidiwa kwamba itakuwa bilioni thelathini; lakini hata hiyo kwenye bilioni thelathini fedha iliyokwenda kwa *maximum* ni bilioni kumi na mbili. Na kwenye utafiti mbali na tuseme upande kilimo tu ambao unahitaji zaidi ya bilioni thelathini kwa haraka lakini utafiti wa mambo mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyio suala la kupatiwa fedha kwenye mfuko wa utafiti yaani *COSTECH* ni muhimu sasa Serikali wakati tunakuja kwenye *finance bill* tuwe na vyanzo mbadala na vyanzo vingine ili tuhakikishe kwamba tunafanyaje ili angalau kwa mwaka waweze kupata si chini ya bilioni mia moja ili tuweze kusaidiana katika masuala mbalimbai ya utafiti; na bila utafiti hakuana kitu ambacho kitawenza kuendelea ndani ya nchi hii. Kwa hiyo ninaomba wakati Waziri anapokuja basi watueleze kwamba wamepanga vipi, kwamba suala la *COSTECH* kupatiwa fedha za kutosha ili tuweze kwenda kwenye utafiti mbalimbali tunaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilikuwa binafsi naipongeza Serikali kwa kuanzisha mfumo huu wa kuboresha zile shule za zamani; na nilikuwa pia naomba muanze kuifikiria Shule ya Sekondari Gidas. Ni shule ambayo ilikuwa ni *middle school* enzi hizo, imejengwa 1947 nayo muifikirie. Lakini pia Wizara mnapopanga fedha kwenda kwenye shule mbalimbali za kuboresha muangalie Wilaya zenye shule nyingi na idai kubwa ya shule, isifanane na Wilaya ambazo zina shule chache yaani uwiano kati ya Wilaya ambazo zina shule nyingi na zile ambazo zina shule chache pia fedha ziende kwa uwiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda Serikali illiangalie, niipongeze Serikali kwa kukubali kuwa na *PPP* kwenye mambo ya vyuo. Chuo cha kwanza cha *PPP* kiko Babati, Mamire pale. Ni mpango mzuri ambapo kwa kushirikiana na wadau mbaimbali wa *private sector* ambapo Mheshimiwa Jenista aliweza kuja kuzindua kile chuo mwaka juzi, nampongeza kwa hilo, alichukua mammuzi magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mngeweza kujifunza kutokana na Mamire, nina uhakika kabisa hivi vyuo vingine vyote ambavyo Serikali hamuwezi kufanya pekeenu, hebu mjifunze kutokana na hii *PPP* mnawenza kupata *partners* kwenye vyuo vyote, kama tunavyofanya kwenye afya, kwa kushirikiana na taasisi za dini. Kama mnaona hiyo moja ni

nzuri, hiyo ya Mamire basi inaweza kuwa ya mfano. Vyuo vingine vyote vyua ualimu na vyuo vikuu vikaingia kwenye *partnership* ili vizweze kusaidiwa na Serikali kwa namna ya kuboresha vyuo hivyo na namna ya kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo ni muhimu sana; nilikuwa naomba Serikali ifikirie, Chuo Kikuu cha Sokoine, Chuo pekee cha Kilimo hapa Tanzania, nilikuwa naomba kiondoke kweye Wizara ya Elimu kirudi Wizara ya Kilimo kwa sababu Wizara ya Elimu wanafanyakazi nzuri. Wao vyuo vyote ni sawa kwao, watoto kwao ni sawa lakini ikipelekwa Kilimo kwa sababu ndio wenyewe uhitaji na wahitimu wa pale wote ndiyo wanakwenda kwenye sekta hiyo ya Kilimo, mifugo, uvuvi na masuala ya misitu, wao wataionea umuhimu na watakuwa wanaisimamia kwa ukaribu zaidi.

Kwa hiyo, ningeomba ninyi mbaki kwenye sera lakini Chuo Kikuu hiki cha Sokoine mkrudishe Wizara ya Kilimo ili Wizara iweze kusimamia vizuri na mtaona kwamba ubora wa elimu pale na namna ya kusimamia na namna ya kufanikisha matokeo yatakuwa ni bora zaidi kwa sababu wao ndiyo walengwa na wao watakuwa na moyo zaidi wa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Aisharose Matembe na Mheshimiwa Mary Chatanda ajiandae

**MHE. AISAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema. Naipongeza Serikali kwa bajeti nzuri waliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu kwa mustakabali wa elimu ya vizazi vyua sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo bajeti hii itatekelezwa ipasavyo tuna imani kubwa kwa Watanzania kunufaika na mfumo wa elimu ya sasa. Hata hivyo kuna maeneo ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo ili kuhakikisha tunayaboresha na pia vilevile kukuza kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mafanikio makubwa ambayo yamefikiwa kwa kipindi kifupi katika sekta ya elimu lakini bado kuna changamoto ambazo Serikali inatakiwa kuzipatia ufumbuzi. Eneo la kwanza ambalo ningependa Serikali ilifanyie kazi kwa haraka ni uhaba wa walimu na miundombinu isiyokidhi mahitaji kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi nchini ukiwemo Mkoa wangu wa Singida kuna uhaba mkubwa wa nyumba za walimu. Kwa mfano, kwa Mkoa wa Singida pekee una uhaba wa nyumba za walimu 1,986 jambo hili linasababisha walimu wengi kuishi uraiani ambako hakuna utulivu na pia linawavunja moyo wa kuweza kuwafundisha wanafunzi wetu inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha hotuba ya Waziri wa Elimu ukurasa wa 89, *TEA* imetenga shilingi bilioni 9.7 kwa ajili ya kazi mbalimbali zikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu, mabweni pamoa na matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mkoa wa Singida upewe kipaumbele kwani una uhaba mkubwa wa nyumba za walimu, vyumba vyaa madarasa na matundu ya vyoo. Vile vile Mkoa wa Singida unakuwa kwa kasi sana na Jiografia yake ni ngumu na maeneo mengi hayafikiki kwa urahisi. Kwa mfano shule ya msingi ya Mangoli iliyopo Jimbo la Manyoni Mashariki ipo umbali wa kilometra 137 kutoka Manyoni Mjini. Shule hii ni nyumba moja ya mwalimu yenye vyumba vivili, imapelekea kuvunjika kwa ndoa za walimu hao kwani upande mmoja wanalala wake zao na upande mwingine wa nyumba hiyo wanalala walimu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii kweli walimu wetu wataweza kuwafudisha wanafunzi kwa umakini?

Mheshimiwa Ndalichako nakuomba ulichukulie suala hili kwa umakini mkubwa kuweza kuhakikisha nyumba za walimu zinapatikana kwa wingi. Pia naishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa nyumba za walimu, mabweni pamoja na matundu ya vyoo na uende sambamba na ujenzi wa vyoo unaozingatia sehemu za kujihifadhiwanafunzi wa kike wanapokuwa katika siku zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lenye changamoto kubwa ni uhaba wa walimu na hasa wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari. Kwa kuwa nchi yetu kwa sasa inaelekea katika uchumi wa viwanda, na tunahitaji kuzalisha wataalam wengi ambao watakuja kuviendoesha viwanda hivi, ningeomba Serikali ilichukulie jambo hili kwa umakini mkubwa. Kwa mfano kwa Mkao wa Singida tu una uhaba wa walimu wa sayansi 660 katika shule zetu za sekondari na kwa upande wa shule za msingi kuna uhaba wa walimu 3,947 kwa masomo ya sayansi na sanaa. Naishauri Serikali iangalie utaratibu wa uhakika wa kuzalisha walimu ili kwenda sambamba na mipango ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa mkakati wake wa kusambaza vifaa vya maabara katika shule zetu za sekondari, ni mpango mzuri na ninaomba uwe endelevu. Kwa kuwa kwa mwaka 2017/2018 kuna shule za sekondari kwa Mkao wa singida ambazo hazijapata vifaa vya maabara ninaomba Serikali iangalie jambo hili basi ipeleke vifaa vya maabara katika shule zetu za sekondari kwa Mkao wa Singida. Ninawapongeza sana wananchi wa Mkao wa Singida kwa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa maabara na pia vilevile ninaiomba Serikali iweze sasa kuona umuhimu wa kumaliza maabara zile ambazo zimefikia maeneo ya *lenter*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali iuangalie kwa jicho la tatu Mkao wa Singida kwani una uhaba mkubwa sana wa vyumba vya madarasa. Kwa shule za sekondari tu kuna uhaba wa vyumba 122 na kwa shule za msingi kuna upungufu wa vyumba vya madarasa 4,849.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru Kampuni ya *Tanga Cement* ambao wamekuwa msitari wa mbele kusaidia jamii kuboresha miundombinu ya elimu. Ahsanteni sana *Tanga Cement* na nawaomba muendelee na moyo huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naipongeza Seriakli kwa mkakati mpya wa kuwasaidia vijana ambao wako mitaani kupata mafunzo ya ufundi kwa njia ya vocha kuitia Bodi ya Mikopo na Mkoaa wangu wa Singida ni mionganoni mwa Mikoa minne ambayo imeanza kutekeleza mpango huo. Lakini changamoto iliyopo ni kwamba fedha za mafunzo ya ufundi kwa vitendo kutoka bodi ya mikopo hadi sasa bado hazijapelekwa. Ningiomba Serikali ifanye haraka kupeleka fedha hizo kwa vijana hao zaidi ya 200 wapo stranded na sasa hawasomi kwa vitendo masomo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nawapongeza Mheshimiwa Ndalichako, Mheshimiwa Ole Nasha na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu. Nawapo moyo, endeleeni na moyo huo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Chatanda atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiande.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nichukue nafasi hii kuunga mkono hotuba ya Waziri, aliiwasilisha vizuri na nimpongeze na nimtake asife moyo kwani Roma haikujengwa kwa siku moja. Hizi changamoto na mambo mengine yote yanayozungumzwa kwa maana ya kuchangia na kushauri ayachukue kama ni sehemu ya changamoto kuweza kuyafanya kazi. Kama ambavyo nimesema Roma haikujengwa kwa siku moja basi mtaendelea kuyafanyiakazi kadri siku zinavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze yeye Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ya Elimu kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Wizara hii ni ngumu na ni nzito, lakini kwa sababu imekabidhiwa kwa Profesa na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais inawezekana aliona kwamba amkabidhi Profesa Mama Ndlichako kwa sababu amebobeia katika masuala hayo ya elimu anaweza akasaidia kuendelea kuiboresha elimu katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kumshukuru sana na kuishukuru hii Wizara. Shule ya *Korogwe Girls* ilipata tatizo la kuunguliwa na bweni, lakini walipopata taarifa waliweza kuja kutushika mkono, wakatusaidia na kuhakikisha kwamba lile bweni linarejea ili kuusudi watoto waweze kukaa na kuendelea na masomo, tunawashukuru sana kwa huduma ile mliyotpatia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee kushukuru vilevile kwamba shule ile ni kati ya shule ambazo ni shule kongwe ambazo zimepewa fedha za ukarabati. Nalo hilo naendelea kushukuru, tunashukuru sana, isipokuwa labda niombe tu kwamba shule ile ya *Korogwe Girls* ipo katikati ya Mji wa Korogwe na ni shule ya wasichana. Sisi wenyewe tumeanza kwa jitihada zetu kujenga uzio ili iweze kuwa ndani humo hasa ilizingatiwa kwamba ni watoto wa kike wale lakini humo ndani kuna wenyewe ulemavu Waziri mwenyewe unafahamu. Nilikuwa naomba sana Mwenyezi Munguakupe wepesi katika haya nitakayokuomba ikiwezekana mtusaidie angalau tuweze kumaliza uzio wa shule ile ili watoto wale wa kike waweze kukaa mle ndani. Eneo lile ni kubwa sana kwa maana ile kazi tulioianza sisi wenyewe tutashindwa kuimaliza, kwa hiyo ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri ulione hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ya jana pamoja na kwamba inawezekana wengine haikuwapendeza lakini kwa maeleo yake mazuri jinsi nilivyokuwa nimemksiliza mimi, nimeamini kabisa kwamba ana nia nje na Serikali hii, ana nia njema na

wananchi wake wa Tanzania kwahiyo nampongeza kwa hotuba ile alioitoa hasa pale alipozungumza kwamba wako wafanyakazi ambao wamepandisha madaraja lakini walikuwa hawajalipwa zile stahiki zao sasa watalipwa. Ziko stahiki za wafanyakazi ambazo zilikuwa hazilipwi sasa zitalipwa, hiyo ni hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaiomba Serikali kwamba sasa madeni yote yanayohusiana na wafanyakazi maadam Mheshimiwa Rais ana nia njema itakapofika wakati madeni hayo yote na stahiki zao zote waweze kulipwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Shule ya Sekondari Semkiwa ambayo Mheshimiwa Waziri ulikuja ukaiona pale, tuliaku lika ukaja kuweka jiwe la msingi, kwa maana ujenzi wa bweni ambalo sisi tulitumia nguvu zetu na tukalijenga lile bweni kwa ajili ya watoto wetu wa kike. Wazazi wanakushukuru sana Semkiwa. Baada ya kuona ile jitihada ukatusaidia kutupa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bweni lingine shilingi milioni 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda vizuri Mwenyezi Mungu anatusaidia na tuna uhakika kwamba tutalimaliza na ikiwezekana sasa uje ufungue rasmi yale mabweni yote mawili kwa jitihada zako zile ambazo umeweza kututembelea pale na kuweza kutuongezea. Ila nikikumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba ultuahidi pale vitanda na magodoro pale lile bweni ilikuwa ni vitanda 48 na magodoro 48, kwa lile bweni ambalo tulikuwa tumeshalijenga. Ni matumaini yangu kwamba utatusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikuombe tena Mheshimiwa Waziri kwamba nina Shule ya Sekondari Mgombezi iko nje ya Mji wa Korogwe, ina vijiji sita. Nina shule ya Chifu Kimweri iko nje ya Mji wa Korogwe, ina vijiji vitano. Watoto wa kike wanatembea kilometa nne mpaka tano kwenda shule tena kwenye makatani, mnajua kule kuna mkonge, kwenye mkonge mule kwenda shule na kurudi, nilikua naomba sana. Kwa mfano Mgombezi, kule Mgombezi

tayari tumejenga bweni moja, sasa kama utatusaidia kutuungeza bweni lingine ili watoto wa kike hawa waweze kukaa na kusoma wakiwa pale shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii ya Chifu Kimweri tumeshaanza kujenga bweni. Nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa shule hizi mbili ambazo zina umbali mrefu wa watoto wa kike kutembea, niwaombe sana, mimi najua Mwenyezi Mungu atakupa wepesi tu katika haya ninayoyasema ili angalau uweze kunisaidia hizi shule mbili ambazo ziko mbali sana nje ya Mji watoto wa kike waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Nwenyekiti, suala la upuandishwaji wa madaraja; mimi nashukuru zoezi hili sasa linamuelekeo sasa kuendelezwa. Sasa niombe basi mna ile tabia ya kuwapandisha madaraja halafu hamuwapi zile fedha kulingana na madaraja yao. Niombe liende sambamba, mtu akipandishwa daraja basi liende sambamba na haki yake ile anayostahili kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kuanza kujenga Chuo cha VETA pale Korogwe, tuna eneo kubwa sana kule Mgombезi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Kwanza nianze kwa kusema kwamba kama Taifa tunahitaji mjadala mkubwa sana kwenye sekta ya elimu. Elimu yetu inapitia kipindi kigumu sana, elimu ya Tanzania

inapitia kipindi kigumu na hili limethibitishwa hata na Rais wa awamu iliyopita Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete; na hili pia limethibitishwa na Rais ya awamu ya nyuma Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Tusiitazame elimu katika sura ya kutoa ajira peke yake ni vyema tukaitazama elimu katika sura pana hasa sura ya kichumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote ambazo ni magwiji kiuchumi siri kubwa wali-*invest* kwanza kwenye sekta ya elimu. Taasisi zote, mamlaka zote za kiuchumi na za kifedha zinathibitisha kwamba elimu ndiyo sarafu ya dunia. Kwa sasa tafsiri yake ni kwamba elimu ndiyo inayoshikilia uchumi wa dunia kwa sasa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nchi ambazo zimeshaendelea ambazo siri yao kubwa ni kwenye sekta ya elimu, walli-*invest* kwa kiwango kikubwa mfano ni China. Mwaka 1970 alikuwepo Rais mmoja anaitwa Deng aliwhahi kupiga simu saa tisa usiku akampigia Rais wa Marekani Jimmy Carter akimuomba apelike wanafunzi 5,000 kwa ajili ya kupata mafunzo kwenye teknolojia kwenye vuo vya teknolojia. Jimmy Carter kwa kuona umuhimu wa simu ile usiku akamwambia badala ya wanafunzi 5000 lete wanafunzi 1,00,000. Alifanya vile kwa sababu pia kwanza alihisi huenda kuna uvamizi kwenye nchi yake, lakini kwa umuhimu wa muda ule kupigiwa simu ile akaona yule mtu amethamini sana suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Trump analalamika kwamba China wanaiba teknolojia, anashindwa kujua kwamba ilikuwa ni mpango wa China wa miaka mingi baada ya wanafunzi kupelekwa Marekani kupata elimu. Dunia inakwenda kwa kasi sana, ni lazima tuende na kasi hiyo kwa sababu bila kufanya hivyo tutaendelea kuwa wasindikizaji. Nimesoma moja ya jarida la *Harvard Business* la Mei 2017 linaonesha kwamba kwa miaka 10 mfululizo kuanzia mwaka jana kutakuwa na *capital flight* ambayo imeanzia Marekani ikaenda China sasa inatoka China inakuja Afrika, inakwenda kutengeneza ajira takribani milioni 85 mpaka milioni 100. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kama Taifa tumeandaaje vijana wetu kwa ajili ya fursa kama hii? Kwa sababu hii *capital flight* kwenye *manufacturing sectors* ambayo itakuja Afrika kama vijana wetu wangekuwa na uwezo ambao wakiwa *skilled* wakiweza ku-*compete* kwenye sekta ya ajira mionganoni mwa vigezo vikubwa ambavyo vitaweza kutumika kwenye mitaji hii ambayo itakuja Afrika ni pamoja na wafanyakazi kwenye nchi husika wakiwa na wafanyakazi ambao watakuwa ni *skilled*. Ninasikitika kwamba kwa Tanzania tunaweza kukosa fursa hii kwa sababu ya kuendelea kupuuza sekta ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inapambana kutengeneza *Stiegler's Gorge*, wakati Serikali inapambana kutengeneza *standard gauge* kama njia za ku-*influence investment, don't forget about education*. Hii ni sifa mojawapo kubwa ambayo wawekezaji wengi wanaitumia wanapokwenda kuwekeza. Nisikitike zaidi kwamba elimu yetu imefikia hatua kwamba unaweza ukakuta kwamba *graduate* anashindwa kuandika hata sentensi moja kwa lugha ya kiingereza. Unaweza ukakuta *graduate* anashindwa kuandika barua ya kuomba kazi kwa Kiswahili anashindwa kuandika *format* haya ni majanga ambayo kama taifa tunaendelea kutia aibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kadhaa ya kuishauri Serikali. Moja Serikali ni lazima muongeze juhudhi za kufanya *auditing* kwenye *education*, mfanye ukaguzi wa kina, na uwe katika *international standard* kwa sababu kunaonekana kuna kizungumkuti sana kwa wakaguzi wetu hata hawa wakaguzi wanaofanya ukaguzi wanapashwa kufanyiwa ukaguzi pia, hii ni kwa sababu inaonesha kuna mapungufu makubwa sana katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo nataka kuishauri Serikali ni kwamba mchujo wa ufaulu wa wanafunzi ni lazima uzingatie uwezo wa wanafunzi, msifanye siasa kwenye hili. Leo *division* kesho *GPA* sijui kesho kutwa kitu gani!

Wale wanaostahili kufaulu wafaulishwe wale wanaofeli wafelishwe, tusianze kufanya siasa kwenye elimu. (*Makofi*)

Suala la tatu, Serikali lazima mu-*invest* kwa nguvu kubwa kwenye elimu ya kati, ile fedha ya *skills development levyambayo mmeitoa na kuipeleka kwenye mkopo wa elimu ya juu irudisheni VETA*. Hii elimu ya kati inakufa, huu uchumi wa viwanda nani anaenda kufanya kazi hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu Serikali mnapaswa muwakumbuke. Moja ya vitu ambavyo Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu ya Tano mnakosea ni kusahau walimu wetu. Serikali hii imepuuza walimu, Serikali hii inanyanya walimu, Serikali hii haioni mchango wa walimu, Serikali hii haioni kama kuna umuhimu wowote wa kuwasaidia walimu. Kenyatta hapa ameongeza asilimia tano mishahara ya wallimu, ninyl mnaona walimu kama *using machine, I don't know mnawaonaje walimu wetu wa Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba muwakumbuke walimu wetu hawa, muwakumbuke na muwathamni kweli kwa sababu wao ndio chanzo cha maendeleo yoyote ya kiuchumi kwa sababu kuititia elimu wanayoitoa tunaenda kupata watu ambao ni *productive*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye Chuo cha *UDOM* na na-declare *interest* mimi ni mwanafunzi wa pale namalizia *masters* yangu pale. Hiki chuo kilikuwa kina mpango wa kusajili wanafunzi mpaka 40,000; lakini mpaka sasa wamesajiri wanafunzi 25,000 tu, na wanashindwa kufanya mwendelezo kwa sababu ya ninyi kwenda pale kuweka Wizara zenu sita. Haijulikani mnaondoka lini haijulikani mko pale, yaani hamjielewi. Chuo cha *UDOM* wakati kinajengwa *planning* yake haikuzingatia kwamba kuna Wizara sita zinakwenda kukaa pale, barabara ambazo ziko *UDOM* ninyi mnajua wanafunzi wanakoishi na madarasa yalipo kuna umbali wa *kilometers...* (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunaendelea Mheshimiwa Susan Lyimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hongoli na Mheshimiwa Waitara.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii muhimu na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu sana ya elimu hasa kipindi ambapo kumekuwa na changamoto nydingi sana. Nishukuru sana kwamba Wabunge wote nadhani tunakubaliana kwamba suala la elimu sasa hivi ni janga la Taifa kwa sababu tunashuhudia mambo mengi yanayotokea na kubwa niseme kwamba katika elimu siku zote nimesema mwalimu ndio kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa masikitiko makubwa sana Serikali bado haijaliona hilo. Leo walimu wana matatizo lukuki, yamesemwa na wengi. Kuna suala la kupandishwa madaraja, haiwezekani mwalimu alitakiwa apandishwe daraja toka mwaka 2003 mpaka leo yuko pale pale ameenda kusoma bado hajapandishwa daraja na hawa ni wengi na ndiyo sababu takwimu zinaonesha kwamba takribani asilimia 70 hawana *morale* wa kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi mishahara yao bado lakini niseme tu kwamba lingine kubwa katika elimu ni vitabu na mitaala. Huwezi kuwa na vitabu mizuri kama huna mitaala mizuri. Mwaka jana kipindi kama hiki nilliongea na watu na wengine walichangia kuhusiana na ubovu wa vitabu katika nchi hii, jambo ambalo linafanya watoto wetu washindwe kusoma vizuri. Kwa sababu tayari walimu hawana *morale*, kwa hiyo *the only alternative* tungekuwa na vitabu vizuri wanafunzi hawa wangeweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kitabu kinachoitwa kitabu cha uraia na maadili bendera ya Tanzania, kitabu cha darasa la tatu, ile rangi ya manjano zinaonekana mbili kule wameweka nyeusi yaani leo bendera ya Tanzania mtoto mdogo ambaye ubongo wake ni tete na kila anachoambiwa kina *stick* bendera ya Tanzania imebadilishwa, nembo ya Tanzania haina zile alama za shoka

hazipo. Bendera iliyopo na nitaomba mtuambie hii ni bendera ya nchi gani. Bendera yenyе rangi za kijani mbili chini na juu hamna rangi ya *blue* na katikati rangi nyeusi na hizo njano naomba mtuambie hii ni bendera ya nchi gani? Ukija kutujibu utuambie Mheshimiwa Waziri na Naibu wako, mmewahi kukaa mkapitia hivi vitabu baada ya kuambiwa bilioni zaidi ya mia moja zilitumika mwaka jana na baada ya kuongea sana na aliyekuwa kamishina akaondolewa kazini; ninaomba kujua mmeefanya mambo gani au utaratibu gani kama Waziri ni kweli umeona hivi vitabu wewe mwenyewe kama profesa umeviona hivi vitabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha kuandika darasa la kwanza mtoto ambaye katika elimu yake ya awali hajasoma kitabu hakuna kitabu chochote cha shule ya awali, hakuna, anaenda kuanza darasa la kwanza kuandika kitabu cha *page 117* lakini mbaya zaidi analngia la pili kitabu cha *page 40*; *what a contradiction?* Yaani wa darasa la kwanza ambaye ndio anaanza *page* mia moja na zaidi, wa darasa la pili *page 40*. Darasa la kwanza kuandika anaenda siku ya kwanza kuandika anaandika hii; hii anaandika kitu gani? Hili ni somo la kuandika au ni sanaa?

Mheshikiwa Mwenyekiti, haya mambo haya ndio sababu tunasema hatuwezi kukuabaliana na hili jambo, Nataka Waziri aniambie, tulikuwa na kitu kinaitwa *Educational Material Committee (EMAC)* ambao hawa ndio ambao walikuwa wanahariri vitabu na *committee* ikavunjwa kutokana na mambo fulani, mimi naomba kujua baada ya Kamati hii kuvunjwa ni nani wame-replace na ni nani wanahariri hivi vitabu katika hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio sababu ninasema, na watu wamesema; na ninaomba Wabunge wote waende wasome andiko la Profesa Kasmili Lubagumya waone ni jinsi gani elimu yetu ni mbovu kuanzia huku chini na mimi sishangai *university level*/wakishindwa kuandika barua, aidha ya kiswahili au ya kiingereza kwa sababu huku chini hawakufanya chochote. Huwezi ukaamini wanafunzi wa *UDOM* anaulizwa jina la Makamu wa Rais hajui. Sasa

unajiuliza kama mwanafunzi hajui Makamu wa Rais wa nchi hii, mtoto wa darasa la kwanza la pili hatajua sisi tulivyosoma ilikuwa tunajua yaani kila kitu kilikuwa hapa. Sasa katika hali hii ninaamini Waziri mmeamua sasa kuchukua kwamba nchi hii tunaendeshwa na *machivelian principle* kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** ...jamii yetu ni kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee Serikali ya Chama cha Mapinduzi...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** ...imekuwa ikiongeza sana kuhusu; na kila Mbunge wa CCM anayesimama anazungumzia kuhusu...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Huwezi ukamilazimisha nimekataa.  
*(Kicheko/Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** ...inaendelea kuzungumza kuhusu elimu bure. Naomba tusijitoe ufahamu, maana ya bure ni nini? Wakaanza ni bure tulivyopiga kelele wakasema bila malipo, lakini ukisoma kamusi bure maana yake ni kitu kinachotolewa bila malipo yoyote. Ukituba ya Waziri Mkuu inasema hivi; "wataendelea kuchangia kwa hiari maendeleo ya elimu kuitia ofisi ya Wakurugenzi" na kwa wale watu wenye miaka yangu na nyuma tunajua Mheshimiwa Chenge ulisoma enzi hizo kwamba tulivyokuwa elimu bure ilikuwa hata kalamu hununui, daftari hununui ilikuwa sana sana ni *uniform*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo mnapotuambia ni bure wakati michango inaendele haiwezekani na niseme tu

kwamba ndiyo sababu shule za *private* zinafanya vizuri; na Mheshimiwa Waziri nilkuambia na ni rafiki yangu. Kinachofanyika wana kitu kinaitwa *Teachers Parent Association* yaani huwa utatu huo ndio unaosaidia mnakutana wazazi, walimu na wanafunzi, kama mwanafunzi ana tatizo linaleezwa lakini kwenye shule za Serikali sana ni le bodi ambayo inasubiria shilingi 500 jinsi gani inaenda kugawanywa shulenii, ni vurugu tupu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nadhani hili suala la elimu bure bado halijakaa vizuri na limeleta mkanganyiko mkubwa hivyo inaweza kwa kweli kurudisha maendeleo ya elimu nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala kubwa hili la mjadala. Sasa niseme, katika hizo changamoto zote nionaomba sasa, kwa heshima kabisa kwamba tumesema *report* zangu zote au *speech* zangu zote tumekuwa tukiongelea suala la anguko la elimu na sasa mnalionia. Mnamshukuru mzee Mkapa, pamoja na maneno yote aliyokuwa amesema dhidi yetu kwamba sisi malofa lakini leo ameona kwamba elimu yetu iko vibaya na kwamba tunaenda sasa kufanya kazi; na naomba muongoze huo mjadala ili tuhakikishe kwamba elimu yetu inaboreshwaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho nililotaka nilzungumze ni suala la *TETRA*. Sisi tumeongea kwenye hotuba zetu hiki chombo huru cha kusimamia elimu, haiwezekani, tumezungumza mara nyingi tukasema lazima tuwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, unga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli na Mheshimiwa Waitara ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa nafasi na mimi niweze kupata kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha utaratibu wa elimu bila malipo, nimpongeze sana kwa Wizara ya Elimu pia kwa kazi ambazo wanazifanya kwa maana ya Waziri, Naibu Waziri na Katibu wa Wizara hii na Makamishna wote na watengaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya ili kuhakikisha kwamba Watanzania wanaweza kupata elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu wameeleza sana Waheshimiwa Wabunge na wameeleza vizuri sana kuhusu elimu kushuka. Mimi niseme kwamba hili suala halihitaji kuangalia upande mmoja, ni lazima Serikali, wazazi na wadau wote tuweze kushirikiana kuhakikisha kwamba ni namna gani tutaboresha elimu yetu. Mheshimiwa Rais ameweka elimu bure ili kutoa fursa kuhakikihs kwamba watanzania wote wanapata fursa ya kupata elimu ya msingi na sekondari. Kwa hiyo sasa kwa kuwa tayari Rais ameshafungua fursa sasa ni jukumu letu sisi wadau, wana taaluma, pia ni jukumu letu sisi Wabunge kuwaelimisha wazazi namna gani ya kuweza kushirikiana na walimu kwenye mashule ili elimu yetu iweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukibaki tunalaumiana hivi hatutaweza kufanikiwa, lazima sisi sote tushiriki katika kuhakikisha kwamba elimu yetu kwenye majimbo yetu na kwenye maeneo yetu inaboreshw. Kwa hiyo, jitihada za kuboresha elimu zinaanza na wewe Mbunge zinaanza na wazazi waliopo katika maneo husika lakini pia kwa kushirikiana na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juu ya elimu hii ya ufundi. Tunaenda kwenye Tanzania ya viwanda ni lazima kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine, ni

lazima tuwaandae vijana wetu. Mimi nafikiri kama alivyoeleza Mheshimiwa Mwalongo alieleza vizuri sana katika mchango wake aliutoa juzi kwamba ni muhimu tuwe na masomo ya ufundi kwenye shule zetu za sekondari, lakini mimi niseme kwamba ni vizuri tuanze mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kwenye kila shule ya msingi ikiwezekana tuwe na darasa la ufundi, wanafunzi wanapokuwa kwenye shule ya msingi wapate stadi za ufundi pale pale shuleni, kama ilivyokuwa zamani. Tulivyokuwa tunasoma shule ya msingi tulikuwa tunajifunza mambo mbalimbali. Kuna shule nyingine tulikuwa tunajifunza useremala, kuna shule nyingine wanajifunza utengenezaji wa vitu mbalimbali na hatimaye tukapata mafundi wengi, mafundi wengi wanaojenga nyumba sasa hivi huko vijiji na maeneo mengine, mafundi wengi wanaofanya kazi za *welding* yaani uungaji wa vyuma, mafundi wengi wanaofanya kazi za umeme wamejifunza wengine toka shule za msingi na wengine wamejifunza sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukiamua kwamba shule zetu za msingi ziwe na angalau wanafunzi wawe wanapata kipind kimoja cha ufundi, nina hakika kabisa tutapata vijana wengie, tutapata mafundi michundo wengi. Kwa hiyo, mimi nitoe rai kwa Serikali, niiombe tubadilishe sera kidogo tuanzisha shule za misingi kule kule angalau kuwe na kipindi cha ufundi toka shule ya msingi, akienda sekondari akutane na darasa la ufundi na hatimaye wengine pengine waweze kwenda kwenye vyuo vingine huko juu. Kwa hiyo, watoto tukiwaanzisha mapema watapenda ufundi na watapenda kusoma masomo hata ya sayansi ili waje kuwa mafundi mazuri baadae. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haiwezekani kuanzisha kwenye shule zote basi angalau kwenye kata tuchague shule moja ambayo itakuwa ni shule ya msingi ya ufundi ili watoto waweze kujifunza pale, na ikiwezekana hata wale wengine wanaokaa maeneo yanayozunguka ile shule wanaweza wakaenda kujifunza elimu ya ufundi pale kwenye ile shule ya ufundi katika kata zetu. Kwa hiyo, tukianzisha

utaratibu huu tutawezesha vijana wetu wengi kwanza kuwa na uwezo wa kujajiri kwa sababu amejifunza ufundi fulani. Kwa hiyo, niombe sana Wizara tujaribu kuchukua mawazo haya ili tuweze kusaidia ili vijana wetu wengi waweze kuenenda na uchumi wa kat, uchumi wa viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea sana juu ya suala la lugha ya kufundishia. Imekuwa ni mjadala wa muda mrefu sana. Tumekuwa tukijadili kwamba *either* tuamue twende kwenye kiingereza au twende kwene kiswahili, na muda mwingu tumekuwa tukifundisha shule za msingi kwa kiswahili lakini wanafunzi hawa wakienda sekondari wanakutana na lugha ya kiingereza. Hii imekuwa ikileta *confusion* kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia watoto wa sekondari walio wengi hawalelewi lugha ya Kiingereza na wengine wakiwa wanajibu mitihani wanaandika kwa kiswahili; na kwa kuwa wameandika jibu ambalo sio lugha rasmi, wametumia lugha isiyo rasmi wamekuwa wakikatwa kwa maana wakipata kosa kwenye yale majibu yao. Kwa hiyo kumbe Watanzania wengi wanaelewa kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kwanini tusiamue sasa tukaanza darasa la kwanza mpaka Chuo Kikuu tukafundisha kwa kiswahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wamesema kwamba tutakuwa tumejifungia, hapana! Mbona nchi hizi zilizoendelea, tumeona China, tumeona Korea wanafundisha kwa lugha yao ya Kikorea lakini ndiyo nchi ambazo tunasema leo kwmaba zinakuwa uchumi kwa kasi kubwa sana. Na sisi tuamue, tusibakie tu kwenye kiingereza, tusibakie tu kwenye hii lugha ya wakoloni, turudi kwenye kiswahili. Tuanze kufundisha kiswahili toka darasa la kwanza, sekondari na hatimaye Chuo Kikuu, naamini Watanzania kwa sababu ni lugha mama wataelewa vizuri na wataweza kujibu majibu kwenye mithani vizuri na ufaulu utapanda kwa kuwa wanatumia lugha ambayo wao wenyewe wanaelewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia juu ya Kitengo cha Udhibiti Ubora. Kitengo hiki cha Udhibiti Ubora kipo hoi, hawana magari, hawana fedha za kujaza mafuta kwenda kukagua shule na tumesema kwamba Udhibiti wa Ubora ndilo jicho la Serikali, ndilo jicho tunalolitumia kuangalia nini kinachoendelea kwenye shule zetu. Niombe sana Serikali iwezeshe kitengo cha udhibiti ubora waweze kupata magari lakini pia waweze kupata fedha za kuweza kujaza mafuta na kwenda kukagua kwenye sule zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ilivyo, kama Halmashauri haina fedha, wadhibiti ubora hawawezi kwenda kwenye shule, hawana uwezo wa kwenda kwenye shule kufanya ukaguzi... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea, Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Migira dakika tano mwishoni yeye.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika eneo hili muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hapa ambapo mwenzangu ameishia. Kumekuwa na mjadala wa muda mrefu sana juu ya ama kutungia kiingerea au kiswahili. Hili ni jambo ambalo kwa kweli Mheshimiwa Waziri, Profesa inatakiwa Serikali ilitolee maamuzi mapema kwa sababu kadri tunavyovuta muda maana yake tunazidi kuchelewa kufanya maamuzi ya mambo yetu na kuweza kuboresha elimu yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nadhani hili ni jambo la muhimu sana kwa sababu wamelifanyia kazi, tafiti zimefanyika, wataalam wameandika na Profesa anajua. Kwa hiyo si jambo la kuvutana tena, aje atueleze nini msimamo wa Serikali, tunafanyaje? Tunaamua kutumia kiingereza

kufundisha kutoka chekechea mpaka Chuo Kikuu au tunaamua kutumia kiswahili? Tuamue ili tusiwe na *double standard* katika elimu yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningombwa Mheshimiwa Waziri atusaidie, nimesoma bajeti yake ambayo ameleta kwenye Bunge hili tukufu ili tuijadili, na bahati nzuri huyu ni mwalimu. Lakini jana wafanyakazi wa nchi hii popote walipokuwa, hata wagonjwa waliamka vitandani wakakaa wakitazama kumsikiliza Mheshimiwa Rais kwamba angalau kwa sababu aliwaahidi kwamba ataongeza mishahara angeweza kusema neno jana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa bahati mbaya sana ameeleza mipango mingi ya Serikali, lakini hakusema ataongeza mishahara kwa watumishi lini na hasa walimu ambao wamekuwa na malalamiko kwa muda mrefu sana. Hili ni jambo ambalo kwa kweli na ile *speech* ya Rais Mheshimiwa Magufulি Rais wetu wa Tanzania na Rais wa Kenya ziliwekwa pamoja *parallel*, kwa hiyo, wakawa wanalinganisha kwamba Uhuru Kenyatta ye ye ameongeza asilimia tano, lakini sisi tunasema tunaangalia kwanza, tunatoa ahadi mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kumbukumbu ziwe sawa. Rais aliwaahidi wafanyakazi ataongeza mshahara mwaka jana mwezi wa tano, sasa mwaka huu tena ameenda kuahidi kwa hiyo nadhani mumsahauri vizuri, kama jambo haliwezekani, hilo jambo lisitamkwe, watu wanakuwa na matumaini hewa...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ...hilo ni jambo la msingi sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naam!

**MWENYEKITI:** Hebu kaa kidogo utulie. Hivi wewe unataka kuliaminisha Bunge na Watanzania kwamba jana Mheshimiwa Rais alitoa matarajio hewa kwa Watanzania na watumishi wa Tanzania? Hapana, alisema hali ya uchumi itakaporuhusu atafanya hivyo. Mimi nakuomba sana, changia tu hoja yako lakini usilete hizi kebehi kebehi. Mheshimiwa endelea. (*Makofii*)

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesema kwa sababu alishahidi mwaka jana sasa mwaka huu au kama jambo haliwezekani lissemwe, watu wanabiri. Nadhani ujumbe umeleleweka kwamba ahadi zitolewe pale inapowezekana, maelezo mengine yameleleweka na mimi nimekuelewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina shida kubwa sana ambazo Mheshimiwa Waziri alipaswa atueleze kwenye bajeti hii. Kwa mfano, kumbukumbu zinaonesha kwamba tuna shida mpaka ya matundu ya vyoo katika nchi hii. Kwa mfano shule ya msingi peke yake kuna upungufu wa matundu ya vyoo 239,716, kwenye bajeti ya waziri anaonesha kwamba watajenga matundu ya vyoo ambayo ni asilimia 0.73 ndiyo yatakayojengwa kwa mwaka huu wa fedha. Sasa nimejaribu kupunguza hapa hayo ni matundu 2,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 lakini ukipunguza hapa kwa matundu 239,000 maana yake tuna upungufu wa matundu ya vyoo 235,000 bado unaweza ukaona shida ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la madarasa, kwenye bajeti anaonesha kwamba mwaka huu atajengwa madarasa 2,000, lakini shule za msingi peke yake tuna upungufu wa madarasa 107,000 ukipunguza maana yake tunadaiwa madarasa 107,000. Nyumba za walimu, upungufu uliopo unaonesha shule za misingi 178,435, sekondari 69,816 lakini Mheshimiwa Waziri anasema watajenga nyumba 56. Ukitafuta asilimia ni 0.023, ndiyo asilimia itakayojengwa. Kwa hiyo ningedhani kwamba malalamiko ya wananchi na

walimu na wadau ni kwamba inatakiwa tuoneshe hizi kero zilizopo tunapunguza kwa kiwnago gani? Kama unapunguza asilimia 0.02 kwa kweli sio sawasawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine masomo; kwa maana ya upungufu kwa somo. Kama unaambiwa tuna nchi ya viwanda, halafu walimu wa hesabu tuna upungufu wa walimu 7,291, biolojia ni walimu 5,181, kemia 5,377, fizikia ni 6,875; na hapa nichukulie kwa mfano Mkoa wa Dar es Saalam kuna *laboratory technicians* pale mahitaji ni 67 tulikuwa nao mwaka jana saba tu peke yake maana yake hao walimu pamoja na madai yao na mapungufu, changamoto mbalimbali wanafanya kazi ya kufundisha mara mbili na hakuna malipo ya ziada. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo limechagizwa na Serikali, kuhusu elimu ya bure, na mimi nimekuwa nikipingga mara zote kwamba Tanzania hakuna elimu ya bure, kuna elimu imepunguzwa gharama zake. Serikali ilichofanya imeondoa ada, lakini mambo mengine yatabaki na tukubaliane haiwezekani Taifa hili kila kitu kikatolewa bure bure, watu wote watakuwa wazembe, itakuwa ni ulemavu. Kuna wajibu wa wanafunzi wenye wafanye mitihani wafaulu, kuna wajibu wa wazazi na walezi wasimamie na kuna kazi za kufanya, kuna wajibu wa walimu wafanye kazoo yao na kuna wajibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haiwezekani leo kwa mfano shule haina maji wale wazazi wangekaa vizuri pamoja wakajadiliana, wanaweza wakachimba visima shulenii na maji yakaondoka. Kuna upungufu wa madarasa, wangeweza kuchangisha, darasa moja wangechanga billioni 21, una shule ina wanafunzi 2,000 wale wazazi ambao hawana uwezo wangewekwa pembeni, wale wazazi wenye uwezo wakubaliane, jambo hili linawezekana.

Kwa hiyo, mnapowaaminisha wananchi kwamba elimu ni ya bure watu wanabweteka, inawezekanaje watu wawazae watoto wao, wawapeleke shulenii, wakae miaka minne wasichangie gharama hawawajibiki, hili taifa litakuwa

Taifa la wazembe kweli kweli. Huu uzembe, ni ugonjwa ambao unalelewa ambao hatuungi mkono. Kuna watu ambao wanapaswa kusaidiwa na kuna watu ambao wanaweza kufanya kazi hiyo na michango ni ya hiari, wale ambao wanaweza wafanye kazi hiyo, hili jambo si sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaonesha asilimia 60 au zaidi ya wanafunzi ambao wanamaliza *form four* hawa wanapata *division zero, division four*, Wabunge na wananchi wanauliza, hawa watoto baada ya kupata zero na *for* wanaenda wapi? Ndiyo maana inakuja hoja hapa ya VETA, na mnataka watoto wapate mimba katika umri mdogo. Sasa mtoto anamaliza darasa la saba hakwenda sekondari au kaenda kapata zero, hana ufundi wowote hata kufika hawezikupika, hata bustani hawezikulima, hivi vyuo vya ufundi ni muhimu sana. Mheshimiwa Ndlichako haya ndiyo majibu unatakiwa uje hapa utuoneshe, mkakati ukaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu, shule za sekondari na shule binafsi. Mimi ni mwaliimu na nimefanya utafiti mdogo. Shule yangu moja, ni-*declare (to declare)* ilikuwa ya mwisho lkatika shule za Tanzani *form four* mwaka jana, inaitwa Nyebulu Sekondari. Nimeenda shuleni pale walimu wanasesma na mnawazuia *private* wasigawanye, lakini kuna shule za vipaji maalum, maana yake tayari huu ni ubaguzi, wamelekwa pale wenye uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule za mikoa wamepelekwa, kuna shule za kata, hizi za kata ndizo *class c*. Mheshimiwa Ndlichako, kwanza mmetunga maswali ya kuchagua mpaka hesabu na mnataka nchi ya viwanda na nilipowauliza mkasema hapa ni muda, suala sio muda! Kama mtu hana uwezo wa kwenda *high school*, asiende, lakini akibaki mahali uwepo mpango mkakati wa kumsaidia apate uwezo wake wa kuishi. Msipeleke watoto shuleni kisiasa, wazazi wanaamini wameenda shule kumbe kimsingi wamelekwa, unapata asilimia ndogo unaenda sekondari. Miaka minne unakula ugali wa baba na mama, shambani huendi, huchangii Pato la Taifa, unapata zero. Huyu mtoto

atajengewa chuki kwenye jamii yake, watu wanatakiwa wajue, kama huna uwezo wa kwenda sekondari usiende ufanye kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa, unatungaje maswali ya kuchagua ya hesau halafu taifa liendeleee? Unatungaje kazi hiyo? Halafu mnachokifanya katika mfumo wa maswali ya mtihani ana ana ana doo, watoto waansinzia, anaangukia hapa nda! Halafu ninyi mmechukua wanafunzi ambaao hawana uwezo kwenye shule za kata mmerundika kwenye darasa moja yaani asie na uwezo amekaa na asie na uwezo mwenzake, nani anamuuliza mwenzake swalii? Hii ni changamoto, halafu mnataka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa! Mheshimiwa!

**MHE. MWITA M. WAITARA:** ... mambo gani haya mnataka kutuletea hapa. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, unafahamu hili ni Bunge? Nikisema muda wako umekwisha, umekwisha! La pili, narudia, Mheshimiwa Rais mwaka jana hakuahidi. Nasema kama kuna Mbunge hapa na aliyeanzisha hii Mheshimiwa Waitara, kama una ushidi *please* leta mezani hapa, tumalize biashara hiyo. Tuache hayo ya kutumia nafasi hizi na kuanza kuhamasisha mambo ambayo si sahihi. Mheshimiwa Bafadhili, dakika tano.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi napenda niende haraka haraka, nianze na suala zima la walimu waliostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna walimu ambaao wamestaafu hadi leo hawajapewa posho zao za usafiri kurudi makwao. Mpaka leo wamebaki katika vituo vyaa kazi. Sasa

tunaomba Serikali ituambie lini itawalipa mafao yao hayo?  
(*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia kuhusu walimu. Kuna walimu ambao wanadai baadhi ya malimbikizo yao, lakini baya zaidi kuna baadhi ya walimu walismamia mitihani ya darasa la nne na darasa la saba toka mwaka 2015 hadi leo hawajalipwa pesa zao hiso za kusimamia mitihani. Nadhani kosa sio la Wizara lakini naiomba Wizara ihakikishe, iulizie hizi Halmashauri. Nadhani kuna ubadhirifu fulani katika hizi Halmashauri, kwa sabbau pesa zinatolewa, lakini walimu husika hawapewi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu suala la UMITASHUMTA. Wanafunzi wa shule za msingi kuanzia sasa hivi nadhani wako katika michezo hii ya UMITASHUMTA, nadhani Serikali inatoa pesa, lakini bila shaka zile pesa ni kidogo. Kwa sababu kuna baadhi ya shule wako mbali na vituo vinavyofanyika hiyo michezo, hivyo inabidi wapate usafiri wa kwenda kule, kwa hiyo, inawagharimu walimu wao wenyele wajitolee pesa zao kutokana na uhaba wa ile pesa inayopelekwa katika shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hao hao maskini ya Mungu hawana fedha za kutosha kujikimu wao wenyele lakini pia wanaona kheri wawasaidie wale wanafunzi, kwa sababu utakuta mwanafunzi wakati mwingine anatoka nyumbani kwao hajala inabidi mwalimu ajitolee awaununulie angalau hata karanga watafune, pesa ile inatoka mfukoni kwa mwalimu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali inapoandaa hii michezo ya UMITASHUMTA ihakikishe kuwa wanaweka fungu kubwa ambalo litawasaidia walimu kuwawezesha watoto waweze kwenda kucheza ile michezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuna hiki kitega uchumi cha CWT. Enzi hiso tuliambiwa kuwa ni kitega uchumi ambacho kitawasaidia walimu na jengo hili limejengwa Dar es Salaam, llala Boma pale *Mwalimu Nyerere House*. Lakini cha kushangaza sijui kitega uchumi hiki kinawasaidiaje walimu kwa sababu kuna walimu wengine kama sisi

tumestaafu, kuna walimu wengine wamekufa na kitega uchumi bado kiko pale pale. Je, hawa waliostaafu na hawa waliokufa watasaidiwaje na kitega uchumi hiki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mimba za utotoni. Kweli watoto wetu wa kike wanapata mimba, miaka tuliyosoma sisi ilikuwa mtu akipata mimba ilikuwa ni mambo ya ajabu sana, lakini sishangai sana kwa sasa hivi kutokana na utandawazi uliopo. Mambo ni mengi, watoto wanaangalia luninga na wanakuta mambo mengi ambayo na wao wanafanya majaribio.

Ombi langu kwa Serikali, naomba ikiwezekana wafanye *mobile clinics* wawapitie kila wakati watoto wetu wa kike. Kwa sababu mwanafunzi atakapoona, eeh, nitakuwa kila wakati nafuatiiliwa fuatiliwa afya yangu, kwa hiyo ataliogopa lile tendo kulifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile wanafunzi wetu wanapokuwa shulenii wanakuwa ni wengi mno madarasani kiasi ambacho mwalimu anashindwa kusahihisha, anashindwa kuwapa kazi za kutosha na hiyo haitoshi, utakuta mwalimu kutokana na wingi wa wanafunzi, darasa moja ni wanafunzi 80 anachagua baadhi ya wanafunzi wa madarasa ya juu wamsaidie kusahihisha. (*Makofii*)

Hata mitihani inasahihishwa na baadhi ya wanafunzi wa madarasa ya juu. Utakuta mwanafunzi karudi shulenii swali amelipata lakini amewekewa kosa na *markszake* nimekatwa na akienda kwa mwalimu akimwambia, mwalimu, hili swali nimelikosa, anamwambia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa asubuhi hii ndiyo tumejitahidi mpaka hapo, tunaenda vizuri. Mchana tutaanza na Mheshimiwa Rehema Migilla dakika tano, atafuatiwa na

Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso. Tutaangalia, muda ndio huo! Hatujakaa vizuri. Tujitahidi tu, ndiyo maana leo kidogo mmeniona nimekuwa mkali sana mambo ya Mwongozo sikuruhusu kwa sababu yak u-manage muda.

Waheshimiwa nina tangazo, leo Jumatano tarehe 2 Mei kutakuwa na ibada kwa wakristo wa madhehebu ya Kikatoliki mara baada ya kusitishwa kwa shughuli za Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wengine wote wanaopenda kushiriki ibada hiyo mnakaribishwa. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo. Nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha nilitaja Waheshimiwa Wabunge tutakaoanza nao Mheshimiwa Rehema Migilla, Mheshimiwa Edwin Sannda na Mheshimiwa Moshi Kakoso wajiandae. Wewe ni dakika tano tu Mheshimiwa.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi jioni ya leo na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa uhai na afya mpaka leo muda nipo humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri anayofanya na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia lakini ina mapungufu katika baadhi ya sekta zake, nianze na NECTA. Kwa kipindi kirefu Baraza la Mitihani limekuwa

likitunga mtihani wa darasa la saba kwa kutumia aina moja tu ya maswali yaani *multiple choice*. Sasa unapotunga mtihani kwa kutumia *multiple choice* peke ina maana hau-*provide room* kwa huyu mwanafunzi kuweza kujieleza kwa zaidi. Vilevile mtihani wa hivyo haupimi hizi *skills* zingine za *language* kama vile kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili hawa watoto wetu waweze kufanya vizuri na kwenye mitihani ijayo ni lazima basi mitihani itungwe kwa ku-*mix other types of questions* ili mwanafunzi aweze kuwa na nafasi ya kujieleza zaidi. Kwa sababu sasa hivi mwanafunzi anafanya mtihani kwa kutumia aina moja tu ya maswali, swalii la kwanza mpaka la 50 na anafanya tu *betting* kwa sababu anahisi tu kwamba hili litakuwa jibu na kuna wengine wana bahati anaweza akajibu lile jibu na likawa jibu sahihi kweli. Kwa hiyo, naomba wizara iangalie utungaji wa maswali haya ili kuweza kupima *other skills of language* kwa hawa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuangalie namna gani wanavyojibu hii mitihani ya darasa la saba. Wanafunzi wetu wanajibu hii mitihani kwa kutumia karatasi za *OMR*. Serikali imetumia hizo karatasi kwa ajili ya kujirahisishia wao usahihishaji, lakini hawampimi huyu mwanafunzi namna gani anaweza kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi karatasi hazimpi mwanafunzi uwezo wa kuandika zaidi ya kuweka *shading* pale kwenye lile jibu. Unakuta mtoto anafaulu kwenda *form one* ilhali hajui kuandika chochole lakini amefaulu, *this is shame*, naomba Serikali iliangalie suala hilli kwa undani ili watoto wetu waweze kufanya mitihani yao vizuri na waweze kufaulu kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi inakuwaje hadi mtihani wa hisabati unakuwa na *multiple choice*, mtihani kuwa na *multiple choice* ina maana unamsaidia huyu mwanafunzi kuelekea jibu. Mwanafunzi akokotoe mwenyewe, naomba sana wizara tuache mtihani wa hisabati uwe wa kawaida na usiwe na *multiple choice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu *Loans Board*. *Loans Board* wanafanya kazi nzuri sana, watoto wengi wa kimaskini wameweza kwenda vyuo vikuu na kutimiza ndoto zao. Hata hivyo, hii *Loans Board* imekuwa ni mwiba sana kwa hawa wafanyakazi hususan Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wazi kabisa mwaka 2016 mlifanya mabadiliko ya sheria kutoka kulipa asilimia nane mpaka 15. Jamani, huyu mtumishi wa Tanzania ana makato mengi sana yanayomkabili, ana *income tax*, ana *PSPF*, ana makato ya *NSSF*, ana makato ya *CWT*, makato mengi kiasi kwamba mshahara unabakia mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo sheria imekiuka ile thamani ya kubakia mshahara 1/3 imekiuka, kwa hiyo, inampa mtihani mkubwa sana huyu mtumishi kufanya kazi kwa mashaka na *stress* nyingi. Kwa hiyo naomba basi kama hii sheria ipo na sheria sio maandishi ya *Qur-an* au Msahafu kwamba hayawezi kufanyiwa marekebisho. Naomba basi sheria kama ipo iletwe kwa sababu ni sheria kandamizi, inawakandamiza watu wengi sana hata sisi inatukandamiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba hii sheria iletwe humu au Serikali sasa itoe tamko wale watu waliokumbwa na hii sheria ina maana *loans beneficiaries before 2016* basi walipe ile ile asilimia nane na hawa ambao wako baada ya 2016 walipe kwa hiyo asilimia 15, itakuwa inawasaidia hawa wafanyakazi. Kwa kweli wanafanya kazi kwa *stress* nyingi maisha yamekuwa ni magumu vitu vimekuwa bei juu wanashindwa kufanya kazi kwa ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, ila hukusema unakandamizwa wapi, sasa mimi sijakuelewa sana. Tunaendelea Mheshimiwa Edwin Sannda, Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Almas Maige ajiandae.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote nichukue fursa kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Daktari John Pombe Joseph Magufuli, lakini pia na timu yake yote ambayo anakwenda nayo. Naona tunakwenda vizuri sana kwenye mwelekeo tunaoutarajia. Pia nimpongeze dada yangu Profesa Ndalichako kwa kazi nzuri ambayo mnakwenda nayo na hotuba nzuri ambayo mmewasilisha hapa, wewe pamoja na Naibu wako Ole Nasha na timu nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri lakini yapo mambo ambayo nadhani kuna kila sababu ya kuyajazia nyama au kuyaboresha hivi. Nitakuwa na mambo machache nikianza na suala zima la walimu.

Mimi nadhani katika kuinua ubora wa elimu katika kuhangai sana na suala zima la ufaulu wapo wadau kadhaa muhimu sana, wanafunzi, wazazi pia na walimu. Kwenye upande wa walimu, upatikanaji wao na uendelezaji wao nadhani tuangalie vizuri kidogo. Ningependekeza badala ya kuchukua walimu ambao wanakuwa wamefaulu labda daraja la pili au la tatu, ili mtu uwe mwalimu utoke kama *top class student* ili ukaweze kuwasaidia hawa ambao unajaribu kwenda kuwaelimisha. Kuchukua hawa ambao huku nyuma huku wamefaulu labda wastani na nini inaweza isiwe sawa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua huenda kuna changamoto ambayo tutakumbana nayo hapo mbele lakini napenda sana kusisitiza sana walimu watokane na wanafunzi wanaofaulu juu kabisa kwenye darasa lao. Kama ambavyo kwenye vyuo vikuu wapo wale *top student* ambao ndio wanaenda kuwa *tutorial assistants* matokeo yake baadae wanakuwa *lecturers* huko mbele. Kwa nini nasema

hivi tunataka kuboresha elimu tunataka kupata kizazi ambacho kina upeo mkubwa ni lazima upate wenzao wanaowafundisha wawe na upeo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ikifikia hapo; najua kuna changamoto mojawapo ya labda kuboresha maslahi ya walimu ambayo ni lazima tuanze mahali. Suala la kuboresha mazingira ya kazi za walimu lazima tuanze mahali. Ifike wakati mtu akisema mimi nakwenda kusomea ualimu anajivuna. Kazi na taaluma ya ualimu iwe ni wito wa kujivunia kama ambavyo tunaona wenzetu wanasheria akikaa anaweka kifua mbele anasema mimi / *am a learned brother* au *architect* au madaktari, twende namna hiyo. Huko nyuma kazi ya ualimu ilikuwa na heshima sasa hivi mtu anakwenda ili mradi akafanye kazi. Nasisitiza sana wanaokwenda kusomea ualimu tuwe tunawatoa kutoka wale waliofaulu vizuri kabisa, *top class student*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo ukishawapata hawa walimu umuhimu wa kuwajengea uwezo endelevu unatakiwa. Si ilimradi nimefaulu nimekuwa mwalimu basi naendelea, na muda unapita *education* yangu huku kichwani inakuwa wakati mwingine *obsolete* au *una-rust*, unaota kama kutu hivi. Kuwe na utaratibu wa kuhakikisha hawa watu kuna mfumo na mpango endelevu wa kuwaendeleza, *continuous learning, continuous training* hapa na pale katika suala zima la kuwapatia *capacity building*, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka niongelee suala zima la shule zisizo za Serikali. Hizi shule zimeonekana zikifanya vizuri sana miaka yote, tangu huko nyuma. Sasa mimi swali langu najiuliza hapa katika kutafakari, kama hawa wenzetu wanafanya vizuri ina maana wana kitu tunaita *best practice*, kwa nini tuisiwaitumie wao, tushirikiane nao ili na sisi tuweze kuboresha huu upande wa kwetu? Yaani ni lazima kuna *button nzuri wanazozi-press, the right button* zinazowapelekea wafaulu. Suala zima la nidhamu, suala zima la kuwa-*strict* kwenye uendeshaji wao, mahusiano kati ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inavyoonekana sasa hivi shule za binafsi, zisizo za Serikali ni kama maadui hivi kwa shule za Serikali, jambo ambalo si sawa. Tuwatumie tuwaweke karibu, tuanzishe utaratibu wa kuwashirikisha kwenye kutengeneza sheria zetu kwenye kutengeneza kanuni, miundo, mifumo, haya matamko yanayotoka haya, maelekezo yanayotoka, miongozo inayotoka basi isiwe kana kwamba inakwenda kuwakandamiza, iwe kana kwamba ina-support their existence kwa sababu ndio wanatunyanya. Ni lazima tushirikiane nao ikiwezekana na kama itaonekana inafaa kiwepo chombo huru ambacho kitaunganisha pande zote ambazo zitakuwa zinatengeneza mwelekeo mzuri wa elimu yetu. Nasisitiza sana hilo la pili kwamba shule zisizo za Serikali ziwe *part and parcel* ya kuanda mikakati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ninataka kuongelea suala la vyuo vya ufundii. Najua tumewekeza sana kwenye upande wa elimu ile *tertiary*, lakini upande wa elimu ya ufundii nako kidogo inabidi tuongeze uwekezaji. Tuweke mkazo kwenye vyuo hivi kwa sababu kwanza inaendana na dhana kubwa tunayokwenda nayo sasa hivi ya uchumi wa viwanda.

Pili, kuna kundi ambalo huwa halifanikiwi kwenda kwenye elimu ile rasmi ya *form five* na *six* na hatimaye chuo kingine basi wapite huku kwenda kutengeneza ajira, kuwa-capture wale vijana ambao wanakuwa hawakupata fursa wasije wakazagaa mtaani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naji-time nimeona...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Boniphace Getere ajiandae.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana mimi kuniruhusu nichangie hoja hii ya Hotuba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa muda huu mfupi nilopewa nitachangia mambo machache lakini muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa muhimu ni kuipongeza Wizara hii niliyofanya kazi nydingi sana kukuza elimu yetu nchini. Nampongeza sana Mheshimiwa Ndalichako na timu yake pia silisahau Baraza la Mitihani. Mimi nimefanya kazi Baraza la Mitihani kwa miaka 15 na naelewa kiasi gani tulipata taabu, miaka minne imepita hatujasikia mitihani imevuja. Jambo hili ni muhimu sana lieleweke kwamba Baraza limefanya kazi nzuri sana chini ya Mheshimiwa Waziri Ndalichako pamoja na Katibu Mtendaji wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo ningependa kuchangia changamoto, mimi kwangu naona changamoto kubwa sana kwenye wizara hii ni lugha ya kufundishia. Mimi naelewa ziko nchi ambazo zimeendelea sana kwa sababu ya kutumia lugha ya kufundishia ambayo watoto wanaelewa. Kusema kiingereza sio elimu ni lugha tu. Mimi nimekaa Uingereza kuna watu hata kuandika hawajui wanajua kiingereza sana. Mfumo wetu wa elimu wa kufundisha darasa la kwanza mpaka la saba kiswahili halafu watoto wakahamia kiingereza *secondary school* au shule ya upili unaleta matatizo makubwa sana, wanafunzi hawaelewi masomo na hii ni kikwazo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sana kwamba kuendeleza kiingereza ni kuendeleza mambo ya kutawaliwa, kutumia lugha ya watu wengine. Sisi tumeweza kufanya vizuri sana kutumia kiswahili chetu pia tunasema kiswahili ni tunu ya Tanzania. Ningependa tunu hii ipewe heshima yake, ningependa mimi kuona watoto wanafundishwa kiswahili, wanaelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko nchi ambazo zimeendelea sana kwa mfano Uingereza wanatumia

kiingereza, vile vile Uturiki wanatumia kituruki, Ufaransa wanatumia kifaransa, Ujerumani wanatumia kijerumani na wengine Waarabu wanatumia kiarabu na watoto wao wanaelewa vizuri sana. Lugha hii ni kikwazo kikubwa sana kwa kufundishia watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi hata kama tungepiga kura leo wangapi wangependa kusoma kiswahili. Watoto wanasoma kiingereza, shule ya upili na kuendelea huku chini msingi ni kiswahili wakimaliza shule na chuo kikuu, Bunge tunaongea kiswahili, Serikali inatumia kiswahili tunawaacha watoto hawa hawaelewi la kufanya. Pia liko tatizo na Mheshimiwa Ndalichako nimekuwa nasema mara kwa mara la kuondoa shule za ufundi. Tunaongelea Serikali ya viwanda hatuna mafundi, hatuna mfumo mzima mafundi sanifu na mafundi mchundo haupo. Watu wale wanaotoka *VETA* hawatoshelezi kufanya kazi ya ufundi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndalichako nimekuwa nasema mimi ni zao la Chuo cha Ufundı Moshi (*Moshi Technical College*), *Ifunda Technical College* pamoja na *Tanga Technical College*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndilo jopo ambalo linafanya kazi viwandani. Itatupa taabu sana baada ya kuwaacha muda mrefu; fikirieni sasa hapa shule za kata na za sekondari, kila halmashauri itenye shule fulani zifundishe ufundi kwenye *level* ya *form four* itasaidia kupata mafundi vijijini hata wa kutengeneza mikokotenı ya ng'ombe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya ufundi ndiyo *key issue* ya *development* ya nchi zote, hata Ujerumani wako vizuri kwa sababu wana mfumo huo wa ufundi ambaao wanaweza kuongoza shulenı zao, sisi hapa tumeupoteza nafasi hiyo. Mfumo uliokuwa unatumika zamani wa *diploma engineers* na *engineers* umekuwa ni kitu muhimu sana kwa Ujerumani, sisi tumeupoteza. Nimekuwa nikisema hapa, ilikuwepo *system* nzuri, imepotelea wapi? Naomba Serikali irejeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ni jambo gumu kuishauri Serikali wewe mtu mmoja ikatekeleza lakini naongelea ndani ya Ukumbi wa Bunge hili, naomba Bunge lichukue umuhimu wake wa kuishauri Serikali. Serikali tafadhalini sana, nasema kwa uhakika, kwamba watu wote wanaofanya kazi viwandani sasa walitokea shule za ufundi ambazo sasa hazipo, imebakia *Moshi Technical*, Ifunda na nyingine zina masomo ya kawaida. Tumekwama hapo Mheshimiwa Ndalichako, naomba unisaidie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mimi napata taabu sana sana, nimetokea sekta binafsi, waajiri tumekuwa tunalalamika sana. *Skill development training* inatokana na uendelezaji wa ujuzi wa wafanyakazi. Kuiweka *VETA* chini ya Wizara ya Elimu ni *mispacement*, imepotoshwa kidogo, lakini najua inaingiza mapato Serikalini. Si vibaya hata kama *VETA* itabakia Wizara ya Kazi na Ajira, lakini hela ikaenda inapotakiwa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi inakuwa vigumu sana sisi waajiri kufanya kazi ya kuchangia mfuko wa elimu ya juu amba si hata tuliolenga ilipoanzishwa hii *VETA*. *VETA* ilianzishwa ku-*develop skill* za wafanyakazi wetu sisi tuliowaajiri si wanafunzi wenye elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua tunasaidia lakini tume-*misplace* kitu kikubwa sana pamekuwa na ombwe kubwa ya tulichokitaka sisi. Mimi ningeshauri sana mjadili huko kwenye Serikali rudisheni hii *VETA* pale pale ilipokuwa zamanii lakini hela kama zinatakiwa kwa ajili ya elimu ya juu ziende, lakini sisi tupeleke wafanyakazi wetu sehemu ambayo ni ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tungependa waajiri tupeleke wafanyakazi wetu *VETA* ambayo iko chini ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa muda huu siwezi kufanya jambo lingine tena. Nashukuru sana na ninaunga mkono hoja mia kwa mia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maige. Tunaendelea na Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Sixtus Mapunda wajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Kakoso hayupo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunashuhudia Wizara hii kwa muda mrefu, lakini kwangu nilichokiona muhimu sana katika hii Wizara ni uadilifu wa Wizara. Uadilifu wa Wizara ya Elimu sasa hivi umekuwa mkubwa sana kwa sababu fedha zote zinazotoka kwenye Wizara zinakwenda chini zinafika salama na zinafanya kazi salama. Zamani ilikuwa fedha zikja huku zinarudi tena Wizarani huko huko lakini siku hizi zinafanya kazi vizuri sana. Kwa hiyo, nisifu uadilifu wa Wizara hii umekuwa mkubwa, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima, Katibu, Naibu na wote wanafanya kazi vizuri sana, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako malalamiko machache ambayo naona pale vijijini kwa sababu vitabu vile vya wanafunzi wa darasa la nne wanafanya mitihani havijaenda, lakini nimepiga simu kule wameniambia ndio vimeanza kwenda. Kama vinaenda kweli naomba vifike salama kwa sababu wanafunzi wanavihitaji vifike kwa wakati lakini tunafikiri kwamba Serikali imefanya vizuri kupeleka hivyo vitabu mapema na vinaendelea kusambazwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu Jimbo langu la Bunda na hili nimelisema muda mrefu. Wizara ya Elimu imetupa majengo mazuri sana kwenye Shule ya Makongoro ambayo ina wanafunzi wa *high school* na wale wa kidato cha nne lakini jengo la Bwalo la Makongoro

limejengwa mpaka kwenye lenta limeshindwa kumalizika na fedha yake ilikuwa imepungua. Tunaomba Wizara itusaidie kwenye hilo jengo ili liweze kumalizika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekondari ya Nyamang’unta na Sekondari ya Salama kuna majengo ya maabara yameshindwa kukamilika. Tunaomba mtusaidie ili yaweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Salawe na Shule ya Msingi Stephen Wassira, majengo yalianguka na watoto wawili walifariki na taarifa zilitolewa kwenye vyombo vy ya habari na tukatoa taarifa Wizarani, TAMISEMI inajua na Wizara ya Elimu inajua. Mliahidi kutusaidia tunaomba mtusaidie hizo shule mbili ziweze kupata majengo yake kwa sababu watoto walipotea na wananchi walipata mateso ya kuhangainka muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule za Chamriho Sekondari na Mihingo Sekondari watoto wake wanatoka kilometa 17 kutoka eneo la kijiji wanachokaa na wasichana wale wakianza 50 wanamaliza 12 au watano. Kwa hiyo, tunahitaji shule hizi mbili zipate mabweni ili watoto wa kike waweweze kusoma katika eneo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala muhimu sana ambalo mimi sijui kama mnalionia lakini lina-affects sana hii *industry* ya elimu kwa maana ya kiwanda cha elimu hiki ambalo ni masuala ya mikopo. Kama hatutaweza kudhibiti mikopo ya mabenki kwa walimu; mwalimu anapokea mshahara wa shilingi 2,000,000 lakini anaenda kupokea mshahara wa shilingi 150,000 na siyo walimu tu na watumishi wengine wote wa Serikali hii, kama hizi sheria za mikopo za mabenki kwa watumishi wa Serikali hatuwezi kuzidhibiti vizuri maana yake ni kwamba hakuna uaminifu utakaokuwepo. Ni lazima tuone mshahara unabaki kama sheria inavyosema. Mtu anapokea mshahara shilingi 300,000 anapokea shilingi 50,000 wengine wanapokea shilingi sifuri. Kwa hiyo, tufanye tathmini ya kujua hii mishahara ya watumishi na hasa walimu ambaao wakati fulani hawana hela za akiba tuone tutadhibiti

vipi ili walimu waweze kutumika vizuri kwenye shule zetu.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni kiwanda na tatizo liko hapa elimu yetu nzuri au mbaya? Ili kutambua elimu nzuri au mbaya ni namna gani tunazalisha? Je, tunazalisha watu wenye ubora kulingana na soko liliyo au ni watu wasio na ubora kulingana na soko? Kwa sababu unaweza kuzalisha jambo, kwa mfano sasa hivi tunazungumza habari ya viwanda na kama tunazalisha watu wa historia, tunazungumzia watu ambao hawako kwenye mambo ya ustawi wa jamii na kwenye mambo ya ufundi kama walivyosema wenzangu, shule za ufundi hazipo, hivi tunalenga nini hasa?

Kwa hiyo, kwenye soko letu tunakokwenda huku mbele halitakuwepo, hatutapata watumishi wanaoweza kwenda kwenye viwanda. Elimu inataka unazalisha nini, ni suala la *demand and supply*. Kwa hiyo, tuweze kujua kwamba elimu yetu hii tunayozalisha watoto wakoje, ndiyo hilo wanasema *quality education* na *quality in education*, ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, tuangalie michango yetu inakwendaje. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la matangazo la Baraza la Mitihani. Mimi huwa mara kwa mara najiuliza sana, mtu anakaa pale kwenye *tv* anatangaza, mitihani kidato cha kwanza au mitihani *primary* shule bora, *St. Mary, St. Augustine*, sasa unalinganisha na nini? Shule yangu ya Mihingo ina mwalimu mmoja toka inaanza. Shule yangu ya msingi watoto wanasoma nje, wana matatizo mbalimbali, unakuja kusema imekuwa ya mwisho kwa kulinganisha na nini, unalinganisha nani sasa? *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba mambo haya tuweze kuweka *categories* ili tulinganishe maana sasa hii mitihani tunalinganisha na nani? Huyu amekuwa bora kwa kulinganisha na nani? Hivi kweli leo unaweza kuleta hapa Barcelona ukasema inacheza sjui na Yanga halafu useme imekuwa ya kwanza eti kwa sababu tu ni sheria inaruhusu?

Kwa hiyo, nafikiri hata mitaala hii nayo tuiangalie upya wakati fulani haileti maana sana kwenye mambo haya ambayo yanakuwepo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi tumezungumza kwenye mambo ya sera. Mimi nafikiri huo mfumo unaouzungumza kwamba kuwepo na kongamano zito, alizungumza Mzee Mkapa, akazungumza Mzee Jakaya na hata Mheshimiwa Magufuli akitoka mtasema Mheshimiwa Magufuli alizungumza. Kwa hiyo, nafikiri kwamba hii mijadala hii iendelee kuwepo na hakuna mtu anazuia mijadala, nami nawaomba Wizara ya Elimu pale watu wanapotaka kufanya mijadala ya elimu basi tuwaunge mkono ili tuweze kuona kitu bora tutakachokuja kufanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu Benardetha Mushashu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa na mimi nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wakuu katika Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa mpango wake wa elimu bila malipo. Serikali imetoa hela nyingi, inatoa zaidi ya shilingi bilioni 23.8 kila mwezi kugharimia elimu lakini katika waraka uliotoka na wazazi walipewa majukumu fulani, wazazi walibakiwa na jukumu la kuhakikisha kwamba wanatoa *uniform* pamoja na chakula kwa ajili ya watoto wao. Wasiwasi wangu ni maelekezo yaliyotoka Wizarani au tuseme TAMISEMI kwamba hiki chakula ili mwanafunzi aweze kukila shulenii utaratibu utakuwa tofauti na ule uliokuwa unatumika kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua umuhimu wa chakula au umuhimu wa lishe. Mtoto akiwa na njaa hawezi kujifunza na akaelewa. Tunatambua kwamba Watanzania chakula cha jioni tunakula kati ya saa 11.00 jioni mpaka saa 2.00 usiku, mtoto tangu saa hizo hajapata kitu chochote, anaamka asubuhi hakuna *breakfast* anaenda shuleni anasoma tangu asubuhi mpaka jioni, hawezi kuelewa kitu chochote.

Naomba basi Wizara ya Elimu ile ya kusema kwamba chakula kikichangwa, michango ikichangwa, wazazi wenyewe waji-*organise* awepo mtu atakayeratibu kukusanya hivyo vyakula ndiyo viweze kupikwa mashuleni watoto wale, nafikiri si sahihi. Hili ni jukumu la msingi la walimu, kwa hiyo, jukumu la chakula kinaliwa na nani na saa ngapi waachiwe walimu lakini wazazi watimize jukumu lao la msingi la kuhakikisha kwamba watoto wao wanapata chakula mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu mashuleni ni mkubwa sana kitaifa, lakini vilevile ukiangalia kwenye Mkoa wa Kagera ninakotoka kuna upungufu wa walimu zaidi ya 6,773 katika shule za msingi na katika shule za sekondari kuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa sayansi na hisabati. Najua kila nchi ina mipango yake na ina namna ya kuandaa wataalam. Napendekeza kwa hili Serikali ingefanya mpango, tuna Chuo Kikuu cha Dodoma hapa, kina majengo yako pale, wangeweka mkakati sasa wa kwamba hicho chuo sasa hivi kitumike kuwaandaa walimu wa sayansi, hisabati pamoja na walimu wa shule za msingi ambao wanakosekana kusudi katika miaka miwili, miaka minne tuwe tumemaliza hili tatizo. Chuo cha Dodoma kipo na kinaweza kikafanya mpango huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonesha kwamba kwenye shule za msingi namba ya watoto wa kiume na wa kike inalingana; ukienda sekondari namba ya watoto wa kike na wa kiume zinakaribiana na ukienda kwenye vyuo vikuu namba ya watoto wa kike inaendelea kupungua lakini kwenye masomo ya sayansi imepungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, wamegundua kwenye vyuo viwili kuna 17% tu ya wasichana wanaosoma masomo ya sayansi kwenye vyuo vikuu. Hii ni hatari, haiwezekani Tanzania tukasema kwamba tunaendelea wakati nusu ya Watanzania wanaachwa nyuma ambao ni wanawake. Pia tukumbuke kwamba hawa wasichana ambao mnawaona kwamba ni wachache sana katika masomo ya sayansi kwenye vyuo vikuu ni walewale watoto wa kike ambaye akitoka shuleni, akirudi nyumbani kwanza amsaidie mama kutengeneza chakula na kufanya usafi. Yule yule mtoto wa kike ikitokea mzazi au mlezi ni mgonjwa lazima abaki nyumbani kumsaidia. Hawa watoto wa kike akiwa shuleni anashawishiwa na watoto anaolingananao, anashawishiwa hata na mababa watu wazima, yote inamletea msongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiwa kwenye jamii au darasani kuna mtazamo kwamba masomo ya sayansi na hisabati ni kwa ajili ya wanaume, wasichana hawafai huko. Kwa hiyo, siku za nyuma tulikuwa na mpango kila walipokuwa wanamaliza *form six* wale watoto wote wa kike ambao walikuwa wanakaribiana na ufaulu ambao unatosha kumuingiza chuo kikuu walikuwa wanapelekwa chuo kikuu wiki sita kabla ya kufungua vyuo vikuu, wanapewa *some kind of an induction course* na baada ya hiyo *course* walikuwa wanapewa mtihani, wanashinda na wengi walifanya hivyo na wakashinda kuliko hata wale waliopata *division one*. Niiombe Serikali huu mpango urudishwe ili watoto wa kike wanaomaliza *form six* ambao ushindi wao ni mzuri kidogo yaani wameteremka kidogo kuliko ule unaohitajika....

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** ...wapelekwe chuko kikuu kusudi waweze kufanyiwa hiyo *induction course*...

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Taarifa.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Hii itaweza kungeza wanafunzi katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera mnajua kwamba lilitokea...

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** ...tetemeko na shule nyingi ziliharibiwa, miundombinu iliharibiwa na watu walifariki. Niipongeze Serikali kwa kazi nzuri mliyoifanya pale *lyungo secondary school*, mmeijenga imekuwa ya kileo ni maghorofa matupu. Hongereni sana na Nyakato inaendelea kutengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka kuwaambia kwamba bado kuna shule kama *Bukoba secondary school* na *Rugambwa secondary school* zote ni za Serikali, ni shule kongwe na ziliathiriwa na tetemeko. Nauliza Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati shule hizi kwa sababu walimu na wanafunzi kwenye shule hizo wanaishi katika hali hatarishi kwa sababu kwanza yale majengo ni ya zamani, halafu yalitetemeka lakini sijaona mpango uliopo kwa ajili ya kuzitengeneza au kuzirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufikia uchumi wa kati ambao utatawaliwa na viwanda na ili hii ndoto itimie lazima watoto wajifunze sayansi. Tuna upungufu mkubwa sana wa maabara. Mkoa wa Kagera tu tuna upungufu wa maabara 352 ambayo ni 62% ya mahitaji na hizi maabara zote zimejengwa kwa nguvu za wananchi. Napendekeza Serikali ingetenga hela maalum kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanajenga maabara kila shule za *chemistry, physics, biology, geography* na ikiwezekana *computer lab* ili tuweze kufikia kwenye huo uchumi wa viwanda ambao tunauzungumzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni vyuo vya *VETA*. Napongeza mpango wa Serikali wa kuendelea kujenga hivyo

vyuo vya VETA. Uchumi wa viwanda utahitaji hawa mafundi wa katikati. Ni bahati mbaya sana mimi wakati nasoma na nafundisha tulikuwa hata na shule za ufundi lakini na zenyewe zimekufa. Napendekeza kwamba tuendelee na mpango huohuo ili katika kila...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwalimu. Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa sekunde tano nimpongeze sana Waziri na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya lakini harakaharaka niende kwenye Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, pamoja na kazi nzuri ambayo Wizara inafanya niombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye shule ya sekondari ya Iwawa majengo yamechakaa sana na barua zimekuja kwako ambapo karibu shilingi bilioni 2.6 zinahitajika ili kuweka sawa shule ile. Ikumbukwe shule ile ilikuwa ya kwanza kimkoa wa Njombe na ni shule ya Serikali, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, lakini pia shule ya sekondari ya Lupila, ni *A-Level*, chondechonde uikumbuke. Shule ya sekondari ya Kipagalo uikumbuke na shule ya sekondari ya Ilkuo.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, baada ya kusema hayo niseme tu kwa ufupi. Tumekuwa tukijadili sana kuhusu elimu na ubora wa elimu. Kabla sijachangia, nihoji maswali mawili au matatu.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, elimu bora ni ile ambayo inatoa majibu ya matatizo tuliyonayo katika nchi au katika jamii, ndio elimu bora na siyo vinginevyo. Swali linakuja, je, elimu tuliyonayo leo kutoka darasa la kwanza mpaka vyuo vikuu inafasili matatizo ya Watanzania? Maana nguvu ya

Watanzania ni kilimo, uvuvi na ufgaji lakini toka darasa la kwanza mpaka vyuo vikuu hakuna mahali ambapo elimu hiyo inatiliwa mkazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha nyingine hata kama wanafunzi wa kidato cha nne wote Tanzania wangekuwa daraja la kwanza kwa ufaulu, kidato cha sita wakapata daraja la kwanza na vyuo vikuu wakapata daraja la kwanza, kwa maana ya *first class*, utawapeleka wapi? *What next?* Hawawezi kujajiri na hawawezi kuajiriwa. Kwa hiyo, hoja leo si suala la *quality education as far as our education system is concerned*, ni issue ya *relevance of education system*. Elimu tuliyonayo ni *irrelevant*, kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mwanafunzi wa kidato cha nne hakuna anachoweza kufanya, kidato cha sita hakuna anachoweza kufanya, hata tukimpa wa shahada ya kwanza hakuna anachoweza kufanya. Ndiyo maana ninapandekeza lazima tufanye *overhaul of education system*. Tutengeneze masomo kuanzia darasa la kwanza mpaka hilo la saba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninashauri darasa la kwanza liende mpaka darasa la nane, kwa nini? Kwa sababu masomo ya darasa la sita na la saba kwa kiasi kikubwa ndiyo yanayosomwa *form one* na *form two*, isipokuwa ni lugha inabadilika. Tukienda darasa la kwanza mpaka la nane tuende sasa darasa la tisa mpaka la kumi na mbili inaishia hapo, tunaondoa *five* na *six*. Sababu ya kuondoa *five* na *six* ni kwa sababu hakuna uhusiano wa masomo ya kidato cha tano na sita na *degree* yoyote ndani ya nchi yetu. Ukimchukua leo mwanafunzi wa kidato cha nne ukampeleka kuanza *degree* ya kwanza atafanya vizuri tu, mkitaka jaribuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili haraka haraka ni la lugha. Jamani Mheshimiwa Mwenyekiti na Wabunge wenzangu ni vizuri mfahamu Kiswahili, Kiingereza, Kireno, Kijerumani ni lugha ambazo tumeamua kuzifuata kwa sababu ya kutawaliwa. Hakuna mtu ambaye amezaliwa

kabila lake wanaongea kiswahili au kiingereza ama kireno ama kifaransa. Kama mwalimu Nyerere na wenzake wangeamua Tanzania tuongee Kingereza tungekuwa tunaongea kiingereza hivi hivi na tungekuwa tunajivunia kwamba ni lugha yetu. Kwa hiyo, kiswahili siyo lugha ya kwetu ni lugha iliyotokana na kutawaliwa na waarabu, sawasawa na kiingereza, kireno na kifaransa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali la kujiuliza, je, hawa watawala wetu walifanya uchaguzi wa maana? Kwa sababu *kiswahili as of today* nchi hazizidi nne zinazoongea Kiswahili kwa ufasaha lakini kiingereza Afrika peke yake ni nchi 25, kihispaniola ni nchi zaidi ya hizo. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sasa kufikiri kwa usahihi kwamba walimu wanaomaliza vyo vikuu wapewe *dossier* ya kufundisha *primary schools* ili walimu wenye shahada waanzie shule za msingi kufundisha Kiingereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Makete, baba yangu ni Mahanji mama yangu ni Mkinga, kwa hiyo, naongea kwa ufasaha kikinga na kimahanji. Naongea kwa ufasaha pia kimagoma, kiwanji, kibena, kikisi kwa sababu ndio makabila yanayopatikana Makete. Je, kwa kujua kiswahili ambayo ni lugha mpya, nimewenza kuharibu lugha yangu ya baba na mama? *The answer is no.* Kiswahili hakijaharibu kimahanji, kikinga, kimagoma changu na Wabena, Wasukuma na Wachaga vivyohivyo. Kwa hiyo, kujua kiingereza hakuharibu kiswahili chako bali kinakuongezea nguvu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa kwenye mkutano pale Dubai, mimi ni *Financial Adviscer*. Pale Dubai kuna madereva 12,000 katи ya hao wanaoendesha *tax*, 2,700 ni Wakanya, sababu wanajua lugha. Sisi kwetu tunawa-barred, tunawa-determined wetu kwa sababu ya lugha, lugha *is a problem*. Kwa dunia ya sasa ukiwa *conversant* na lugha nydingi ni mtaji.

Mheshimiwa Mwneyekiti, kwa hiyo, niombe sana mliangalie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka niende kwenye elimu ya juu. Naomba sana fedha zinazopelekwa COSTECH kwa maana ya Tume ya Sayansi zioanishwe na shahada za uzamili na uzamivu kwenye vyuo vikuu. Kwa lugha nyingine Serikali i-*identify* maeneo ambayo wanataka kufanya utafiti COSTECH wa *execute* hiyo programu, vyuo vikuu vya *private* na vya Serikali viombe ili mtu akifanya utafiti wake anaisaidia Serikali kupata majibu ya maeneo wanayotaka lakini wakati huohuo unaongeza idadi ya shahada za uzamivu na uzamili ili twende kwa pamoja. Tukifanya hivyo, tutaongeza sana idadi ya wanazuoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TCU*, tusipoangalia itakuwa ni tume ya chuo fulani kimoja kwa *nature* ya waajiriwa wake. Niombe sana viongozi wa *TCU* ni lazima wawe na weledi hiyo moja na wawe wamesoma vyuo mbalimbali ili akiwa pale asitizame chuo kimoja. Pili, awe pia amefundisha vyuo mbalimbali ili pia awe na weledi wa anachotaka kusukuma vinginevyo itakuwa ni Tume ya Vyuo Vikuu lakini kwa kweli inayokuwa *dictated* na chuo kimoja, itakuwa ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo *TCU* waongoze weledi na hasa kwenye kutambua watu wanaomaliza shahada kwenye nchi zilizoendelea. Watoto wetu wanapomaliza vyuo vikuu vya nje...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa kwa mchango wako mzuri, nakupongeza.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Huyo ndiyo anahitimisha mgawanyo wa leo wa idadi ya wachangiaji kwa vyama vinavyowakilishwa humu Bungeni, tumetenda haki.

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii nitajikita katika maeneo yafuatayo; moja, ni ukweli usiopingika kuwa Vyuo vya Ufundı Stadi (*VETA*) ni muhimu kwa sasa ukizingatia kuwa nchi hii inaelekea kuwa ni nchi yenye mwelekeo kuwa ni nchi ya viwanda vidogo, vyta kati na vikubwa, hivyo, tunahitaji wataalam wa ufundi katika kuendesha mashine katika viwanda hivi na suluhisho la wataalam hawa litapatikana kwenye vyuo hivi. Niipongeze Serikali kwa jitihada inazozichukua kujenga vyuo hivi. Nishauri vyuo hivi vijengewe katika Wilaya na Mikoa yote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vyuo hivi pia utasaidia katika kupunguza changamoto ya ajira kwani vyuo hivi vitasaidia katika kufanya vijana wote wajajiri katika maeneo mbalimbali ya ufundi. Niuombe uongozi wa Wizara uharakishe zile asilimia tano za *Skill Development Levy* zinazokusanywa na Wizara ya Fedha zinafuatiliwa na kupelekwa katika *VETA* na *FDC's*. Umuhimu wa vyuo hivi nimeuona katika Mkoa wa Shinyanga jinsi *VETA* inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni ukaguzi wa shule. Eneo hili nalo lina changamoto katika kuimarisha ubora wa elimu, utendaji wa kazi wa walimu na tathmini ya elimu yetu yote. Haya hayawezi kufanya bila kuimarisha Idara ya Ubora na Ukaguzi wa Elimu. Maeneo mengi katika Wilaya au Majimbo yote Idara hii haipo vizuri kwa kukosa vitendea kazi kama magari mfano ni Jimboni kwangu Kilindi. Jiografia ya Wilaya imekaa vibaya, lakini hakuna gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiimarisha eneo hili hakika malalamiko ya kudidimia kwa elimu katika shule za msingi na sekondari yatapungua. Vilevile kuna umuhimu kwa Serikali kuboresha maslahi ya watumishi wote wanaosimamia eneo

hili la elimu, hayo yamezungumzwa sana. Zamani kitengo hiki kilikuwa imara na matokeo yake yalikuwa yanaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusu Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi. Napongeza mamlaka hii kwa kazi kubwa inayofanya ikiwa ni pamoja na kusimamia ukarabati wa shule zetu za sekondari nchini. Hili ni jambo jema sana kwa sababu shule hizi zilikuwa zimechakaa sana. Maamuzi haya hakika yanafanya hata watoto wetu wanaosoma katika shule hizi ufaulu wao kuongezeka kwa sababu watasoma katika mazingira mazuri, hiki ni kigezo cha kuinua ufaulu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, zipo changamoto ambazo naomba zifanyiwe kazi. Mamlaka lazima iwe na utaratibu mzuri unaoeleweka katika shule zote, mfano kama mtatumia *force account* basi itumike katika shule zote. Mfano ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Bwiru wametumia mfumo wa *force account* na kazi imefanyika vizuri, lakini katika Shule ya Sekondari *Nganza Girls* zote hizi zipo Mwanza wametumia mkandarasi. Wote hawa walitengewa kiasi cha shilingi milioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni kwamba mkandarasi wa Nganza sekondari ametumia jumla ya shilingi 1,300,000,000 ongezeko limekuwa ni kubwa. Hivi *TEA* walifikiria au walitumia vigezo gani katika utaratibu wa kazi yenye madhumuni yanayofanana? Nashauri Serikali isimamie eneo hili kwa sababu dhamira ya Serikali ni kukarabati shule zote za sekondari Tanzania, tusipokuwa makini ni shule chache zitakarabatiwa. Wizara isimamie vinginevyo majukumu ya ukarabati yatolewe katika Mamlaka hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ombi kwa Shule ya Sekondari ya *Kilindi Girls* kupatiwa fedha za uzio. Katika Jimbo la Kilindi tunayo shule ya sekondari moja ya wasichana ambayo inapokea wasichana kutoka maeneo mbalimbali ukiacha Kilindi, Handeni, Korogwe na Wilaya jirani wote wanakuja kusoma hapo ila tatizo kubwa hatuna uzio unaozunguka shule na hii ni hatari kwani shule hii

inazungukwa na makazi ya watu. Ili kulinda usalama wa watoto wetu na pia katika kuleta ufaulu katika masomo. Niombe Wizara itusaidie kutujengea uzio (*fence*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri iliyofanyika chini ya uongozi wake Mheshimiwa Waziri Profesa Joyce Ndalichako (Mbunge) akisaidiwa na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. William Ole Nasha (Mbunge). Pia niwapongeze watendaji wote chini ya uongozi wake Dkt. Akwilapo na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Nyasa, natoa shukrani nydingi kwa jinsi ambavyo wamelisaidia na leo nimeona tena Chuo cha *VETA* Nyasa kikiwa katika mpango wa kujengwa, nawashukuru sana. Naomba pia niwatajje wazee wa *P4R*, *DPP* wetu Ndugu Gerald na timu yake, kazi haikuwa nyepesi, nasema hongereni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru pia *TEA* kwa kuliona jimbo langu. Nawashukuru wote kwa upendo toka nikiwa nao hata nilipoondoka. Hali ya jimbo langu ilikuwa mbaya sana kimiundombinu ya elimu. Hata hivyo, nazidi kuomba juu ya Shule ya Lumalo na Shule ya Sekondari Nyasa kuhusu bweni ambalo halijaisha toka *SEDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kusisitiza juu ya umuhimu wa kuwezesha *R&D Institutions* ili kufanya tafiti mbalimbali zitakazowezesha uwekezaji wa tija. Kwa kuwa *TIRDO* ndiyo jicho la vivanda, kama ilivyo jina lake, niiombe Wizara kupitia *COSTECH* kuisaidia taasisi hiyo iweze kutimizia majukumu yake na hasa la kufanya *mapping* ya rasilimali ili hata anapokuja mwekezaji yeyote tuwe tuna taarifa za kutosha. Watafanya kwa kushirikiana na taasisi zetu za vyuo kulingana na aina ya utafiti.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kuongelea kuhusu upungufu wa walimu wa sayansi. Suala hili limekuwa ni changamoto katika maeneo mengi nchini kwani mpaka sasa idadi ya wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi ni tofauti na wanafunzi wanaosoma masomo ya sanaa. Hivyo, Wizara ichukue jambo hili na kulifanya kazi ili tuweze kumaliza tatizo hilo la walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni nzungumzie shule binafsi. Kulingana na mchangano wa shule binafsi katika Serikali suala hili liangaliwe kwa kupunguza kero zile zinazowafanya watu wa shule binafsi wavunjike moyo ili kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni suala la elimu bure. Naomba suala hili liangaliwe upya kwani kuna changamoto ambazo zinaikabili sekta ya elimu ikiwemo kutopeleka pesa shulenji jambo ambalo linawakwamisha kufanya mambo ya msingi ambayo wamejipangia kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu madai ya walimu. Ili tuwe na matokeo chanya ni lazima kuwe na mazingira rafiki kwa walimu pamoja na wanafunzi. Madai ya walimu yamekuwa ya muda mrefu ambayo kwa sasa yanawaathiri wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, walimu wa sekondari kupelekwa kufundisha shule za msingi. Suala hili halijawahi kutokea katika nchi yetu na linaweza kuathiri wanafunzi kwani wanafunzi wa shule ya msingi wanahitaji kujengewa msingi na walimu wenye /level/hiyo.

Suala la sita ni upungufu wa vitabu. Kulingana na umuhimu wa vitabu katika kuboresha ufaulu wa wanafunzi, Wizara iweke kipaumbele kununua vitabu na vitabu viandaliwe kwa ubora ili wanafunzi wapewe elimu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, kiandaliwe chombo maalum kwa ajili ya kusimamia elimu ili kuleta tija. Jambo

hili likisimamiwa vyema litaleta matokeo chanya kwa Wizara ya Elimu na itakuwa rahisi kumaliza matatizo yanayoikabili Wizara kwani watakuwa wanatembelea na kujua matatizo.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongea kuhusu miundombinu. Miundombinu katika shule za Serikali ni mibovu na ndiyo inayosababisha wanafunzi kufanya vibaya katika shule za Serikali. Ziko changamoto nyingi katika elimu ya Tanzania. Elimu bure, mabweni, upungufu wa vitabu shulenii, walimu kupunguzwa na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya elimu bure Serikali hii ya Awamu ya Tano imekurupuka vibaya na imesababisha matokeo mabaya. Ukiangalia gharama za kumnunulia *uniform* mwanafunzi, chakula, malazi, umbali na changamoto za familia hususan vijijini unakuta mtoto anasafiri umbali wa kilometra 20 kufuata shule na akifika shule kachoka, ana njaa na anawaza atarudije kwao baada ya masomo kwa umbali huo na huku usalama wake huo ni wa hofu kiasi hicho. Mnawafikiriaje wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu kama hayo hususani vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri maslahi ya walimu yazingatiwe, nyumba za walimu wa shule za sekondari na msingi bado hali ni mbaya na usalama wao vijijini. Hii imesababisha walimu kukosa *morale/motisha* wa kufundisha kwa moyo kwa sababu ya changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule ya sekondari ya Wasichana Mpanda, shule hii ya wasichana haina uzio na ukizingatia eneo lilitobaki kuzunguka shule ni pori na kuna wanyama aina ya viboko kipindi cha usiku huzunguka kwenye mabweni na husababisha wanafunzi kuishi kwa hofu hapo shulenii. Shule ya *Mpanda Girls* imezungukwa na wafanyabiashara, *stand* ya magari ya mizigo na biashara za wajasiriamali hivyo usalama wa wanafunzi hawa umekuwa mdogo na wa hofu. Waendesha magari makubwa kuweka *stand* hii pale imesababisha wanafunzi kupata mimba kutokana na mazingira yaliyopo, ni mabaya. Hivyo Serikali

izingatie jambo hili la kuweka uzio ili usalama wa wanafunzi uimarike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu wanafunzi wenye ulemavu. Shule za Msingi Azimio, Kasahato na Nyerere zilizopo katika Manispaa ya Mpanda zimeelemewa mzigo wa wanafunzi walemauvu na bado wana changamoto za madarasa ya kufundishia watoto hao, wanafundisha katika madarasa yasiyo na madirisha. Je, Serikali inawasaidiaje watoto hawa pamoja na walimu ambao kimsingi wanafundisha katika mazingira hayo magumu na vitendea kazi pia havitoshi? Serikali ina mkakati gani wa kumaliza matatizo haya ya wanafunzi walemauvu na vifaa vyao husika?

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kuongelea Bodi ya Mikopo. Ili kuweka tija na kuondoa malalamiko ya mara kwa mara ya mikopo kwa wanachuo, nashauri Serikali izingatie suala la Bodi ya Mikopo kuwa na *revolving fund* ambapo fedha hizo zisiwekwe Mfuko Mkuu ili Bodi iweze kuwekeza na kutunisha mfuko ambao utasaidia kuchangia gharama za kuendesha taasisi na baadae Serikali itaondoka katika kutoa fedha kuwezesha Bodi hii. Hivyo basi, Serikali itoe fedha kwa Bodi na kuwezesha *revolving fund* kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Bodi iwe chini ya Wizara ya Fedha. Kwa kuwa Bodi inahusika na masuala ya fedha ni vema ikawa chini ya Wizara ya Fedha ili kupata msaada zaidi wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashirika ya misaada, kwa kuwa kuna taasisi nydingi za kiraia na mashirika ya kimataifa ambayo yanahusika kusaidia masuala ya elimu na ufadhili, je, Bodi ya Mikopo inashirikiana vipi na taasisi hizi ili misaada pia ipitie kwao kwa wenyewe uhitaji maalum?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kuongelea kuhusu sera, sheria na kanuni. Sheria iliyopo ni ya tangu mwaka 1979 ambapo imekuwa ikifanyiwa marekebisho

nyakati mbalimbali, lakini sera zake bado hazijafanyiwa maboresho ili kuendana na sheria. Nashauri Serikali ipitie upya sera zake ili zikidhi mahitaji ya sasa kwa kushirikisha wadau wa elimu na ndipo sheria iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusu mitaala, kumekuwa na mabadiliko katika mitaala, nashauri Serikali iangalie ufanisi wa mitaala kwani mabadiliko yamekuwa hayakidhi uhitaji na kumekuwa na mkanganyiko kwa watumiaji. Hivyo, nashauri Serikali isimamie mitaala na vitabu ambavyo vitakuwa muhimu kwa watoto shulenii kulingana na umri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu usajili wa shule za Serikali. Serikali ina wajibu mkubwa kutoa elimu nchini na sasa elimu bure. Tatizo ni kuwa TAMISEMI bado ina changamoto ya bajeti na kuhusisha wananchi kujenga miundminu ya shule na watoto wa vijijini ndiyo wanapata shida kufika shule zilizo mbali kati ya kilometra sita mpaka 14. Tatizo kubwa na vigezo vya usajili na kusababisha shule zinazojengwa na wananchi kukosa sifa. Nashauri Serikali ipunguze masharti kwa shule za Serikali, iwe angalau na vyumba vinne, matundu sita ya choo, nyumba moja na ofisi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni vyuo vya elimu na shule za mazoezi. Tanzania kwa sasa vyuo vya ualimu viro vingi kwa ngazi za cheti, diploma na shahada lakini wahitimu wanaotoka shule au vyuo hivyo wamekuwa hawana uwezo wa kuridhisha katika utaalam, ujuzi na maarifa. Hivyo, nashauri Serikali itoe mwongozo kila chuo kikuu kiwe na shule ya mazoezi mfano mzuri ni wahitimu wa *DUCE* wapo vizuri sana kwa kuwa wana shule ya mazoezi. Mpango huo unaweza pia kushushwa ngazi za chini yaani *diploma* na cheti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kukariri darasa. Nashauri mfumo uboreshwe ili kusaidia watoto kufaulu pia kuwezesha kuendelea na masomo. Jambo la kuangalia ni kwa kiasi gani mitaala hii inachangia watoto kukariri darasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Serikali na Wizara na watendaji kwa kazi wanazoendelea kufanya.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya kuboresha elimu kwa Watanzania. Mimi nizungumzie suala la vitabu kwa mtaala mpya kwa shule za msingi. Baada ya mtaala huu kusambazwa shuleni walimu walipewa mafunzo juu ya mtaala mpya lakini vitabu vinavyofaa kwa mtaala huo vimechelewa kufika. Hii inawapa kazi ngumu sana walimu hasa wa darasa la kwanza mpaka la nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu na Wilaya nzima ya Itilima vitabu hakuna kabisa. Kwa hiyo, tuna mtaala mpya lakini vitabu havipo. Naiomba Serikali iharakishe kuleta vitabu ili walimu waone unafuu wa kufundisha watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Profesa Ndalichako kwa kufanya juhudhi ya kuwafanya watoto wetu waweze kuwa na ufaulu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kusema kwamba watoto wetu wengi wanakwenda masafa marefu kufuata shule. Shule nyingi ziko mbali sana na makazi ya watoto, hivyo basi, naishauri Serikali iweke sehemu ambazo wazee watalipia ili watoto waweze kukaa pamoja na kuweza kubadilishana mawazo na kusoma kwa pamoja kwa wale ambaa watakuwa na uwezo wa kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwa wale wanafunzi ambaa wanaonekana wana uwezo mzuri wawekwe pamoja kuanzia shule za msingi. Ikiwa wataanza kuwekwa pamoja kukawa na madarasa maalum na baadae wawe na madarasa maalum sekondari basi tutapata wanafunzi wazuri wa sayansi na masomo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia tatizo sugu la maslahi ya walimu. Walimu wanaishi katika mazingira magumu sana nashauri waboreshewe maslahi yao. Bila ya mwalimu kupata utulivu basi hawesi kuwa na moyo wa kufundisha vizuri, anakuwa na mawazo mengi sana hajui atalala wapi, atakula nini na huku ana familia inamtegemea. Naiomba Serikali ijitahidi sana kuboresha maslahi haya ya walimu ili watoto wetu waweze kufundishwa kwa utulivu na waweze kupata ufaulu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuhusu vyoo katika shule zetu. Watoto wa kike wanapata shida sana wanapokuwa kwenye hedhi wanashindwa kuhudhuria masomo. Hivyo basi, naishauri Serikali ihakikishe katika shule zetu kuna matundu ya vyoo pamoja na maji.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo inafanya jambo zuri kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wa nchi hii wa elimu ya juu kuweza kulipia masomo yao ya vyuo vikuu. Pamoja na hayo, kuna changamoto nyingi juu ya upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu. Kwanza idadi ya wanafunzi wapatao mkopo wa elimu ya juu ni kidogo sana, idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitaji mkopo wa kuendelea na elimu ya juu wanakosa fursa hiyo. Naishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ili na Bodi ya Mikopo ipate fungu kubwa la kuweza kuwakopesha wanafunzi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hayo, hao ambao wanapata mkopo kuna changamoto ya vigezo. Ili upatiwe mkopo wa elimu ya juu unahitajika kukidhi vigezo mbalimbali jambo ambalo ukiacha vigezo hivyo baadhi ya wanafunzi huwa wanapatiwa mikopo hiyo bila ya vigezo. Hivyo, naishauri Wizara husika kuzingatia vigezo na kutoa mikopo kwa wale wanaostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ya Bodi ya Mikopo ni ukusanyaji wa mikopo hiyo. Mategemeo ni kurejeshwa kwa mikopo hii ili na wengine waweze kukopeshwa na wao wajiedeleze ila hili linategemea kupata ajira kwa wahitimu waliokopa ili Serikali iweze kuwabana na kukatwa kwenye mishahara yao kwa kiasi kilichokubaliwa na kurejeshwa Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni pale wahitimu wengi wanapokosa ajira na kubaki mitaani bila kazi na hatua za kuwafanya walipe wakati hawana ajira ni ngumu. Hivyo, naishauri Serikali mara tu wahitimu wetu wa elimu ya juu wanapohitimu Serikali isiwe na kigugumizi cha kuwaajiri kwani ajira zao ndiyo njia ya kurejesha mikopo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu inahitaji kuwekewa miundombinu mikubwa. Wakati umefika wa kwenda na wakati na moja ya miundombinu ni lugha ya kufundishia. Kwa sasa naiomba Serikali kutilia maanani na mkazo juu ya lugha ya kiingereza. Sisemi kwamba lugha ya kiswahili iachwe lakini mkazo mkubwa uwekwe kwenye lugha ya kiingereza kwani ndiyo lugha inayotumika katika mambo yote ya kimaendeleo ya duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inaingia katika uchumi wa viwanda, viwanda vinategemea wafanyakazi wenye taaluma na wataalam wetu tunategemea kuwapata katika vyuo vyetu vya ufundi. Nashauri Serikali kwa makusudi ilibebi suala hili na iziwezeshe shule na vyuo vya amali viweze kutoa mafundi wazuri ambao tutawatumia katika kukuza uchumi wetu wa viwanda. Walimu wa vyuo hivyo wapewe motisha na wawezeshwe ili na wao wawawezeshe wanafunzi wao kitaaluma kwa mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu motisha kwa walimu. Naiomba Serikali isiwasahau walimu kwani ndiyo mambo yote. Ikiwa walimu wanabaki na malalamiko kila kukicha basi na ufanisi kwa wanafunzi wetu utakuwa mgumu. Naishauri Serikali kukisikiliza kilio cha walimu kwa kuboresha maslahi yao. Ahsante.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa machango wangu katika hotuba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pia napenda kumpongeza kwa dhati Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika vyema hotuba yao na kuiwasilisha kwa ufasaha katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni Chuo Kikuu cha Dodoma. Chuo hiki ni mionganini mwa vyuo muhimu sana katika nchi yetu hasa ukizingatia kuwa kiko katika mji mkuu wa nchi yetu. Kinahitaji maboresho ya hali ya juu katika rasilimali watu ili kiende na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kuona kuwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kuwa amegharamia masomo kwa walimu/wafanyakazi 377 katika nyanja tofauti. Suala langu katika wafanyakazi hao ni kwamba Waziri hajaeleza wafanyakazi 377 aliowapatia mafunzo ni kati ya wangapi yaani ni asilimia ngapi ya 377 waliopata mafunzo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundini Stadi. Naipongeza Wizara ya Elimu kwa kuimarisha mamlaka hii. Hii ni mamlaka inayowagusa wanafunzi wa kipato cha chini na makundi tofauti. Ameeleza namna inavyojitahidi kuongeza vyuo katika maeneo kadhaa nchini. Nashauri katika ujenzi wa vyuo hivyo uzingatie uwepo wa makundi yote. Majengo yawe na *facilities* kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili nao wafaidi matunda ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu linahusu kusaidia kufungua Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Nkasi, Paramawe kwenye majengo ambayo yako kumi na nne tullyopewa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Majengo hayo yamekwishakaguliwa na *VETA* Kanda ya Nyanda za Juu Mbeya na kuridhika kabisa kwani yana umeme na maji. Pia tumetoa eneo la ekari 50 kwa ajili ya Chuo cha *VETA* Paramawe – Nkasi, kwa hiyo, pa kuanzia tunapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana ziara ya Rukwa, Nkasi Waziri alahirisha, ilikuwa ufile sehemu yaliyopo majengo hayo mazuri sana. Tunaomba sana msaada wa Waziri. *VETA* Kanda ilikwishayakubali na kuridhika kabisa. Tunaomba sana msaada wa hali na mali. Majengo yakikaa sana yanaharibika na utunzaji wake ni gharama sana.

**MHE. ANNA J. GIDARYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu uhaba wa walimu. Walimu ni nyenzo muhimu katika nchi yetu lakini kwa muda mrefu kumekuwa na uhaba wa walimu. Pamoja na kuwa vyo vingi vimetoa idadi kubwa ya walimu waliokidhi vigezo vya kuajiriwa, lakini Serikali imeshindwa kuwaajiri walimu hawa. Katika shule za sekondari zote nchini kuna uhaba mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi. Nashauri Serikali ifanye mkakati wa haraka na wa makusudi kuondoa tatizo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni walimu wa sekondari kupelekwa kufundisha shule za msingi. Tunatambua kuwa tuna uhaba wa walimu katika shule zetu. Kitendo cha Serikali kuwachukua walimu hawa wa sekondari kwenda kufundisha katika shule za msingi si sawa kabisa kwa kuwa kila ngazi ya ualimu ina miongozo ya namna ya ufundishaji kwa masomo husika na madarasa yanayofundishwa na walimu wenyewe. Ni vema sasa Serikali ianze upya utaratibu wa kuajiri walimu kulingana na madaraja yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni ujenzi wa miundombinu ya madarasa kwa watoto wenyewe ulemavu. Katika maeneo mengi nchini miundombinu ya madarasa haikuzingatia mahitaji ya watoto wenyewe ulemavu, jambo ambalo linawafanya watoto hawa kusoma katika mazingira magumu mfano miundombinu ya madarasa, vyoo na hata njia za kupita siyo rafiki kabisa. Nashauri Serikali ihakikishe kuanzia sasa shule zote zinazotarajiwa kujengwa ziwe na mfumo maalum kwa watoto wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kuhusu Vyuo vya Ufundzi (*VETA*); kwa kuwa kwa sasa kwa kipindi kirefu Serikali haina mpango wa kuajiri pamoja na changamoto nydingi za watoto wengi kutofaulu wanapomaliza elimu ya msingi na hata kidato cha nne na kushindwa kuendelea na masomo jambo ambalo limesababisha wimbi kubwa la vijana mtaani na kuzurura hovyo. Serikali imepoteza nguvu kazi ya Taifa kwa kushindwa kujenga vyuo vingi vya ufundzi. Nashauri Serikali ijenge vyuo vingi vya mafunzo ya ufundzi kwa kila mkoa kadri iwezekanavyo ili kunusuru kundi hili la vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Sera ya Viwanda na Biashara, nashauri Serikali ifufue na kuimarisha Vyuo vya *VETA* katika mambo yafuatayo:-

- (i) Ifundishe mafundi mchundo ili kukidhi mahitaji ya viwanda vitakavyoanza;
- (ii) Mafunzo maalum ya ujasiriamali yatolewe; ma
- (iii) Chuo cha *VETA* Tabora kipelekewe vifaa vya kisasa kwani ni chuo kikubwa; kipelekewe walimu wa kutosha na gari la mafunzo ya *driving* na wanafunzi wanaomaliza mafunzo wapewe mitaji ili wajikwamue kimaisha na kuendeleza ujuzi wao (cherehani, vifaa vya ujenzi na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rushwa, nashauri mitaala ianzie kidato cha kwanza mpaka cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa walimu, nashauri Serikali iangalie kujaza nafasi kwenye shule zenyе upungufu mkubwa hasa vijiji ni wa walimu wa masomo ya sayansi na hesabu, kukamilisha maabara nchini na kuwapa mikataba walimu wa masomo ya sayansi na hesabu waliostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa shule kongwe, nipongeze Serikali kwa kukarabati shule kongwe hapa nchini. Naishukuru kwa kuona umuhimu wake kama vile Shule ya Wasichana Tabora lakin bado kuna kero kubwa ya uzio kwenye shule zote za Mkoa wa Tabora ambazo ni *Tabora Girls, Tabora Boys, Milambo na Kazima*. Niombe Serikali kuongeza bajeti kwenye shule hizo ili tukamilishe maana ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya watu mbalimbali wanaoidai Serikali. Niombe Serikali tulipe madai ya wazabuni, walimu na wakufunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya wasiojiweza/wasioona. Niombe wapewe walimu wa kutosha katika ngazi ya shule za sekondari na vyuo.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Ole Nasha kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wanafunzi wawe na ufaulu wa kiwango cha juu ni lazima Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Iboreshe na iwaongezee walimu mishahara na posho;

(ii) Iwapandishe madaraja wale walifundisha zaidi ya miaka mitatu;

(iii) Ijenge madarasa ya kutosha na maktaba pamoja na maabara katika shule za sekondari na shule za msingi;

(iv) Ijenge nyumba bora za walimu na ni muhimu ziwe na umeme ili walimu waweze kuandaa maazimio na maandalio ya kazi kwa masomo ambayo wataya fundisha siku inayofuata darasani;

(v) Isajili shule za awali (chekechea) ili kuweza kutambulika kisheria. Pia itengeneze mitaala kwa shule hizi na ziwe na miundombinu inayolingana na uhitaji wa watoto hao wa chekechea;

(vi) Ipeleke mashulen i vitabu vya kiada na ziada kwa wakati;

(vii) Itengeneze mitaala ya sekondari inayomuanda a kijana/mwanafunzi kujajiri. Mfano kuwe na masomo ya *needle work, cookery, wood work, metal work, fine arts* na kadhalika kama ilivyokuwa zamani katika shule mfano Morogoro sekondari.

(viii) Iwe na mtaala wa michezo ili kuweza kukuza vipaji kwa wanafunzi wetu;

(ix) Ijenge ofisi za walimu na kuweka samani katika ofisi hizo ili walimu waweze kuzitumia katika shughuli za kiofisi;

(x) Ijenge vyoo vya walimu na wanafunzi katika shule zetu. Mfano, katika Shule ya Msingi Yombo Dovya iliyopo Kata ya Makangarawe, Wilaya ya Temeke hakuna matundu ya vyoo vya kutosha; na

(xi) landae angalau mlo mmoja kwa siku katika shule zetu ili kusaidia wanafunzi waweze kuhamasika kuhudhuria masomo. Pia kupata mlo ambao utawasaidia kuwa na afya njema na kuelewa vyema masomo yao maana mwanafunzi akiwa na njaa hafundishiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namtakia Waziri wa Elimu na Naibu wake afya njema na Mwenyezi Mungu awape umri mrefu ili waweze kuyatekeleza majukumu yao ya kila siku.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kuwa watoto wasio na uelewa wa haraka kukaririshwa hakuepukiki kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu. Ni ukweli usiopingika kuwa wapo ambao wanaingia kidato cha kwanza kupitia maswali ya kuchagua ambayo hata mwanafunzi akifumba macho ana uwezo wa kupasi. Katika hili, naomba tufike mahali tubadili mtindo wa maswali tuwe na mtindo wa kupima uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niongelee kuhusu motisha kwa walimu. Naishauri Serikali kuwatia moyo walimu badala ya kuwavunja moyo kwani wanafanya kazi katika mazingira magumu. Inapotokea kupewa majibu yasiyostahili kutoka kwa viongozi wa Serikali au mfano Wakuu wa Wilaya kuwapa adhabu, hekima ingeweza kutumika kutatua matatizo yanayojitokeza. Nashauri Serikali kuweka mazingira rafiki ya kufundishia mfano walimu kuwa na nyumba karibu na mahali wanapofundisha. Niishauri Serikali kuhakikisha inaongeza fedha kwenye eneo la vifaa vyta kufundishia mfano karatasi za kutungia mitihani ili kutoa mitihani ya mwezi kiurahisi kwa ajili ya kupima maendeleo ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, napenda kuongelea kuhusu ukaguzi. Niishauri Serikali kujipanga kwa ajili ya kuhakikisha vifaa vinakuwepo kama magari ya kuwapeleka wakaguzi kwenye shule mbalimbali kwa ajili ya kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, niishauri Serikali kuwekeza katika kumkomboa mtoto wa kike kwa kuwajengea mabweni ili kuwaondoa katika shida hii ya kupata ujauzito wakiwa shulenii. Watoto wa kike

wameshindwa kufikia malengo yao ya baadae kutokana na mazingira yasiyo rafiki katika kujifunzia, mfano umbali mrefu na mapori kwa ajili ya kuzifikia shule hizo hivyo humo njiani kukutana na majanga ya kubakwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni ucheleweshaji wa fedha. Serikali inachelewesha fedha hivyo mipango mingi kushindwa kutekelezeka kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, nishauri juu ya chakula shulenii. Mpango wa chakula shulenii unasaidia wanafunzi kuwa na utulivu na kujifunza kwa urahisi. Niishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuwepo chakula shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba ni uhaba wa walimu. Niishauri Serikali kuliangalia hili kwani mwalimu kufundisha watoto mia moja darasa moja na ana vipindi vinne kwa siku na hivyo kuwa na madaftari 400 ya kusahihisha kitu ambacho hawezo mwalimu kufanya kwa usahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niishauri Serikali kuweka utaratibu wa kukariri ili kuboresha elimu ya Tanzania.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa kifupi sana juu ya Wizara hii ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Taifa lenye watu wasioelimika daima halitakaa liendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiendelea kushuhudia anguko la elimu licha ya Serikali kujitahidi kutoa elimu bure. Tumeendelea kushuhudia *quantityna* siyo *quality* kwenye elimu yetu. Kuzidi kuongeza usajili wa wanafunzi bila kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia ni sawa na kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeshuhudia upungufu wa walimu na kushuhudia uwiano wa wanafunzi kwa mwalimu ukiwa 1:50 na shule za awali 1:1159. Hata ije miujiza gani hapa hamna ufaulu. Vilevile uhaba ni mkubwa sana kwenye upungufu wa walimu na masomo ya sayansi hasa

*biology, physics, chemistry na mathematics* na ukizingatia tunasema Tanzania ya viwanda bila kuwa na msingi imara ya sayansi tangu shule ya msingi na maabara ni kazi bure. Cha kusikitisha zaidi walimu tulionao wengi wamekata tamaa kwa sababu mbalimbali kama kutokuwepo kwa motisha, kutopandishwa madaraja, mishahara duni, mazingira duni ya kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi za Serikali hazina miundombinu imara ya kufundishia mfano madarasa, vyoo, maabara, nyumba za walimu, ofisi za walimu na kadhalika. Hizi ndio sababu kubwa ukilinganisha na shule za binafsi ambapo wao uwiano kati ya mwanafunzi na mwalimu ni ya kuridhisha, idadi ya wanafunzi darasani ni chini ya 40, maabara za kisasa, maktaba na idadi ya walimu ni wa kutosha. Ni wakati muafaka sasa tuwe na mjadala mpanga kama Taifa juu ya hatma ya elimu yetu na nini kifanyike na hili lifanyike mapema sana. Bila hivi tutaendelea kuwa kichwa cha mwendawazimu huku tukifurahia idadi kubwa ya kusajili wanafunzi na ufaulu duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa ufupi naomba kukarabatiwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tarime (*TFDC*) ili kiweze kutoa elimu yenye tija ikizingatiwa kinahudumia Tarime, Ranya na Serengeti na ikiwezekana kijengwe *VETA*. Katika bajeti ya mwaka huu imeainisha vyuo 20 vitakarabatiwa na ama kuongezewa majengo.

Naomba sana Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tarime nacho kiingie kwenye ukarabati wa majengo na karakana zake ambazo zimechoka na majengo mengine hayajakamilika. Hili nimekuwa nikiliulizia sana, hivyo, naomba sana katika hivyo vyuo 20 na cha Tarime kiwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ukarabati wa shule kongwe ya Tarime ambayo ina michepuo zaidi ya saba na inachukua wanafunzi toka nchi nzima na ni shule ya *A-Level* tu kwani miundombinu yake imechakaa sana ni ya tangu mwaka 1973, hii siyo sawa kabisa. Vilevile tupewe gari la wagonjwa na ile *Land Cruiser* iliyochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuboreshwa kwa Chuo cha Ualimu Tarime. Naomba pamoja na uboreshaji huo ikiwezekana kibadilishwe na kuwa chuo kikuu hasa ikizingatiwa ukanda ule hatuna chuo kikuu ili kuboresha elimu na kuweza kuchukua wanafunzi wengi wanaokosa udahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu uhitaji wa shule ya wasichana Jimboni kwangu ukizingatia jamii ya Wakurya awali tulikuwa nyuma katika kusomesha watoto wa kike. Kwa kuzingatia pia Mkoa wa Mara tupo tano bora kwa idadi ya mimba za utotoni na kuacha shule kwa watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo langu (Halmashauri ya Mji wa Tarime) hatuna *high school* ya wasichana au hata mchanganyiko, bali tunayo *high school* moja tu ya Tarime ambayo ni wanaume tu siyo mchanganyiko, hivyo inatoa fursa kwa wavulana tu ambao wanatoka shule za kata mchanganyiko na hivyo kuacha wasichana. Kwa kuzingatia haya, naomba sana Serikali itupe fedha za kujenga *high school* ya wasichana maana tayari tuna uwanja pale Tagota, Kata ya Kenyamanyoni. Pia tunatarajia kupata fedha za Mogabiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba sana Halmashauri ya Mji, tunahitaji fedha kwa ajili ya *high school* ya wasichana tu ili tuwe na uwiano wa *high school* ya Tarime ambayo nayo ni chakavu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba majibu na utekelezaji.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba hii na kuiwasilisha vizuri Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuelekea kwenye uchumi wa viwanda kwa hakika tunahitaji wanasayansi

wengi zaidi Tanzania, tuna tatizo kubwa sana la upungufu wa walimu wa sayansi katika shule zote. Wanafunzi wanaochukua mchepuo wa sayansi wamekuwa wanakatishwa tamaa, pia wengi wamekuwa wanafanya vibaya kwenye mitihani ya mwisho. Tumejenga maabara hakuna walimu wa kufundisha *practicals* na *theories* pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kaliua karibu shule zote za sekondari za kata zina mwalimu mmoja tu na nyingine hakuna kabisa. Naomba Serikali isaidie upatikanaji wa mabweni ya wanafunzi katika shule ya *Kiliua High School* ambayo ndiyo shule pekee ya *high school* kwa Kaliua. Inawachukua wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali, lakini hakuna mabweni ya kutosha. Baadhi ya wanafunzi wanatumia madarasa kama mabweni kwa sababu ya shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa sana la kukosekana kwa nyumba za walimu hasa kwa shule za vijiji. Walimu wengi wanapangwa kufanya kazi, wanapokuta hakuna nyumba na mazingira magumu ya kufundishia wanaondoka kwenye vituo walipopangwa na wengine wanaacha kazi. Tunaomba Serikali ilete mpango maalum kuhakikisha miundombinu mashulenii inaboreshwaa hasa nyumba za walimu, vyoo na maktaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya vyuo vikuu vya umma ina hali mbaya, udahili wa wanafunzi unaongezeka kila mwaka lakini miundombinu yake haiboreshwii ikiwepo *library*, madarasa, maabara na kadhalika. Matokeo yake wanachuo wanasimama madarasani huku wakifundishwa pengine wanafanya *shift* *ku-share lectures room*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke kipaumbele kwa Chuo Kikuu cha SUA, Morogoro, chuo pekee Tanzania kinachotoa elimu ya juu kwa masuala ya kilimo na mifugo. Asilimia 75 ya Watanzania wote ni wakulima, wafugaji, tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda, kilimo lazima kipewe kipaumbele. Waziri Profesa Ndalichako naomba utupe mkakati maalum kwa chuo hiki ili wanafunzi

wanaotoka pale walete *impact* kubwa kwa wakulima na wafugaji Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubora wa elimu wa vyuo wa elimu ya juu; *TCU* ina jukumu la kuhakikisha vyuo vikuu hapa nchini vinakidhi vigezo vya udahili wa wanafunzi kutoa ithibati, kuhakikisha ubora wa elimu na kuidhinisha programu zinazofundishwa vyuoni. Katika kutekeleza majukumu *TCU* imekuwa inachelewa ufuutiliaji wa vyuo vya *private* na matokeo yake wanashatuka baadae ambapo wanafunzi/wanavyuo wameshadahiliwa, wameanza masomo na hata wamefanya mitihani ya mwisho. *TCU* inachukua hatua *too late* wakati wanafunzi wameshalipa ada wanafunzi wamefanya mitihani ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata taarifa ya *TCU* kugundua madhaifu makubwa katika Chuo cha *Mount Meru* wanafunzi kupewa yeti wakati walifeli, walimu zaidi ya asilimia 75 kuacha kazi kwa kutolipwa mishahara kwa miezi zaidi ya sita. *TCU* imeagiza wanafunzi wale warudi chuoni ndani ya miezi mitatu wafanye mitihani upya, hapa wazazi watalipa fedha nyngine. Hili ni tatizo kubwa, tunaomba maelezo ya kutosha wakati chuo hiki kinaendesha mitihani mpaka kutoa yeti walikuwa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kila Wilaya kuna chuo cha *VETA*; vyuo vya *VETA* vipatiwe vitendea kazi vyote muhimu na walimu wenye ujuzi wa kutosha kusaidia kufundisha watoto wetu wapate stadi na ujuzi wa kuendesha maisha yao na kuendeleza Taifa. Fedha inayotolewa na waajiri kwa ajili ya kukuza vipaji na kutoa mafunzo ya vitendo, *Skill Development Levy (SDL)* itolewe iende *VETA* ifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudzi za Serikali kuongeza fedha za malipo ya vyuo vikuu na kufikia idadi ya wanafunzi 122,623 bado wanafunzi wanaopata mikopo ni michache na wanaohitaji ni wengi zaidi. Serikali iongeze zaidi fedha ya mikopo kwa wanafunzi ili kila mtoto wa Kitanzania aweze kupata elimu ya juu.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Mawaziri wote, Mheshimiwa Profesa Ndlichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Naibu Waziri Mheshimiwa Ole Nasha, kwa usimamizi mzuri wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ndiyo msingi muhimu sana wa maendeleo ya mwanadamu na uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Pamoja na changamoto nyingi tunazopitia kama nchi, nimpongeze sana Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa elimu bila malipo kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Hii inasaidia Watanzania wanyonge nchini kupata fursa ya kupata haki yao ya msingi yaani elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya nchi yetu sasa ni kujenga uchumi wa viwanda. Ili kufikia uchumi huo wa viwanda ni lazima sekta ya elimu iwaandae vijana wetu mashulenii kupata elimu ya ufundi yaani stadi au ujuzi mbalimbali. Ili kufikia azimio hilo nashauri Serikali yetu ianzishe utaratibu wa kuwa na somo la ufundi kuanzia shule ya msingi. Kila shule ya msingi na sekondari angalau kuwe na darasa, angalau kipindi kimoja ambapo watoto wetu walioko shule za msingi watajifunza stadi mbalimbali kama vile uashi, useremela, ushonaji, uhunzi au uungaji vyuma, umeme na kadhalika. Hii itasaidia watoto kupenda masomo ya ufundi na baadae kupata fursa ya ajira kwenye viwanda vidogo vidogo na vikubwa hata kujajiri wenyewe. Katika kufanikisha jambo hili, tunaweza tukachagua shule moja ya msingi katika Kata na tukaanzisha darasa hilo la ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha ya kufundishia na kujifunzia. Tumekuwa na mjadala kwa miaka mingi nchini juu ya lugha ipi itumike kwa kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wetu. Historia ya nchi nyingi ambazo uchumi wake umekua kwa haraka sana katika miongo hii ya karibuni ni kutokana na kuongezeka kwa ubora wa elimu. Ubora wa elimu unatokana na kutumia lugha inayolewaka kwa wanafunzi na walimu wanaowawezesha wanafunzi kujifunza. Mfano, nchi za China, Korea, Malaysia na

kadhalika. Watanzania tunapozaliwa tunaanza kujifunza lugha za kienyeji (*mother tongue*) tukiingia darasa la kwanza tunakutana na lugha ya kiswahili na tunatumia kujifunza kwa miaka saba. Baada ya miaka saba, Mtanzania akienda sekondari anakutana na lugha mpya ya kiingereza. Matokeo ya mchanganyiko huo, wanafunzi wetu wanakuwa wakishindwa kumudu masomo ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kwenye mitihani ya Taifa ya kidato cha pili na nne, watoto wamekuwa wakiandika kwa lugha ya kiswahili katika kujibu maswali. Mtahiniwa anaweza akawa anajua kabisa hoja anayotakiwa kuieleza au kujibu, lakini kwa kuwa ameelewa kwa kiswahili wamekuwa wakishindwa kuandika kwa lugha ya kiingereza na badala yake anaandika kiswahili na kukosa alama kwa kuwa anatumia lugha isiyo rasmi kwenye somo husika. Hivyo nashauri ni muhimu Serikali iamue tufundishe masomo yote kwa kutumia lugha ya kiswahili ambayo ndiyo lugha mama na inaeleweka kwa Watanzania wote. Lakini kama tunadhani kiingereza ndiyo lugha bora zaidi, basi tufundishe kiingereza toka chekechea mpaka chuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti ubora wa elimu nchini; kitengo hiki ni muhimu sana katika kuangalia au kusimamia ufundishaji na ujifunzanji wa wanafunzi. Idara ya ukaguzi pamoja na umuhimu wake, lakini inakabiliwa na matatizo makubwa mawili, uhaba wa magari na kukosa fedha za kununulia mafuta ili waweze kuzifikia shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule zinakaa miaka mitatu mpaka minne bila kukaguliwa. Hii ni hatari kubwa sana kwa maendeleo ya elimu katika nchi yetu. Wizara ya Elimu ione umuhimu wa kuwawezesha wadhibiti ubora kufika mara kwa mara kwenye shule zetu ili kufanya ukaguzi na kujua kama walimu wanafuata miongozo vizuri, pia mikakati na njia za kufundishia zinatumika vizuri. Hii itasadia walimu kufundisha vizuri na kuwafanya walimu wawe mahiri katika masomo yao. Hili litaongeza ufaulu wa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, naipongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo hiyo. Pamoja na ongezeko hilo bado Wizara hasa Bodi ya Mikopo iwe makini katika kufanya tathmini ya wanafunzi wenye sifa ya kupata mikopo. Kuna baadhi ya watoto wanaotoka kwenye familia maskini wanakosa mikopo. Kigezo cha kwamba kipaumbele ni wale waliosoma shule za Serikali ndio hawana uwezo siyo sahihi sana, kuna watoto wamekuwa wakisomeshwa na Waheshimiwa Wabunge, Makanisa na watu wengine wasamaria wema baada ya kuona wazazi wao hawana uwezo au yatima, lakini wanapohitimu masomo yao na kuingia Chuo Kikuu hukosa mkopo kwa kuwa wamesoma shule zisizo za Serikali. Hivyo naomba sana Serikali itathmini kwa makini juu ya vigezo vya kupata mikopo kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zoezi la kuhamisha walimu kutoka sekondari kwenda kufundisha shule za msingi; zoezi hili limewakatisha tamaa walimu kwa kuwaharibia malengo yao. Wapo walimu ambao walikuwa na malengo ya kufundisha sekondari na kuendelea kusoma zaidi ili wafundishe Vyuo vya Ualimu, hata Chuo Kikuu. Unapomrudisha mtu ambae alikuwa analenga huko ukampeleka kufundisha shule ya msingi unaharibu malengo yake kitu ambacho ni kibaya na ninaamini hamuwezi kuwfanyia watoto wenu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, maandalizi ya zoezi hili hayakuwepo ni kwa nini Serikali haikutangaza ili wale wanaopenda kurudi kufundisha *primary wajitokeze* kwa hiari yao (naamini wapo) na wale wasiopenda wabaki. Ni hakika wapo walimu ambao wamebaki kufundisha sekondari bila

kupenda kukaa huko. Hii ingetoa nafasi mtu kwenda kwa utashi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, zoezi hili limegubikwa na fitna, ukabila, siasa na rushwa pale ambapo Afisa Elimu na Mwalimu Mkuu hawapatani na mwalimu fulani anampeleka *primary* kama adhabu.

Mheshimiwa Mweneyekiti, napenda pia kuongelea taratibu za uteuzi wa wanafunzi wanaohitimu darasa la saba kwenda sekondari hasa shule za kata. Katika uteuzi huu umbali hauzingatiwi, watoto wanatolewa kwenye shule za karibu na kuwapeleka mbali na nyumbani umbali wa kilometra saba hadi 10 kwenda na kurudi. Wazazi wanashindwa kutoa nauli kwa watoto wao. Naomba umbali uzingatiwe hasa kwa watoto wa kike ambao wanapewa mimba na bodaboda wanaowasafirisha kwenda mashulenii.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema kwa siku ya leo. *Alhamdulillah.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwashukuru Mawaziri wote wa Wizara hii Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Naibu wake Mheshimiwa Ole Nasha kwa kazi nzuri wanazofanya kuhakikisha elimu yetu inasonga mbele. Naomba nichangie Wizara hii kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani; nitoe pongezi nyingi kwa kazi nzuri zinazofanya na Baraza hili hususani ya kuandaa mitihani ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya walimu. Pamoja na kazi nzuri lakini napenda nitoe ushauri hasa kwenye utungaji wa mitihani wa kumaliza elimu ya msingi (*standard vii*). Kwa muda mrefu mtihani huu umekuwa ukitungwa kwa kutumia aina moja ya maswali (*multiple choice questions*) kutoa swali la kwanza hadi 50 pasipo kutunga aina nyingine ya maswali hasa yale yenye

kupima stadi nydingine kama kuandika. Hivyo nashauri Baraza litunge mtihani kwa kuchanganya aina nydingine ya maswali ili tuwapime wanafunzi wetu hasa kwenye kuandika na kushirikisha ubongo wao. Pia nashauri mtihani wa hisabati usitungwe kwa *multiple choice* ili kuwafanya wanafunzi wakokotoe wenye we pasipokupewa msaada wa majibu ya kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lugha ya kufundishia, wanafunzi wetu wengi wanafeli mitihani kwa kushindwa kujua lugha ya kufundishia hususani kiingereza pale wanapokwenda sekondari, hivyo naiomba Serikali kusisitiza lugha ya kiingereza ianze kufundishwa vizuri na walimu mahiri tangu elimu ya awali kwani ndiyo lugha atakayoitumia sekondari hadi chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Taaluma ya Ualimu, ni ukweli usiopingika kuwa walimu wetu wengi waliingia kwenye kazi ya ualimu kama kazi mbadala baada ya kazi za *career* zao kukwama hivyo kufundisha pasipo weledi na kwa ubora unaotakiwa hali inayopelekeea kuzalisha wanafunzi wabovu. Hivyo naiomba Serikali kuanzisha Bodi ya Taaluma ya Walimu ili kuweza kuhakikisha elimu yetu inatolewa kwa ubora unaotakiwa na pia inatolewa na walimu bora na siyo bora walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (*HESLB*), niipongeze Wizara kuititia Bodi ya Mikopo kwa kuwawezesha wanafunzi maskini kupata mikopo ya kuwawezesha kutimiza ndoto zao za kusoma elimu ya chuo kikuu. Lakini bodi hii imekuwa ni mwiba kwa wale wanufaika pale wanapoanza kurejesha mikopo hiyo kwani baada ya mabadiliko ya Sheria ya mwaka 2016 ambapo makato yalibadilika toka asilimia nane hadi asilimia 15 pasipokumuangalia mwalimu anakabiliwa na makato mengi kama kodi, *NHIF*, *PSPF* na *CWT* hali inayopelekeea mshahara kuwa chini ya 1/3. Niishauri Serikali kuwapunguzia mzigo wa makato walimu hawa kwa kuacha asilimia nane kwa wale walionufaika kabla ya mwaka 2016 na wale wanufaika baada ya sheria ya mwaka 2016 ndiyo waendelee

na asilimia 15 kwani sheria siyo maandika ya Biblia au Qurani hivyo inaweza kuletwaa Bungeni na kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule binafsi, hawa ni wadau muhimu sana katika kuisaidia Serikali kutoa elimu kwa wananchi. Lakini shule hizi zinapambana na changamoto nyingi sana katika uendeshaji hasa changamoto ya kodi na tozo mbalimbali, lakini pia gharama za ukaguzi za kudhibiti ubora. Hivyo, naomba Serikali yetu Tukufu izipunguzie kodi hizo ili zijiendeshe vema. Pia ningeomba Serikali iwe na utaratibu wa kuongea na wamiliki wa shule hizi juu ya changamoto mbalimbali na namna pia ya kuzitatuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukaririsha wanafunzi. Napenda niishauri Wizara kwenye suala la kukaririsha wanafunzi hasa pale inapobainika wamefeli mitihani au hawajui kusoma wala kuandika warudie tu. Pia kwenye shule binafsi ambazo imeonekana suala la kukaririsha ni mwiba kwao wapewe masharti kuwa kama wanafunzi ameshindwa kufikisha alama zinazotakiwa basi aruhusiwe kukariri ila kwa sharti la kutolipa ada upya kama kweli wanataka ku-*improve quality* na siyo *academic business*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mwendelezo wa mchango wangu wa maongezi. Tofauti na juhudi ndogo inayowekezwa na Serikali katika kumuandaa kijana kuweza kujajiri nje ya mfumo wa ikama ya Serikali, pia Serikali imeshindwa kusimamia sekta binafsi hususani *financial institutions* ili kuweza kutoa ajira za kutosha kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBL* leo ime-*downsize* waajiriwa wake kinyume kabisa na matakwa ya sera ya ajira. *TBL* amehamishia *payroll*/Mauritius kwa kuwa kwa kuhamishia *payroll* nchi ya Mauritius *definitely* mwekezaji anaingia *tax heaven* na kwa kufanya hivyo kumenyima vijana wetu ajira.

*TBL* imebaki na *gate keepers* na Idara ya Uzalishaji. Tanzania imebaki kuwa na idadi kubwa ya walevi ikiashiria pengine ndio sehemu ya faida ambayo nchi imejipanga kupokea kuititia uwekezaji wa *TBL*. Swali langu ikiwa hivi ndivyo, nini hatma ya Mfuko wa Bodi ya Elimu ya Juu? Vijana hawaingii kwenye soko jipya la ajira na walioko kwenye soko la ajira wanatolewa nje pasipo kauli yoyote ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taasisi za fedha (*banking industry*) it almost kama haipo. Benki za *Standard*, *NBC*, *Stanbic* pamoja na *Barclays* kazi ya *IT* yote inafanyika Kenya, ukija sehemu ya malipo kazi hizi zinafanyika nchi ya Chennai - India na servers za *IT* zikiwa hosted nchi ya *South Africa*. Personally nimewahi kumfuata Waziri wa Mipango kwenye kikao cha Bunge la Bajeti mwaka 2017/2018 na alichonieleza ilikuwa hii ni *common practice* kwa nchi za Afrika na hata Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu inazalisha vijana wa kutosha fani ya *IT - DIT* na *UDSM- Engineering Department* na kwenye baadhi ya taasisi za elimu ya juu, lakini kwa utamaduni huu hatuwezi kufikia malengo ya urejeshwaji makini kwa Bodi ya Mikopo. Aidha, wakati Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mpango akinijibu hoja hii ambayo nilimfikishia mezani kwake na akanijibu kuwa hii ni *common practice* amesahau nchi za Uganda na Mozambique wanafanya vizuri kabisa kazi za *IT* katika sekta za mabenki ziko *hubbed* nchini mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali ni vema Wizara ya Elimu ikafanya kazi hoja za *CAG* juu ya wasiwasi wake na uhimili wa Mfuko wa Bodi ya Mikopo. Ikiwa Mashirika ya uwekezaji yataachiwa yajiedeshe holela kwa kufuta ajira za vijana wetu hii itapelekea:-

(i) Kuchochea kasi ya ukosefu wa ajira kwa nchi yetu;

(ii) *Ku-drain skills, capability and knowledge* za vijana wetu wa fani ya *IT* kwa kuendelea ku-outsource kazi nydingi nje ya nchi kwani mwisho wa siku hata Serikali ni vigumu

sana ku-realize dividend na kupoteza fedha nyingi na hata kuondosha ari ya kuzalisha ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho Serikali ione namna bora ya ku-motivate walimu elimu ya juu. Madai ya walimu elimu ya juu hayafanyiwi kazi, walimu wamesimamishwa *promotions* kinyume kabisa na matakwa ya miundo ya utumishi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I submit*, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, naomba kutoa mchango katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi vyuo vikuu vyote duniani huwa na kazi tatu ambazo ni *training, research na consultancy*. *Research grants* hutolewa kwenye vyuo vikuu kwa kuzingatia ubora wa *research zinazofanyika na publications* kwenye *Four Stars Journal*. Utaratibu huu huhamasisha vyuo kufanya tafiti bora na kuchapisha makala mbalimbali kwenye *journals* za Kimataifa. Nashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia utaratibu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya zilizo nyingi hapa nchini kuna upungufu mkubwa wa walimu katika shule za msingi na sekondari pia katika Wilaya ya Miseni tuna upungufu wa walimu 750 katika shule za msingi. Pamoja na utaratibu huu mkubwa, utaratibu unaotumika kugawa walimu wachache wanaopatikana hauko sawa. Kwa mfano, mwaka 2014 katika Wilaya tatu Mkoani Kagera zilizopangiwa zaidi ya walimu 700 kila Wilaya huku Wilaya nyingine zikipangiwa chini ya walimu 10, jambo hili siyo zuri lazima uwekwe utaratibu mzuri wa kugawa vizuri walimu katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la wakaguzi kutotembelea shule za msingi. Kwa mfano, shule ya msingi Kajunguti iliyo Wilaya ya Miseni kwa muda mrefu

Wakaguzi hawajatembelea shule hiyo. Aidha, shule hiyo ina walimu wanne tu na walimu hao hawakai kwenye kata hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Gera kina changamoto nyingi. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Elimu alitembelea Chuo hicho na kutoa maelekezo mbalimbali ya kusaidia kuboresha ukarabati wa chuo hicho pamoja na maelekezo hayo mazuri hakuna utekelezaji wowote uliofanyika hasa kuhusiana na VETA kutakiwa kutumia fedha zao kukarabati baadhi ya majengo ya chuo hicho, baada ya VETA kutumia vibaya milioni 100 kukarabati baadhi ya majengo chini ya kiwango. Naomba Wizara ifuatilie suala hili kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono asilimia 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza viongozi na watendaji wote walioko katika Wizara hii kwa kazi nzuri waliyofanya wakiongozwa na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, hakika nawapa pongezi kubwa kwa bidii na uzalendo mlionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, kuna changamoto kubwa zinatakiwa kupatiwa ufumbuzi/ majibu ili kuleta tija na iweze kupatikana kwa nchi na wananchi kwa ujumla. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo; Vyuo vya Ufundı - VETA na uwekezaji mkubwa, Serikali kutumia mitaala kwa lugha ya kiswahili kwa vyuo vya ufundı/VETA kwa ajili ya vijana wanaomaliza darasa la saba, vyuo vya kati kutobadilishwa kuwa vyuo vikuu na elimu ya watu waliyoikosa (elimu ya watu wazima).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ufundı (VETA) kumekuwa na *speed* ndogo katika uwekezaji na ujenzi wa vyuo vya ufundı katika nchi yetu na kuzingatia kuwa eneo hili ndilo linalobeba vijana wengi ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa lolote duniani. Kutowekeza katika vyuo vya ufundı

kutasababisha wimbi la vijana kutojishughulisha na kazi na hasa vijana wengi kukimbilia kufanya biashara za kimachinga ambazo ni za kubahatisha na pia kuijunga na makundi ya hovyo/ulevi, kushiriki kwenye mitandao yenyе kuharibu maadili yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwekeze kwa kiwango kikubwa katika ujenzi wa Vyuo vya Ufundı (*VETA*) majengo, walimu, vifaa vya kujifunzia, wataalam wa fani ambazo zitakidhi soko la ndani na nchi jirani zinazotuzunguka, mitambo na teknolojia zinazoendana na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia mitaala ya kiswahili kwa Vyuo vya Ufundı (*VETA*) kwa ajili ya vijana wa darasa la saba kumekuwa na ufanisi mzuri kwa vijana wetu waliomaliza darasa la saba ambaao hujishughulisha na kazi ya ufundi kutengeneza magari, mafundi wa umeme wa magari, mafundi *welding*, mafundi waashi, mafundi mchundo, mafundi wa umeme wa majumbani, mafundi wa *computer* na kadhalika. Hawa wote kwa asilimia kubwa ni vijana waliomaliza darasa la saba na *form form*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo yote ni vema Serikali ikatumia mitaala ya kiswahili kwa Vyuo vya Ufundı na *VETA* ili itumike kwa vijana wetu wa *standard seven* na *form four* ambaao wote hawa ndiyo nguvu kazi kubwa inayojihusisha na fani za aina mbalimbali za ufundi. Kwa mafunzo hayo, vijana wataweza kuongeza tija na ufundi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyuo vya kati kubadilishwa kuwa vyuo vikuu; kumekuwa na ongezeko la kubadilisha vyuo vya kati na kuwa vyuo vikuu hali hii inadhoofisha vyuo vya kati ambavyo ndivyo vyenye kulenga kutengeneza ajira kwa vijana wengi. Naomba Serikali isitishé suala la kubadilisha vyuo vya kati kuwa vyuo vikuu na badala yake vyuo hivyo viimarishwe kwa kiwango kikubwa na miundombinu ya ufundi, wataalam, wakufunzi na kadhalika, uwekezaji wa vyuo hivyo kwa kuzingatia soko la ndani kama inavyofanyika nchi ya Singapore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Singapore inawekeza kwa kiwango kikubwa katika sekta ya elimu ya ufundi kwa kulenga soko la ajira kwa vijana na kuangalia soko la ndani na nje (nchi jirani). Nchi hiyo inatengeneza vifaa vingi vya kielektroniki kama vifaa vya umeme vya aina zote. Hii imesaidia vijana wengi kwa asilimia 95, vijana wako viwandani wanazalisha bidhaa mbalimbali.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, nianze kwa kuunga mkono hoja iliyopo mezani, sambamba na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri ya kuendeleza sekta ya elimu nchini na hili linathibitishwa na masuala yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni masuala ya elimu bure kwa watoto kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Serikali kila mwaka imekuwa ikitenga karibu shilingi bilioni 263.6 kwa ajili ya kuhudumia elimu ya watoto wa Kitanzania, ni budi kuipongeza Serikali kwa hatua hii kwani ni Serikali chache duniani zinatoa au kupatia wananchi wake elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ni kubwa ambalo Serikali ya Awamu ya Tano inafanya kwenye sekta hii ya elimu ni pamoja na mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu hapa nchini. Kila mwaka Serikali imekuwa ikitenga karibia 483 bilioni kwa mwaka kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi, hili ni jambo la kuungwa mkono maana karibia wanafunzi laki moja wamekuwa wakinufaika na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya pongezi hizo, pia nijikite kwenye changamoto zinazoikabili sekta hii ya elimu nchini nazo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utitiri wa nyaraka zinazokinzana katika kusimamia elimu ya msingi, sambamba na Sheria ya Elimu kutokukidhi mahitaji ya wakati uliopo. Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 (Na. 25) imepitwa na wakati,

haiendani na mahitaji ya sasa na hili liljitokeza baada ya mabadiliko ya Sera ya Elimu mwaka 2014. Aidha, kumekuwa na utitiri wa nyaraka unaotumika kusimamia utoaji wa elimu nchini ambazo kimsingi kwa sehemu kubwa zinakinzana. Ninapenda kuishauri Serikali ione umuhimu wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978, ifanyiwe marekebisho ya haraka ili iweze kuendana na Sera mpya ya Elimu ili iweze kuendana na wakati uliopo au mahitaji ya sasa. Pia Serikali iangalie namna ya kuifanyia marekebisho kupitia upya nyaraka na miongozo inayokinzana na kufanyiwa marekebisho ili kukidhi mahitaji ya wakati uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni mfumo wa ufundishaji wetu hasa kwa masomo ya kiingereza na kiswahili kwa shule zetu za awali hadi msingi hususani darasa la pili. Tafiti za kisayansi zinaonesha ufundishwaji wa lugha kwa binadamu huweza kujifunza vizuri na kwa urahisi lugha yoyote akiwa katika umri mdogo. Hivyo ni vema misingi ya ufundishaji wa lugha ikajengwa kimfumo ili kuwawezesha watoto kumudu lugha hizo kuanzia madarasa ya awali. Wakati sera inatambua kiswahili na kiingereza kuwa ni lugha rasmi zinazotumika katika ngazi mbalimbali za elimu nchini, bado ufundishaji wake haujajengwa kimkakati kuanzia elimu ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo sasa kwenye mfumo wa ufundishaji wanafunzi wanaosoma shule zinazotumia kiswahili kama lugha ya kufundishia kuanzia elimu ya awali, hawasomi somo la kiingereza hadi wafike darasa la tatu na kwa wale wanaosoma shule zinazotumia kiingereza kama lugha ya kufundishia, hawatakiwi kusoma kiswahili hadi wafike darasa la tatu ingawaje wote wanatarajiwa kufanya mitihani inayofanana kwa masomo hayo wafikapo darasa la nne.

Mheshimiwa Mwneyekiti, jambo hili kama litaachwa liendelee litakuwa na madhara makubwa kwa vijana wetu maana makundi yote wanakosa umahiri wa lugha nyingine kwa kukosa misingi yake kuanzia hatua za awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika changamoto hii ya mfumo wa ufundishaji katika lugha, ninapenda kuishauri Serikali iangalie upya juu ya suala hili hususani masomo ya lugha ya kiingereza na kiswahili, yafundishwe sambamba kuanzia elimu ya awali ili kuwajengea msingi unaofanana na mzuri vijana wetu na hivyo waweze kumudu vema masomo yao katika ngazi ya sekondari na elimu ya juu. Ni vema Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iongeze uwekezaji hasa katika ufundishaji fasaha wa somo la kiingereza ambalo ndilo linalotumika kuanzia elimu ya sekondari kwa shule zote hadi elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mihula na siku za masomo kwa shule za awali, msingi na sekondari nchini inayochochewa na changamoto kubwa ya usafiri nchini hasa kwa watoto wadogo wa shule za awali na msingi huhitaji kusoma kwa muda mfupi na kupumzika. Hivyo, nashauri Serikali iruhusu utaratibu wa kuwa na mihula mitatu kwa shule za msingi, awali na sekondari nchini kama inavyofanywa na nchi nyingi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa namna gani mfumo wetu wa elimu unaomuandaa kila mwanafunzi kwenda chuo kikuu, unawaandaa vijana kuingia katika mfumo wa Tanzania ya viwanda kama tunavyojadili Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mhitimu wa chuo kikuu wa Tanzania ni mwanafunzi wa aina gani? Mtu aliyefuzu katika sera *ya policy maker* ndio huyu anaenda kwenye utaalamu wa kuendesha na kusimamia viwanda (uchumi wa viwanda). Nashauri mfumo wa elimu yetu ubadilike kabisa, kuwepo na mjadala wa kitaifa, watu waseme tunahitaji wahitimu wa namna gani. Mfano, tunaweza kuwa na mfumo wa darasa la kwanza mpaka la nane, *then miaka miwili au mitatu ya kum-train mtu katika ujuzi fulani (specific areas of interest)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala wa kitaifa juu ya hatma ya watoto wanaopata ujauzito na ikabainika hawakujitakia (*victims*) wapewe nafasi ya kurejea shulenii badala ya kinachoendelea sasa hivi. Tafiti zinaonesha kuwarejesha watoto hawa shulenii (waliozaa) hakujaongezea idadi ya wanaopata mimba shulenii, hili suala badala ya kufanya siasa jamii ipime na kuamua kwa kutumia *case studies* za nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuharakishwa kwa vitabu vya kiada katika ngazi zote ili kutengeneza uelewa wa pamoja, mada za vitabu hivi pia *zi-reflect* mazingira na mahitaji ya Taifa na utandawazi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya usajili wa shule uzingatie huduma muhimu za wanafunzi ukiwemo uwepo wa miundombinu ya maji, vyoo vya uwiano sawa kwa wanafunzi na madarasa, kuliko tunachokiona leo. Asilimia 60 – 70 ya shule hasa za Serikali hukosa miundombinu, hivyo kuwa kero kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa chuo cha ualimu na vyuo vya ufundi katika Wilaya mpya ya Kyerwa, eneo hili lina vijana wengi lakini hakuna chuo chochote wala *high school* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubagua wanafunzi wa kupewa mikopo kwa kigezo kuwa ametokea shule nzuri sekondari, wanafunzi hawa hawatendewi haki. Pengine walibahatika kupata mfadhili katika hatua hizo. Kwa kuwa huu ni mkopo hawatendewi haki kunyimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya walimu na wahadhiri. CAG ameanisha kuwa Chuo Kikuu cha Ardhi kinadai malimbikizo ya mishahara ya walimu na marupurupu yao, hii inapunguza morali kwa watumishi hao, Wizara iombe Serikali kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sera ya elimu bure. Sera ya Elimu Bure haitekelezeki kwa kuwa changamoto ni

kubwa sana katika maeneo ya shule hizi, madai ya wasichangie ni mufilisi, pengine kauli mbiu ingebadiili na kuwa changia elimu bure iwe bora, wazazi wangeshiriki kwa chochote kuboresha mazingira ya kufundishia (miundombinu) vyoo, madarasa, vyakula na kadhalika.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pamoja na pongezi hizo ninapenda kuiomba Wizara, Wilaya yetu ya Mbogwe ipo katika mchakato wa kuanzisha kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari ya Mbogwe, je, Serikali haioni kwamba muda umefika sasa kuhakikisha kwamba shule ya sekondari Mbogwe inafunguliwa rasmi hasa baada ya ujenzi wa mabweni na bwalo tayari vimekamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lillipo ni kutokuwepo kwa chanzo cha uhakika wa maji, niiombe Serikali itoe kipaumbele cha kuifungua shule hii ya Mbogwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu ni muhimu kuanzishwa kwa vyuo vya ufundi katika kila Wilaya, niiombe Serikali yetu ihakikishe chuo cha ufundi kinaanzishwa katika Wilaya yetu ya Mbogwe, pia tunaiomba Serikali itoe kipaumbele katika kuhakikisha kuna kata tunazojitahidi kukamilisha shule zao za kata za Wanda, Isebya na Ngemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamejitahidi sana katika kuchangia nguvu zao katika kujenga madarasa na maabara pamoja na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi ni changamoto kubwa. Kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi, niiombe Serikali itupatie ili hatimaye vyuo vya ufundi viweze kupata wanafunzi wazuri wa kuweza kujunga na vyuo hivi vya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha naiomba Serikali kuhakikisha inatusaidia kupatiwa fedha zaidi ili kuhakikisha

nyumba za walimu pamoja na vifaa vyta kujifunzia ikiwa ni pamoja na vitabu na vifaa vyta maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa mkakati wake wa kutoa elimu bure kwa elimu ya msingi hadi sekondari. Naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuwa hai mpaka leo hii, na kuniwezesha kufika mahali hapo salama na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara husika ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuandaa Bajeti nzuri yenye mrengo wa kimaendeleo na uboreshaji wa sekta zote muhimu zinazohusiana na Wizara hii, sekta ya elimu, sayansi na teknolojia. Bajeti hii inakwenda kutekeleza mipango mbalimbali iliyopangwa kufanyika katika Awamu hii ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuendelea kutoa elimu bure nchi nzima kuanzia shule za awali mpaka kidato cha nne. Hii ni hatua nzuri inayopaswa kupongezwa kwani idadi ya watoto wetu wanaoanza shule imezidi kuongezeka maradufu. Hatua kama hizi zinahitaji kupongezwa na kuishauri Serikali pale panapojitokeza changamoto ili Serikali iweze kuboresha na watoto wetu waweze kupata elimu bora yenye tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto kubwa sana kwa upande wa walimu wa masomo ya sayansi, aidha, upungufu huu unachangia pia kutokuwa na wanafunzi wa kutosha katika masomo ya sayansi, aidha, upungufu huu utatupelekea kutotimiza ile ndoto ya Tanzania ya viwanda kwani dhana nzima ya viwanda inahusishwa na sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuendelea kutilia mkazo katika masomo ya sayansi na ikiwezekana

kutoa motisha kwa walimu ambao watakwenda kusomea sayansi na wale watakaokuwa wanafundisha masomo hayo, aidha na kwa wanafunzi pia ili kuwafanya wapende masomo ya sayansi kwa upande wa wanafunzi na kwa upande wa walimu motisha hiyo itawafanya kufundisha kwa hamasa kubwa watoto wetu na hivyo kufika lengo la kuzalisha vijana wengi watakaomiliza michepua ya sayansi na kuja kulisaidia Taifa letu kukuza uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe inapeleka walimu wa kutosha hasa maeneo ya vijiji, kwani ndio kuna changamoto kubwa ya upungufu wa walimu na nyumba za kuishi. Aidha, tuna changamoto kubwa ya upungufu wa walimu wa nyumba za kuishi. Aidha, naishauri Serikali kuhakikisha inaongeza matundu ya vyoo katika shule zetu zote nchini na hasa shule za vijiji ndizo zinazokutana na changamoto kubwa za mapungufu hayo kwani hata muamko wa wazazi katika kujitolea na kuchangia kwa hiari masuala ya kujenga matundu ya vyoo, nyumba za walimu na madarasa imekuwa ni mgumu sana kulinganisha na shule za mijini, ambazo nyingi hazina changamoto hizi. Hivyo, ni vema katika bajeti hii hasa ikazingatia masuala muhimu katika kuboresha sekta nzima ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kuhusu ubora wa mifumo ya elimu yetu nchini, malalamiko hayo yanapaswa kuchukuliwa kama fursa na Serikali na si ya kuyabeza kwani wadau wa elimu wote ni Watanzania na wanataka maboresho ama mabadiliko yafanyike ili kuokoa sekta nzima ya elimu na mdororo unaoweza kuja kuleta shida hapo siku za mbeleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikae na wadau wa elimu kuchukua mawazo yao na kusikiliza ushauri unaotolewa na sisi Wabunge na kuufanya kazi bila kuwa na elimu bora yenye tija, hatuwezi kuwa nchi ya viwanda na tutasababisha watu wetu kuwa watumwa ndani ya nchi yao kwani watakuja wawekezaji kutoka nje na kukosa wataalam kutoka ndani na hivyo kuja na watalaam toka nje kuja kushika nafasi hizo na kuwafanya wazawa kuwa watumwa.

Ili kuliepuka hilo Serikali haina budi sasa kuwekeza vyta kutosha katika elimu ili kuwa na Taifa bora ni lazima sekta ya elimu iwe imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakuwa tunajidanganya tukisahau sekta ya elimu na kuzipa kipaumbele sekta nyingine huku tukisema nchi imepiga hatua, ni wajibu wa Serikali kuzipa kipaumbele sekta zote lakini zile zinazobeba mustakabali wa nchi zikaangaliwa kwa upana wake, tukumbuke hakuna hatua nchi inapiga kama watu wake wakiwa wanapata elimu isiyokuwa bora na isiyoendana na viwango vyta kimataifa.

Mheshimiwa Spika, jimboni kwangu tuna changamoto nyingi sana katika sekta ya elimu, mimi nikiwa kama mwakilishi wa wananchi na mdau mkubwa wa elimu nimejaribu kutatua baadhi ya changamoto hizo kwa gharama zangu nikishirikisha wadau mbalimbali ili tu wananchi wangu wapate elimu bora, nimeshawahi kutoa vitabu mbalimbali kwa elimu ya msingi na sekondari, kuchangia madawati, ujenzi wa ofisi za walimu, madarasa na matundu ya vyoo na nimekuwa nikifanya hivyo kila mara na pale inapobidi ili kupunguza changamoto hizo pasipo kuisubiria Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Serikali inapokuja katika jitihada zake za kuleta maendeleo basi ikute sisi kama wadau tumeshaanza kushiriki ili Serikali nayo iweze kumalizia, lakini bado tuna changamoto nyingi ambazo sasa Serikali naiomba ije na majibu ili wananchi wajue zitatatuliwa kipindi gani? Tuna changamoto ya vyumba vyta madarasa na kupelekeea chumba kimoja kutumiwa na wanafunzi hadi 150 katika shule ya msingi Mtongani, japo changamoto hiyo ipo katika shule zote, lakini kwa shule hiyo tajwa hapo imeelemewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tuna changamoto ya samani za ndani katika ofisi za walimu zilizopo, hakuna *furniture* hivyo kuwafanya walimu wanapokuwa katika majukumu yao ya kila siku kuyafanya katika mazingira

magumu sana, na tatizo hilo lipo kwa shule zote, na baadhi ya shule zina upungufu mkubwa wa ofisi za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tuna changamoto pia ya nyumba za walimu, walimu wetu Kibaha Vijijini hawana nyumba za kukaa na ikitokea ikawepo basi nyumba moja huwapasa kukaa walimu zaidi ya wawili, hali hiyo sio nzuri kwani huwarudisha nyuma walimu wetu kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya matundu ya vyoo, hali hii huwafanya walimu na wanafunzi kutumia sehemu moja jambo ambalo si utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wanalalamika sana kuhusu stahiki zao ambazo ni za muda mrefu, hali hii ya madai haya huwarudisha nyuma kiutendaji walimu wa jimboni kwangu, tuna changamoto ya upungufu wa walimu mkubwa sana, walimu waliopo ni wachache na hawatoshelezi na kukidhi vigezo, naiomba Serikali kuititia Wizara ije na majibu ya changamoto hizo tajwa wakati wa majumuisho ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kujuu ina mkakata gani kutatua changamoto nilizokwisha zitaja hapo juu ili wananchi wa Kibaha Vijijini wapate elimu bora na walimu pia wawe katika mazingira mazuri na ifike mahali walimu wakisikia wanapelekwa Kibaha Vijijini basi wafurahie na isiwe kama ni adhabu kwani kutakuwa tayari na mazingira rafiki ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Elimu, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako, Naibu Waziri Mheshimiwa Ole Nasha, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri, na vilevile kwa kazi kubwa wanayoifanya

kuhakikisha elimu inaendeshwa vizuri nchini kwetu katika kukuza rasilimali watu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge la Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa taarifa nzuri iliyojaa uchambuzi na mapendekezo mazuri na ya kimkakati ambayo yakizingatiwa yote kwa ujumla wake yanaweza kuboresha kwa kiasi kikubwa sana sekta hii ya elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, napenda nijikite kwenye suala la *VETA*. *VETA* ni taasisi ya Serikali ilioanzishwa kwa ajili ya kutoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi, hizi zikiwa ni stadi za kazi kwa ajili ya kuandaa vijana na jamii kwa ujumla waweze kuijingiza katika shughuli zenyе kuwapatia kipato cha kujikumu kimaisha na pia kuchangia katika pato la Taifa. Taasisi hii ya *VETA* inafanya kazi kubwa ya kuwapa vijana wetu stadi za kazi, lakini pia inatoa nguvu kazi kwa ajili ya viwanda. *VETA* pia ndio mojawapo ya mihimili ya kufanikisha mkakati wa Serikali kuanzisha viwanda. Bila nguvu kazi yenye stadi zinazohitajika na viwanda hatutaweza kufanikisha mkakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kulingana na sheria ilioanzisha *VETA* ya mwaka 1994, *VETA* ni taasisi ambayo inaendeshwa kwa michango inayotolewa na waajiri kwa njia ya *Skills Development Levy(SDL)* ambapo waajiri wanakatwa asilimia 4.5 ya fungu la mishahara (*wage bill*) kila mwezi. Hata hivyo *VETA* inapata theluthi moja tu ya makato hayo, theluthi mbili zinabaki Serikalini. Sehemu kubwa ya waajiri wanatamani *VETA* ipate 100% ya makato yote yaani 4.5% inayokatwa ili soko la ajira lipate mafundi mahiri walioiva vizuri na mafunzo toka *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi inatakiwa iwajibike kwa waajiri ambao ndio wana gharamia uendeshaji wa taasisi hiyo. Hawa waajiri wako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Watu Wenye Mahitaji Maalum. *VETA* ipo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kimsingi *VETA* inatakiwa iwajibike kwa waajiri kwa njia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kuhakikisha waajiri kuwa mafunzo yanayotolewa na *VETA* yanaendana na mahitaji ya waajiri na kuwa mitaala ya *VETA* inayotumika kufundishia inabadilishwa mara kwa mara kulingana na mahitaji ya waajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili kuhakikisha matumizi ya fedha za *SDL* (1/3 *SDL*) ambayo ni michango ya waajiri kuendeshea *VETA* inatumika kama iliyokusudiwa. Pia waajiri wakipendezwa na matumizi ya michango yao wanaweza kutafuta njia nyingine za ziada za kuisiaidia *VETA* ili ikidhi matarajio yao waajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu uliopo sasa ambao waajiri na *VETA* wapo kwenye Wizara mbili tofauti, *VETA* haitaweza kuwajibika kwa waajiri moja kwa moja. Hivyo uhusiano wa *VETA* na waajiri wanaoigharamia ni dhaifu. Hii inaweza kufanya waajiri kukosa imani na utendaji wa *VETA* maana hawana mamlaka juu ya utendaji wao. Waziri wa Elimu hana nguvu ya kisheria ya kuitisha kikao cha waajiri kuzungumzia masuala ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi zinazohitajika katika soko la ajira, kwa sababu hawa waajiri wako chini ya Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Waziri anayehusika na kazi hana nguvu ya kisheria ya kuiagiza mamlaka inayosimamia mafunzo ya ufundi stadi yaani *VETA* kurekebisha mitaala yao kutegemea mabadiliko katika soko la ajira maana *VETA* iko chini Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi kwa sasa inahusisha waajiri (wenye viwanda) kutoa mafunzo wakishirikiana na kupokezana na vyuo vya ufundi stadi (*Dual Apprenticeship Training*). Utaratibu huu unahitaji ushirkiano wa karibu sana kati ya waajiri (viwanda) na vyuo vya ufundi stadi. Hali ya namna hii inahitaji miongozo ya Wizara mama. Tunapokuwa na Wizara mbili tofauti ni vigumu sana kutengeneza miongozo hiyo kwa sababu tofauti za majukumu ya Wizara husika na hata usimamizi wake unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri *VETA* iwekwe chini ya Wizara moja na waajiri yaani Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Watu Wenye Mahitaji Maalum. Hii italeta mahusiano mazuri kiutendaji na italeta ufanisi kiutendaji kwenye kipindi hiki muhimu cha kuandalia mafundi stadi kwa ajili ya ustawi wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina vitengo vingi sana. Wizara inashughulikia Elimu ya Juu, Elimu ya Vyuo vya Kati, Elimu ya Sekondari, Elimu ya Msingi, Elimu ya Awali, Elimu ya Watu Wazima, Elimu ya Ufundu, Elimu ya Mafunzo ya Ufundu Stadi, Taasisi ya Mitaala *T/E*, Baraza la Mitihani, *TCU*, *NACTE*, *VETA*, *TEA*, Maktaba ya Taifa, Bodi ya Mikopo na taasisi nyingine. Pia changamoto zilizopo katika Wizara hii ni nyingi sana na ni vigumu kuweza kupata muda wa kusimamia kikamilifu elimu na mafunzo ya ufundu stadi ambayo ina mtizamo tofauti na idara nyingine za elimu. Pia kuna hatari ya kufananisha elimu ya ufundu stadi na elimu ya msingi au sekondari ambapo sehemu kubwa ya elimu ya ufundu stadi ni vitendo kuliko nadharia tofauti na elimu ya sekondari na msingi. Upana na utawala wa Waziri wa Elimu (*span of control*) ni pana sana jambo ambalo linaweza kuathiri ufanisi katika utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko nchi nyingi duniani ambazo sekta ya ufundu stadi ipo chini ya Wizara ya Kazi mfano, Korea Kusini, Indonesia, Singapore, Malaysia na kadhalika. Nashauri Serikali irejeshe *VETA* iwe chini ya Wizara ya Kazi kama ilivyokuwa zamani na hasa kipindi hiki tunapojenja uchumi wa viwanda ili *VETA* iweze kuwa na ushirikiano wa karibu na waajiri kwa nia ya kutoa stadi zinazohitajika kwenye soko la ajira yaani *demand driven training* *A/NING* katika kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Wizara imeonesha kwenye ukurasa 26 na 27 umezungumzia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (*VETA*). Wilaya ya Ileje kuititia Mbunge tulipata ufadhilli wa Balozi wa Japan na kujenga majengo ya *VETA* na kutokana na uwezo mdogo

wa Wilaya tuliwasiliana na Wizara yako na kuomba Serikali iichukue hii *VETA* na kuiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauriwa tuongeze eneo, na kupima eneo la *VETA* ndipo Wizara kuitia *VETA* Makao Makuu wataichukua na kuiendesha. Yote haya yamefanyika na kwa barua ya Halmashauri ya lleje ya tarehe 05 -11-2017 kuainisha kuwa tayari masharti yote yamekamilishwa na sasa tunaomba Serikali ichukue *VETA* Wilaya kuiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuona kuwa katika hotuba ya Waziri hakuna popote *VETA* ya Wilaya ya lleje kuainishwa ili hali ni ahadi na maagizo ya Wizara yenewe, *VETA* hii imesimama kwa miaka mitatu sasa hata mfadhili yaani Balozi wa Japan amesikitika sana na ameshindwa kuendelea kusaidia hadi *VETA* izinduliwe na ianze kazi. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze wana lleje hii *VETA* yetu wataichukua lini? Kwa hiyo, nguvu za Mbunge na mfadhili ziende bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa pendekezo kuwa Wizara ioneshe jinsi mitaala ya elimu ya ufundi stadi inaendana na mkakati wa Serikali ya uchumi na viwanda. Vilevile mitaala ya ufundi stadi iboreshwe na kuwekewa madaraja ya *standard seven, form four, form six* na wa diploma kwa maana ya *kuzi-upgrade VETA* nyingine *into polytechnics* ambazo zinatumia ujuzi juu na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara sana kwa kutupatia fedha za kukarabati shule za msingi kongwe tatu. Kati ya shule kongwe za msingi 14 za Wilaya ya lleje, shule zilizosalia nazo ni kongwe, na miundombinu yake ya mwanzo na ni za ujenzi wa kutumia udongo. Kwa hiyo, ni hatarishi kwa wanafunzi maana zimeharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lleje haina maktaba ya Wilaya tofauti na Wilaya nyingine, hili ni tatizo. Kuweka maktaba kungesaidia hata watu wengine kupenda kujisomea zaidi ya wanafunzi na watu wazima, lakini vilevile kwa wanafunzi na raia wanaohitaji kujiedeleza kimasomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejitokeza mtindo wa kugeuza vyuo vya kati kuwa vyuo vikuu, hii ni hatari. Vyuo vya kati viendelezwe kuwa vyuo bora kwa kutumia teknolojia sahihi na uhitaji wa viwanda na viweze kuzalisha watoa huduma katika viwanda vidogo na kwa viwanda vikubwa. Kwa mfano Singapore wameboresha vyuo vya kati, vinachangia ajira kwa asilimia 95 kwa kuimarisha mitaala ya kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwangukia Mheshimiwa Waziri anisaidie nipaye shule ya sekondari ya wasichana lleje tena yenye mrengo wa sayansi, hisabati na teknolojia na lugha za kigeni. Tunajitahidi kujandaa kama Wilaya kuanza shule hiyo, lakini Wilaya yetu ni maskini mno, ila wananchi wamejitolea maeneo mawili hata ya Ibada na Mlaly ya ekari 22 kila moja kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari za wasichana kidato cha kwanza hadi cha nne. Naomba sana Mheshimiwa Waziri anipe jibu la kututia moyo lleje hususan kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lleje ina changamoto nyingi. Kubwa ni upungufu wa walimu 201 wa elimu ya msingi na wa shule ya sekondari hasa wa sayansi takibrani 50; na zaidi Idara ya Elimu Msingi haina gari tangu mwaka 2010. Shule za A-Leve/ni mbili tu Wilaya nzima. Tunahitaji kuongezewa shule nyingine mbili. Miundombinu ya shule zetu zote ni mibovu, haina vyoo, ofisi za walimu, nyumba za walimu, mabweni na madarasa. Tunaomba sana sisi wa Wilaya za pembezoni tuangaliwe kwa jicho la huruma, tumesahauliwa kwa muda mrefu. Tunaomba utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika kuona hadi sasa Serikali hajapeleka vitabu vya kiada vya darasa la nne licha ya kwamba wanafunzi hawa wanajandaa na mitihani ya Taifa ya darasa la nne. Je, Serikali haioni kama inatengeneza mazingira ya kuwafelisha wanafunzi kwa kutopeleka vitabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtihani wa kidato cha nne mwaka 2017 shule zilizoibuka bora 100 za Serikali ni sita tu kati ya hizo. Kwa miaka mingi sasa shule za watu binafsi zimekuwa zikifanya vizuri ukilinganisha na shule za Serikali. Utafiti unaonesha kwamba matokeo mazuri ya shule binafsi unatokana na motisha kwa walimu, mishahara mizuri kuliko ile ya Serikali na mazingira bora ya kufanya kazi. Tangu mwaka 2014 Serikali hajawahi kupandisha mishahara kwa watumishi wakiwepo walimu. Hivyo walimu wengi wa shule za umma wamekosa *moral* ya kufanya kazi kwa bidii. Litakuwa jambo jema kama Serikali itajifunza mbinu za kufundishia na kujifunzia kutoka shule binafsi. Pia mishahara ingeboreshwa kwa watumishi wa umma ili walimu waliokata tamaa warudishe *moral*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe hauna chuo cha *VETA* hivyo naishauri Serikali ijenge chuo katika mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongozi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ya kuboresha elimu kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ushauri na mapendekezo yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maombi ya kusaidiwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni shule ya sekondari Mgombezi ambayo ipo nje ya Mji wa Korogwe Mjini, ina vijiji sita na vitongoji kumi. Watoto wa kike wanatembea kilometra tano kwenda na kurudi, kwenye mashamba ya mkonge, usalama wa watoto hawa ni mdogo na mwendo

ni mkubwa kiasi kwamba wanachoka kwa kutembea kabla ya kuanza masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya sekondari Chifu Kimweri iko nje ya mji, ina vijiji vinne, vitongoji saba watoto wanatembea umbali mrefu kiasi kwamba wanachoka kabla ya masomo. Naomba iangaliwe kupewa fedha za ujenzi wa mabweni ili watoto wa kike wabaki shulenii kwa ajili ya kuwanusuru na majanga yanayowasibu barabarani na nyumbani kukosa muda wa kujisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Korogwe Mjini tumetenga eneo la kujenga chuo cha ufundi Mgombazi, tunaiomba Serikali isaidie kuwaunga mkono wananchi ambao wameanza kwa nguvu zao wenyewe kama inavyosaidia kwenye vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kutoondoa masomo ya uraia na historia shule za msingi na sekondari na vyuo vya ualimu. Aidha, wakuu wa vyuo, walimu wa shule za msingi na sekondari wanaokaimu nao wapewe mafunzo ya uongozi (*ADEM* - Bagamoyo) kama zamani na kukaguliwa mara kwa mara kuinua elimu vyuoni na sekondari pia hasa Chuo cha Ualimu Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri na Naibu Waziri wake kwa uchapakazi wao zaidi kwa hotuba iliyoletwa kwetu imeandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Nkasi kuna zaidi ya sekondari 22 zinazofanya kazi lakini zote zinakabiliwa na changamoto mbalimbali, za upande wa Nkasi Kusini jimboni kwangu zina shida sana za walimu wa sayansi. Naomba Serikali ituletee walimu hawa kila wanapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, majengo ya maabara bado hayajakamilika katika shule nyingi zikiwemo shule za

sekondari za Milundikwa, Chala, Ninde Wampembe, Sintali, Kala, Kipande, Nkundi, Kate na Ntuchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maalum kabisa shule ya sekondari ya Milundikwa iliyohamishwa toka makazi ilipokuwa na kupelekwa Kasu ina shida ya kukosa hata nyumba moja ya mwalimu na ukizingatia ni shule ya *boarding* kwa kidato cha tano na sita. Watoto wa kike wanakaa peke yao mabwenini, hawachungwi kabisa na *matron* wakati wa usiku wakipata shida. Naomba nyumba hata moja tu. Vilevile miundombinu yake yote iliyobaki hakuna mabweni ya watoto wa kiume, lakini madarasa bado hayatoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zote za kata hazifanyiwi ukarabati zikijengwa. Serikali haizipatii fedha ya ukarabati zinaharibika tena, upo umuhimu kuzipa fedha ya ukarabati. Tunaomba Wizara iwe inatembelea shule hizi za pembezoni kuona hali mbaya iliyoko huko ili waweze kubuni namna ya kuwapa motisha watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu waliohamishwa kwenye shule ya sekondari ya Milundikwa iliyotwaliwa na Jeshi kwa maelekezo ya Serikali hawajalipwa haki zao. Naomba walipwe ili waendelee kuchapa kazi kwa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chala naiomba Serikali kutofanya ukarabati wa chuo kwenye majengo yake ya sasa kwani si mali yetu na Askofu wa Jimbo la Sumbawanga ambaye ndiye mwenye majengo ametoa ilani ya kufukuza chuo ili ayatumie majengo yake. Wananchi kuititia vikao vya *WDC* tumeamua kutoa majengo ya iliyokuwa iwe shule ya sekondari Isoma ambayo ina majengo mengi yanayotosha kuanzia na ukarabati ukifanyika pale itakuwa ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari nyingi hazina miundombinu ya maji na mfumo wa maji machafu. Shule zote nilizotaja hazina maji ya uhakika na hivyo

miundombinu ya maji ya usafi wa vyoo na matumizi yake ni changamoto mfano *Nkundi secondary school*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali mtekeleze yote niliyoyachangia hapo juu.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri Profesa Ndalichako na Naibu wako Ole Nasha kwa hotuba yako nzuri iliyosheheni mambo mengi mazuri kuhusu elimu nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia hoja katika masuala matatu; kwanza, elimu ya awali (tazama hotuba ukurasa 78), pili; elimu maalum (tazama hotuba ukurasa 81) na tatu; Programu ya Lipa kwa Matokeo (*EP4R*) ukurasa wa123 – 124.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza elimu ya awali, Serikali iweke kipaumbele katika uanzishwaji wa shule za chekechea, shule za awali kabla ya darasa la kwanza (*preschools*). Kwa kuwa msingi mzuri wa elimu huanzia katika shule za awali, nashauri ijihusishe rasmi katika uanzishwaji wake na kuajiri walimu waliofuzu kutoa elimu kwa ngazi hiyo (*early childhood development*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iandae mitaala ya elimu ya awali. Nashauri Serikali ianzishe taasisi mahsusini ya elimu ya awali kama ilivyo Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siri ya mafanikio katika shule za binafsi ni kwa sababu wamezingatia kumuendeleza mtoto kuanzia umri mdogo kabisa (*3 -5 years*) kabla ya kuanza elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuelekeza juhudini za kuboresha elimu nchini kuanzia ngazi ya elimu ya awali,

naomba Serikali izingatie kuwa shule za awali zilizoko ndani ya shule za msingi nchini haziwasaidii watoto wadogo walio chini ya umri wanaotoka au kukaa mbali na shule, hususan kwa jamii za wafugaji wanaoishi mbali na shule. Hivyo Serikali izingatie haja ya kusogeza huduma za elimu bora ya awali hadi kwenye vitongoji. Elimu hii itolewe na walimu waliosomea tofauti na sasa ambapo elimu hii ndani ya vituo vyta ngazi ya vitongoji hutolewa na walimu wasio na ujuzi (*failures* wa darasa la saba au kidato cha nne) wanaoajiriwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu maalum; ukienda ukurasa wa 81 wa kitabu cha hotuba ya Waziri kifungu cha 80(i) na (ii) utapata maelezo yasiyojitosheleza kuhusu usimamizi wa elimu maalum. Natoa rai kwa Serikali/Wizara ijipambanue kwa ufasaha zaidi kuhusu elimu maalum. Naunga mkono suala la elimu jumuishi lakini nashauri kuwepo kwa vitengo mahsus ni dani ya shule zetu kuanzia chekechea hadi vyuo kwa ajili ya nyanja mbalimbali za elimu maalum. Mbadala wake zianzishwe shule mahsus kwa ajili ya ulemavu wa aina tofauti. Shule za viziwi (chekechea – vyuo), vipofu (chekechea – vyuo), wenye mtindio wa ubongo (chekechea – vyuo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu programu ya lipa kulingana na matokeo katika elimu (*EP4R*), huu mpango ni mzuri sana. Naomba uongezewe bajeti na wigo wa miradi ya kutekelezwa upanuliwe kulingana na mahitaji ya shule husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika Wilaya yangu ya Longido fedha hizi pamoja na mambo yameshaelekezwa, lakini pia zielekezwe katika kununulia gari la shule. Sekondari zetu saba zilizo katika *remote areas* ambapo huduma muhimu na dharura ikitokea ziko mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za sekondari za bweni Wilayani Longido ambazo zinastahili kuwa na gari la shule ni pamoja na shule ya wasichana Lekule iliyoko Gelai Lumbwa umbali wa kilometra 90 kutoka barabara ya lami na makao

makuu ya Wilaya, Flamingo sekondari Kata ya Meirugoi ambayo ipo zaidi ya kilometra 90 kutoka barabara ya lami, shule ya sekondari Ketumbeine iliyoko umbali wa kilometra 60 kutoka lami, shule ya Enduimet sekondari kilometra 110 kutoka Longido Mjini na barabara ya lami, sekondari ya Tingatinga kilometra 50, sekondari ya Engeremibor kilometra 40, sekondari mpya tarajiba ya Matale kilometra 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule za *private* na Serikali; ni ushauri wangu kwa Serikali yangu tukufu kuwa wazazi wanaopeleka watoto shule binafsi wanapeleka kwa hiyari yao, na shule hizo huchuja au kupanga viwango vyta kuingia kwa utashi na hutangaza. Hivyo hakuna sababu ya Serikali kuingilia kati. Serikali izidi kuimarisha walimu wenye sifa za kufundisha sekondari wawe ni wale wenye ufaulu mzuri kwenye shahada zao. Serikali iondoe kodi ambazo haziko kwenye shule za Serikali. Hili likifanyika litasaidia kupunguza ada. Pale ambapo shule za Serikali zitakuwa zimeboreshwa, jamii itahamia kwenye shule za Serikali. Mimi nasomesha watoto shule za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*), chombo hicho ni muhimu lakini kama Serikali haitakuwa makini katika kuajiri, basi itajikuta kuwa imekuwa Tume ya Chuo Kikuu kimoja badala ya vyuo vikuu vyote. Kama ilivyo sasa, karibu viongozi wote wanatoka Chuo Kikuu Dar es Salaam, hivyo mtazamo wa *TCU* ni wa Chuo Kikuu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri; ili kuboresha utendaji wa *TCU*, viongozi wake ni lazima wawe wenye kupata shahada zao katika vyuo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; viongozi wa *TCU* wawe ni wale wenye uzoefu wa kufundisha katika vyuo tofauti, hususani ndani na nje ya Tanzania. Hili likifanyika litaiwezesha *TCU* kuwa na maamuzi yasiyolemea upande wa chuo kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udahili wa wanafunzi *TCU*, naiomba sana Serikali idahili wanafunzi na kuwapeleka kwenye vyuo vyote binafsi na Serikali kwa kufuata miundombinu. Hali ilivyo sasa kwenye vyuo vya Serikali vina wanafunzi wengi kuliko uwezo wa vyuo hivyo. Hii ni pamoja na *UDSM, DUCE* na Mkwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *COSTECH*– Tume ya Sayansi fedha zinazoelekezwa kwenye Tume ya Sayansi za utafiti zioanishwe na Shahada za Udaktari au Uzamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu watakaofundisha sekondari wawe ni wale ambao wana daraja la kwanza au la pili (*first class or upper second class*). Faida ya hili litaongeza heshima kwenye kada ya ualimu maana itajulikana kuwa mwalimu ni mtu aliyefanya masomo vizuri. Hii ni sawa na wahadhiri wa vyuo vikuu. Jambo hili pia hufanyika Malawi na Zambia. Katika nchi hizo mtu akitambulisha kuwa ni mwalimu wa shule za msingi au sekondari anapewa heshima kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya pili ni kwamba watoto wetu wataanza kufundishwa kiingereza na watu wanaoweza kuongea lugha hiyo. Hivyo hakutakuwa na ukakasi katika kuongea na kuandika kiingereza kwa kada zote. Hata kama mtu ataishia darasa la nane, atakuwa na uwezo wa kuongea kiingereza. Katika ulimwengu wa sasa lugha pia ni mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dubai kuna madereva *taxi* 12,000. Katika hao takwimu zinaonesha karibu 2,700 ni Wakenya na hakuna takwimu za Watanzania sababu kubwa ni lugha ya kiingereza.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa kasi kubwa inakumbwa na ongezeko la idadi ya watu. Hali hii kwa njia moja au nyingine itaathiri utendaji wa Wizara ya Elimu. Mheshimiwa Waziri ameliona hili na amejipanga vipi katika kuwashudumia wananchi hawa kwa kuongeza idadi ya walimu na mahitaji mengine ya lazima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahitaji ya viwanda, nchi yetu inaelekea kuwa Taifa la viwanda. Viwanda vinahitaji rasilimali watu watakaofanya kazi yenyе ufanisi na zenye tija. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu ni lazima iandae mikakati kwenye vyuo vyetu vikuu ili kuwawezesha vijana wetu wanaohitimu mafunzo yao waweze kufanya kazi katika viwanda kwa ufanisi na tija ili kutimiza ndoto ya nchi yetu kufikia maendeleo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto za elimu ya juu, kama Mheshimiwa Waziri alivyosema katika hotuba yake (*page 42*) kwamba elimu ya juu ni nguzo muhimu ya kuiwezesha Serikali kufikia malengo yake ya maendeleo kwa kuzalisha rasilimali watu. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze katika vyuo vyetu kuna wahadhiri wa kutosha? Iwapo ni wachache, je, hawana manyanyaso kwa wanafunzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba mafunzo ya baadhi ya shahada uzamili hapa nchini si chini ya miaka minne na mafunzo hayo hayo ni chini ya miaka miwili kwa nje ya nchi? Namuomba Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba mafunzo ya shahada ya uzamivu katika vyuo vyetu yana usumbufu. Unaweza kusoma mpaka ukajukuu bado hujapata kuhitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaombe wahadhiri wetu wa vyuo vikuu wafanye wajibu wao kama walivyotumwa wa kuzalisha rasilimali watu kwa maendeleo ya Taifa letu. Wahadhiri wawe tayari kurithisha ujuzi wao kwa vizazi vipyaa na kufanya hivyo ndiyo taifa letu litakaposonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema. Vilevile nipende kukupongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, mama yangu, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, kwa jitihada na kazi unayoifanya katika kuhakikisha elimu yetu inapiga hatua mbele. Lakini

pamoja na jitihada za Serikali, bado sekta ya elimu ina changamoto kubwa sana, hivyo kwa bajeti ambayo imetengwa hamtaweza kumaliza changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara ya walimu; walimu ni watu muhimu sana katika maisha yetu kwani wote tumefika hapa tulipo kutokana na walimu, lakini leo hii mwalimu anaonekana kama hana thamani na ni kazi ya waliofeli kuwa waimu wa shule za msingi kwani mishahara wanayopata ni midogo sana kiasi kwamba walimu wanaishi kwa shida na pesa wanayopata ni ndogo sana. Niiombe sana Serikali, mwalimu apewe kipaumbele, aongezewe mshahara ili naye afurahie kazi yake. Walimu wengi hawafurahii kazi ya ualimu, wanafanya kwa shida tu kutokana na wanachokipata kuwa kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu ya shule zetu; shule nydingi hazina miundombinu mizuri vijijini na hata mijini, madarasa mengi hayapo katika mazingira mazuri, wanafunzi wanateseka sana kwani hata vyoo nya shule zetu nydingi bado ni changamoto kubwa. Sasa tuijulize hawa watoto wanasonaje bila kuwa na vyoo? Kwa hali hii lazima watoto hawa wataendelea kupata magonjwa kama kipindupindu. Lakini hata vyoo ambavyo viro ni vichafu sana, hakuna hata maji, niiombe sana Serikali iweke maji katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu nydingi hakuna madarasa ya kutosha, watoto wanasona chini ya miti, juu na mvua, vyote vyao. Ninaiomba sana Serikali ijenge madarasa ya kutosha. Kwa mfano katika Wilaya ya Kigoma Vijijini, shule nydingi hazina madarasa ya kutosha, kama vile shule za Nkema, Mwandiga, Nyamhoza, Kizenga, Bugamba, Kiziba na Nyamigura madarasa ni machache sana, lakini vyoo hakuna, madawati hakuna. Niiombe sana Serikali iweke miundombinu ya shule zetu kuanzia katika madarasa, madawati, vyoo na vifaa nya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wenye mahitaji maalum; watoto hawa katika suala la elimu bado

wamesahafulika sana, kwani bado shuleni hawapo wengi lakini pia miundombinu ya shule zetu bado inambagua mtoto mlemavu. Watoto hawa hawana vifaa vyao maalum na vilevile walimu wa watoto hawa bado ni wa kutafuta, vyoo vilivyopo watoto hawa wanapata shida sana kutumia kutokana na jinsi vilivyojengwa, havimpi *support* mlemavu huyu ili aweze kuvitumia. Wapo watoto hawawezi kutembea kabisa, wanatambaa na vyoo ni vichafu sana, hakuna maji, tunamuweka mtoto huyu katika hali gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Mwandiga, Kigoma Vijijini kuna shule ya Nkema, ina watoto walemavu lakini shule hii haina madarasa, vyoo, watoto hawa wanapata shida kubwa, walimu wa watoto hawa hakuna. Niombe sana Serikali iwajali watoto hawa kuanzia katika vifaa, walimu, miundombinu ya ujenzi, madarasa na vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chombo cha kusimamia elimu; kama kweli tunataka kupandisha hadhi elimu yetu, ni muhimu Serikali iunde chombo kimoja ambacho kitakuwa na kazi ya kusimamia elimu yetu. Chombo hiki kiwe maalum kwa kuangalia elimu yetu, kiweke mikakati ya kuhakikisha elimu yetu inapiga hatua; chombo hiki kisimamie kuanzia ngazi ya shule za msingi mpaka vyuo vikuu, hii itatusaidia sana kuboresha elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandishaji madaraja kwa walimu; hii imekuwa changamoto kubwa sana kwa walimu. Serikali imekuwa ikipandisha walimu madaraja kutoka daraja moja A kwenda B, lakini mwalimu huyu anaishia kupata barua tu, stahiki zake kama ongezeko la mshahara hapati kwa wakati na wapo ambaao wamestaafu lakini mafao yake amepigiwa hesabu kwa daraja A wakati alipanda daraja miaka 16 iliyopita; hii siyo haki kabisa. Kiukweli walimu wanateseka sana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali mtu apewe stahiki yake mara tu aapopanda daraja, kama ametokea daraja A mwezi Mei, basi mwezi huo huo apookee mshahara wake wa daraja jipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu michezo ya UMITASHUMTA, michezo ni uhai kwani hujenga afya na vilevile hutengeneza mahusiano mazuri ya ujirani mwema. Lakini sasa hivi michezo hii haina nguvu, imesahaulika sana. Niombe sana Serikali irudishe michezo shulenii, inasaidia sana wanafunzi kiafya, kimwili na kiakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu walimu wa sayansi, hili limekuwa tatizo sugu, shule zetu hazina walimu wa sayansi, hii inafanya wanafunzi kuchukia masomo ya sayansi, sasa kama tunataka kuwa nchi ya viwanda ni lazima tuweke walimu wengi wa sayansi ili tupate wataalam wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa ya awali kabisa kuwa naunga mkono hoja hii ya Mhesahimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako (Mb) Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa asilimia mia moja. Aidha, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa William Ole Nasha (Mb) Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Waziri wake kwa uaminifu na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Profesa Ndalichako amethubutu kutembelea Wilaya ya Namtumbo na kukagua maendeleo ya ujenzi wa Chuo cha VETA kinachojengwa katika eneo la Suluti, Wilaya ya Namtumbo. Niombe radhi kwa niaba ya wananchi wa Namtumbo waliojipanga kumpokea lakini walichelewa kuja au tuseme kwa fikra za wananchi hao Mheshimiwa Waziri aliwahi sana kuingia Wilayani humo, akizingatia kauli mbiu ya kipenzi cha wana Namtumbo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wetu ya "Hapa Kazi Tuu!"

Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako (Mb) wananchi wangu watafurahi sana kama utawapa fursa ya kukukaribisha kama mkombozi wao kwa kuwazawadia mambo makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Wilaya na hivyo mafunzo yatakapoanza kutolewa tutapata fursa ya kushiriki katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili utoaji wa fedha (milioni 180) zilizowezesha kujenga majengo ya kisasa ya shule ya msingi mpya katika Kitongoji cha Miembeni/Chatisa na Kijiji cha Likuyu Mandela na hivyo kuondoa jengo hafifu lililoezekwa kwa nyasi liliokuwa likitumika kwa watoto wa darasa la kwanza hadi tatu na kama sehemu ya shule ya Likuyu Mandela walitenganishwa na Mto Usio na daraja la uhakika na lisilopitika kipindi cha masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kukipokea Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mputa na kuwawezesha wanafunzi kufanya mitihani yao chini ya mitaala ya *VETA*. Mheshimiwa Waziri , chuo hiki kina changamoto lukuki ambazo zinahitaji kushughulikiwa na Wizara yako.

Mhesimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri licha ya kuzikabili changamoto za Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mputa, utusaidie kuweka msukumo wa hali ya juu kwa majengo ya Chuo cha *VETA* cha Namtumbo yakamiliike kujengwa kwa wakati kwa awamu zote mbili ikiwa ni pamoja na kujengwa mabweni ya wanachuo na kantini ili mafunzo yaanze kabla ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Waziri, tunacho Chuo cha Ualimu cha Nahoro kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Songea na Namtumbo (*SONAMCU*). Nimehakikisha mfuko wa jimbo (*CDCF*) unachanga katika kutekeleza masharti ya kukiwezesha kiendelee kutoa mafunzo ya ualimu ngazi ya astashahada.

Aidha, mmetufungulia shule nne za kata kati ya 23 tulizonazo kutoa elimu ya kidato cha tano na sita. Nguvu za wananchi zimechangia katika kujenga majengo mapya yaliyohitajika katika kuziwezesha shule hizo za sekondari za

Kata za Nanungu, Luegu pamoja na Namabengo kuweza kutoa elimu ya kidato cha kwanza hadi cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri atusaidie kuboresha utoaji wa elimu katika shule hizo hususan majengo, walimu na vitabu.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la upungufu wa walimu wa shule za msingi; hakuna elimu bila walimu, elimu bure bila walimu haitasaidia kama hakutakuwa na idadi ya kutosha ya walimu wenyewe weledi na motisha ya kufanya kazi ya kufundisha. Ningependa kujua Serikali imeajiri walimu wangapi mpaka sasa ili kukabiliana na upungufu huo? Serikali ina mkakati gani endelevu wa kuhakikisha tatizo la upungufu wa walimu linatoweka kabisa? Serikali imepanga kuajiri walimu wangapi katika mwaka wa fedha 2018/2019?

Mheshimiwa mwenyekiti, niongelee tatizo la uhaba wa vitabu katika shule zetu za msingi, unakuta kitabu kimoja kinasomwa na watoto watano mpaka sita, hii inaleta usumbufo mkubwa kwa watoto wetu na uelewa kuwa mdogo. Je, ni lini Serikali itahakikisha tatizo hili la upatikanaji wa vitabu linakwisha katika shule zetu? Mbali na upatikanaji mdogo wa vitabu bado vitabu hivyo vina mapungufu makubwa ndani na tatizo hili limekuwa likijirudiarudia pamoja na Wabunge kulisemea humu ndani. Je, tatizo ni nini? Ni akina nani wanafanya uhakiki huo wa vitabu? Kwa sasa hivi tunategemea nini kwenye uelewa wa watoto wetu? Itakuwaje kama vitabu vina makosa kwa watoto wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka juzi nilimuomba Mheshimiwa Waziri kulifanyia kazi kwa haraka suala la wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi waweze kupelekwa kwenye shule za sekondari za wanafunzi walio

na ulemavu, lakini hilo halikufanyika. Wanafunzi hawa wamechanganya na wanafunzi wasio na ulemavu, hii hatuwatendei haki watoto hawa. Kwa mfano shule ya watoto wenye ulemavu Njia Panda darasa lilikuwa na watoto 20 na wote wamefaulu, nimpongeze mwalimu mkuu na walimu wote wa shule hiyo kwa kazi nzuri waliyofanya kwa watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba kwa sababu uelewa wao ni wa taratibu, hivyo wanatakiwa kuwa na walimu wanaowafundisha na kuwafuatilia kwa karibu. Si kwamba watoto hawa hawana akili ila wanahitaji ufuatiliaji. Hawa watoto kumi waliofaulu wamepelekwa shule ya ufundi Moshi wanane na wanafunzi wawili wamepelekwa shule ya sekondari Mbulu. Niombe kujua, Serikali ina mpango gani na watoto hawa? Ni lini shule za sekondari za watoto wenye ulemavu zitajengwa za kutosha ili watoto wetu wapelekwe huko ambapo watapata walimu na vifaa kwa ajili ya aina ya ulemavu walio nao? Tusipofanya hivyo watoto hawa watafeli wengi na maisha yao hayatakuwa na mwisho mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichangie kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri inayofanya hasa katika sekta hii ya elimu, sayansi na teknolojia. Nampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa maamuzi yake ya kutoa elimu ya msingi bure. Watanzania wengi hasa wenye kipato cha chini watapata haki ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri katika maeneo machache; moja, nashauri Serikali iangalie namna ya kurejesha asilimia mbili iliyochukuliwa mwaka 2014 kutoka *Skills Development Levy* asilimia nne kwenda kwenye Bodi ya Mikopo kwa ajili ya dharura. Kwa sasa urejeshwaji wa

mikopo hiyo ni nzuri basi asilimia mbili irudi kwenda kwa *skills development* (*VETA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya vyuo vyetu nya ufundi (*VETA*) ni mbaya sana na tunahitaji mageuzi makubwa. Leo hii kila kitu ni kutumia teknolojia ya *computer* (*IT*). Kwa mfumo wetu wa sasa wa *VETA* tunatumia mfumo wa miaka ya nyuma ambapo hazifundishi kutumia *IT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ufundi kwa mfano wa magari (umeme) yote inategemea mfumo wa *IT* wa kutumia *diagnostic equipment*. Umeme wa majumbani pia vyombo na vifaa vyenye (*sensors*) kutumia programu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawahitimu wengi wa vyuo vikuu (shahada)/wenye digrii. Kwa sera ya viwanda tunahitaji kuwa na mafundi (*technician*). *VETA* kwa mfumo wa kisasa unaweza kuwa mkombozi wa ajira kwa Watanzania. Mfumo wa elimu wa *apprentice* utasaidia Watanzania mbalimbali wenye ujuzi wa ufundi kupata elimu rasmi na kujiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Wizara kutukubalia *VETA* Manyara kupata mradi wa Wajerumani wa mafunzo ya *apprentice*. Tunashukuru pia kwa kutuweka katika bajeti ya kukarabati na kuongeza karakana ya Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia mnapogawa fedha za miradi ya kukarabati mgawe kwa uwiano kwa kufuata idadi za shule katika Halmashauri na idadi ya watoto na mazingira. Sisi Halmashauri ya Babati tumepata shule moja tu, shilingi 60,000,000; Halmashauri yenyewe shule mbili kati ya 137. Wilaya zenye shule 30 zimepata shule mbili zaidi ya shilingi 170,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri *COSTECH* ipatiwe vyanzo nya kudumu ili angalau ipate shilingi bilioni 100 kwa mwaka. Hali ya utafiti nichini ni mbaya na sehemu kubwa inategemea ufadhili wa nje kwa kuendesha tafiti zao; tukumbuke mfadhili hutoa anapokuwa na maslahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kirudishwe chini ya Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji kwa usimamizi, wataweza kikitendea haki kwa kufuatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe unaifuu wa kodi ya mapato kwa mashirika na wadau kwenye michango yao ya kwenye sekta ya elimu au huduma za jamii.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naomba kuchangia hotuba ya bajeti hii ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; binafsi nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Joyce Ndalichako, dada yangu kwa kumudu Wizara hii na sote tunaona namna anavyochapa kazi. Namuombea asirudi nyuma, azidi kusonga mbele ili kuhakikisha anatatua changamoto za elimu, ukosefu wa nyumba za walimu, ukosefu wa vyoo, ukosefu wa madarasa, ukosefu wa maabara na vifa vya kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi nijielekeze kwenye changamoto mbalimbali zinazoikabili Halmashauri yetu ya Uvinza.

Mhesimiwa Mwenyekiti, moja; tunazo shule ambazo zinajengwa na wananchi na kumaliziwa na Halmashauri na pia Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano shule ya sekondari Mwakizego; shule hii imepokea hadi walimu wa Serikali na ina jumla ya madarasa kumi. Imejengwa ili kupunguza umbali wa watoto wetu kutembea hadi llagala sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe dada yetu Mheshimiwa Joyce Ndalichako mambo mawili; kwanza, kuisajili shule hii kabla ya mwaka wa bajeti tarehe 30 Juni, 2018. Pili, nimuombe aje atembelee shule hii ili aone jitihada za wananchi wa Mwakizega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hawa wapya inakaribia miaka miwili hawalipwi pesa zao za uhamisho hadi leo. Sambamba na hili walimu wengi wana malalamiko ya kutolipwa pesa zao za stahiki zao mbalimbali ikiwemo na kucheleweshewa kupandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule mbili za *Lugofu Girls High School* na *Lugofu Boys*; shule hizi ziko kwenye majengo yaliyoachwa na *UN* (Kambi ya Wakimbizi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi pia Serikali imezisahau, kwa nini wasipewe pesa kwa ajili ya kujenga mabweni mazuri ya kisasa na vyoo? Kwa nini vyoo wanavyotumia haviko kwenye hali nzuri kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo shule za msingi nyingi ziko kwenye hali mbaya sana, tunayo shule ya msingi Anzerani ina madarasa mawili zaidi ya miaka minane na nyumba ya walimu *two in one*, imepaliliwa lakini hakuna pesa za kuimalizia.

Tunaomba Wizara itupatie upendeleo wa fedha za ujenzi wa madarasa ili tuweze kujenga madarasa kwenye shule zote zenye uhaba wa madarasa. Kwa mfano shule ya msingi Msimba ina darasa moja kwa zaidi ya miaka 10. Sambamba na haya tunao uhaba mkubwa wa walimu wa shule za msingi, hali ya miundo mbinu ni mbaya, vyoo na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Uvinza hatuna Chuo cha *VETA* na wanafunzi wanaomaliza shule ya msingi na sekondari wengi hawapati ufaulu wa kuendelea na shule za sekondari na *high school*; kwa nini Serikali isianzishe Chuo cha *VETA* llagala ili kunusuru vijana hawa?

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza viongozi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya; Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako (Mb) Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Naibu Waziri Mheshimiwa William T. Ole Nasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu ubora wa walimu na mabadiliko ya mitaala; ubora wa walimu umeelezwa na wachangiaji wengi kuwa umeshuka; maelezo haya si sahihi, wengi wanazungumzia matokeo ya shule ya *private* kama kigezo cha kushuka kwa elimu kwa shule za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri changamoto zilizopo ambazo wengi wanahusisha na kushuka kwa elimu zifanyiwe kazi. Changamoto hizo ni upungufu wa miundombinu ya shule za vijijini, mafunzo kazini kwa walimu na kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna madai ya kubadilika mara kwa mara kwa mtaala jambo ambalo si sahihi, wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi tangu tupate Uhuru mtaala umebadilishwa mara ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wa sekondari kuhamia msingi, naipongeza Wizara kwa uamuzi huu kwani walimu wamepelekwa shule za msingi ambako kulikuwa na uhaba mkubwa wa walimu. Walimu hawa wamepata mafunzo ya kuweza kuwapa ujizi na maarifa hata watoto na si kama wanavyodai wajumbe wengine kuwa walimu wa sekondari hawawezi kufundisha; si ya kweli. Vyo vingi siku hizi wanawapeleka walimu tarajiwa wa *diploma* na *degree* kwenye mazoezi ya kufundisha (*BTP*) kutumia shule za msingi za jirani na chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wasimamizi Ubora wa Elimu; Idara hii inakabiliwa na changamoto ya rasilimali fedha na vitendea kazi, ili kuweza kukagua shule zote na kutoa ushauri uliotarajiwa katika kuboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi hii haina fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo ya magari yao. Nashauri

Wizara kutenga fedha nydingi na kuwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri nydingi zinapoanzishwa basi na Wadhibiti Ubora wa Elimu wapelekwe. Halmashauri ya Mji wa Nanyamba haina Wadhibiti Ubora wa Elimu hivyo ukaguzi wa shule inategemea wale wa *Mtwara DC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyuo vikuu vya binafsi, vyuo hivi vina changamoto nydingi ikiwemo uhaba wa wahadhiri, majengo na mazingira yasiyo rafiki ya kufundishia na kujifunzia. Serikali iongeze ufuatiliaji katika vyuo hivi ili vile visivyokuwa na sifa au vinavyoshindwa kutimiza vigezo vifungwe.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (*The Mwalimu Nyerere Memorial Academy*) kilichopo Kigamboni Dar es Salaam kuna *faculty* (fani) ambazo watu wamesomea lakini huko kwenye soko la ajira wanaambiwa *faculty* hizo hazitambuliki katika mfumo wa ajira (*caurdon*). Nakutajia *faculty* hizo ni *Politics And Management of Social Development* na *Gender and Development (GD)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali naomba sana ufanuzi wa jambo hili kwa kuwa ni killio cha wahitimu wengi ambao hivi sasa wapo mtaani zaidi ya miaka mitatu bila ya kupata ajira Serikalini. Mheshimiwa Waziri, jambo hili ni aibu kwa Serikali kwa kuwa chuo hiki ni cha Serikali na miongoni mwa vyuo vikongwe hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa ni kwamba chuo hiki hakijakamilika kwa jengo la hosteli la ghorofa tatu, ambalo limeanza kujengwa zaidi ya mika mitano sasa. Jengo hili lilikusudiwa kuwa *hostel* ya wanafunzi wa shahada ya pili (*Masters Degree Students Hostel*) mwaka huu nimeona mmetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya *Development Project*. Sasa je, hii bilioni moja ndiyo inakwenda hapo au sehemu nydingine tofauti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, tupatieni fedha ya mabweni katika Shule ya Sekondari Mchinga ili shule iweze kupandishwa hadhi kuwa ya A-Level. Shule ni kubwa, ipo sehemu nzuri na imezungukwa na shule nyingi za sekondari hivyo *catchment area* yake ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri, nitumie lugha ya sanifu ya kiswahili, chonde chonde, itazameni Mchinga sekondari, muipatie mabweni ili shule iweze kupanda hadhi hiyo. Shukrani sana.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia Wizara hii muhimu ya Elimu, Sayansi na Technolojia. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri ya kuanza kuboresha elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uboreshaji wa elimu kumekuwa na changamoto kubwa ya walimu kukosa ujuzi na mbinu za kufundishia, sambamba na walimu kutovutiwa na mazingira ya ufundishaji, jambo ambalo linawafanya kutofundisha kwa bidii na hivyo kusababisha kushuka kwa ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi zimepelekea kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao ya kuhitimu. Uchambuzi wa matokeo ya mitihani ya taifa ya kidato cha pili na cha nne mwaka 2017 unaonesha wastani wa asilimia 60 ya wanafunzi waliofanya mitihani hiyo walipata daraja la nne na sifuri. Nashauri Serikali ijikite katika kushughulika na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa walimu, kwa mujibu wa takwimu za *BEST* za mwaka 2016 na 2017 idadi ya walimu kwa shule za msingi imeshuka kutoka walimu 191,772 mwaka 2016 hadi kufikia 179,291 mwaka 2017, ikiwa ni anguko la asilimia 6.5 na kufanya uwiano wa walimu na wanafunzi kuwa 1:50. Aidha, katika shule za awali, idadi iliopungua ni walimu 1,948 na kufanya uwiano wa walimu

na walimu na wanafunzi kuongezeka kutoka 1:135 mwaka 2016 hadi kufikia 1:159 mwaka 2017 badala ya 1:25 ambao ni uwiano unaokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za sekondari kuna uhaba mkubwa wa walimu kwa baadhi ya masomo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hisabati kuna upungufu wa walimu 7,291, bailojia kuna upungufu wa walimu 5,181, kemia kuna upungufu wa walimu 5,373 na fizikia kuna upungufu wa walimu 6,873; hii ni kwa mujibu wa takwimu za *BEST* za mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Elimu ya Msingi za Mikoa (*BEST Reginal Data 2017*) walimu 7,743 wanatarajiliwa kustaaifu kati ya mwaka 2018 na 2019. Aidha, takribani walimu zaidi ya 30,000 wana umri wa zaidi ya miaka 51 ya kuzaliwa, hivyo na wao wanatarajiliwa kustaaifu muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa hakuna elimu bila walimu Serikali inatoa majibu gani katika maswali yafuatayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu gani kimesababisha upungufu wa walimu ukizingatia kwamba kuna idadi kubwa ya wahitimu wa fani ya ualimu katika vyuo vya ualimu vilivyopo nchini? Je, Serikali imeajiri walimu wangapi mpaka sasa ili kukabiliana na upungufu huo? Serikali ina mpango gani endelevu wa kuhakikisha kwamba tatizo la upungufu wa walimu linatoweka kabisa? Serikali imepanga kuajiri walimu wangapi katika mwaka wa fedha 2018/2019 kama sehemu ya mchakato wa kupunguza tatizo la upungufu wa walimu?

**MHE MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kunisaidia ujenzi wa mabweni mawili ya shule ya sekondari

Malampaka. Haya ni nyongeza ya mabweni mengine yaliyojengwa baada ya Waziri wa Elimu kutoa fedha pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati wa kuwa na refa wa ubora wa elimu wa kitaifa ambaye atakukwa huru kufuatilia ubora, usimamizi na uendeshaji wa shule zetu za msingi na sekondari. Huyu atasimama katikati ya shule binafsi na shule za Serikali. Refa huyu atafanya *the playing ground* kuwa *leveled* kati ya shule ya Serikali na shule binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sana Serikali ije na mapendeleko ya kuunda chombo hiki ili kisaidie kuendesha shule zetu za msingi na sekondari kwa usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni upungufu wa walimu na vitabu katika Wilaya yangu ya Maswa hususani Jimbo langu la Maswa Magharibi. Katika shule za msingi tuna upungufu wa walimu 727. Shule za sekondari tuna upungufu wa walimu 108 wa masomo ya sayansi na walimu 88 wa masomo ya sanaa hasa kiingereza. Naiomba Serikali wakati wa kugawa walimu wanapoajiriwa iangalie maeneo yaliyo na upungufu mkubwa ili yapewe kipaumbele kama ilivyo Wilaya yangu ya Maswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuna upungufu wa vitabu vyta ya masomo ya sanaa upande wa sekondari. Vitabu vyta darasa la nne kwa mtaala mpya havipo kabisa mkoaa mzima wa Simiyu. Naiomba Serikali itatue changamoto hii ili watoto wetu wapate elimu bora si bora elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vyetu vyta ya maendeleo ya jamii bado vinaweza kutoa ujuzi na utalaamu tunaouhitaji ili kuendeleza masuala ya ufundi kwa watoto wetu. Hata hivyo vyuo hivi vina miundombinu iliyochakaa sana. Moja ya vyuo hivyo ni Chuo changu cha Maendeleo ya Wananchi cha Malampaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara iangalie ni kwa namna gani chuo hiki kinaweza kukarabatiwa na kupatiwa vifaa vyta kufundishia pamoja na kuongezewa

walimu. Vilevile naomba Serikali iangalie upya mitaala ya kufundishia ya vyuo hivi. Kwa maoni yangu mitaala iliyopo ni ya zamani halendani na mazingira tuliyo nayo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na hotuba yake nzuri ilijojaa kutatua kero za elimu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali yangu tukufu inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa elimu bure kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne. Ili kuendeleza juhudini hizi niishauri Serikali iwave vitendea kazi wakaguzi wa elimu katika Wilaya kwani idara hii ndiyo ambayo itakayoweza kusimamia hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali ijenge vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya kwani itakuwa mkombozi kwa watoto wetu wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari walioshindwa kuendelea na masomo, kwani watoto hawa wakipitia kwenye vyuo vyetu vya *VETA* walio wengi watakuwa wanajajiri wenyewe kupitia maarifa waliyoyapata kwenye vyuo vyetu vya *VETA*. Hii itakuwa mwarobaini kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali iangalie stahiki zote za walimu. Kuna malimbikizo makubwa ya walimu ambayo bado hawajapewa na walimu hawa wanbung'unika, hili si jambo zuri kwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo walimu wanaoishi vijijini wanaishi katika maisha magumu sana. Kwa sababu hiyo, niiombe Serikali yangu tukufu ijenge nyumba za walimu hasa waishio vijijini pamoja na kumalizia madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi pamoja

na maabara. Wananchi wameshajenga maabara hizo na kazi iliyobaki ni upande wa Serikali pamoja na kuongeza walimu wa kutosha katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na baadhi ya watendaji katika Halmashauri kuingilia kazi za wakaguzi. Niiombe Serikali itoe tamko kwa watendaji hawa kutoingilia kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kuwa wanafunzi wote wakatiwe bima ya afya, hasa kwa wale wambao wanaishi *boarding*. Serikali ihakikishe watoto hawa wanapata bima hiyo ili waweze kupata matabibu bure kwani hii inaleta usumbufu mkubwa hasa kwa walimu, maana inatokea mtoto anaumwa na mwalimu mnakutu hana hela na mwalimu hawezи kumuacha mwanafunzi kumpeleka hospitali atakopa au atatumia maarifa yake kuhakikisha mtoto anapata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali yangu ipunguze masharti ya kusajili shule hasa hizi za msingi. Hata ikiwa shule hizi zina madarasa mawili isajiliwe tu ili kuondoa usumbufu kwa watoto wetu hasa kwa wale wanaokaa mbali na shule na hii itapuguza watoto kutotoroka shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Elimu ya Watu Wazima; elimu hii ni muhimu sana kwani ilifika mahali watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ilipungua mpaka asilimia sita ya Watanzania, lakini sasa hivi imeongezeka mpaka kufikia asilimia 30. Hii ni ishara ya kuwa elimu hii haitiliwi mkazo katika Taifa letu. Hivyo basi niiombe Serikali itilie mkazo elimu hii ya watu wazima, ukizingatia sasa hivi kuna mfumo mzuri wa kuwafundisha watu wazima na wale watoto ambao wameshindwa kabisa kusoma na kuandika, inaitwa *Graph Game*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wewe mwenyewe ni shahidi kwani wadau wa *GG* walikuja mpaka kwako na wadau hawa wamesaidia sana katika Jimbo la Lushoto kwa baadhi ya shule kwani kuna watu wazima zaidi

ya 200 kwa sasa wanaojua kusoma na kuandika. Pia kuna watoto ambao walishindikana kabisa kujua kusoma na kuandika, lakini walivyotumia mfumo wa *Graph Game* sasa hivi wanajua kusoma na kuandika na ndio wanaoongoza madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niishauri Serikali yangu tukufu iwasaidie wadau hawa ili wawze kukomboa watoto wetu pamoja na watu wazima hawa. Serikali iwajengee uwezo wadau hawa wa *GG* na hili Mheshimiwa Waziri ili ulione kuwa ni mkombozi wa Watanzania naomba upange ziara ya kutembelea Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la michezo shulenii, hii elimu ya michezo haitiliwi umuhimu wakati tunajua kama michezo ni taaluma kama taaluma nyingine. Kwa hiyo, kujengwe vuyo vyta michezo au hivyo hivyo vyta *VETA* vifundishe na somo la michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ni vema nikamshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa mbingu na ardhi, mwangi wa rehema. Pia nakupongeza wewe binafsi kwa jinsi ulivyokuwa makini katika kulisimamia Bunge letu na kwa umakini mkubwa sana. Ninaomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu ufaulu mbaya na usiofurahisha kwa wanafunzi wa kidato cha nne na cha sita. Kwa kweli asilimia ndogo ya ufaulu wa chini ya asilimia 30 siyo mzuri, ni vyema Wizara ingepanga haraka utaratibu mwagine kuhusiana kuongeza taaluma kwa walimu (*in service training*) kwa mada ambazo baada ya utafiti zingebainika kama zina matatizo kwa walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *National Examination Supervision*, kumekuwa na kero zilizoambatana na masikitiko ya kwamba ni walimu gani wenye sifa za

kusimamia hii mitihani? Kuna wakati walimu wa chekechea pia hawapewi fursa kusimamia mitihani ambapo ni kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu nyongeza ya mishahara ya walimu. Idadi ya wanafunzi inaendelea kuongezeka na walimu wamekuwa wakiendelea kufundisha katika mazingira magumu sana na kipato chao kinaendelea kushuka na kuonekana walimu nchini ni watu dhaifu sana na maskini. Ni vyema bajeti ya elimu iwe ni pamoja na kuwaongezea mishahara walimu. Hili liangaliwe sana ili kuwalinda walimu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. WILLY Q. QAMBALO:** Mheahimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la Vyuo vya Ufundji (*VETA*). Tanzania imedhamiria kuwa na Chuo cha *VETA* katika kila Wilaya na hili ni jambo jema. Wilaya ya Karatu kwa kushirikiana na wadau wake wa maendeleo wamejenga Chuo cha Ufundji Stadi (*VETA*) na majengo ya msingi yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo Karatu ni msajili wa chuo hicho na hatimaye uendeshaji wake. Tunashukuru tumepata usajili wa muda miezi sita na tayari fani mbili zimeanza. Naomba Serikali kutupatia usajili wa kudumu na kisera kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kuendesha Chuo hicho kwa kutupatia walimu na vifaa vya ufundishaji. Tunao upungufu mkubwa sana wa watumishi. Wilaya ya Karatu ina upungufu wa walimu wa msingi 546 na sekondari 66. Idadi hii ya upungufu ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya msingi Endamaghang Wilayani Karatu ni maalumu ya bweni kwa watoto wa jamii ya Wahadzabe na Wabarbaig ambao kwao bado mwamko wa elimu ni mdogo sana. Shule hiyo ina changamoto na upungufu mwangi sana. Shule hiyo haina umeme japo nguzo zimepita hapo. Pia walimu hawatoshi kabisa, nyumba za walimu hazipo na mabweni kukosa vifaa

kama magodoro na mashuka. Wahudumu mfano wahunzi na wapishi hawatoshi na hawapati mafao yao kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wetu nchini wanazo changamoto nyingi sana ikiwemo mishahara midogo, kupandishwa madaraja na pia nyumba zao. Naishauri Serikali kuondoa changamoto hizi ili watumishi katika sekta ya elimu wapate moyo wa kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamejitahidi kujenga maabara na changamoto kubwa iliyopo sasa ni watumishi wa kada ya *laboratory technicians*. Serikali ipeleke watumishi wa ngazi hii Wilaya ya Karatu. Tumejitahidi sana kujenga shule za sekondari 31 kwenye kata 14. Serikali sasa itupe upendeleo wa kukamilisha maabara katika shule 18 ili hatimaye watoto wetu wapate kujifunza kwa vitendo.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa maandishi hoja hii muhimu ya elimu. Kwanza nianze na *motivation* kwa walimu. Serikali imeshindwa kutoa motisha kwa walimu wa shule za sekondari na msingi ndiyo maana ufaulu umeshuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu madai ya msingi ya walimu kupandishwa madaraja, kulipwa *areas* (malimbikizo), likizo, uhamisho na kadhalika. Madai hayo yote yasiposhughulikiwa kwa wakati hali ya ufaulu katika shule za Serikali itaendelea kuwa mbaya na kamwe hazitaweza kushindana na shule binafsi ambazo kwa sasa zimechukuliwa *role* ya Serikali badala ya shule za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni uhamisho walimu wa *artskwenda* shule za msingi. Tumeshuhudia walimu wengi wakiripotiwa kwenye vyombo vyya habari kwamba wamejinyonga na wengine kufa kwa msongo wa mawazo. Kuendelea kuwashusha walimu kutoka shule za sekondari kwenda shule za msingi pasipokuwaandaa kisaikolojia (*counseling*) bado wanajiona kama ni *demotion* kwao na inawavuruga moyo. Inahitajika *motivation* ya aina yake kwa

walimu hao ili waweze ku-cope na mazingira mapya wanayoenda kukutana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ifikirie namna ya ku-*motivate* shule binafsi ambazo zinatoa aibu Taifa hili. Shule binafsi zimesaidia kupandisha kiwango cha ufaulu kwa kiasi kikubwa kwenye Taifa hili na hii imefanya wazazi wengi sasa wanasomesha watoto kwenye shule za *private* badala ya kupeleka Kenya, Uganda na Malawi kama ilivyokuwa zamani, hivyo pesa zilizokwenda nje ya nchi sasa zinabaki hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isipunguze masharti katika shule hizi hasa kuwapunguzia gharama zilizokuwa muhimu ili kuziwezesha shule hizi kuendelea kufanya vizuri? Badala ya Serikali kupambana na shule za *private* kuweka masharti magumu, sasa wazipe fursa na kuwajengea uwezo na mazingira rafiki ili waendelee kuwekeza kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure bado haijaisaidia nchi hii. Sasa hivi imekuwa ni malalamiko kila kona, bado Serikali imeshindwa kupeleka huduma muhimu kwa wanafunzi katika shule za msingi; chakula mashulenii hamna. Moja ya sababu zilizotolewa na Taarifa ya Kamati ya Wizara ya Elimu ni kukosekana kwa chakula mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bure wanafunzi wana njaa; elimu bure wanafunzi hawana madawati shulenii, wazazi bado wanachangishwa, elimu bure bado wazazi wanalipia gharama za ulinzi, maji, umeme na kununua vitabu. Hiyo siyo elimu bure, ni lazima Serikali ingefuta ghrama zifuatazo; chakula, ulinzi, vitabu mashulenii na kadhalika.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara hii sana kwa mambo mazuri sana waliyowatendea wakazi wa Jimbo langu, kama vile ujenzi wa nyumba vya madarasa *primaryna secondary*. Wizara hii imesaidia sana ujenzi wa sekondari ya Makongoro kwa

mabweni na nyumba. Shule hii ina kidato cha kwanza na cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba shilingi milioni 72 kumalizia ujenzi wa bwalo la Chalanda, watoto wanalia nje, mvua na juu lao. Sekondari ya Mekomario tunajenga bweni, tunaomba samani za bweni (vitanda, meza na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sekondari za Nyamangita, Salama Rihingo na Chamriho, Nyamangutu. Naomba ujenzi wa maabara. Kwa upande wa Salama, jengo la maabara lipo katika kata, tunaomba fedha za kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chamriho na Mihingo watoto wanasaifiri kilometra 17 kutoka eneo la shule ya sekondari. Tunaomba Wizara mtusaldie maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii, akiwepo Naibu Katibu Wizara ya TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, nilitoa taarifa ya kubomoka na kuanguka kwa shule za msingi Sarawe na Stephen Wasira ambapo watoto wawili walifariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi kutoa msaada wa dharura kwa shule hizi mbili. Naomba ahadi hii itekelezwe, kwani mwakilishi na Serikali (Mkuu wa Mkoa) kwa niaba ya Serikali na Wizara ya Elimu walihidi kusaidia kutoa msaada wa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo sugu ambalo liki mya, tatizo la mikopo ya watumishi na hasa walimu ambao ndio wengi. Walimu wanakopa kuliko uwezo wao, hakuna *limit* ingawa zipo sheria za mikopo, lakini hazifuatwi. Naomba Wizara ifanye tathmini ya kuhusu jambo hili. Tafuteni udhibiti wa namna mikopo ya mabenki katika eneo la walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya wanafunzi iwe kwa wanachuo toka Diploma hadi Chuo Kikuu na mikopo

iwe kwa ngazi zote au mwaka wa kwanza hadi wa tatu bila kujali hakuna mwaka wa kwanza au wa pili au wa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako na Naibu Waziri kwa kazi nzuri pamoja na kuwasilisha bajeti yao ili tujadili. Yapo mambo ambayo nilikuwa nataka kupatia ufanuzi na pia kutoa ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa usambazaji wa vifaa vya elimu kwa shule maalum za watoto wenyewe ulemavu. Nampongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwa utaratibu wake wa kuvikagua kama viro na kama vinatumika. Ni suala zuri sana kwa sababu kuna baadhi ya shule huwa zinapokea vifaa hivyo na kuviacha bila kutumika na wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba kuwepo na utaratibu maalum wa kuwa na Mkaguzi Maalum wa vifaa hivi ili aweze kukagua na kuvifanyia ukarabati. Pia kuna baadhi hawana wataalam wa kufundisha, kwa wale wasiojua kuvitumia hasa walimu wao. Pia walimu katika shule hizi wote wangepatiwa elimu ya mawasiliano kwa watu wasiosikia. Shule hizi pia ziwekewe uzio kama Lugalo iliyopo Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ukarabati wa shule kongwe. Naipongeza Serikali kwa zoezi la ukarabati wa shule kongwe nchini, kwani shule hizi zilikuwa na miundombinu chakavu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Bima ya Afya katika Vyuo Vikuu. Nilibahatika kukutana na Serikali za Vyuo Vikuu vilivyopo katika Mkoa wa Iringa. Changamoto yao kubwa ni kuhusiana na Bima ya Afya wanafunzi wanayochangia pesa ya matibabu lakini hawapewi kadi za matibabu kwa sababu vyuo vinakuwa havijapeleka pesa

katika mfuko. Ushauri wangu kwa hili, ni vyema Bima ya Afya waweke dawati katika vyuo ili malipo yalipwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu chakavu katika vyuo, ni vyema pia Serikali ingekuwa na programu pia ya kuvifanya ukarabati wa majengo shule hasa mabweni wanayoishi wanavyuo, mfano Chuo cha Mkwawa, mabweni yao hayajakarabatiwa kwa muda mrefu. Pia kuna upungufu wa madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea kukopesha vijana wetu mikopo ya elimu ya juu. Naomba kigezo cha kupatiwa wanafunzi waliosoma katika shule za *private*, lingekuwa liondolewe kwa sababu kuna wanafunzi ambao ni yatima, wanasomeshwa katika shule hizo kwa ufadhilli maalum au kuna wazazi waliokuwa wakati huo ni waajiriwa, lakini baadae wakastaifu uwezo wa kulipia vifaa, wao wanakosa. Pengine Serikali ingeangalia uwezekano wa mikopo hiyo kukopeshwa na taasisi za fedha ili hata kudai au kukusanya mkopo huo unakuwa rahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kushukuru kwa nafasi hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Ndalichako kwa hotuba nzuri na yenyе kuleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mafia kwa kushirikiana na Mbunge wao wamefanikisha kujenga Chuo cha Ufundı, VETA. Majengo na miundombinu ya chuo hicho yameshakamilika na wanafunzi wameshaandikishwa na wameanza masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo sasa ni usajili wa chuo. Tumesrafanya taratibu zote na Wakaguzi wa Kanda, wamekuja Mafia na kukikagua chuo na wameonesha kuridhika kwao na majengo, miundombinu na wana taaluma na wakufunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara itusaidie kuharakisha usajili huu kwani Mafia ni miongoni mwa maeneo ya pembezoni na kuwavusha wananchi waje Dar es Salaam. Ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la shule binafsi kudahili wanafunzi na kisha kuwachekecha kwa mtihani migumu ili kupata wanafunzi *best* na kupata viwango bora, ni jambo ambalo Wizara lazima ilitupie macho, kwani linawanyima haki vijana wetu kwa uroho wa wamiliki wa shule ili kupata viwango bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kupongeza juhudzi zinazofanywa na Wizara yako katika kuboresha hali ya elimu Tanzania. Tumeshuhudia sehemu mbalimbali za nchi madarasa, madawati, mabweni katika shule za msingi, shule za sekondari na hata vyuo. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu sera ya nchi juu ya kila Wilaya kuwa na *VETA*. Nipende kurudia tena katika Wilaya ya Igunga, Kata ya Choma Chankole tulipata ufadhili wa ujenzi wa madarasa manne kutoka ufadhili wa *NGO* ya *World Vision IDP Manonga*.

Tunawashukuru sana na tayari wameshakabidhi katika Halmashauri. Sababu ya kutokuwa na fedha za kutosha, tunaomba sasa Wizara itusaidie ujenzi wa ofisi na mabweni ili chuo hiki kianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukitupatia shilingi milioni 400, tunao uwezo wa kuboresha zaidi *VETA* hii kuwa ya kisasa. Naomba sasa Wizara ipokee ombi hili kwa mara nyingine tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya kupitisha bajeti yako.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri mnayoifanya. Nachangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ambao umefanywa wa kugawa vifaa vya maabara katika shule za sekondari unapaswa kupongezwa sana, ila katika mgao uliopita Wilaya ya Muheza tulipata mgao wa shule saba tu. Naomba kwenye mgao huu Muheza tuongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Muheza hatuna Chuo cha *VETA*. Naomba tuone uwezekano wa kujenga. Kipo Chuo kimoja maeneo ya Kiwanda Potwe ambacho kipo chini ya Ustawi wa Jamii. Chuo hiki hakifanyi vizuri na uongozi wa Wilaya utaomba kifanywe *VETA*. Ombi hilo likifika naomba lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kuleta ombi la *Muheza High School* iweze kuangaliwa na iruhusiwe kuwachukua wanafunzi wa kutwa. Hii itasaidia wanafunzi waliofaulu na kukosa nafasi, maana shule hiyo imejengwa kwa nguvu za wananchi.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Waziri wa Elimu, lakini kuna baadhi ya wasaidizi wake wanamwangusha sana. Kwa mfano, *VETA* Mikumi imefanya jambo bayaa sana kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi, kwani *VETA*-Mikumi wakishirikiana na Chama cha Mapinduzi (CCM) wameanzisha utaratibu mbaya sana na unawanyima haki wananchi wanyonge kwa sababu wananchi wanaambiwa ili mtoto aweze kupokelewa kuingia *VETA* - Mikumi ni lazima awe na kadi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekasirika sana na wako mbioni kuandamana kudai haki yao ya msingi

ya kujunga na Chuo hiko cha *VETA* – Mikumi, kwani mpaka sasa fomu zote za *VETA* zinagawiwa na makada wa Chama cha Mapinduzi na kuwanyima fursa wananchi wengine wa vyama vingine na hata wale wasiokuwa na vyama. Maana tunavyo jua, Vyuo vya *VETA* siyo mali ya CCM bali ni vyuo vya umma na vinatakiwa kutoa fursa sawa kwa wananchi wote bila kuangalia itikadi zao, dini wala makabila yao. Cha msingi wawe wamekidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka na utendaji wa kazi wa Mheshimiwa Waziri kwa wananchi. Naomba sana atakapokuja kuhitimisha atoe karipio kali kabisa kwa *VETA* - Mikumi na wasitishe zoezi wanadolifanya mara moja na watupe majibu ni nani aliyewatuma kunyanyasa wananchi kwa kuwabagua kwa vyama vyao? Mwisho wale waliohusika na zoezi hili, wawajibishwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri hatatoa majibu ya kueleweka, nakusudia kushika shilingi ya mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu bado inawahitaji wamiliki wa shule binafsi kama wadau wa elimu, ni vyema yafuatayo yakazamwa upya. Kodi nyingi zinazomwelemea mmiliki wa shule ambazo hatima yake ni kuwazidishia mzigo wazazi katika ada, ni vyema kodi nyingi hizi zikaondolewa kama ilivyo katika sekta ya afya. Serikali iendelee kudhibiti ubora wa elimu. Hoja ya shule binafsi kujitengenezea udhibiti isikubaliwe kwa kuwa imekuwa ikitumika vibaya kwa baadhi ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upungufu wa walimu wa sayansi. Naiomba Serikali iendelee kutafuta suluhu ya upungufu wa walimu wa sayansi na naomba kuishauri Serikali kuruhusu wahitimu wa kada za sayansi za vyuo mfano, *engineering* na kadhalika ambao wapo mtaani kuajiriwa kama walimu kwa kuwa masomo yanafanana.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, wataalam na wasaidizi. Hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *skills development levy*; kwa kuwa Wizara ya Elimu ndiyo yenyeye dhamana, ni vyema ikashauri vyema zaidi juu ya madhumuni ya msingi ya uanzishwaji wa tozo hii. Ni *skills* zipi zilikusudiwa? Je, kuna mabadiliko ya aina ya *skills*? Je, ukusanyaji wa tozo hii wa matumizi yake unahitaji kufanyiwa marejesho? Kwa kifupi, jambo hili linatakiwa kutazamwa upya kwa makini zaidi na kwa kushirikisha wadau (wachangiaji) ili na wao wapate huduma zaidi ya kuendelea kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Vyuo vya Ufundidi Stadi. Wilaya ya Tunduru jiografia yake ikiweka mbali sana na Vyuo va Ufundidi. Hivyo kuwafanya wahitimu wa elimu ya msingi na hata wa sekondari kukosa fursa hiyo ambayo ingeweza kuwakwamisha kiuchumi na wakachangia uthumi wa Taifa. Pia tunamwomba kuwa *considered*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, inawezekana kupandisha hadhi Chuo cha Maendeleo ya Jamii Nandembo na kuwa Chuo cha VETA na elimu zote zikatolewa hapo hapo? Tunaomba kuwa mionganoni mwa wanufaika katika miradi ya ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo kama ilivyoidhinishwa katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 124 (*item iv*).

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yote ya Wizara kwa utekelezaji wa majukumu yao ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu ya kutofanya vizuri kwa vijana wetu katika mitihani ya kidato cha nne na sita ni lugha ya kiingereza. Lugha hii ndiyo inatumika katika kufundishia vijana wengi lakini hawaelewi kiingereza. Napendekeza kwamba vijana baada ya kumaliza

darasa la saba kabla ya kuanza masomo ya sekondari watumie mwaka mmoja wa matayarisho na kuwaweuka katika kukielewa kiingereza, yaani tuwe na utaratibu wa *pre-form one* kwa mwaka kwa kuwawezesha katika kukielewa kiingereza na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Malinyi tunaomba Mheshimiwa Waziri kupitia *TEA* juu ya ukamilishaji wa bweni la wasichana katika shule ya sekondari ya Kipingo Malinyi. Ombi lilikubaliwa lakini hadi leo hakuna utekelezaji. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atupatie kipaumbele, ombi la Malinyi Wilaya ambayo haina kabisa shule ya sekondari ya bweni wala hakuna *high school* kwa Wilaya yote ya Malinyi. Ahsante.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu kwa kuisimamia vizuri kuwa kiwango cha elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii ikiangalie Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Ulembwe. Chuo hiki kiko katika hali mbaya sana. Kwa kuwa miundombinu ni chakavu sana, naomba majengo yale yaboreshwe na kuezekwa kulingana na hali ya sasa. Wilaya ya Wanging'ombe haina Chuo cha *VETA*. Nimeomba majengo ya mhandisi mshauri yaliyopo pale Wanging'ombe yakubaliwe kutumike kwa kutoa elimu ya mafunzo ya ufundi *VETA*. Wizara ya ujenzi imeonesha nia ya kulikubali ombi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri kwa kunikubalia kukarabati shule mbili, moja ni shule ya msingi ya Dulamu na nyingine shule ya sekondari ya Usuka. Shule hizi miundombinu yake imekuwa *modal* kwa Wilaya yangu. Naomba mpango huo uendelezwe katika mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mpango mzuri wa kuendeleza elimu ya ualimu nchini. Tatizo liliopo hivi sasa ni upungufu mkubwa sana wa walimu na hasa shule ya msingi vijijiini. Ziko shule zina walimu wawili tu kwa wanafunzi wa madarasa saba, hili ni janga. Ni vyema Wizara ijue namna ya kutatua janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba mfululizo kwa miaka mitano sasa kuanza kwa kidato cha tano na sita kwa shule za sekondari za Makoga na ile ya Wanike. Naomba majengo yaboreshwe na kukarabatiwa. Naomba sana zikubaliwe kupokea wanafunzi kwa mwaka huu 2018/2019.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna kata 15 na kuna shule za sekondari za kata nane tu ambazo zote ni za kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Ninaomba angalau shule ya kidato cha tano na sita, moja au mbili ili kuwachukua wanaomaliza katika shule hizo. Kwani wengi wanaomaliza kidato cha nne wanabaki vijijiini bila kuendelea mbele kidato cha tano wala vyuo. Hivyo kukatisha tamaa wanafunzi na wazazi wao kuonekana kuwa watoto walimaliza kidato cha nne wanaishia kuishi kijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna upungufu mkubwa wa madarasa, nyumba za walimu, maabara, mabweni na miundombinu ya *library*. Shule zote nane hazina *library*, hazina mabwalo ya chakula wala majiko ya kupikia chakula. Kutokana na tabia ya wananchi wa kusini, tunalazimika watoto wakae mashuleneni kwenye shule zote za kata ili kupunguza utoro na kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

Mhesimiwa Mwenyekiti, ipo idadi kubwa ya wanafunzi wanaopelekwa mashuleneni kuliko miundombinu iliyopo. Mwaka 2016 na 2017 baada ya Sera ya Elimu bila malipo, watoto wengi wamekuwa wanafaulu kupelekwa kidato cha kwanza bila kuangalia miundombinu iliyopo katika shule hizo.

Hivyo Serikali iangalie namna ya kuwapeleka mashulenii kulingana na miundombinu ya mabweni, madawati, madarasa hata vyoo katika shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi. Shule zote zilizopo kwenye Jimbo langu, kuna upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi, hivyo kufanya watoto wachukue masomo ya sayansi na wote kusoma masomo ya *arts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunaomba Serikali kuajiri walimu wengi wa sayansi hasa hesabu, *physics*, *chemistry* na *biology*. Somo la kilimo (*agriculture*) lipewe kipaumbele kwa sababu ajira hamna, vyuo ni vichache, havitoshi ili watu tu wajifunze kilimo chenyeh tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu, kuna Shule za Msingi ambazo mpaka leo zimeezekwa kwa nyasi pamoja na nyumba za Walimu. Ninaomba Serikali ione namna ya kuzisaidia shule hizo ambazo ni Mbati ya leo Mkambala, Mchangani, Mrusha, Tupendane, Tukaewote na Mchangamoto.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu michango iliyokithiri kwa shule za *private*. Shule za msingi na sekondari za *private* wanatozwa michango mingi mmo. Shule za *private* za msingi zinatozwa shilingi 1,000 kila mtoto kwa ajili ya ukaguzi wa shule; shilingi 1,000 kila mtoto kwa ajili ya michezo; shilingi 3,500 kwa kila mtihani wa *mock* wa kila mtoto; shilingi 15,000 kila mtoto kwa mitihani ya kitaifa. Hata shule zinazosaidia watoto nao wanatozwa michango hiyo. Naiomba Serikali ipunguze utitiri huu wa michango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kukariri masomo. Watoto wengi wanaokwenda kusoma kwenye shule za *private* wanabadilika na kuwa na matokeo mazuri kutokana na utaratibu wa kukariri. Hivyo watoto wengi wanakazana

kusoma kwa sababu wanaogopa wasiposoma kwa bidii watarudia. Hivyo wanakazana sana. Naiomba Serikali irudishe utaratibu wa kukariri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watoto ambao wana vigezo vyta kupata mikopo lakini hawapati mikopo hiyo. Naiomba Serikali iangalie wanafunzi wenyewe vigezo wapewe mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na mmomonyoko wa maadili katika nchi yetu, naiomba Serikali kuingiza kwenye mitaala suala zima la maadili. Kwa kuwa wanafunzi wa kike wanapata ujauzito kutohana na kuishi mbali na makazi yao, lakini pia wanafunzi wengi wa kike wanapanga mitaani, naiomba Serikali ihakikishe inaongeza hosteli kwa ajili ya watoto wetu wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iingize masomo ya ujasiriamali kwenye mitaala ili baadae watoto wetu wajue namna ya kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara kwa taarifa yake ya bajeti. Nitaongea machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu walimu wastaifu. Kuna walimu waliostaifu toka mwaka 2016 lakini mpaka leo bado hawajalipwa posho ya nauli ya kuwarudisha makwao. Serikali inatuambia nini kuhusu wastaifu hawa ambao hawajui hatma ya posho yao ya nauli ya kuwarudisha makwao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni UMISHUMTA. Shule za msingi zinashiriki michezo hiyo. Je, Serikali inatuambia nini kuhusu shule kuwezesewa fedha kwa ajili ya kuwashudumia wanafunzi wakati wanashiriki michezo? Kuna baadhi ya wanafunzi wanatoka mbali kwenda kushiriki michezo na wakati huo wengine wanatoka majumbani kwao ikiwa

hawajakula chochote? Je, Serikali haioni ushiriki wa wanafunzi hao wao katika michezo mbalimbali utadhoofika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu madai ya walimu. Kuna baadhi ya Halmashauri zinadaiwa fedha na walimu zikiwemo za likizo na kusimamia mitihani ya darasa la nne na la saba. Tunaomba Serikali ifuatilie Halmashauri huenda kuna baadhi ya Halmashauri zinafanyia ubadhirifu maslahi ya walimu. Hii pia inachangia kushuka kwa morali ya walimu kufundisha madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu jengo la Kitega Uchumi la CWT liliopo llala Boma, Dar es Salaam. Chama cha Walimu kilichangisha walimu sehemu mbalimbali kwa ujenzi wa jengo hilo. Kuna walimu waliostaifu au kufa ambao walichangia fedha zao. Je, Serikali itueleze, walimu wananaufaika vipi na kitega uchumi hicho? Je, wale waliostaifu au kufa watanufaikaje?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo kubwa la wanafunzi kuwa na uwezo wa kusoma, kuhesabu hata kuandika katika shule zetu za msingi za Serikali. Hii inatokana na ripoti ya dunia ya 2014. Watu wengi wanakosa ujuzi wa mbinu za elimu za kufundishia. Hii inachangia pia na watu wengi kutokupata motisha kazini, hawalipwi madai yao; sehemu kama vijijini unakuta hakuna nyumba za walimu za kuishi, shule nydingine hazina madarasa, baadhi ya wanafunzi huketi chini, hakuna vitabu, baadhi ya shule unakutana na walimu wawili tu na ndio wanafundisha masomo yote kuanzia darasa la awali mpaka darasa la saba. Je, kwa vitendo hivi patakuwepo na ufaulu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha idadi ya walimu wa shule za msingi imeshuka kutoka walimu 191,772 mwaka 2016 hadi kufika 179,291 mwaka 2017. Hili ni anguko la 6.5% na kipelekeea mwalimu mmoja kufundisha kwa uwiano wa 1:50 ukizingatia uwiano unaokubalika ni mwalimu 1:25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na nyumba imara lazima msingi uwe imara. Hii inapelekea mpaka kuelekea sekondari, wanafunzi hawafanyi vizuri sababu ya upungufu wa walimu wa hisabati 7,291, baiolojia upungufu 5,181, kama upungufu 5,373; na fizikia 6,873. Takwimu hizi zinatokana na *BEST*2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika karne hii ya sayansi na teknolojia hapa Tanzania Serikali itakuwa inatafuta wataalam kutoka nchi za nje. Sioni ni kwa jinsi gani tunaweza kuzalisha wanasayansi wetu kwa mtindo huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mikakati gani wa kushughulikia tatizo la upungufu wa walimu wa shule za msingi na sekondari? Kwa mwaka 2018 Serikali imejipanga kuajiri walimu wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kuwekeza katika elimu, lakini bajeti imekuwa ikiidhinishiwa bajeti pungufu, mfano mwaka 2017/2018 Bunge iliidhinisha shilingi bilioni 4.7064 kwa sekta ya elimu, lakini ilipungua kwa 1.3% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2016/2017 ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 4.7707 nayo ilipungua kwa shilingi bilioni 64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali inashindwa kutenga 20% ya bajeti kwa ajili ya sekta ya elimu na kupelekea Wizara kushindwa kutimiza majukumu yake. Kwa mwelekeo huu, ubora wa elimu hapa nchini hauwezi kupanda hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni jukumu la Serikali kuhakikisha inatenga fedha za kutosha ili waweze kutenga fedha za kumsaidia mtoto wa kike aweze kuhudhuria shuleni kwa siku zote, kuhakikisha vyoo vyote vinakuwepo na maji na kuwekeza katika utoaji wa taulo za kike bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini walimu watalipwa posho na madai yao yote ukizingatia wengine wapo katika mazingira magumu sana ya kazi, wengine wana mikopo na kadhalika?

**MWENYEKITI:** Sasa tunaanza kupalilia njia ya mwenye hoja. Nitaanza na Mheshimiwa Dkt. Kijaji, dakika tano.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayofanya hasa katika sekta hii ya elimu. Pia niwapongeze sana Mheshimiwa Profesa Ndlichako na mtani wangu Mheshimiwa Ole Nasha kwa kazi njema ambayo mnaifanya katika sekta hii. Mimi naamini mnaandika historia na historia itawakumbuka, mnafanya kazi njema sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ya jambo ambalo linabezwa humu ndani la elimu bila malipo au elimu bure. Hili ni jambo kubwa kabisa ambalo alianza nalo Mheshimiwa Rais wetu na tukaanza kwa kupeleka shilingi bilioni 18.77 tulipoanza Serikali ya Awamu ya Tano. Tumeongeza tukaenda shilingi bilioni 20.24 leo tunapoongea kwa kila mwezi tunapeleka zaidi ya shilingi bilioni 23.876. Hii ni dhamira njema ya Serikali ya Awamu ya Tano kwamba inataka kuwaondoa watoto wa maskini, wale amba walikuwa hawaendi shule sasa waende shule wasome bila tatizo. Si vizuri sana tukabeza kila jambo kwa sababu tu mimi ni mpinzani, mimi ni vile lakini hapana, tutende haki katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa kulisemea katika dakika hizi chache ni mchango wa sekta binafsi kwenye sekta hii ya elimu. Kama Serikali tunathamini sana mchango wa sekta binafsi katika sekta ya elimu na ndiyo maana mwaka jana katika mapendekezo waliyotuletea sekta binafsi tuliondoa tozo nne kwa sekta binafsi katika elimu. Hii ni dhamira ya dhati ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumekumbwa na tatizo moja kwamba huwa tunaweza kuongelea zaidi matumizi bila kujiuliza mapato yanapatikana wapi. Hili tukiweza kulielewa vizuri kwamba tuondokane sasa na matumizi tuanze kufikiria mapato, mapato yetu yanatoka

wapi. Tunaposema tuondoe hiki na kile na sheria na kanuni zetu zimeweka wazi unapopendekeza ondoa kodi hii lete mbadala basi tulete kodi ipi ili iweze kufidia yale mapato ambayo yameondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikari ya Awamu ya Tano ni njema kabisa, tulianza na tunaendelea kutekeleza. Tayari *task force* ipo kazini, juzi tulikuwa *think tank meeting* kwa ajili ya kupitia maombi mbalimbali yaliyoletwa na wadau wetu mbalimbali ya kikodi na ushuru mbalimbali, tunaendelea kuyafanya kazi. Nakiri tumepata maombi pia kutoka kwa ndugu zetu hawa wa sekta binafsi kwenye elimu na sisi tunaendelea kufanya kazi lazima tushirikiane kwa pamoja kuona maendeleo ya Taifa letu yanapelekwa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda kulisemea kwa uchache kwa siku ya leo ni hili pia ambalo linabewa ndani ya Bunge lako tukufu kwamba Serikali haiwathamini na haiwajali walimu, siyo sahihi na nasema hili kwa sababu moja tu. Baada ya kuingia madarakani tulikuwa na tatizo kubwa la watumishi hewa, tumefanya kazi vizuri wameweza kuondoka watumishi hewa. Tumefanya uhakiki wa madai ambayo watumishi wote walikuwa wanadai tumemaliza na sisi sote Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi mwezi wa pili Serikali yetu imelipa madai ya shilingi 43,005,747,874 na tumelipa deni hili kwa watumishi wote. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tusikilizane tuelewe nini Serikali inafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shilingi bilioni 43 tulizolipa zilikuwa ni kwa ajili ya watumishi 27,118. Kati ya watumishi hao walimu walikuwa 15,593. Kwa hiyo, tuiangalie hii *ratio* kabla ya kutafuta *cheap popularity* kwamba Serikali haiwajali walimu si sahihi hata kidogo. Lazima twende kwa

takwimu tuiieleze vizuri tuweze kujua nini Serikali ya Awamu ya Tano inafanya. Niwaambie walimu tuko pamoja na ndiyo maana Serikali imeongeza kufikia shilingi bilioni 23 kwa sababu tunakwenda kuwalipa walimu pesa yao ya madaraka. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, nawaomba sana walimu wetu waendelee kuchapa kazi Serikali ya Magufuli ya viwanda, tunatambua mchango wao. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kabla sijaendelea na wachangiaji wengine, nitangaze wageni waliopo hapa. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 107 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia amba ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo cha Mipango. Karibuni sana. (*Makof*)

Kuna wageni waliotembelea Bungeni hapa kwa ajili ya mafunzo, nao ni wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosomea taaluma ya sheria wakiongozwa na Ndugu Kigoma Marwa. Karibuni sana. (*Makof*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Kakunda, dakika saba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru sana. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Profesa Ndalichako na Mheshimiwa Ole Nasha,

Waziri na Naibu Waziri kwa kazi yao nzuri sana wanayoendelea kuifanya katika sekta ya elimu na sisi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunaendelea kuwategemea sana katika utendaji wetu wa kila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naipongeza Kamati wametoa maoni, ushauri mzuri sana. Kwa kweli nakiri kwa mwaka huu wametoa ushauri ambao utatusaidia sana katika utendaji wetu wa kila siku. Ushauri kuhusu namna bora ya kuendesha sekta ya elimu, kuboresha ushirikiano wa wadau mbalimbali ikiwemo namna ya bora ya kutoa huduma za elimu kwa watoto wenyewe ulemavu, nasema tumeupokea na tunaufanya kazi na tumeupokea kikazi zaidi. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa maoni na ushauri na ushauri wao tumeupokea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wetu wa utekelezaji wa kazi za kila siku katika Halmashauri na mjadala wa kitaifa, Halmashauri zote hutekeleza kazi zao kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 145 na 146 na sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa. Uvezeshaji wao unasimamiwa na Sheria Na.19 ya Tawala za Mikoa. Kwa hivyo, usimamizi kwa ujumla katika Serikali za Mitaa ni wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wote tunaofanya katika sekta ya elimu tunaongozwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Kwa muktadha huo, maoni na ushauri kuhusu kuwa na mjadala mpana wa kitaifa kuhusu mfumo wa elimu, majukumu ya wadau, uwajibikaji, tunajua pale wilayani kuna Idara tatu zote zinasimamia elimu: Kuna Afisa Elimu wa Wilaya, Mdhibiti wa Ubora na kuna Katibu wa TSC. Wote hawa wanahusika na maendeleo ya elimu kwa majukumu mbalimbali katika wilaya. Vilevile kuna masuala ya kuhusu ngazi za vidato, haki za watoto wa kike na watoto wenyewe ulemavu.

Kwa hiyo, suala la kuwa na mjadala mpana wa kitaifa kuhusu masuala mbalimbali kama hayo, sisi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI hatuna tatizo nao kabisa na tumeupokea. Wiki

ijayo tutakutana katika ngazi ya Naibu Mawaziri na mwenzangu wa Wizara ya Elimu, tutazungumzia namna ya kuuandaa huo mjadala pengine labda baada Bunge hili la Bajeti likikamilika basi tunaweza tukuitisha kama ambavyo tumeshauriwa na Waheshimiwa Marais Wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya walimu, namshukuru Naibu Waziri wa Fedha amegusia, walimu 15,000 tayari wameshalipwa. Hata hivyo, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba tumekamilisha uhakiki wa madeni ya walimu 126,893 ambapo madai yao sasa yamepungua hadi shilingi 61,515,587,938 na haya tumewasilisha Hazina kwa ajili ya hatua zaidi. Serikali imeshaahidi madai yote yatakayothibitika kuwa halali yatalipwa. Kwa hiyo, tunaomba walimu wote wawe na subira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhamisho wa walimu wa masomo ya sanaa kutoka sekondari kwenda shule za msingi, tunesikia maoni lakini tunapenda kusisitiza kwamba uhamisho huu uliwalhusu walimu 21,165 wa masomo ya sanaa ambao walikuwa wamezidi idadi kwenye shule za sekondari kwa maana kwamba walikuwa na vipindi vichache sana. Kwa hiyo, ili kusudi waendelee kuwa katika ajira ya utumishi wa umma kama walimu hadi watakapostaafu tuliona kwamba ni matumizi sahihi ya rasilimali za Serikali kuwahamishia kwenye shule za msingi ili wakaendelee na kazi kwa mshahara ule ule na kwa daraja lile lile. Serikali inaamini kwamba ukiacha wale ambao hawana uzoefu na zana za kufundishia shule za msingi ambao watahitaji mafunzo maalum elekezi ya muda mfupi, wale waliojiendeza na wakahamia sekondari kutoka shule za msingi hawahitaji sana mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nakiri kwamba zimekuwepo changamoto kadhaa katika utekelezaji wa zoezi hilo ikiwemo baadhi ya waliostahiki kupata kulipwa posho hawakulipwa na hili natoa agizo kwamba pale ambapo Wakurugenzi wamekosea wafanye marekebisho haraka sana. Vilevile kulikuwa na malalamiko ya kuhamishwa wale wenye *degree* na wakaachwa wale wenye diploma,

isipokuwa kama mwalimu mwenye diploma yuko peke yake anafundisha somo hilo ina maana kumhamisha mwalimu yule watoto wale watakosa somo hilo hata kama ni Historia au kiingereza, mwalimu huyo mwenye diploma anayefundisha somo hilo peke yake itabidi abaki wataondoka walimu wengine. Kwa hiyo, suala hili linahitaji umakini sana katika kulifuatilia. Waliokosea tumeshawaagiza warekebishe na naomba walimu wote wenye malalamiko watuandikie kupidia Katibu Mkuu, TAMISEMI ili hatua zichukuliwe haraka na hiyo ni pamoja na wale waliosimamia mitihani hadi sasa posho hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makato ya asilimia mbiliya CWT. CWT iliundwa kwa mujibu wa sheria sawa na vyama vingine vya wafanyakazi. Kwa hiyo, masuala ya kwamba wamekatwa asilimia mbili wanatakiwa wayajadili kwenye vikao vyao vya kisheria ili kusudi wakubaliane kama wataendelea kukatana au namna gani kwa sababu hatuwezi kuwaingilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira za walimu, sasa hivi tunaandaa mchakato wa kuajiri walimu 16,130; kati ya hao 10,130 ni wa shule za misingi na 6,000 wa sayansi katika sekondari kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madaraja, zoezi ambalo lilikuwa limesimama limeanzishwa tena tangu Novemba, 2017. Kwa sasa upandishaji wa madaraja unaendelea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shule ya sekondari ya Lindi, napenda kuwaondoa wasiwasi Wabunge wote kutoka Mkoa wa Lindi. Shule ile itajengwa na itakamilika mwaka 2018/2019 na wiki kesho itakuwa ni agenda mojawapo katika kikao chetu cha Naibu Mawaziri wanaoshughulikia elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ambayo ni ya ujumla makubwa napenda kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, dakika kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nitangulie kusema kuwa naunga mkono hoja hii na Mheshimiwa Waziri mimi Mbunge wa Newala Mjini watu wangu wamenituma nikuambie kwamba wanaridhishwa sana na utendaji kazi wa Wizara yako, wanapongeza sana mlivyopanua Kiuta sekondari sasa kuwa *high school*, ulivyosaidia kule Mnyambe na ulivyosaidia madarasa. Wananchi wanasema wataendelea kushirikiana na Serikali kutekeleza wajibu wao pale inapobidi nguvu za wananchi zinahitajika. Kwa sababu tunavyofahamu Serikali yetu haikuwahi kuahidi kwamba kila kitu kitatolewa bure, tunafanya ubia katika Serikali na wananchi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, baada ya kusema hayo, nataka niseme leo nimesoma *press release* ya Mbunge, namheshimu sana lakini mambo yaliyosemwa mle mengine wanasema ukikaa kimya, *quietness means consent*, ndiyo maana nimeamua nisikae kimya, nijibu hoja.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, hoja inayozungumzwa pale kwamba Mheshimiwa Rais aliahidi kuongeza mshahara mwaka huu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Naomba mnisikilize,

watu wazima wakikaa kwenye faragha wanasikilizana, mimi hamjaniona nawazomea hata siku moja. Mnasema mambo wakati mwingine yanaudhi lakini nakaa kimya, ndiyo nidhamu ya Bunge. Hivi mzee mzima na mvi kama hizi nianze kuzomea ooh, ooh, aah. Basi mna mtu wa kumuiga mfano mbona hamniigi mfano? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa Iringa, Mgeni Rasmi alikuwa Rais nimemsikiliza *live*, hayo mnayosema moja, maana unajua Kiswahili kigumu, inawezekana tukasikiliza wote wawili mimi nikaelewa vingine na wewe ukaelewa sivyo lakini kwa sababu ni mtaalam wa lugha ya Kiswahili nataka kusema alivyosema Rais jana. Amesema hivi, mwaka jana sikuahidi kupandisha mishahara. Akasema siku zote Serikali inapandisha mishahara kulingana na uwezo wa kifedha. Lingine akasema kupanga ni kuchagua, tuna shida ya kujenga reli, reli ile ya kwenda Kigoma zinaanguka kila siku tangu 1905 mpaka leo zaidi ya miaka 100, tunajenga reli ya kisasa, tumenunua ndege, hauwezi ukaleta watalii kutoka nje unawapeleka Ngorongoro unataka wapande ndege nazo za nje, *domestic flights*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema nawaomba Watanzania wenzangu tuchape kazi. Waliopo mashambani waongeze uzalishaji kama mimi mkulima wa korosho, mliopo ofisini mchape kazi na mliopo viwandani muongeze uzalishaji. Hali ya uchumi itakaporuhusu, maneno ya jana ya Rais na mimi nilikuwa pale futi moja kutoka kwake, sasa ooh nilisikia, nilisikia, mimi nilikuwa futi moja pale ubavuni kwake, akasema hali ya uchumi itakaporuhusu nitapandisha mshahara tena sitangoja sikuu ya *May Day*.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Sasa nikuambieni pale kupanga ni kuchagua, yeye akasema kwa ufahamu wake kupanga ni kuchagua, akasema ilibidi tuamue, je, tuongeze mishahara tubaki tulivyo na barabara mbovu, bila ndege, bila reli (*standard gauge*).

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Kuzomea ndiyo tabia yenu lakini hakuachi mimi kusema. Mimi siwezi kuacha kusema kwamba kuna watu wameamua ku-behave kana kwamba wako sokoni, mimi nitasema tu. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema hali ya uchumi itakaporuhusu nitapandisha mshahara, sitangoja *May Day*, nikiambiwa tu mahesabu kule Hazina yamekubali siku hiyo hiyo napandisha, ndivyo alivyosema. Kupanga ni kuchagua, akasema ilibidi tuamue, je, tutekeleze haya kwanza au tugawane hela kwa kuongeza viwango vya mishahara. Leo mtu anasimama hapa anasema Rais kasema uongo, mwaka jana allituahidi, mwenyewe amekanusha hakusema, msimtli maneno mdomoni ambayo hakuyasema. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena aliyetoa *press* aliwahi kufanya kazi utumishi, kuna mahali anasema watumishi sisi tunalipishwa...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Nasoma hapa ninyi, humu ndani unaruhusiwa kuwa na *note book* siyo kusoma risala, mimi naandika hapa *point form*, mimi ni mwalimu najua kuandika *lesson notes*, najua namna ya kuijandaa. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *press release* inasema wafanyakazi wanalipishwa *skills development levy, wrong. Skill development levy* analipa mwajiri halipi mfanyakazi. Hivyo hayo maneno unategemea uyapate kwa mtu *senior citizen, senior retired civil servant* hajui kama *skills development levy* inalipwa na mwajiri na hawesi kwenda kufuta ile maana ameiandika.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Nasema hivi ...

**MBUNGE FULANI:** Anapotosha Bunge.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Kuongea bila  
kuruhusiwa na Spika tumewazoea ndivyo mlivyo. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, nilitaka niweke sawa hilo, sasa nataka nichangie  
upande wa ajira ya walimu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA  
UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, kama mtakavyokumbuka Oktoba, 2016 tulifanya  
zoezi la uhakiki wa watumishi. Katika uhakiki ule ilibainika  
baadhi yao walikuwa na utumishi hewa wakiwemo na  
walimu. Mara moja baada ya kuona idadi ya walimu  
imepungua kilichotokea ni kwamba Serikali imeajiri  
watumishi tayari...

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Kanuni gani?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Kanuni ya 64 (1) na vipengele vyake.

**MWENYEKITI:** Inasema nini?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Subiri basi nisome.

**MBUNGE FULANI:** Ngoja aisome mbona hasira Mwenyekiti.

**MBUNGE FULANI:** Ngoja asome basi mbona unampelekesha hivyo, siyo vizuri?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hiyo inasema, bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, sasa mimi naenda kwenye (b) inasema; hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji wakati alipoanza kuchangia, *no*, Jenista Mhagama naomba naongea na Kiti.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Yes, yes. Mzungumzaji alianza kuongea vitu ambavyo haviko kwenye mjadala na vimetokea nje ya Bunge.

**MWENYEKITI:** Nimekuruhusu mimi, naomba usilete uchokozi na watu wengine humu.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Wao wenyewe wanachokoza.

**MWENYEKITI:** Ongea na Kiti.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisimame na Kanuni ya 64(b) ambayo inasema; hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala. Mjadala ulio mezani kwetu ni Wizara ya Elimu na Mheshimiwa Waziri wako katika kujibu hoja za Wizara iliyo mezani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mzungumzaji alianza kujibu *press* ambayo imetokea nje ya Bunge hili na nje ya hoja ambayo iko mezani. Naomba uingilie hili suala, ajikite kwenye hoja. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Waitara ameongea nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Semesi, unafahamu tukiwa watulivu na tukatulizana vichwa vyetu utasikia hoja ya mwenzako. Kumbukeni Mheshimiwa Waitara, mimi nilikuwa hapa nilijaribu kumwongoza...

**MBUNGE FULANI:** Ni *two wrongs*.

**MWENYEKITI:** *Two wrongs do not make one right*, nakubaliana. Mheshimiwa Waziri aliyekuwa anachangia sasa hivi nakurejesha kwenye mstari na ndiyo nilisema mimi unataka nikutake uweke ushahidi, tusifike huko. Sasa Serikali ndiyo maana imo Bungeni humu kama linatokea jambo la kupotosha lazima linyooshwe mara moja ili wananchi wajue ni nini ambacho Mheshimiwa Rais amesema. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ameliweka vizuri kwamba mwaka jana Mheshimiwa Rais hajatoa ahadi hiyo, huo ndiyo uamuzi wangu. Mheshimiwa Waziri endelea. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa darasa ulilotoa. Unajua wakati mwingine unaweza ukaongea kwa jazba ukasahau hata ulichokuwa umekisema. Serikali inasimama hapa kujibu hoja za Wabunge. Hili ninalolisema mmelisema. Hivi mlitaka

mkisema jambo la uwongo tukae kimya tu? *Quietness means consent.* (*Makofi/Kicheko*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** *Comrade endelea na mambo ya msingi.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini dakika wanazoninyang'anya hizi utanifidia.

**MWENYEKITI:** Endelea tu Mheshimiwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo imezungumzwa na pande zote mbili; upande wa upinzani na upande wa CCM ni suala la msingi la ajira kwa walimu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Wala sihitaji kujibiwa namu-address Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa walimu jana Mheshimiwa Rais alipohutubia kule Iringa aliwaambia wafanyakazi kwamba watumishi 22,150 wataajiriwa mara moja. Katika hao 7,000 sawa na asilimia 31.6 watakuwa ni walimu. Hii tunatekeleza bajeti ya mwaka huu tulio nao sasa na tutakapoanza mwaka mpya, juzi mmepitisha bajeti ya watu wengine 49,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme kwamba hakuna mtu ndani ya Serikali anayependwa pawe na uhaba wa walimu, kila jitihada zitafanyika. Kama

nilivyosema kwa upande wa afya siku ile, nilisema kama kuna zahanati yoyote iliyofungwa kwa kukosa watumishi nileteeni, wako walioniletea tumeshafanya utaratibu tunawapeleka watu kwa sababu niliahidi hakuna zahanati itakayofungwa kwa kukosa watumishi. Nasema tena kwa upande wa elimu hapa nilipo mimi ndiyo Waziri wa Utumishi, hakuna shule itakayofungwa kwa kukosa walimu, unayo jimboni kwako nenda kanilettee tutafanya mpango kupeleka walimu mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka niseme kuna halmashauri nyingine walimu mnawarundika shule moja hasa shule za mjini. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge wote hapa tushirikiane...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Hatujibzani kama sokoni. Tushirikiane pale ambapo walimu wamezidi tuwapeleka sehemu ile ambako kuna shida ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilisimama hapa kuunga mkono hoja, haya niliyosema sijaogelea nje ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea. Mheshimiwa Ole Nasha Naibu Waziri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, dakika 20.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa maelezo mafupi kuhusu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge katika kujadili bajeti ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kunteua kutumikia katika Wizara hii nyeti. Itoshe kusema kuwa, napata furaha sana kufanya kazi na Serikali hili ya Awamu ya Tano ambayo katika kipindi kifupi imefanya mambo makubwa yanayolenga kumkomboa Mtanzania na hasa Mtanzania mnyonge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa maelekezo na ushauri wake kwangu ambao umeendelea kunijenga siku hadi siku. Pia nawashukuru Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku ndani ya Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kipekee kabisa kumshukuru mke wangu mpendwa na watoto wangu kwa upendo, maombi na uvumilivu wao katika kipindi ambacho nimekuwa mbali nao nikilitumikia Taifa. Vilevile nawashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Ngorongoro kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa shughuli zangu za maendeleo Jimboni. Napenda kuwaahidi kuwa sitawaangusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako tukufu kwa

michango yao mizuri tangu kuwasilishwa kwa hotuba ya bajeti ya Wizara yetu. Nawaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha kwamba tunatoa elimu bora kwa watoto wa Kitanzania na kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, sasa naomba nitoe ufanuzi kuhusu baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Mtaniwia radhi kwa sababu ya wingi wenu na muda nilionao sitaweza kuwataja lakini naomba nizijibu hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hoja yetu waliihaka Serikali kutoa ufanuzi juu ya suala la upatikanaji wa vitabu hasa vya Darasa la IV wakieleza kuwa kuchelewa kwa vitabu hivyo kutaathiri wanafunzi wa darasa husika ambao wanatakiwa kufanya Mtihani wa Taifa mwaka huu. Serikali inatambua kuwa upatikanaji wa vitabu ni muhimu sana katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji wa mtoto na wote ni mashahidi kuwa suala hili limekuwa ni kipaumbele cha Serikali kwa muda mrefu. Kuthibitisha hili mtakumbuka kuwa pale vitabu vya darasa la pili na tatu vilipokosewa, Wizara haikusita kuchukua hatua mara moja za kiutendaji na kinidhamu kwa wote waliohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa vitabu vya kiada vya darasa la kwanza hadi la nne vinaendelea kuzalishwa na kusambazwa kwa shule zote kwa masomo yote. Zoezi la usambazaji wa vitabu hivyo limeanza katika mikoa 12 na litakamilika tarehe 30 Mei, 2018 kwa mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi vimechelewa kuchapishwa na kusambazwa kutokana na zoezi kubwa la kurudia uhariri wa uchapishaji wa vitabu vya darasa la kwanza hadi la tatu vilivyobainika kuwa na makosa ya kiuchapaji na kimaudhui. Zoezi la uhariri na uchapishaji limefanyika kwa umakini mkubwa na kwa kuwashirikisha wataalamu mbalimbali wa vyuo vya ualimu na vyuo vikuu ili kuhakikisha tunakuwa na vitabu vyenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Wabunge ambao wametoa hoja kwamba vitabu ambavyo vinasambazwa vina makosa. Sitakuwa na nia ya kujaribu kujibizana na Waheshimiwa Wabunge ambao walidai kwamba kuna makosa kwa sababu kwa sasa sijajiridhisha na nakala za vitabu wanavyotumia, lakini mimi na Wizara tuko tayari kukaa nao kuangalia vitabu wanavyosema vina makosa ni vitabu gani na kama kawaida iwapo kuna makosa tutasahihisha lakini vilevile wale ambao wamehusika watachukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hoja yetu waliitaka Serikali kuhakikisha kuwa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu inaanishwa mapema ili kuweza kuwa na walimu ambao wana ubora. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu ya 2018 ambao pamoja na mambo mengine, utaweka masharti ya Sheria ya Uanzishwaji, Utawala na Uendeshaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu, tunategemea kwamba Muswada huu utakamili baada ya kufanyiwa kazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni katika kipindi kifupi kijacho.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja yenu hiyo ya msingi imetiliwa maanani na hivi karibuni tunategemea kuwa na sheria hiyo ili Bodi hiyo ya Kitaalamu ya Walimu iweze kuanza kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hoja yetu walitaka kujua ni Wanzanzibar wangapi wanapata mikopo ya elimu ya juu, kiasi kinachotengwa kwa wanafunzi kutoka Zanzibar na ni kwa nini wanafunzi Wanzanzibar hawapati mikopo kwa asilimia 100. Lengo la kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu mwaka 2004 ni kuwawezesha wanafunzi wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za elimu ya juu kupata elimu hiyo. Serikali inakaribisha wadau wengine zikiwemo taasisi za kifedha kuwakopesha wanafunzi kwa masharti wanayoweza kuyamudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria ilioanzisha Bodi ya Mikopo, mikopo ya elimu ya juu inapaswa kutolewa kwa Watanzania wahitaji na wenyе sifa (*needy and eligible*). Sheria pia imetaja vigezo vikuu vinavyopaswa kuzingatiwa kuwa ni lazima mwombaji awe Mtanzania, awe amepata udahili wa masomo ya shahada au stashahada katika taasisi inayotambuliwa na Serikali na asiwe na vyanzo vingine vinavyoghamramia masomo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria hiyo, Bodi inayo mamlaka ya kuweka utaratibu wa kuwabaini wahitaji. Kwa sababu hiyo, kila mwaka Bodi huandaa mwongozo kwa kushirikisha wadau unaopaswa kuzingatiwa na waombaji na kuweka masharti ya utoaji mikopo kwa mwaka husika. Kwa mwaka 2017/2018 mwongozo uliotolewa ulizingatia waombaji wenyе mahitaji maalum wakiwepo wale waliofadhilliwa katika masomo yao ya sekondari au stashahada, yatima na wenyе ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya elimu ya juu hutolewa kwa Watanzania wahitaji wenyе sifa kutoka eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa upande wa Zanzibar katika mwaka wa masomo 2017/2018 jumla ya Watanzania 1,380 wanaosoma katika vyuo vitano vilivypopo Zanzibar walipata mikopo kutoka Bodi na hii ni sawa na asilimia 41 ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mikopo haitolewi kwa kuzingatia eneo analotoka mwombaji, sifa kuu ya wanufaika hao 1,380 waliopata mikopo ni Utanzania wao na wanawenza kuwa wanatoka katika eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini wanaosoma katika vyuo vilivypopo Zanzibar. Hivyo basi, siyo rahisi kupata takwimu za Wazanzibar au wanufaika wengine kutoka eneo lolote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Msisitizo ni kwamba mikopo haitolewi kwa kuzingatia kwamba mwombaji ametoka upande gani wa Jamhuri yetu ya Muungano, kinachotakiwa ni kwamba sifa ni Utanzania, lakini na zile sifa zingine ambazo zimeainishwa kwenye sheria inayoanzisha Bodi ya Mikopo.

Aidha, napenda kusisitiza kuwa, ni muhimu kufahamu kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inafanya kazi kwa karibu na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu Juu Zanzibar ili kuhakikisha kuwa hakuna Mtanzania mwenye sifa anakosa mkopo wa elimu ya juu na anapata mkopo kutoka katika taasisi zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia katika utoaji wa mikopo ni uwiano wa kijinsia kwa wanufaika; ukomo wa ada wa masomo inayotolewa na Bodi ya Mikopo na umuhimu wa kuboresha Bodi ya Mikopo ili iondokane na utegemezi.

Kuhusu uwiano kati ya wanufaika wa mikopo 122,623 kwa mwaka 2017/2018 wanawake ni asilimia 34.5 na wanaume ni asilimia 65.5. Aidha, kuhusu ukomo wa ada, ni muhimu kufahamu kuwa kwa sasa Serikali imeweka ukomo wa ada itakayotolewa kwa mnufaika wa mikopo kuwa ni ile inayotozwa katika vyuo vya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha Bodi ya Mikopo, kwa sasa Serikali inaendelea kusimamia maboresho ya kimfumo ili kuimarisha ufanisi utakaoongeza tija na kuiwezesha Bodi ya Mikopo kuelekea kwenye kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kuchangia hoja yetu walitaka kujua kwa nini shule nyngi za Zanzibar katika matokeo yake ya kidato cha nne na sita ndiyo hushika mkia na walitaka vilevile kujua kama Bodi ya *NECTA* inajumisha wajumbe kutoka Zanzibar. Upangaji wa shule katika viwango vya ubora na ufaulu hufanyika kwa vigezo vikubwa viwili ambavyo ni wastani wa ufaulu wa wanafunzi kimadaraja na wastani wa ufaulu wa wanafunzi katika masomo yao. Nafasi ya shule katika ubora wa ufaulu inategemea wastani ambao shule imeupata katika vigezo vilivyoainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mitihani la Tanzania hutumia mfumo madhubuti wa usahihishaji unaofahamika maarufu kama (*conveyor belt*) ambapo

msahihishaji mmoja husahihisha swalí moja tu alilopangiwa na hivyo kufanya *script* moja ya mtahiniwa kusahihishwa na watahini wengi, jambo ambalo huondoa uwezekano wa upendeleo kutokea. Nchi nyngi za Afrika zinatumia mfumo huu baada ya kujifunza kutoka Tanzania. Mifano ya hizo nchi ambazo zimejifunza kwetu ni pamoja na Zimbabwe, Zambia, Uganda na Ghana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Bodi ya Baraza la Mitihani la Tanzania inajumuisha wajumbe kutoka Zanzibar ambao hushiriki katika shughuli zote za usimamizi na maamuzi ya Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hoja yetu walitaka kufahamu na kutaka Serikali itoe ufanuzi juu ya suala la kumsimamisha masomo mwanafunzi Abdul Nondo wakieleza kuwa utaratibu uliotumika ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaingia katika *merits* za kesi kwa sababu kesi iko Mahakamani, lakini itoshe tu kwa sasa kusema kwamba napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Taasisi za Elimu ya Juu, ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam huongozwa na sheria ndogondogo za wanafunzi. Sheria hizi ndogo zimekewka kwa minajili ya kuwalinda wanafunzi, kwani kuna kanuni za kitaaluma zinazomtaka mwanafunzi kutimiza kiwango maalum cha chini cha mahudhurio cha mahudhurio (75%) ili kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwanafunzi mwenye kesi kama hii ingekuwa vigumu kukikidhi kanuni hiyo na wakati huo huo kutimiza matakwa ya mahakama. Hata hivyo, mwanafunzi anaposhinda kesi hurudishwa chuoni na kuendelea na masomo kama kawaida. Kwa hoja hii ni dhahiri kwamba uamuzi ambao unachukuliwa kutokana na *by laws* za *University of Dar es Salaam* unalinda haki ya huyo mwanafunzi zaidi ya kuziminya kwa sababu inamfanya asiweze kufukuzwa chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limeibua hisia na limejadiliwa kwa muda sasa ni lile ambalo limekuwa likizungumzwa sana na Mheshimiwa Goodluck Mlinga na hilo ni suala la kutaka Serikali kutoa ufanuzi juu ya tabia ya baadhi ya walimu wa vyuo vikuu kuwafelisha wanafunzi kwa kutaka rushwa ya ngono. Serikali imelipokea suala hili, naomba itambulike kuwa Serikali ya Awamu ya Tano haina uvumilivu kwa vitendo vyovytote vya rushwa ikiwemo rushwa ya ngono shulenii au vyuoni. Nitoe wito kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu vitendo hivi pindi wanapovibaini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba mwanafunzi mpaka ahesabike kwamba amefeli haitokani na mtizamo wa mwalimu mmoja tu. Kuna taratibu ambazo zimekewwa kupitia *marks* ambazo amepata pamoja na kazi zake kwa ujumla ili kuweza hatimaye kuamua kama amefeli au hajafeli. Kwa hiyo, niwaondolee shaka kwamba hata kama ikitokea kuna mwalimu mmoja anafanya vitendo hivi haiwezi ikawa ndiyo inaathiri ufaulu wa mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vikuu vina taratibu maalum za kushughulikia masuala ya unyanyasaji wa kijinsia. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina sera iitwayo *Anti-Sexual Harassment Policy* ambayo inatoa mwongozo wa namna ya kushughulikia masuala haya. Hata hivyo, wanafunzi wengi inavyoonekana hawatumii sana msaada huu. Tunaendelea kuwasihii kama watapata matatizo kama haya waende kwenye Ofisi ya Mshauri wa Wanafunzi (*Dean of Students*) na watapata msaada unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba suala hili linazungumziwa vyuoni, nataka nitoe rai kwamba suala la maadili ni la kitaifa. Wakati Mheshimiwa Mlinga alivyotoa hoja hii kwenye mitandao ya kijamii watu wengine vilevile wameendelea kuonyesha kwamba unyanyasaji wa kijinsia au mahusiano yasiyosaidia wanafunzi hayafanyiki katika ngazi za vyuoni tu lakini wamesema hata baadhi ya

Waheshimiwa Wabunge nao wamejiingiza kwenye mahusiano ambayo hayasaidii wanafunzi.

Kwa hiyo, nitoe rai kwamba kwa sababu suala la maadili ni la kitaifa, hata sisi Waheshimiwa Wabunge tuhakikishe kwamba hatuingii kwenye mahusiano ambayo hayawasaidii wanafunzi wetu na tuwaache wamalize masomo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nawashukuru sana na naunga mkono hoja, ahsanteni kwa kuniskiliza. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa namuita mtoa hoja ili ahitimishe hoja yake; Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, una dakika zako arobaini. (*Makofii*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo niliwasilisha tarehe 30 Aprili, 2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi yangu na kwa uongozi wake ambao umetukuka. Kwa dhati kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye yeye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali na hakika yeye ni kiranja kweli kweli, anatusimamia kweli kweli. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakushukuru sana kwa uongozi wako mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kukushukuru wewe wa kuniongozea mjadala wa hoja yangu tangu nilipoiweka mezani na mpaka sasa tunapohitimisha. Nakushukuru sana umeongoza hoja hii vizuri sana. (*Makofii*)

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Peter Serukamba na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Juma Nkamia kwa ushirikiano mkubwa sana ambao ninaupata kutoka kwa Kamati hii. Nawashukuru sana kwa mchango mzuri ambao wameutoa katika hoja yangu na ninaahidi kwamba nitaendelea kuwapa ushirikiano na kuendelea kufanya kazi maoni na ushauri mzuri ambao wanapipatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wangu kwa ushirikiano mzuri anaonipatia, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote ambao tumeshirikiana katika kuhakikisha kwamba tunafaikisha hoja hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwashukuru washirika wa maendeleo lakini kipekee naomba nimshukuru Bi. Alice Birnbaum ambaye ni Mwenyekiti wa Washirika wa Maendeleo kutoka Canada lakini yeye ndiye Mwenyekiti wa Wadau wa Maendeleo ya Elimu; Ndugu Pantaleo Kapich kutoka *UNICEF*; Ndugu John Lusingu kutoka *DFID*, Ndugu Helen Reutersward kutoka *SIDA*; Ndugu Faith Shayo kutoka *UNESCO* na Ndugu Mwanahamisi Singano kutoka Sekretarieti ya *Development Partners*. Hao wamekuwa na mimi tangu nilipowasilisha hoja hii na mpaka sasa hivi wapo wanaangalia ninavyohitimisha, nasema ahsanteni sana, *thank you very much*. Naamini kukaa kwenu hapa mmesikia hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nikija kwenu kuomba ili...

## **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, hebu subiri kidogo Mheshimiwa Waziri, niambie ni kanuni ipi imevunjwa?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Kanuni ya 99(14)...

**MWENYEKITI:** Inasema nini?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Kanuni ya 99 (14) naomba niisome, inasema, bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ya 154, maneno yoyote ya utangulizi, utambulisho, salamu za pole, pongezi au shukrani pamoja na kutaja majina ya Wabunge waliochangia hoja havitaruhusiwa kwa Mbunge au Waziri wakati wa kujadili hotuba ya bajeti. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri endelea. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, hata maandiko matakatifu yanatufundisha kwamba tushukuru Mungu kwa kila jambo. Hawa watu wametusaidia tumejenga madarasa, kwa hiyo, mimi nawashukuru, naomba niendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, pia naomba niwashukuru sasa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii. Naomba nimalizie kwa kumshukuru mama yangu mzazi pamoja na mdogo wangu ambao wapo hapa kwa kuendelea kuniunga mkono, ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, baada ya maelezo hayo, naomba niseme kwamba hoja yangu imepata michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge ambapo jumla ya Wabunge 117 wamechangia hotuba. Waheshimiwa Wabunge 77 wamechangia kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge 46 ambao wamechangia kwa kuongea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa kuwa kanuni haziniruhusu kuwataja Waheshimiwa Wabunge waliozungumza, majina yao ninayo hapa na nitaomba orodha yao iingie kwenye *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa unyenyekevu kabisa naomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmechangia. Kwa kweli michango yenu imekuwa ni mizuri sana na inaonesha ni jinsi gani

ambavyo mnaithamini elimu. Kuonesha jinsi ambavyo michango imekuwa mizuri, leo tumepata mpaka na pambio kutoka kwa Mheshimiwa Mbatia, ametuimbia na wimbo wa chekechea. Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana na ninawaahidi kwamba michango yenu yote nimeipokea na nitaizingatia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda sitawenza kujibu hoja zote, lakini naomba nizungumzie mambo machache ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa wengi, lakini pia nitajikita kujibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu. Kwa bahati nzuri hoja ambazo zimetolewa na Kamati pia zimekuwa ni hoja ambazo zimezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kwa hiyo, napotoa maelezo nitakuwa sitaji hoja imetoka kwa nani lakini nitakuwa najikita kwenye hoja moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulikuwa unawahisha shughuli kaka yangu hapa wewe tulia tu hakuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie hali ya elimu, ni suala ambalo limezungumzwa sana, limezungumza na Kamati yangu, lakini pia limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana ambao wamechangia. Katika hoja hii wamesema kwamba hali ya elimu katika nchi yetu inashuka na kuna changamoto nyingi katika utoaji wa elimu katika nchi yetu, miundombinu, upatikanaji wa walimu na vifaa toshelezi vya kufundishia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuelezea kwamba elimu katika nchi yetu imekuwa ikipita katika vipindi mbalimbali. Tumekuwa na kipindi ambacho tulikuwa na changamoto sana ya uandikishaji katika shule za msingi na sekondari, tukaja na Progamu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi almaarufu kama *PEDP* ambayo iliongeza udahili wa wanafunzi katika shule za msingi.

Pia tulikuwa na udahili mdogo wa wanafunzi...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulikuwa na changamoto ya udahili mdogo katika shule za sekondari na tukawa na Programu ya Mpango wa Maendeleo ya Sekondari. Vilevile kulikuwa na mkakati wa dhati kabisa wa kujenga shule ya sekondari katika kila kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii imekuwa na mafanikio makubwa sana. Ukiangalia idadi ya shule za sekondari zilizokuwepo, mwaka 2005 zilikuwa 1,202 na kutokana na mikakati hii hadi kufikia mwaka 2010 jumla ya sekondari zilizokuwepo nchini zilikuwa 3,508. Mafanikio haya yalienda sambamba na ongezeko kubwa la wanafunzi ambao waliongezeka kutoka wanafunzi 524,324 hadi kufikia 1,401,330 kutoka mwaka 2005 hadi 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya ya ongezeko kubwa la wanafunzi ni dhahiri kwamba yaliambatana na changamoto kama vile miundombinu ambayo sasa haitoshelezi kama vile madarasa, ofisi za walimu, mabweni na maabara lakini pia ililetu uhaba mkubwa wa walimu. Sote tunafahamu tulipokuwa tunatekeleza mpango wa *PEDP* na *SEDP* kulikuwa na upungufu mkubwa wa walimu. Serikali illifanya jitihada za kukabiliana na changamoto ya walimu kwa kuwa na mikakati mbalimbali ambapo bado utoshelezi haujafikiwa hasa katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua haya, Rais wetu wa Awamu ya Tano, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli alipokuwa ameingia madarakani alikuwa anatambua fika kwamba amekabidhiwa nchi ikiwa na changamoto ambazo zilitokana na mafanikio ya kuongeza upatikanaji wa nafasi za elimu kwa watoto wa Kitanzania kwenye elimu ya msingi na elimu ya sekondari. Kwa kutambua hayo, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania alipokuwa analizindua Bunge hili tarehe 22 Novemba 2015, alizungumza na naomba kunukuu; "Natambua juhudini kubwa zimefanyika katika upanuzi wa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu. Serikali ya Awamu ya Tano itajielekeza katika kuongeza ubora wa elimu inayotolewa ikiwa ni pamoja na kuongeza mkazo katika masomo ya sayansi." Mwisho wa kunukuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hayo ili kukumbusha kwamba elimu imekuwa ikipitia katika vipindi mbalimbali na Mheshimiwa Rais alitambua changamoto zilizokuwepo na alizungumza ndani ya Bunge lako Tukufu. Nimpongeze sana Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu ametekeleza ahadi yake kwa vitendo. Ndani ya kipindi chake cha uongozi tumeona akitekeleza kwa vitendo uboreshaji wa elimu na nitaeleza kwa uchache mambo ambayo yamefanyika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na uboreshaji wa elimu, Mheshimiwa Rais akaanzisha utoaji wa elimu bila malipo. Kwa kweli hiyo ni *commitment* kubwa huku unaboresha elimu na wakati huo unatoa elimu bila malipo. Utoaji wa elimu bila malipo nao umekuja na mafanikio makubwa sana, idadi ya wanafunzi waliojijandikisha darasa la kwanza iliongezeka kutoka 1,386,592 hadi kufikia 1,896,584. Kwa hiyo, kwa maneno mengine changamoto ya madarasa ikazidi kuongezeka kutokana na ongezeko la wanafunzi ambao wanakwenda shuleni. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika sekta ya elimu ni kazi ambayo inaonekana wazi kabisa, hajifichia. Nenda katika Halmashauri yoyote utaona kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika sekta ya elimu. Kuna miundombinu ambayo inajengwa, lakini vilevile kumekuwa na kuhakikisha kwamba tunapeleka vifaa vya maabara. Kwa kweli, niseme tu kwamba Waheshimiwa Wabunge suala la kuboresha elimu ni *commitment* ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na analitekeleza kwa vitendo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwa uchache mambo ambayo yamekwishafanya kutoka Serikali Kuu, tukumbuke kwamba ujenzi wa miundombinu ni jukumu la TAMISEMI, hizo kazi zinafanywa na Halmashauri zetu, lakini kwa kutambua uzito na mzigo ambao halmashauri ziliikuwa zinaelemewa Serikali ya Awamu ya Tano imeona pia nayo ishiriki katika kuangalia yale maeneo ambayo yana changamoto kubwa tumekuwa tukipeleka kuwaunga mkono. Kwa hiyo, tayari jumla ya madarasa 1,947 na mabweni 338 yamekwishajengwa. Tumekuwa tukizungumzia hapa adha ambayo mtoto wa kike anaipata kutembea umbali mrefu kwenda shuleni. Serikali ya Awamu ya Tano inalionna hilo na kwa kupitia Serikali Kuu tayari tumekwishajenga mabweni 338 sambamba na yale ambayo yanajengwa na Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile matundu ya vyoo tumekwishajenga 4,501; nyumba za walimu 95; maktaba nne, majengo ya utawala 21 na mabwalo 14. Haya ni yale ambayo yamefanywa na Serikali Kuu, lakini hayajajumuisha idadi ya vyoo ambavyo vimejengwa katika Halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tumeshuhudia jinsi ambavyo shule zetu kongwe ziliikuwa zipo katika hali mbaya, ziliikuwa zipo choka mbaya kweli kweli, lakini Serikali ya Awamu ya Tano inakarabati shule kongwe na tayari tumeanza na shule 46 na mpaka sasa hivi tumekwishakamilisha shule 20 na ukarabati wa hizi shule nyingine unaendelea na shule zote kongwe 88 zitakarabatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hata vyuo vyetu nya ualimu vilikuwa katika hali ya uchakavu. Tumekwishafanya ukarabati katika vyuo nya walimu 22 na dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko hata kwake Tarime tumefika tunafanya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaendelea na uboreshaji wa miundombinu katika sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na vyuo vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuonyesha dhamira ya Mheshimiwa Rais wetu muungwana, akiahidi anatekeleza, hata bajeti ya mwaka huu ambayo nimesimama Waheshimiwa Wabunge na naomba wote kwa pamoja muiunge mkono kwa sababu elimu ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu na kwa hiyo elimu haina itikadi, naomba mtuunge mkono bajeti yetu ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi 916,841,822 hadi shilingi 929,969,402. Kwa hiyo, hiyo, inaonesha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano katika kuboresha elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge hata Roma haikujengwa kwa siku moja, lakini jitihada kubwa zinafanyika, muendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu na nina hakika kwa hapa tulipoanzia tutafika na elimu yetu itakaa vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya pia usambazaji wa vifaa, tumekuwa tukinunua vifaa vyaa maabara na tumepeleka katika shule 1,696. Kama mnakumbuka ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwa pia kuboresha mambo ya ufundishaji wa sayansi. Tunatambua pia kwamba ili elimu iweze kwenda vizuri lazima kuwe na mwalimu bora. Kwa hiyo, Serikali imekuwa ikiwekeza pia katika mafunzo kwa walimu kazini. Katika hili tumefanya sana, tumeweza kutoa mafunzo kwa walimu wa awali 16,129; tumetoa mafunzo kwa walimu wanaofundisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ambazo Mheshimiwa Mbatia naona naye atakuja kuungana nao ili aweze kufundisha kwa nyimbo zake zile nzuri walimu 65,232; tumetoa mafunzo kwa walimu wenye mahitaji maalum 800 na vilevile tumetoa mafunzo kwa walimu wa sekondari 12,726 kati ya hao walimu wa sayansi 10,614 na walimu wa lugha 2,112. Hayo ni kwa uchache tu kwa sababu ya muda siwezi kuelezea mambo ambayo Serikali ya Awamu ya Tano inafanya kuboresha elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuungane na tuhakikishe kwamba ule upungufu ambao tunaweza tukaenda kwa kasi zaidi,

ushauri wenu tunaupokea, tutaufanyia kazi lakini tunatambua kwamba tumetoka mbali katika historia ya elimu yetu. Tusiangalie tu Awamu ya Tano, lakini kama nchi historia ya elimu yetu imekuwa katika mapito mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala ambalo limezungumzwa sana hapa la wahitim u kumaliza bila kuwa na umahiri unaotakiwa. Wamezungumzia watu wanamaliza elimu ya msingi, hawajui kusoma na kuandika, watu wanamaliza vyuo vikuu, mtu anachukua sheria lakini hawezi kuandika hukumu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba niseme kwamba Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji katika sekta ya elimu. Niungane mkono na Kamati yangu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, wamenkuu Taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu viashiria vya utoaji huduma (*service delivery indicators*) ambazo zinaonesha kwamba walimu wanakuwa shulenii, lakini hawaingii madarasani au wakati mwininge hawafiki shulenii kabisa. Hali hii inaonesha kutowajibika kwa viongozi ambao wamepewa dhamana ya kusimamia elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba hapa katika sekta ya elimu tuna bahati kwa sababu tuna usimamizi mpaka kwenye ngazi ya kata, tuna Afisa Elimu Kata.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kutoa maagizo kwa Maafisa Elimu wote nchini kuhakikisha wanafanya kazi yao ipasavyo, wasimamie kwa karibu elimu na kuhakikisha kwamba walimu wanafundisha kama inavyotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaase waache mtindo wa kumchukulia mwalimu sasa kama ndio mtu wa kulaumiwa yanapotokea matatizo, mwalimu ndiyo anaachishwa kazi. Kwa nini usubiri matokeo ya mtihani shule yake ikifanya vibaya ndiyo umuachishe kazi, ulikuwa wapi mwaka mzima kumfuatilia, kuangalia anafanya nini, unasubiri matokeo ya mtihani yeye ndiyo umfukuze kazi. Hiyo sio sawa, ni uonevu kwa wakuu wa shule kwa sababu na wenyewe

wana viongozi juu yao, kwa nini wao ambao wanatakiwa kuwasimamia wasiwajibishwe? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaagiza Maafisa Elimu wafanye kazi yao vizuri. Maafisa Elimu wa ngazi ya Kata unakuta mtu ana shule tano tu, utashindwaje kuzisimamia au utashindwaje kuona matatizo. Kwa hiyo, katika hili Serikali itahakikisha tunaimarisha usimamizi ikiwa ni pamoja na kuwaondoa viongozi ambao ni mzigo, ambao ndiyo wanaotufikisha hapa. Serikali inafanya kazi kubwa ya kuwekeza, lakini kama hakuna usimamizi imara katika sekta ya elimu tutakuwa kama vile tunatwanga maji kwenye kinu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa taasisi za elimu ya juu na vyuo vya kati, wahitimu wanamaliza hawawezi hata kuandika hukumu, tunavyo vyombo ambavyo vimepewa mamlaka kisheria vya kuhakikisha vinadhibiti ubora katika elimu ya kati na elimu ya juu. Tunalo Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu na tuna Tume ya Vyuo Vikuu nchini. Kwa hiyo, hii nayo inadhihirisha kwamba pengine zana wanazozitumia katika kufanya ukaguzi zinahitaji kufanyiwa mapitio. Kwa sababu tumekuwa tukiona hapa Tume ya Vyuo Vikuu imekuwa ikifungia vyuo kwa sababu havina sifa, tumeona hapa Baraza la Taifa la Ufundu limekuwa likifungia vyuo lakini nadhani ipo haja ya kukaa chini kwa taasisi hizi kupitia upya zana wanazozitumia kukagua vyuo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa maagizo kwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu, wakae chini wapitie upya vigezo ambavyo wanatumia kuangalia ubora wa vyuo vyetu vikuu. Angalieni mitaala inayotumika, angalieni sifa za walimu ambao wako katika vyuo vikuu, angalieni mpaka na aina ya mitihani ambayo inatolewa, namna inavyosahihishwa ili muangalie vigezo vyote kwa ujumla wake. Kwa sababu haiwezekani tuwe tunafungia vyuo halafu bado hata vyuo ambavyo tunaviona vinafaa vinatoa wahitimu ambao hawahitajiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutoa wahitimu ambao hawana sifa zinazotakiwa halikubaliki. Naviagiza hivi vyombo kufanya kazi yao bila kumuogopa mtu ye yote. Chuo chochote ambacho kitabainika hakina sifa, iwe ni cha Serikali, iwe ni cha binafsi, kama hakina sifa kifungiwe. Hatuwezi tukaendelea kuangamiza Taifa hili kwa kuzalisha watu ambao hawana sifa. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la hali ya ufaulu nchini. Suala hili pia limeongeleta sana na hata Kamati yetu imetoe takwimu kubwa na mimi nikiri kwamba hali ya ufaulu ilivyo hata na mimi natamani kwamba wanafunzi wangeweza kufaulu kwa wingi zaidi kuliko wanavyofaulu sasa. Kama nilivyotangulia kusema Waheshimiwa Wabunge ni kwamba maendeleo na hasa katika sekta ya elimu ni hatua kwa hatua. Kwa hiyo, tumekuwa kwa kweli na ufaulu ambao ukiangalia asilimia kubwa ya wanafunzi wanakuwa katika daraja la nne na daraja la sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba mtu anayefaulu kwa daraja la kwanza amefaulu zaidi kuliko wa daraja la nne lakini niombe tu tusije tukaweka dhana kwamba mtu aliyepata daraja la nne hafai kabisa, kwa sababu kwa vigezo tulivyonavyo sasa daraja la nne amefaulu. Suala ambalo tunaweza tukazungumza ni kama labda pengine tunaona viwango viko chini tunaweza tukafikiria hata kuviungeza lakini kwa sababu kwa viwango tulivyojiwekea daraja la nne mtu amefaulu, tusiongee katika lugha ambayo ni kukatisha tamaa. Kwa hiyo, nimesema kwamba kupata *division one* amefaulu vizuri zaidi, lakini kwa utaratibu uliopo sasa hivi hata aliyepata *division four* amefaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme pia kwamba suala la idadi ya ambao wamepata *division one* mpaka *three* kama nilivyosema si ya kuridhisha kwa kiwango ambacho hata Serikali ingetamani. Sisi hatuwezi kuchakachua matokeo, tunatoa matokeo kadri ambavyo yapo, lakini Serikali inachokifanya ni kutekeleza wajibu wake, kuweka

miundombinu na kuhakikisha walimu wanapatikana. Kwa hiyo, pia nitumie nafasi hii kuwaomba wanafunzi nao watekeleze wajibu wao kwa sababu hata mwanafunzi naye pia ana wajibu katika kuweza kufanya vizuri katika mitihani yake, lakini hata mzazi naye ana wajibu kwa mwanafunzi kufanya vizuri. Serikali itaendelea kutekeleza wajibu wake lakini suala la ufaulu mzuri ni *collective responsibility* kati ya mzazi, walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, naomba kwa kweli tushirikiane na Serikali kwa sababu Serikali ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba wanaopata daraja la kwanza mpaka la tatu wanakwenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufaulu umekuwa ukiongezeka kama ninavyosema, japo siyo kwa kasi kubwa, lakini ukiangalia mwaka 2015 waliopata daraja la kwanza mpaka la tatu walikuwa asilimia 25.34; mwaka 2016 walikuwa asilimia 27.60 na mwaka 2017 walikuwa asilimia 30.15. Kwa hiyo, kuna ongezeko dogo lakini tukishirikiana na usimamizi ukawa mzuri naamini hata hii kasi ya ongezeko inaweza ikaenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuiangalie elimu katika mapana yake kwa ujumla. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge ulipoingia humu Bungeni siku ya kwanza na ulivyo leo, sasa hivi tuna miaka miwili na nusu uko tofauti kabisa, hakuna chaki, hakuna ubao lakini hata *interaction* ambayo unaipata pia ni elimu tosha. Kwa hiyo, tunapopima mafanikio ya elimu tuangalie pia katika ujumla wake hata mwamko wa wananchi kupeleka wanafunzi shule pia ni mafanikio katika sekta ya elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani Serikali ilikuwa inatumia nguvu kubwa sana kupita katika kijiji na katika kaya kuwatoa watoto ili waende shulenii lakini sasa hivi tunashuhudia mafuriko ya wanafunzi shulenii. Mimi nasema kwamba haya ni mafanikio katika elimu na mafanikio haya ndiyo yameendelea kuleta changamoto ambazo Serikali inazifanyia kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mwamko wa wananchi katika shughuli za kijamii, unakuta hata mzee anakwenda kushiriki katika kujenga shule na zahanati. Mimi nasema haya ni mafanikio kwa sababu wangekuwa hawaoni umuhimu wa elimu wasingejitokeza kujitolea nguvu zao. Pia hata ukiona mwitikio katika masuala ya kijamii kwa ujumla, masuala ya afya, idadi ya wanawake ambaao wanakwenda kliniki, yote ni mafanikio ya elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekee kwenye suala lingine ambalo limeongelewa kweli kweli, suala la usimamizi wa shule binafsi, lakini pia nitaliunganisha na suala la wanafunzi kukariri. Waheshimiwa Wabunge wameongea sana na wengine wameongea kwa hisia na wengine wameenda mbali kabisa wanasema kwamba Serikali inaonea wivu sekta binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la kukariri na naomba nilizungumze tu vizuri, nami najua Waheshimiwa Wabunge ni waelewa, wakati mwingine pengine inawezekana hamkuwa na taarifa kamili ya jambo hili. Kimsingi niseme kwamba suala la wanafunzi kukariri ni suala ambalo lipo kwa mujibu wa taratibu na kukariri hata wanafunzi wa shule za Serikali wanaruhusiwa kukariri kwa mujibu wa utaratibu ambaao umewekwa.

Kuna mitihani ambayo inatolewa, kuna mtihani wa darasa la nne mwanafunzi ambaye hafikishi alama anatakiwa kukariri na kuna mtihani wa kidato cha pili mwanafunzi anaruhusiwa kukariri. Mbali na mitihani hiyo bado kuna utaratibu ambaao mwanafunzi anaweza kukariri ikiwa mzazi wake anaona kwamba uwezo wa mtoto wake ni mdogo kama ataendelea na hatua aliyofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu huo upo na nizishukuru sana shule binafsi kwa sababu asilimia kubwa wanatekeleza kikamilifu miongozo na taratibu za elimu. Hata hivyo, wapo wachache, tena wachache sana ambaao wanakwenda kinyume na utaratibu na nitatoa mifano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanazungumzia suala la wanafunzi kukariri, lakini tatizo ni zaidi ya hapo, sio tu kukariri, shule zimekuwa zikiwafukuza wanafunzi na kufukuza huko kwa kweli mimi nasema kwingine kumepitiliza. Kwa mfano, tulipokuwa tunaanza mwaka huu 2018, shule ambazo zimetoa taarifa, tulikuwa na wanafunzi 1,029 ambaao wengine wako katika mwaka wa mtihani amefukuzwa tu kwa sababu hajafikia alama, siyo kwamba anakariri, hapana, anaambiwa ondoka, aende nyumbani, mzazi amelipa mamilioni ya fedha na kwa sababu mwanafunzi hakufikisha alama anaambiwa aondoke. Kwani kazi ya shule ni nini, si ndiyo kutoa elimu? Kama mwanafunzi hawezi si umwambie akae hapo umfundishe? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli suala la kuwafukuza wanafunzi si halali. Suala hili linakwenda kinyume na sheria ya elimu kwa sababu hizi shule binafsi nazo zinatakiwa zizingatie sharia hii kwa sababu sheria tunapozitunga hapa Bungeni wote tunawajibika kuzizingatia ikiwemo Serikali na kila mmoja ambaye sheria hiyo inamhusu. Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 inasema wazi kwamba; *primary school shall be compulsory for every child who has reached the age of seven years to be enrolled for primary school.* Sheria hiyo inaonesha kabisa kwamba mtoto lazima asome, ahudhurie mpaka amalize, ndivyo sheria inavyosema, haisemi akifika darasa la sita kwa sababu unamuona hajafikisha alama umfukuze aende mitaani, tutazalisha watoto wa mitaani bila sababu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kutokana na changamoto hiyo ambayo nikitoa mfano shule ya *Panda Hill* iliyoko Mbeya peke yake ilikuwa imefukuza wanafunzi 114, shule moja wanafunzi 114, eti hawajafikisha alama ambayo imewekwa na shule. Hivi shule moja wanafunzi 114 wakishindwa kufanya vizuri ni tatizo la wanafunzi au inawezekana ni tatizo la walimu wao hawakuwafundisha vizuri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi zinachukua wanafunzi ambao ni *cream*, leo wanafunzi 114 unawafukuza? Ni kutohana na sababu hizo za watu kufukuza ndio Serikali ikawa hatu imetoa na maelekezo kwamba wale waliofukuzwa warudi shulenii, suala la kukaririsha halina matatizo yoyote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakinii pia kutohana na changamoto hizo mimi mwenyewe binafsi nilikutana na wamiliki wa shule binafsi. Mwanzoni walikuwa wanaona kama vile Serikali imewaonea, lakinii baada ya kuwapa takwimu kwa kweli na wenyewe walikiri kwamba suala hili shule moja kama hiyo *Panda Hill* imefukuza wanafunzi 114, Shule ya Sekondari ya *St. Pius* ya Dar es Salaam wanafunzi 89 kwa mwaka mmoja wanafukuzwa. Kwa hiyo, wao wenyewe shule binafsi mimi nawashukuru sana, hatu na wao ni wazalendo sana, walisema Mheshimiwa Waziri, hili Jambo ungetuambia sisi wenyewe, tuna chama chetu tungewashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli suala hili wala siyo tatizo kubwa sana ni suala tu sasa la baada ya hayo kutokea tulichokubaliana na wamiliki wa shule binafsi ni kwamba tukae kwa pamoja kwamba pamoja na nia njema ya kuhakikisha kwamba kabla mtoto hajaendelea anakuwa na viwango vizuri, lakinii tuweke na utaratibu wa kulinda watoto wa wanyonge wa Kitanzania ambao wanakuwa milioni za fedha halafu mtu mmoja tu kwa mtihani ambao hakuna anayejua ameutunga kwa vigezo gani, kwa mtihani ambao hakuna anayejua ameusahihisha kwa vigezo gani, analala anaamka anawaambiwa watoto 114 kwenye shule moja waondoke. Jambo hili halikubaliki na Waheshimiwa Wabunge naomba katika hili la kufukuza kwa utaratibu huo mniunge mkono. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna Kamati ya Majadiliano ambayo kuna wajumbe kutoka Wizara ya Elimu na wajumbe kutoka sekta binafsi ambao kwenye sekta binafsi kuna Bwana Laurent Gama wa *TAPIE* ambaye ni Katibu, kuna Bi. Stella Rweikiza wa *TAPIE* na Bwana Moses

Kyando kutoka *TAMONGSCO* ambapo majadiliano yanakwenda vizuri. Wenyewe wamesema pia wataisaidia Serikali katika kuhakikisha hakuna shule za binafsi ambazo zinawachafua kwa sababu wanatambua kwamba samaki mmoja akioza wote wameoza. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hili suala halina tatizo lolote na baada ya muda mfupi tutafikia mwafaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe hoja hii kwa kulieleza Bunge lako tukufu kwamba Serikali inaheshimu na kuthamini sana mchango wa sekta binafsi katika utoaji elimu. Kwa taarifa tu ya Bunge hili, sekta binafsi kwenye elimu ni wadau wakubwa sana ambaao Serikali kwa namna yoyote ile haiwezi ikawachezea au kutothamini mchango wao kwa sababu shule za msingi za binafsi zilizoko nchini ni 1,247; shule za sekondari za binafsi ni 1,192 na wanaosoma hapo ni watoto wa Kitanzania. Sasa ina maana Serikali ikinyanyasa shule binafsi inanyanyasa watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba hakuna mgogoro wowote, hakuna vivu wala chuki kwa shule binafsi. Labda tu kinachowenza kujitokeza ni mawasiliano, pengine inawezekana kuna watendaji ndani ya Wizara yangu wakiona wamiliki wa shule binafsi wanakuwa wanawapa majibu ambayo siyo mazuri. Sasa hilo ni suala la kiutendaji na naomba kama wapo watendaji wa namna hiyo niambiwe, nitawashughulikia kikweli kweli, wasituharibie ushirikiano wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nytingine ambayo imezungumzwa ni suala la udhibiti ubora wa shule na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa ujumla wao wamezungumza sana lakini hata na Kamati yangu wamezungumza na kumetolewa ushauri wa kuundwa chombo cha kudhibiti ubora yaani uanzishwaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Elimu katika nchi yetu. Kwanza nianze kusema kwamba napokea ushauri huu kwa heshima kubwa na niseme kwamba kama niliviotangulia kusema katika maelezo yangu ya utangulizi, nimefaidika sana na michango ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili nalipokea lakini nizungumzie jitihada ambazo kwa sasa Serikali ilikuwa imeanza kuzifanya katika kuboresha hii sekta ya udhibiti ubora wa shule. Kwanza, nimeelezea ile changamoto ya wanafunzi kuwa wengi katika shule zetu, lakini nimeeleza pia na jitihada ambazo Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikifanya katika kukabiliana na changamoto hizo. Ni ukweli kwamba katika baadhi ya shule ile idadi ya ongezeko la wanafunzi halijaenda sawia na idadi ya walimu ambao wanatakiwa kuwepo shulenii. Kwa kutambua hilo, Wizara imekuwa ikiendelea kuimarisha mafunzo kazini na uhaba wa walimu wa sayansi pamoja na mkakati wa wanafunzi wale ambao walikuwa wako *UDOM* ambao mwaka huu kuna *bunch* ambayo imemaliza lakini pia hata katika bajeti yangu mwaka huu tutatenga fedha kwa ajili ya waafunzi ambao wamesoma *Bachelor of Science*, ile *general*, ili wakafanye *Postgraduate Diploma in Education* kuweza kuendelea kutatua changamoto za elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika udhibiti ubora wa shule, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa ufuatiliaji na ujifunzaji kwa sababu Wadhibiti Ubora wa Shule ndiyo jicho letu, ni sawa ambavyo *CAG* ndio jicho la Serikali katika matumizi ya fedha za umma.

Kwa hiyo, Wizara kwanza tumebadilisha mfumo wa ukaguzi, nimeeleza katika hotuba yangu kwamba tumeandaa kiunzi cha udhibiti ubora wa shule ambacho kitaboresha usimamizi wa masuala ya elimu.

Pia tumetoa mafunzo kuanzia ngazi ya shule na Kamati za shule. Kwa mara ya kwanza tumeshirikisha pia Kamati za Shule, kwa sababu ni kweli tunaona kwamba tuwe na chombo cha kuangalia hii elimu yetu lakini niseme kwamba tuna shule za msingi 17,000, tuna shule za sekondari kama 5,500, kwa hiyo, kwa namna yoyote ile chombo ambacho kitakuwa kipo kitaifa bado kitakuwa na changamoto. Mkakati wa Wizara pia ni pamoja na kuimarisha Bodi za Shule abazo ndizo zinazowajibika katika usimamizi wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu udhibiti ubora wa shule tunauboresha na nashukuru katika michango kuna Waheshimiwa Wabunge waliona kwamba tunajenga ofisi 50 za udhibiti ubora wa shule. Pia nimesema tumenunua magari 54, pikipiki 2,894 kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji ngazi ya kata. Waheshimiwa Wabunge pikipiki hizi tutazigawa kabla hatujamaliza Bunge. Kwa hiyo, mkirudi majimboni mtapata pikipiki ili kuimarisha usimamizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tushirikiane katika kuwabana watu wasimamie elimu ipasavyo, hii ndiyo jitihada ya Serikali. Kama nilivyo sema, elimu ni juhudhi za Serikali, wazazi, wanafunzi, wote kwa ujumla wetu tukishikana mkono, nina uhakika kwamba elimu ya Tanzania itasimama. Niwatoe hofu kabisa wale ambao mnasema kwamba elimu ya nchi yetu iko vibaya; niwaambie elimu ya nchi yetu iko vizuri kabisa, ina afya njema na Rais wetu ana utashi, amekwishafanya mambo makubwa, kitu kikubwa ni ushirikiano ambao unatakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata suala la kuwa na mjadala wa elimu limezungumzwa sana. Niseme tu kwamba mjadala katika sekta ya elimu ni mjadala ambao utatuwezesha sisi kubaini matatizo. Niseme kwamba kuna matatizo ambayo tayari tunayafahamu, tunafahamu kwamba kuna shule ambazo zina mrundikano na ndiyo maana tumejikita katika miundombinu; tunafahamu kuna shule zina uhaba wa walimu, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Utumishi ameahidi kwamba ataendelea kulitatua; tunafahamu kwamba kuna shule ambazo watoto wanatembea umbali mrefu, ndiyo maana tumekuwa tunajenga mabweni.

Kwa hiyo, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ilikuwa ni kujikita katika kutatua changamoto ambazo tayari tunazifahamu lakini hii haizui wadau ambao wana mapenzi mema na nchi yetu kuendelea kuibua changamoto nyingine na kuipa changamoto Serikali yao ili sambamba na changamoto ambazo Serikali imeamua inafanyia kazi, kama zipo nyingine zitafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mjadala ji suala ambalo lina afya kwa sababu linalenga katika kuibua changamoto zilizopo ili Serikali, Serikali hii sikiu iweze kuzifanyia kazi na tumekuwa tukishuhudia mjadala kwa mfano tulikuwa na Kigoda cha Mwalimu kilikuwa kinazungumzia masuala ya uporaji wa rushwa na rasilimali za nchi yetu; tumeshuhudia Kibweta cha Mwalimu ambacho kilikuwa kinazungumzia kuelekea uchumi wa kati. Kwa hiyo, tumekuwa na mjadala mbalimbali ambayo ikitokea katika nchi na hivyo basi mjadala kwenye elimu ni suala ambalo niseme kama Waziri mwenye dhamana linapokelewa kwa mikono miwili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshapigiwa kengele na nisingependa kupigiwa kengele ya pili kama nilivyosema michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni mingi ni mizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na moja tu ambalo nalo lilizungumzwa sana kuhusiana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na kwamba hakuna mpango mkakati wa sera na kwamba tunatumia sheria ya mwaka 1978, nikiri kwamba kweli ile sera yetu ya elimu bado hajjawekewa zile sheria na niseme kwamba tayari ile sera ya elimu kwa namna ambavyo iliandikwa kwa bahati mbaya iliandikwa katika namna ambayo inakuwa ni nyaraka au *document* ambayo haiishi, wanasema *a living document* kwamba mle ndani kwa mfano imesema Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa sasa hivi haipo mle ndani inazungumzia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis i pale Wizara sasa hivi haipo na mambo mengine nimetoa kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona kwamba ni vema hata hiyo uandishi wa sera yetu uandikwe katika namna ambayo itakuwa ni *document* ambayo inaweza ikakaa miaka mingi bila kuhitaji kubadilisha badilisha na Mheshimiwa Mbatia naona ameishilikia, lakini tu kwa uchache ni kwamba hii suala la sera ya elimu pia kuna suala kwa mfano na umri wa kwenda shulen kutoka miaka saba

kwenda miaka mitano ilibadilishwa kabla ya hata kubadilisha sheria kwa sababu miaka saba umri wa kwenda shulenii umewekwa ndani ya sheria. Kwa hiyo, tayari hata kuna mkingano katika sheria zilizopo. Niombe katika hii sera ya elimu tunakusudia kufanya mapitio vile vitu ambavyo vinaukinzani tuvibadilishe kwanza kabla hatujaenda kwenye kutengeneza sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo na kwa sababu kwamba muda wa kwenda shulenii miaka saba umetajwa kwenye sheria ya elimu na katika Bunge lako tukufu hamjafanya mapitio ya marekebisho ya Sheria ya Elimu miaka ya elimu ya msingi itaendele kuwa miaka saba hadi pale marekebisho ya sheria yatakapofanyika. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba kutakuwa na wanafunzi ambaao wanamaliza wengine darasa la sita, wengine ni darasa la saba kwa sasa halipo mpaka hii sheria ambayo tunaitumila itakapofanyiwa marekebisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo na ufanuzi huu wa hoja naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge ambaao sikuweza kupata muda wa kujibu hoja zao kwamba hoja zote tutazijibu kwa maandishi na baada ya ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizotolewa ambazo nimeweza kuzieleza pamoja na zile ambazo ninazileta kwa maandishi, sasa kwa unyenyekevu mkubwa kabisa ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tutakapokaa kama Kamati naomba wote kwa pamoja muunge mkono hoja yangu mnipitishie Makadirio ya Mapato na Matumizi ili sasa haya ambayo nimewahaidi niweze kwenda kutekeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono, tunakushukuru sana kwa hotuba yako. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi, Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 18 - Tume ya UNESCO**

Kif.1001-*Administration and HRM*.....Sh. 666, 855, 000/=

(*Kifungu kiliichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kif.1001- *Administration and HRM*.....Sh. 6, 939,228,003/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nina orodha hapa ya majina ya Wabunge ambao kwa mtawanyiko wa vyama kwenye mshahara wa Waziri ili tuokoe muda nina majina haya ili mjifahamu wote huko Waheshimiwa Wabunge kwa upande wa CCM Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Amina Mollel. Kwa CHADEMA Mheshimiwa Susan Lyimo na Mwalimu Kasuku Bilago; CUF nadhani wenyewe wameelewana watasemewa na NCCR Mageuzi, tunaanza, Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha hoja yake amezungumzia suala la wanafunzi kukariri, lakini alivyolizungumza hapa amelizungumza kwa lugha ya upole

sana kana kwamba ni jambo ambalo halijawahi kuleta sitofahamu katika ya Wizara pamoja na Sekta Binafsi. Sasa ningependa angalau sasa tulizungumze kwa kina na Wabunge waelewe hasa maudhui kwa nini Serikali ilikuwa inaweka msisitizo huu watoto kukariri ili hali kwamba mzazi mwenyewe ameridhia kwamba mwanangu labda kulingana na uwezo wake labda ni *slow learner* anahitaji kujifunza zaidi niko tayari kulipa ada na kadhalika, lakini bado Serikali ilikuwa imeweka pamba masikioni. Na kwa kweli kama majibu bado yatakuwa hajaridhisha kama ambavyo hayaridhisa wakati anajibu hoja basi nitakusudia kuondoa shilingi katika mshahara wake, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Mheshimiwa Shangazi katika majibu yangu ya nilivyokuwa najibu hoja nimeeleza kwamba kimsingi Serikali inao utaratibu wa wanafunzi kukariri na utaratibu ule unapokuwa unafuatwa hakuna tatizo lolote na nimesema kukariri kuna taratibu mbili ama kupitia mtihani wa kidato cha pili na mtihani wa darasa la nne au kwa ridhaa ya mzazi mwenyewe.

Kwa hiyo, kama nilivyoeleza ni kwamba kulikuwa na ukiukwaji kwa baadhi ya shule ambazo zilikuwa hazifuati hizo taratibu na ndiyo maana waliota taarifa ni wazazi wenyeve baada ya kuona kwamba bila ridhaa yao watoto wao walikuwa wamefukuzwa shuleni wakaja kutoa taarifa Serikalini na sisi tukachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Shangazi naomba uamini kwamba sijajibu hili jambo kwa wepesi, jambo nilivyolijibu ndiyo hali halisi ilivyo na naomba uniache shilingi yangu ili niweze kupata fedha za kutekeleza haya ambayo ninataka kuyafanya kwenye sekta ya elimu. Naomba unirudishie shilingi tafadhali.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shangazi katika hatua hii hakuna hotuba.

**MHE. RASHID A SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri. Anachozungumza ye ye ni katika vile viwango ambavyo vimewekwa na Serikali kwa maana ya kidato ya cha pili, kidato cha nne na darasa la nne. Lakini hapa mimi nazungumzia kwa ujumla wake haswa katika hizi shule za msingi kwa maana kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba haswa shule za *private* na Mheshimiwa Waziri wakati anajibu mwanzoni alitoa mfano wa shule mbili, tatu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nielewe katika hatua hii kama unataka nenda *straight* sasa katika kutoa hoja.

**MHE. RASHID A SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba nitoe hoja Waheshimiwa Wabunge tujadili kwa mapana jambo hili ili tuweze kupata ufahamu wa pamoja. Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Usikae, Mheshimiwa Kakunda, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Mbogo, Mheshimiwa Mulugo, Mheshimiwa Dkt. Tisekwa wametosha wengi mno, Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa, jamani wametosha hawa tuanze na tunaanza Mheshimiwa Rehema Migilla.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga hoja ya Mheshimiwa Shangazi aliyekuwa anaongea kuhusu kukariri. Suala la kukariri watoto linatokea kwa sababu mbalimbali ikiwemo unakuta labda hajajua kusoma vizuri au matatizo ya utoro unakuta ajafaulu vizuri ile mitihani yake. Lakini unakuta mzazi kama kwenye shule za *private* ameona sasa kuna haja ya huyu mtoto kukariri labda ili afikie *quality* inayotakiwa, Lakini unakuwa baadhi ya shule hazitaki ili hali mzazi mwenyewe amekubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiria kuna haja ya hii suala hili liangalie kwa mapana yake na siyo kuzilazimisha hizi shule eti zisikaririshe ziendele kukaririsha, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER. N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Shangazi kwamba kwa sasa hivi ilivyo na wanavyokataza wanafunzi wasikarishwe. Tunajua kabisa kwamba watoto wetu *learning capacity* zao ni tofauti, wana *different* ya *IQ* na kuna wengine wanavushwa darasa kuna kwa sababu ya uelewa wao wanawajibika kurudia kukarishwa na hata kwa shule za *private* tunavyokuwa wazazi wamepeleka watoto wanakuta wamepewa masharti, wameambiwa kabisa shule hii mtoto asipovuka kiwango hiki itambidi akaririshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi mfumo ulipo ili mzazi aweze kuambiwa mtoto akariri au asikarishwe lazima apate kibali kutoka kwa *RASKwa* jinsi ninavyoilewa hii inaleta ukiritimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tungependa kabisa Mheshimiwa kama Serikali imeona hili jambo ni sawa iwepo sera madhubuti ambayo itaeleza bayana na itatanabaisha kwa hizi shule za za *private* ikizingatia kwamba uwelewa wa watoto wetu unatofautiana, kuna ambao watahitaji kukarishwa kuna ambao wanavushwa madarasa kama hata ilivyokuwa ikifanyika hapo zamani, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Shangazi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi, kwanza niseme kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Shangazi kwa minajili kwamba Serikali iondoe suala ya kukarishwa watoto katika hizi shule za binafsi na ikiwezekana kwa sababu tayari kuna vigezo ambavyo Serikali imekwisha tengeneza darasa la nne, darasa la saba, *form two* na *form four* basi shule zote binafsi zizingatie vigezo vyta Serikali na kuandaa vigezo ambavyo kila shule imojiwekea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Unaunga mkono?

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Shangazi.

**MWENYEKITI:** Mbona umejichanganya Mheshimiwa wewe hayo uliyoleza ndiyo haya ambayo Serikali inasema, haya, tunaendelea na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ni wazi kabisa kwamba kiwango cha uwelewa cha watoto wetu baadhi yao kinapanda kadri wanavyoendelea na masomo. Kijana anaweza akakosa uwezo akiwa *form one* ukimpeleka *form two* akashindwa lakini akirejea *form one* uwezo wake unaongezeka, wanaojenga hoja kwamba watoto wasikarishwe katika *private secondary schools* wanajivika viatu vya wazazi vya gharama. Kuhusu gharama nina mtoto wangu nina uwezo nataka afaulu naweza kumrejesha katika lile darasa hata miaka mitatu kwa sababu milipaji ni na akifaulu ni faida kwa Serikali sio faida kwangu peke yangu kwa sababu hawa watu wanasmeshwa kwa ajili... (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa umeeleweka. Tunaendelea na Mheshimiwa Kalanga Laizer.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Shangazi kwa hoja kwamba nimewahi kushuhudia mfumo ule wa kukariri ambapo mzazi anapaswa kuomba kwa Afisa Elimu mpaka ienda kwa *RAS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi katika utaratibu wa kawaida unapoteza muda gani na rasilimali gani katika kufuatilia taratibu hiyo. Na mimi sijui kwa nini Serikali inapata kigugumizi ni vizuri Waziri angesema tu watoto waruhusiwe kukaririhswa wala asingekuwa na kesi hapa. Lakini majibu yake yamekaa kimtego kwamba anasema haina shida. Lakini ukienda kwenye mfumo wa kawaida hawaruhusu.

Kwa hiyo, kama Waziri anataka kuturidhisha aseme tu kwamba utaratibu wa kukariri tunaukubali na utaratibu

ni huu ambao uwazi na kila mtu anaukubali, lakini majibu yake yana maswali mengi zaidi kuliko majibu ndiyo maana tuna lalamika. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mulugo Philip.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni pana sana linaongelewa tu kwa sababu sisi wengine kwa sababu ni wahusika wa moja kwa moja haliko hivi kama tunavyoweza kiliongelea, limeleta shida sana mwezi wa kwanza. Nashukuru Mungu mwenyewe nilihusika tulikwenda kwa Waziri wa Elimu pamoja na Katibu Mkuu tukakaa, kilichokubalika imeundwa Kamati Maalum shule binafsi wapo kama alivyosoma majina na Serikali wapo pamoja na *TAPIE*, *TAMONGSCO*, wajumbe wale hawajamaliza bado kazi na hata majibu ya Mheshimiwa Waziri ameelekeza kabisa kwamba kule ndiko kutakakoweza kupewa mfumo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja tu kwamba, naunga hoja ya Shangazi kwamba utaratibu huu kweli ukienda kwa Maafisa Elimu wa ma-*DEO*, ma-*REO* ni mgumu sana; Mheshimiwa Waziri atoe utaratibu kamili kwamba hoja hiyo Kamati maalum itakapomaliza kazi wale wailete hapa Bungeni ili wananchi waweeze kuelewa namna ya ukakaririshaji wa hawa watoto. Lakini kukaririsha bado ni muhimu sana kwa sababu ipo *joining instruction* kwenye shule za *private* inaelewaka kabisa, ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** ahsante, Mheshimiwa Dkt. Tisekwa Bunga.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme niongee kidogo kwamba ni mwalimu nafahamu kabisa mwalimu anatakiwa kufanya nini kuweza kuhakikisha watoto wake wote wanafaulu. Kwa hiyo, hili suala la kukaririsha kwa kweli nataka niliangalie kwa mapana kwamba Serikali lazima isimamie kwa mfano *data* hizi walizotoa kwamba watoto 114 unawaambia aidha, warudie au wafukuze kama wamekataa kukariri hawa watoto kweli

*frustrations* na kadhalika. Kwa hiyo, ninachoomba Serikali kwa kweli isimamie kwa sababu shule ya private inafanyakazi nzuri lakini kuna biashara kwa sababu wao wanapata wanafunzi kwa *performance* na wao wana wanafunzi *cream* kwa hiyo, kama wanafunzi wao ni *cream* basi hawa wawafundishe, wawatoe, wakikariri wawili, watatu siyo mbaya lakini hii *number is alarming* lazima Serikali isimamie kwa mambo kama haya. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Shangazi kwamba hata ukiangalia hapa wengi walikariri enzi zao na mpaka tumefika hapa tulipo. Lakini sasa ilivyokuja hoja kwamba watu wasikariri nikawa ninakwenda mbali sana kuna watoto wengine wanamaliza shule na umri mdogo kwa hiyo baba yake kwa kupenda tu kwa vile hajafanya vizuri darasa la saba akamrudisha tena shulenii ili akue shulenii, ili apate kuendelea na masomo, vilevile hata *form four*. Namuangalia sana mtoto wa kike ambaye akiacha kukaririshwa huyu mtoto kwa ridhaa yake ama ya baba yake, huyu mtoto anakwenda kufanya nini?

Kwa hiyo, ni muhimu huo utaratibu ukawekwa vizuri maana kama alivyoliweka Waziri tu hivyo linavyokuwa zima zima watu wanaweza wakapata shida sana huko mtaani. Ni bora wakaweka vizuri kama hivi alivyosema Mheshimiwa Tisekwa shule zisiamamiwe kama ni *private*, wasilazimishwe watu lakini wale wenye hiari yao waachwe wakariri kwa sababu gharama ni za kwao wenyewe, lakini faida kwa Taifa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ryoba Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mazingira ya Tanzania ambayo bado tuna uhaba na changamoto nyingi, upungufu wa walimu, upungufu wa vitabu, haiwezekani watoto wakawa na uelewa mmoja,

wakafaulu wote kwa pamoja. Kwa hiyo, suala la kurudia *is inevitable*, ni vizuri waruhusiwe wanaoweza kurudia. Kwa mfano, nilirudia shule ya msingi hata ninyi hapa wengi tukifuatilia kila mmoja hakuna ambaye hakurudia hapa, wengi walirudia. Kwa hiyo, niwaombe, Mheshimiwa Waziri *consideration* ya kurudia ni muhimu. Wengi hapa wamerudia mara nyingi sana na kuna Profesa mmoja hivi nilikuwa nasikia karudia, kwa hiyo turuhusu watoto wetu waweze kurudia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naungana na Mheshimiwa Shangazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakunda

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri amesimama hapo kujibu hoja, hajakataa kabisa kuhusu kukariri, amezungumzia mfumo rasmi unaoruhusu kukariri kwamba mitihani ya darasa la nne inapofanyika kwa kuangalia hali halisi mtoto anaweza akakariri, sasa huu utaratibu wa kukariri nje ya mfumo rasmi ndiyo ambao umekatazwa sasa hivi. Lazima kuwe na regulations katika nchi, haiwezekani ukaacha tu watu wakawa wanafanya tu *free riding*, haiwezekani lazima kuwe na regulations, udhibiti lazima uwepo. Kwa hiyo, suala lingine kama alivyosema Mheshimiwa Mulugo kwamba kuna Kamati ya pamoja hiyo itakapopeleka mapendekezo tutayajadili ndani ya Serikali na kukubaliana utaratibu mzuri zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Waheshimiwa Wabunge. Ukiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge wote wanaona kwamba liko tatizo ambalo linahitaji kupatiwa majibu na kama kuna tatizo ambalo linatakiwa kupatiwa majibu wanarudi katika kile ambacho Mheshimiwa Waziri

amekizungumza na Mheshimiwa Waziri ametueleza vizuri sana hapa kwamba kwa sheria ambazo tunazo mpaka sasa na taratibu ambazo tunazo mpaka sasa wako baadhi tena amesema wachache, *owners* wa shule wamekuwa wakikiuka taratibu hizo kwa makusudi bila kufuata taratibu tulizojojivekea. Lakini wako *owners* ambao wanamiliki hizo shule za *private* wanafuata hizo taratibu na hakukuwa na shida yoyote na ndiyo maana kwa sababu Serikali ina wajibu wa kusimamia sekta ya elimu na kama ina wajibu, Mheshimiwa Waziri ametueleza vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali iligundua liko tatizo kama tunaloliona sisi hapa ndani na ikitisha kikao kati ya *private sector* na Serikali kuona ukubwa wa tatizo na Mheshimiwa Mulugo ame-*declare* hapa kwamba na yeye ni mdau na yeye anasema tatizo hili ni kubwa na baada ya kuona hivyo Serikali imeamua kuunda kikosi kazi cha pamoja. Sasa kama tumeamua kuunda kikosi kazi cha pamoja kati ya wadau na Serikali ina maana mwisho wa siku tutagundua kiini cha tatizo na tutapata suluhu ya tatizo liliopo na tutarekebisha na kuweka utaratibu na mfumo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuyasema hayo nimuombe sana Mheshimiwa Shangazi aelewe haya majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri hapa ameyaeleza vizuri sana. Amrudishie shilingi na Mheshimiwa Mulugo kwa sababu ni mionganini mwa hao waendeshaji wa hiyo sekta wakae pamoja, wapate hiyo suluhu na ikishapatikana itakuwa ndiyo muarobaini wa tatizo hilo kwa maisha yote kwa watoto wa kitanzania kwa mujibu wa Sheria.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Shangazi, Waziri lakini kwa maelezo...

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa...

**MWENYEKITI:** Ngoja labda ana ya ziada hebu msikilize kidogo labda ana ya ziada.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wameniunga mkono na Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii wakimuunga mkono Mheshimiwa Shangazi nimewasikia, lakini naomba nirudie kusema tena, hili suala tumekwishaliona na nimesema mwenyewe binafsi ndiyo ambaye nilikaa kikao na wamiliki wa shule binafsi na tukaunda hiyo Kamati ambayo ina watu sita, watatu wanatoka Serikalini na watatu wanatoka kwenye shule binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sioni ni kwa nini sasa kama nimekaa kwenye kikao, nimeunda Kamati, watatu wanatoka Serikalini na watatu wanatoka kwenye shule binafsi sioni kama kuna tatizo gani, tungewapa nafasi wakamilishe kazi yao halafu kama kutakuwa na suala lingine tutalizungumzia. Naomba sana Mheshimiwa Shangazi nirudishie shilingi yangu ili niweze kusimamia majadiliano yakamiliike ili suala hili liishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naomba sana Mheshimiwa Shangazi tafadhali sana nirudishie shilingi yangu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wote hawa wanadaiwa hata hela za faraja hawana, kwa hiyo shilingi inaweza ikarudi, lakini tu niseme kwamba kwa kuwa wako kwenye huo mchakato wanaoendelea nao, tungetamani sasa kwamba kuwe na utaratibu rasmi unaotambulika. Kwa mfano, hata hii kusema shule inafelisha watoto 160 halafu wanatakiwa wafukuzwe ina maana pia hapo ni tatizo ambalo pia inatakiwa waone

kwamba upande wa pili nako kuna tatizo haiwezekani watoto wote hawa wakafeli halafu shule ipo na inachkuliwa tu *for granted* kwamba wahamishwe shule. Kwa hiyo, nakurudishia shilingi, lakini ulipie *Faraja Fund*. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felister Bura. Kama hoja ni hiyo hiyo unasema tu kwamba mimi najiondoa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru kwa kunipa nafasi, sina tatizo na utendaji wa Profesa Joyce Ndalichako lakini kuna mambo ambayo yanakwamisha na yanataka kukwamisha utendaji wako na ninajua ukiyafanya kazi mambo yatakwenda vizuri katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Serikali ni kutoa elimu bora nchini kwa watoto wetu na watoto wetu tunatamani wawe maprofesa kama wewe, lakini ufaulu kwa watoto au kwa wanafunzi ni dhana pana na ambayo mchakato wake unahitaji umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumegundua na tunajua kwamba katika shule zetu, vitabu vya darasa la nne havipo na ambavyo vipo vimekosewa. Na sijasikia taarifa yoyote kwamba waliofanya vitabu hivyo vikakosewa na vikaenda mashulenii hawajachukuliwa hatua yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nabu Waziri amejibu hapo kwamba hajajiridhisha na vitabu vilivyopo na watoto wetu hawa wanategemea kufanya mitihani ya darasa la nne muda siyo mrefu, lakini vitabu hakuna.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Natarajia kutoa shilingi kama majibu hayataridhisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

### **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nisema nakubaliana kabisa na dada yangu Mheshimiwa Felister Bura na nitambua fika mimi kama mwalimu kitabu ni nyenzo muhimu sana katika kumfanya mwanafunzi ajifunze na ninakiri hapa niliposimma katika Bunge lako tukufu wakati nkipisha bajeti yangu ya mwaka 2017/2018 kweli kulikuwa na changamoto kubwa sana ya vitabu ambavyo vilikuwa vinatumika shulen. Na Waheshimiwa Wabunge niseme kwamba changamoto zilizokuwepo katika vile vitabu ilikuwa ni zaidi ya vile ambavyo nyinyi mlivizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala ambalo limesababisha uchelewaji wa vitabu vyta darasa la nne kwa sababu kazi ya uandaaji wa vitabu vyta darasa la nne ilikuwa inafanyika sambamba na marekebisho ya vitabu vyta darasa la kwanza mpaka la tatu kwa sababu vitabu 16 vimefanyiwa mapitio na tumevichapa upya na ukiangalia katika kitabu changu nimeeleza kwamba tumetoa nakala 8,460,000 ambazo zimepelekwa shulen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu hivi ambavyo vimetolewa, vitabu vimesimamiwa vizuri kuhakikisha kwamba hakuna makosa. Wale waliosababisha vitabu ambavyo vimeondolewa shulen, kwanza hatua ya kwanza ambayo imechukuliwa katika hatua ya kinidhamu, kuna watumishi 22 wa Taasisi ya Elimu Tanzania waliohusika katika kuandika vitabu vyenye makosa na hatutaishia tu katika kuwasimamisha kazi, kuna gharama za Serikali ambazo zilitumika, kwa hiyo lazima pia wachukuliwe hata mashitaka, wanasheria watatusaidia kwamba ni kifungu gani kwa sababu ni uzembe ambao umelisababishia Taifa hili hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bura ulikuwa unataka kujua hatua zilizochukuliwa, umemsikia?

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa majibu yake hayo aliyoyatoa lakini Wizara hii ina wataalam wengi sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, katika hatua hii sasa kama hujaridhika na majibu...

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja suala hili lijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Hujaungwa mkono, tunaendelea. Waheshimiwa Wabunge Kanuni hawafiki 10. Mheshimiwa Hussein Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na kama hatoniridhisha safari hili tutakwenda kwenye kura, kwa hiyo nitashika shilingi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, nampongeza Waziri kwa *performance* anayofanya na anajitahidi. Nataka tu jambo dogo na nipate *commitment* kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; suala la *quality, access to education* tumefanyakazi kubwa sana kama nchi, lakini suala la *quality of education* ni jambo la msingi na *quality of education* ina *component* nyingi. Mojawapo mna programu ya *Performance for Results*, mnaandika maandiko kupata fedha kutaka kwa *donors*. *Commitment* yako katika suala hili la *ku-improve quality* ya *education* katika *development* ya *infrastructures* za sekta ya elimu hasa elimu ya msingi, *u-commit* kwamba fedha hizi utaendelea kuzisimamia katika Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, utu-*commit* hapa kwamba, kilio cha watanzania juu ya suala la ubora wa elimu sasa mwaka huu wa fedha tunakupitishia bajeti ya 2018/2019 itakuwa ni moja ya *priority*yako ili tuweze kupata majibu ya haya matatizo yote tunayoyajadili sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, akinijibu vizuri nitamuachia shilingi yake.

**MWENYEKITI:** Katika mwaka mmoja? Haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumwambia kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe kwamba suala la ubora wa elimu (*quality of education*) ndiyo limekuwa kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Tano na nimetoa *quotation* ya Mheshimiwa Rais alipokuwa anazindua Bunge alisema kwamba ye ye katika sekta ya elimu atasimamia ubora. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba hiyo imekuwa ni kipaumbele lakini niseme kwamba labda kasi ya kuweka huo ubora imekuwa labda haiendi kwa namna ambayo ni kubwa sana kwa sababu hasa ya usimamizi. Serikali Kuu inafanyakazi kubwa sana lakini kama nilivyosema kwenye majibu, na kuhakikishia katika mwaka huu nitalala mbele na Maafisa Elimu wazembe ambao hawafanyi kazi yao kwa hiyo nitasimamia kweli kweli *quality of education. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala lake la fedha ambazo tunapata kwa washirika wa maendeleo ambao nawashukuru sana wako hapa mpaka leo hii wanaangalia tunavyomaliza mjadala wangu, niseme tu kwamba hizi fedha tunaziomba kwa ajili ya Serikali na manufaa ni kwa ajili ya Serikali, kwa hiyo, sidhani kwamba kunaweza kukawa na ugomvi wowote wa kugombania fedha kwa sababu siyo za Ndalichako, ni fedha za Serikali, nikiomba kwa washirika wa maendeleo ni kwa ajili ya Serikali. Kwa hiyo, naamini kwamba hapa sitegemeli mgogoro wa kusema kwamba hizi fedha ambazo wameziomba kwa Washirika wa maendeleo wakaingia mkataba na Waziri wa Elimu zitaenda mahali pengine lakini hata zikienda Wizara ya Fedha kwa mfano, ni Serikalini lakini naamini kwamba mahali ambapo fedha zimekwenda kwa sababu kuna makubaliano, naamini kwamba yale makubaliano yataheshimiwa na kwamba hizo fedha zitaendelea kubaki pale pale. Naomba Mheshimiwa kaka yangu...tafadhalii.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe subiri kidogo ngoja nitumie tu mamlaka yangu niliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) niongeze muda usiozidi dakika 30 ili tuendelee na hoja hii. Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii tuliyofika, kama ningekuwa msahihishaji Profesa ningekupa *50 percent*, umenijibu suala la fedha kwamba zitaendelea kuwa salama na yule aliyezihangaikia, anayesimamia sera. Kidogo ningeomba Waheshimiwa Wabunge kama wataniunga mkono tujadili *commitment* ya wewe kuanza safari ya *improvement* ya suala la *quality* kwamba kwa mwaka huu wa fedha tunaanza kuhangaika na suala la *quality* ya elimu. Kwa hiyo, ningeomba Waheshimiwa Wabunge kama wataridhika tulijadili kidogo na uweze kutupa *commitment* itakayotupa *confortability* ili tuweze kukubaliana katika hili. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Hujatoa hoja

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Alaa!! Haijaungwa mkono na Wabunge kumi, ni watano tu. Tunaendelea Waheshimiwa. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Profesa Ndalichako kwa kazi kubwa anayoifanya na nimesimama kwa ajili ya suala zima la ubora wa elimu na upatikanaji wa elimu kwamba limekuwa likiyumba mara kwa mara ni kwa sababu ya kutokuwepo kwa uratibu au chombo kinachoratibu elimu. Sasa kutokana na kukosekana kwa chombo kinachoratibu elimu, mabadiliko yote ya Serikali au ya Waziri yamekuwa pia yakija na mabadiliko ya mfumo wetu wa uendeshaji wa elimu. Kwa mfano, kuna Mawaziri walikuja wakaondoa michezo mashulenii, wengine wakaondosha shule za ufundi, wengine wakaamua kuziondosha shule kwa mfano mimi nimesoma sekondari ya Ndanda ikiwa ya kidato cha kwanza

mpaka cha sita ikiwa ya wasichana na wavulana wakaamua iwe ya wavulana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii yote imetokana na kutokuwa na chombo kinachoratibu elimu ambacho kitamuwezesha kila Waziri anayekuja aweze kufuata kile ki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri maelezo.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niwambie dada yangu Mheshimiwa Hawa Ghasia kwamba, Serikali inasimamia vyema elimu kupitia udhibiti bora wa shule na kwamba suala la kuunda chombo cha wallimu labda tulitazame ka mtazamo kwamba utadhibiti ile mtu kufanya mabadiliko. Nadhani kitu cha msingi, elimu yetu iendane na sheria na taratibu kwa sababu kitu kikiwa kwenye sheria huwezi ukakifanyia mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kinachotakiwa hapa tungejikita zaidi katika kuhakikisha wkamba masuala muhimu ya elimu ama yanakuwa katika Sheria ama yanakuwa katika suala ambalo kubadilisha kwake kutakuwa kunapata ridhaa lakini kwenye kuunda chombo cha kusimamia ubora wa elimu, tunayo Taasisi yetu ama Kurugenzi yetu ya udhibiti ubora wa shule ambayo nimeeleza masuala ambayo yanafanyika katika kuimiarisha na kwamba tunatarajia pia hata kuimiarisha hii udhibiti bora. Sasa hivi mdhibiti ubora wa Wilaya anakawa anakagua tu shule za msingi haendi kukagua sekondari sasa hii inakuwa inaleta *inefficiency* katika zoezi zima la ukaguzi kwa sababu jirani na shule ya singi ipo shule ya sekondari.

Mheshimiwa Mweenyekiti, haya yote tumeyaona na tunayafanya maboresho. Ningeomba kabla ya kufikiria kuunda vyombo kwa sababu vyombo navyo vinakuwa na gharama zake, Serikali ipewe muda wa kuangalia hizi hatua

ambazo tumeziweka na kama kutakuwa na umuhimu basi hilo jambo tutaliangali, kwasababu tayari kuna mambo mengi ambayo nimeyaeleza kwenye hotuba yangu ya kufanya katika kuboresha udhibiti bora. Kwa hiyo, naomba sana usinishikie shilingi haya mambo ambayo unayaafanya tutafanya kwa pamoa na ndio maana hata hii ya kukariri tunafanya na shule binafsi kwa kutambua kwamba elimu sio hatimiliki...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja kwa sababu nimezungumzia elimu kwa ujumla, sikuzungumzia ubora chombo cha kuratibu elimu kwa maana ya sera, kwa hiyo natoa hoja kwamba lijadiliwe.

**MWENYEKITI:** Haya nitachukua wawili wawili jamani sababu ya muda, *we cannot continue* namna hii tuanze Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Esther wote wawili, Waheshimiwa Wabunge mtakuja kunilaumu mimi baada ya muda mfupi tu Mheshimiwa Mulugo, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Nsanzugwanko, nitawabeba wote tu si mnataka haya Mheshimiwa Komu, Mheshimiwa Cecil nimechukua wote Mheshimiwa Lyimo nimekukwepa, Mheshimiwa Kasuku nimekuweka Mwalimu au unapenda tu kufundisha tunaanza Mheshimiwa Peter Serukamba .

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hoja nyingi sana za Wabunge sikutamani kusimama, lakini moja ya pendekezo kubwa ambalo tumekuwa tunalitoa kama Kamati kwa miaka mitatu imekuwa ni kwamba nadhani umefika wakati wa kupitia mfumo wetu wa elimu katika mapana yake unaona hapa tunataka ku-*solve* tatizo nusu nusu, kuna mtu anadhani tukiweka chombo tutakuwa tume-*solve* watu wakikariri tutakuwa tume- *solve*, nadhani niombe Serikali umefika wakati kwa sababu elimu yetu imepitia mabonde mengi sana ukianzia toka tumeanza awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu , ya nne mpaka sasa.

Kwa hiyo, nilidahani umefika wakati kama Taifa tukubali tuanzishe tupitie upya mfumo wa elimu kuanzia *kindergarten* mpaka chuo kikuu ili tuangalie kuna nini. Kwa sababu hapa tunachotaka kufanya ni kudhani labda tukileta chombo hiki tuta-solve tatizo mimi sillioni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza leo Waziri anasema ambao nimeshtuka kwamba hata mtu akifaulu kwa kiwango cha *division four* ni ufaulu lakini kweli leo ufaulu ambao tunata tukae hapa kama Bunge hili kwamba tuna kundi kubwa linapata *division four* hivi kweli hili Taifa tunalisaidia?

Naomba sana niombe Serikali itafakari tuupitite mfumo wetu wa elimu tuangalie mitaala tuangalie tunavyopata walimu, tuangalie *role* ya wazazi, tuangalie tunavyo-finance education, tuangalie masaa yanayofundishwa, tuangalie yote baada ya hapo tutakuja na *blue print* ambayo itatusaidia sasa twende, tutaondokana na haya sijui ya kukaririsha yote yataondoka tukishajua *direction* ya kupeleka elimu yetu nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante lakini hoja mahususi iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Hawa Ghasia ni kuundwa kwa chombo mahususi cha Udhibiti cha Kuratibu Elimu nchini hasa Mheshimiwa Serukamba umechangia vizuri, lakini nataka niwarejeshe kwenye hoja *that it's a narrow hoja* ambayo iko mbele yetu, Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nasimama nikiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kila sababu ya kuona kwamba nchi yetu ya Tanzania na kama Taifa ambalo tumejipanga katika kujenga ni mizania yenye haki na usawa lakini pia katika kujenga rasilimali watu ambayo itaheshimika na kuingia kwenye ushindani wa kidunia tuna kila sababu sasa ya kusimama imara. Ninakubali kabisa kuna kila sababu

ya kuwa na chombo hichi ndio chombo pekee kwa ninavyoamini ndiyo chombo cha pekee ambacho kitaleta mizania ya usawa, ha na uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna shule za Wizara ya Elimu, lakini tuna shule za TAMISEMI, lakini tuna shule za watu binafsi, lakini kila maelekezo kila makaripio sijui nisemeje inakuwa inaelekezwa kwenye shule binafsi. Ninasema tuna kila sababu yakuwa na chombo hiki ukiangalia uwekezaji wa Serikali Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ametoa shilingi bilioni 427 kwa Bodi ya Mkopo akitarajia kuvuna mema katika nchi hii lakini tumekuwa na vyombo vingi tunayo *NECTA*, tunayo *TACTIE* ambayo ndio yenye mitaala ndio yenye vitabu, lakini bado tunaona hatupati tija katika utungwaji wa vitabu, hatupati tija katika maelekezo mazima ambayo Wizara inatueleza kwamba imekaa katika kujenga mustabali wa elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *NACTE*, tuna *TCU* hivi vyote ni vyombo ambavyo tunavitengea bajeti katika Bunge lako hili Tukufu lakini ubora bado hatuuoni kwa hiyo tuna kila sababu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha muda wa  
Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Esther Mahawe.

**MHE. ESTHER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niunge hoja mkono ya Mheshimiwa Ghasia, ni kweli tunahitaji sana chombo hiki ambacho kitatenda kazi kwa haki na usawa, kinachofanyika sasa katika shule binafsi na shule za Serikali ni kucheza na *referee mchezaji*, kwa hiyo hakuna *fair play* mfano mzuri tu ni sera ya elimu ilivyokuja KKK hakuna walimu wa *private schools* waliochukuliwa na Serikali kwenda kuwafundisha huo mtaala mpya unatakiwa ukafundishwaje. Hapo ndipo tunapoanza kuona jinsi gani mtoto mmoja ni wa kambo na mwingine ndio mtoto wa ndoa. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri chombo hiki kiianzishwa kitawezwa ku-regulate shule zote za TAMISEMI

pamoja na shule za *private* kwa kuona kwamba ikiwa shule hii labda hawa-*perform* vizuri chombo hicho kitafanya kazi kama ni *private school/wanakosea* chombo hicho kitafanya kazi kwa usawa na mizania inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zinatolewa nyaraka mbalimbali kutoka kwa Wizara ya Elimu ambayo haimfikirii yule mdau namba mbili ambaye ni sekta binafsi, shule tunaambiwa tuendeshe kwa *term* mbili hawajafikiria namna gani hizi shule zinaweza zikaendeshwa kwa *term* mbili wakati zile zilkuwa *term* tatu. Changamoto ni nyingi tunaomba chombo huru cha kuweza kusimamia elimu ya nchi hii kwa mapana na marefu yake, ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa ninaomba kuunga hoja mkono ya Mheshimiwa Waziri. Nchi hii ninachoona nimesikiliza hoja za pande zote mbili kikubwa ninachokiona ni utayari na usimamizi uliokuwa bora ili kuepuka Serikali kuendelea kutumia gharama kubwa kuendelea kuanzisha kila siku mara vyombo, mara sijui tume, mara sijui nini; vitu hivi haviwezi kuweza kufanikiwa ikiwa kama hatuna dhamira ambayo inatoka moyoni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira hii naiona kwa Mheshimiwa Waziri ana dhamira nzuri hivi vyombo ninaona kwamba vitakuwa vinaendelea kuongeza mzigo kwa wananchi wetu gharama ni kubwa. Sasa hivi yenye we tumekaa tunaanza kujadili mpaka kwamba tunahitaji mpaka vyoo, sasa mikopo tunataka, walimu tunataka waongezewe mishahara, tuongeze tena na vyombo mimi suingi mkono hoja ya Mheshimiwa Mbunge. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba niseme namuunga mkono Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa hoja aliyotoa kwa sababu matatizo mengi

ambayo tunayaona katika mfumo wetu wa elimu na hasa hii kitu naona kama *double standard* ni kwa sababu hakuna chombo ambacho ni huru na ambacho kiko *beyond interest* mbalimbali labda hata za sasa na vitu kama hivyo kusimamia elimu. Kwa hiyo, kuna haja sasa hivi kukawepo na chombo na ukiangalia tu *good practice* ni kwa nini kuna Tume ya Taifa ya Uchaguzi? Ni kwa sababu inakaa pale kuangalia haki ya pande mbalimbali ambazo zinashindana, sasa hapa tuna *players* zaidi ya mmoja; tuna shule za Serikali, tuna shule ambazo haziko za Serikali sasa kama tunataka *ku-maintain standard* na kuona kuna *fairness* ni lazima kuwepo na chombo ambacho kiko pale *permanently* na kinaona kinaangalia *interest* na *fairness* ya ubora wa elimu na vitu kama hivyo bila kuenda kwenye vitu ambavyo vinaweza kufanya wewe unakuwa *referee* wakati huo huo wewe ni *player* kwenye *game* nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu hiyo namuunga mkono Mheshimiwa Hawa Ghasia na naiomba Serikali ikubaliane na hili kwa sababu ni jambo ambalo litatusaidia kama nchi tuweze *ku-excell* vizuri zaidi kuliko kuendelea kung'ang'ania na *ku-maintains status quo* ambayo haitusaidii kama Taifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru niunge mkono asilimia mia moja hoja ya Mheshimiwa Hawa Ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana nadhani hoja hii ingemsaidia sana Mheshimiwa Waziori kwa sababu anatambua kwamba elimu katika nchi hii imeshakuwa janga na sababu kubwa ambazo zinapelekecha huko ni kwamba vyombo hivyo anavyovisema vimeshindwa kazi. Nitoe mfano amesema kuna chombo hiki cha udhibiti ubora wa shule. Niko kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chombo hiki kwa mwaka huu ilikuwa imetengewa bilioni moja hajiaenda hata shilingi moja. Sasa kama hiki chombo anachokisema cha udhibiti shule hakijapewa hela maana

yake hakiwezi ku-*perform* lakini tunasema hivi shule za Serikali ni *about* 90% sasa wao wana shule kama Serikali ina shule zake inazisimamia, lakini *at the same time* inasimamia na hizi shule nyingine, *fairness* inakuwa wapi? Kwa hiyo, sisi na siku zote tumesema haiwezekani wao wawe wachezaji, wao wawe makocha, wao wawe marefali haiwezekani haiko popote hakuna *carrot and stick*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kama kweli Waziri unatamani uache *legacy* katika nchi hii hakikisha chombo hiki huru kinaundwa, habari ya kwamba kitatumia fedha ni bora tutumie fedha tuweze kuinua elimu yetu kwa sababu nchi zote zilizowekeza kwenye elimu ndio tunaona zimeendelea. Kwa hiyo, tukianza kusema eti hiki chombo kitatumia fedha *so what?* Ni bora tuendelee kubaki wajinga leo hii Tanzania watu wenyewe elimu *participation rate* ni asilimia tatu tu kwa sababu gani *70 present* wanafeli hivi hatuoni kwamba hili ni janga na kwa maana hiyo sababu mojawapo ni kwamba hatuna chombo ambacho kitasimamia kwa haki lakini vilevile kitakuwa na wataalam wa kutosha kama ambavyo wengine wamesema. Kwa hiyo, niseme kwa kweli...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante hoja nyingi zimezungumziwa na Wabunge kuchangia hoja hii, lakini hoja kubwa hapa nillisema mwaka jana hoja hii kwamba tuwe na kitu *Regulatory Board for Education* nchini kinachowenza kusimamia pande zote tatu nilitoa mfano TAMISEMI wana shule za msingi na sekondari, TAPIA na TAMONGSCO wana shule zaidi ya nusu kama alivyosema leo Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Elimu ina shule za mazoezi za sekondari, ina shule za mazoezi za shule za msingi. Kwa hiyo, hata mitihani inapotolewa ndio maana Baraza limejitenga kabisa ndio maana mambo ya Baraza hapa huwa hatuongelei kwa sababu hayajakaa kisiasa

limejitenga linafanya mambo yake kwa uhuru, ikitoa mtihani hivi Wizara wanashtuka matokeo yamekuwaje TAMISEMI wanashtuka, TAMONGSCO wanashtuka, TAPIA wanashtuka kumbe hata katika usimamizi wa vitu vingine kije chombo kitakachomulika mambo yote haya bila upendeleo mambo ya miula Serikali wanatangaza wao wenyewe wanajitangazia mihula hata hawajui kwamba shule za *private* kuna ada, wamepanga labda mwezi wa kwanza mpaka tarehe fulani mwezi wa tano lakini wao shule zao unakuta wanafunga labda tarehe 12 Juni au labda wanafunga tarehe 2 Julai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kutokana na bajeti zetu tunasema labda tufungue tarehe fulani mwezi wa saba wanasema hapana ni hivi, mambo ya UMISETA yaani kuna mambo mengi sana yameingiliana juu ya hili jambo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba chombo hiki kitakuja kutatua matatizo yote haya ukienda kwenye Idara ya Ukaguzi haina meno, Idara ya Ukaguzi inashauri halafu inampelekea Mkurugenzi ni Serikali ile ile kwenye shule za *private* Idara ya Ukaguzi inakagua inampelekea Katibu Mkuu halafu wanakulima barua tena kwa nguvu na kama hauna hata choo au hauna bweni hawa watoto wamekaa darasani watoto arobaini na ngapi wanakufungia shule, lakini kwenye Serikali mbona hawafungi? Nilisema sana mwaka jana hapa naomba chombo kile kitakapokuja kwa sababu kitakuwa kimekuwa na sheria... Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa umeeleweka vizuri sana, Mheshimiwa Janet Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hawa Ghasia kwa sababu kwa kweli pamoja na mawazo aliyoyatoa Waziri kuwa ana vyombo atavisimamia vizuri zaidi hili tatizo ni la miaka mingi sio la mwaka huu tu au miaka miwili iliyopita na vyombo hivi miaka yote viro, lakini imeonekana wazi ufanisi wake umepungua sana na unaendelea kupungua na vilevile ambavyo kama ambavyo wengine wamesema hivi vyombo viko chini ya Waziri, sioni

wapi mtu wa chombo hicho ataanza kwenda kum-face Waziri wake na kumwambia hapa umefanya vibaya inaweza yakuwa sio rahisi sana lakini tukiwa na chombo *independent* kitakuwa *kina-exercise fairness*, kitakuwa-*efficient* bila kuingiliwa kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo napendekeza sana kuwe na chombo ambacho ni *independent* cha kusimamia masuala mazima ya elimu nchi nzima. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, *if you think education is the expensive try ignorance.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hawa Ghasia, kwanza tuone hali iliyo sasa hivi umuhimu wa chombo hiki, Serikali shule zake zinapofeli yenyeewe inakataa hazijafeli. (*Kicheko*)

Sasa ni nani amwambie amefeli maana yake lazima awepo mwingine wa kukwambia shule zako zina-*under perform* wewe awepo mtu wa kukwambia huku *private* wakifeli Serikali itaawaambia wamefeli wewe ukifeli hata "D" mbili tena umetuambia hapa kwamba jamani ufaulu ni *division fourna division fourni* "D" mbili hivi "D" mbili wanaenda wapi au "C" moja yaani akiwa na "C" moja ni *division four* anaenda wapi na huyo tunasema amefaulu. Kila chombo kingekuwepo kingetusaidia. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine chombo kile kitachosaidia ni matamko haya leo upo wewe Ndalichako unamatamko yako ukitoka atakuja mwingine wapo waliofuta *division waliofuta grade* wakaleta *division* wewe umekuja umefuta *division* kile chombo kingekuwepo ungekuta kimeweka mambo vzuri wewe usingekuwa na vya kufuta. Kwa hiyo, lazima hiki chombo kiwepo *ki-regulate* hali ya *education* nchini mambo yakae vizuri, hatuwezi kwenda tu mmoja naye anayeamua na kwa kweli mtusaidie ni shule gani ya Serikali iliwhahi kufungwa haina choo haipo, ila *private* mnafunga hata vyoo havitoshi matundu yaani vyoo viro

lakini matundu hayatoshi mnafunga ninyi shule zenu hazina hata choo kimoja zinaendelea kudunda, naunga mkono hoja . (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasuku umemkamia sana Mheshimiwa Waziri, mimi ndio naongoza kikao ee! Wewe sasa Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kama ambavyo Wabunge wengine wamechangia hapa ndani naungana mkono na Mheshimiwa Mama Hawa Ghasia pale kwa hoja iliyoko hapa mbele yetu. Nataka tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri ambaye sasa hivi ni Waziri wa Elimu, tumemuona kaka yetu Mulugo pale ambaye naye alikuwa Naibu Waziri wa Elimu kama wewe miaka iliyopita anaanza kujutia maamuzi aliyoyafanya wakati ule na leo anatamani angekuwa hapo kama wewe, kwa vyovyyote vile naamini angeruhusu hiki chombo pale kifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeona Serikali imesema sasa inaboresha elimu, imeongeza wanafunzi wengi tu kwa sababu tunakwenda kwenye elimu ya bure. Wamesahau kitu kimoja kuangalia *quality education*. Wanachoangalia wao ni *quantity education*, watoto wangapi wanakwenda shulen iakini sio kuangalia watoto wangapi wanafaulu kwa ufaulu unaotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Ghasia hapa katoa mfano kuhusu Ndanda Sekondari ndiko alikosoma yeye miaka iliyopita lakini sasa hivi ukifika tena Ndanda sekondari sio shule bora ya Kanda ya Kusini watu wanaongea kuhusu Abei sekondari ndio inaonekana kuwa ni shule bora, sawasawa na hizi shule nydingine za msingi na zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe Mheshimiwa Waziri usipate uzito sana kwenye kufanya maamuzi jambo hilli, hebu tutafute *referee* atakayeweza ku-*balance* haya mambo. Serikali najua mna mahitaji yenu, lakini *private persons* pia nao wana mahitaji yao ya msingi ili mwisho wa

siku watoto watakaosoma shule za Serikali na watoto watakaosoma shule za *private* wapate elimu inayofanana kwa sababu kutakuwa kuna mtu ambaye anakuwa mwamuzi kati ya hawa watu wawili. Tukiacha hivyo, bado tutaendelea kujenga matabaka ya waliopata elimu bora ambao ndiyo watakuja kuwa viongozi wa watoto ambao hawakupata elimu bora kwa sababu kulikuwa hakuna *regulatory authority* pale ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie sababu za msingi za Serikali kuunda *TBS*, nia yao ni kuangalia ubora wa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa, tu...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naomba nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema hivi, hakuna haja ya kuunda chombo kingine kwa sababu hata vyombo hivi tulivyonyavyo Mheshimiwa Waziri uweke mikakati uwe mkali kama uliviyosema kwamba utavisimamia vizuri ili kila chombo kiweze kufanya kazi yake na wajibu wake. (*Makofi*)

Pia msaidiane, mshirikiane na TAMISEMI ili hiyo elimu bora wanayoisema hata hapa mimi ninashangaa sana kwa sababu ili mtu upate cheti ina maana lazima ufuzu na ukifuzu, ukipata *division four* maana umefaulu inategemea ufaulu wako ni wa viwango gani, viwango vinatofautiana tofautiana. Hata ukienda katika nchi zilizoendelea kuna ufaulu ambao unatofautiana, hakuna mtu anayeitwa amefuzu aliepata sifuri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba kabisa hakuna haja ya chombo kingine, tunahitaji fedha hizo ni gharama. Hatutaki watu watujie hapa, hawa ni watu wanaobadilika kama mvua na majira ya Dar es Salaam.

Watakuja kesho watadai hela kwa ajili ya hicho chombo, utashindwa kukisimamia, utashindwa kukilipa, tunahitaji fedha kwa ajili ya maendeleo mengine. Ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la kuwepo au kutokuwepo chombo cha kudhibiti elimu ni la mapana marefu sana. Elimu hii tangu enzi za Mzee Makwetta (marehemu sasa) mpaka leo, sekta ya elimu imepitia katika changamoto kubwa sana. Mimi sielewi ndugu zangu Wabunge unavyoweza kuzungumza suala la kuanzisha chombo *in isolation*, sioni mimi. Lazima jambo hili lizungumzwe *holistically* na maadam sasa Mzee Mkapa, Mzee Kikwete na Waziri hapa amekiri kwamba mjadala mpana wa elimu ni ruksa, ndiyo wakati wake, tuyazungumze kwa upana na marefu yake. Kwa sababu elimu hii tunazungumza udhibiti wa ubora, sio kwamba limeanza leo, ni la siku nyingi sana.

Kwa hiyo, hoja yangu mimi sasa ni kwamba Waziri maadam amekubali hoja ya Mheshimiwa Ghasia imewahi, tusubiri shughuli nzima ifanyike, mjadala mpana ufanyike ili jambo hili lijadiliwe kwa ujumla wake, *holistically*. Hiyo ndiyo hoja yangu. Nakushukuru. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mwenye hoja. Haya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Uliyasema wakati una-*wind up* hoja yako, hebu yarudie vizuri hayo uliyoyasema, ahadi ya mjadala huo ni upi? Katika sura gani maana mkilisema vizuri hilo itasaidia. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, unataka nizungumzie ile niliyokuwa nazungumzia mjadala wa kitaifa?

**MWENYEKITI:** Ili mwenye hoja naye apime sasa kama bado anataka kuendelea na hiyo. Ulilieleza hilo wakati una-*wind up* huo mjadala wa kitaifa.

### **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile nilikuwa najibu hoja kwamba Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanasema uwepo mjadala wa Kitaifa nami nikasema mjadala ni kitu ambacho kina afya na nikatoa mfano wa mijadala ambayo imekuwa ikifanyika, lakini mijadala si lazima iwe inafanyika kutokana na Serikali kwa sababu mtu ambaye anaona kuna haja ya mijadala, nchi hii imekuwa ina utamaduni ana-*initiate* na ndiyo maana nimetoa mifano ya mijadala mbalimbali ambayo imefanyika na kwa misingi hiyo hata kwenye elimu mijadala mpana unaweza ukafanyika ndiyo kitu ambacho nimezungumza wakati wa ku-*wind up*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwenye hoja, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe ambao kwa kweli wamechangia na mimi nina imani kabisa kwamba Serikali imesikia, sasa sina nia mimi ya kuchukua shilingi, kwanza shilingi hainitoshi, kwa hiyo, namrudishia Mheshimiwa Waziri shilingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Michango ya Wabunge katika upande wa sekta ya elimu imekuwa inatoa changamoto nyingi sana na hususan Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Waziri amekiri katika kuhitimisha kwamba ina mapungufu mengi sana na. Mfano tu katika elimu hii ya msingi kwa sasa hivi ibebe sekondari mpaka na msingi na kufuta darasa la sita maana yake shule za msingi takriban 11,000 zikawe kuwa za sekondari. Changamoto iliyopo ni uwekezaji mkubwa utahitajika na wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kauli ya Serikali kwa nini asifute hii Sera ya Elimu ya Mafunzo ya mwaka 2014 na akaja na sera mpya ambayo sasa itaenda kuboreshwa upande wa sheria na kanuni.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaingia kwenye *guillotine*.

### **FUNGU 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kif. 1001 – *Administration and HRM*... Sh.6,939,228,003/=  
Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ..... Sh.995,953,414/=  
Kif. 1003 – *Policy and Planning* ..... Sh.1,137,687,515/=  
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ..... Sh.532,560,600/=  
Kif. 1005 – *Procurement Management Unit* ...Sh.316,806,056/=  
Kif. 1006 – *Government Comm. Unit* .....Sh.183,838,254/=  
Kif. 1007 – *Legal Unit* ..... Sh.209,381,532/=  
Kif. 1008 – *ICT and E-Learning* ..... Sh. 493,492,985/=  
Kif. 2001 – *Basic Education Dev. Office* ...Sh. 70,261,333,153/=  
Kif. 2002 – *School Quality Assurance* .... Sh.36,742,242,180/=  
Kif. 2003 – *Regional & Inter Education Affairs Coordination Unit* ... Sh.165,380,705/=  
Kif. 2004 – *Education Sector Performance Coordination Unit* .....Sh.98,647,695/=  
Kif. 3001 – *Basic Education* ..... Sh.157,767,340/=  
Kif. 3002 – *Adult Education & Non Formal Education* .....Sh.616,864,121/=  
Kif. 4001 – *Secondary Education* ..... Sh.273,345,799/=  
Kif. 5001 – *Teachers' Education*.... ..... 29,032,529,003/=  
Kif. 7001 – *Higher Education*.... .....Sh.274,432,209,954/=  
Kif. 7002 – *Technical & Vocational Training Division*... Sh.21,810,408,928/=  
Kif. 8001 – *Science, Techn. & Innovation*... Sh.32,100,546,763/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

### **MIRADI YA MAENDELEO**

#### **Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Kif. 1001 – *Administration and HRM*... Sh.2,500,000/=  
Kif. 1003 - *Policy and Planning*.....Sh.168,206,923,878/=  
Kif. 1008 – *ICTand E-Learning* ..... Sh. 0/=  
Kif. 2001 – *Basic Education Dev. Office*...Sh.152,995,945,522/=

Kif. 2002 – *School Quality Assurance* .... Sh.13,000,000,000/=  
Kif. 4001 – *Secondary Education* .... Sh.25,000,000,000/=  
Kif. 5001 – *Teachers' Education* ..... Sh.44,612,001,500/=  
Kif. 7001 – *Higher Education* .... Sh.497,089,861,100/=  
Kif. 7002 – *Technical & Vocational Training Division* .... Sh.5,295,319,000/=  
Kif. 8001 – *Science, Technology and Innovation* .... Sh.21,269,351,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa Kamati yako ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge linarudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, mtoa hoja, Taarifa.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kuwa Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makof)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge. *(Makof)*

*(Hoja llitolewa lamuliwe)  
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu,  
Sayansi na Teknolojia Mwaka wa Fedha 2018/2019  
yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri walioafiki wameshinda, kwa hiyo, Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2018/2019 sasa yamepitishwa rasmi na Bunge. (*Makofi*)

Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Profesa Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Naibu Waziri Mheshimiwa Ole Nasha, lakini pia Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, watendaji wa Wizara hii na Maofisa wote wa Wizara, lakini pia pamoja na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Waheshimiwa Wabunge, umekuwa ni mchango mzuri sana kwa siku mbili. Nimesikiliza sana sana kuanzia kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge na michango ya Wabunge imekuwa na afya sana. Nishukuru zaidi kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri katika kuyaelezea vizuri kufafanua vizuri hoja za Wabunge, ameelezea vizuri sana na hata hili ambalo tumemaliza nalo kwenye Kamati ya Matumizi kwa sababu Serikali inasikiliza na ndiyo maana wameahidi kuititia mafungu haya ambayo tumewapa, wakajaribu sasa kuyafanya hayo ya kuboresha elimu, lakini pia na kusikiliza hoja zile zingine.

Waheshimiwa Wabunge, hatuwezi kuyafanya yote kwa wakati mmoja, tunaenda hatua kwa hatua na elimu itaboreka tu. Dhamira ipo na mnaona Serikali imeongeza shilingi trilioni 1.3, naamini tukiendelea namna hii, wanaomba tunapima kazi zao, tunawawezesha kama Bunge wakayafanye, tutaenda vizuri na kufika 2030 tunaweza tukafika kile kiwango cha asilimia mpaka sita ya Pato la Taifa tunaenda kwenye elimu. (*Makofi*)

Hongereni sana, niwatakie kila lillilo jema, Bunge liko nyuma yenu, haya ni mawimbi lakini tutavuka. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Baada ya kusema hayo, sina matangazo na miongozo sasa hivi haitakiwi ila tu niseme kwa kesho mimi mtapata miongozo, leo hapana. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Alhamisi saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.12 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 3 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*